

ITIKADI WA MUNGU KATIKA NAFSI
TATU

[THE DOCTRINE OF THE TRINITY]

Christianity's Self-Inflicted Wound

Anthony F. Buzzard and Charles F. Hunting

Utangulizi.....	3
I. MUNGU WA YAHUDI.....	10
II. YESU NA MUNGU WA YAHUDI.....	21
III. JE, WAFUASI WA YESU WALIFIKIRIA KWAMBA YEYE [YESU] ALIKUWA MUNGU? 25	
IV. PAULO NA UTATU WA MUNGU.....	37
V. KUTOKA ULIMWENGU WA KIEBRANIA WA BIBILIA KUFIKIA KARNE YA ISHIRINI KUPITIA FALSAFA YA KIYANUNI.....	51
VI. UTATU WA MUNGU NA SIASA.....	67
VII. HALI YA KUWEPO-KABLA KATIKA AGANO JIPYA.....	77
VIII. YOHANA, KUWAPO-KABLA, NA UTATU.....	89
IX. ROHO MTAKATIFU: MTU WA TATU AU MUNGU KATIKA HATUA.....	114
X. VITA JUU YA UTATU KATIKA HISTORIA YA KANISA NA MJADALA WA SIASA.....	123
XI. CHANGAMOTO INAYOKABILI IMANI KATIKA UTATU MTAKATIFU.....	140
XII. JE, TUMEBADILISHANA KWA MUNGU MWINGINE?.....	157
XIII. OMBI LA KUREJEA KWA KRISTO WA BIBILIA.....	168
XIV. MUHTASARI: KUAMINI MANENO YA YESU.....	179

UTANGULIZI

Hakuna mahali popote katika Agano Jipya panapatikana kifungu cha maandishi kilicho na jina „Mungu“ ambalo limetumiwa kwa hakika yote kumaanisha yule Mungu aliye nafsi tatu kwa ukamilifu wote, akipatikana /akiishi) katika nafsi tatu.- Karl Rahner

Kitabu hiki kinahusika na swala moja pekee. Je Bibilia inafundisha ya kwamba Mungu ni nafsi moja pekee, muumbaji wa pekee wa mbingu, ama miungu unajumuisha washirika wawili ama watatu walio na usawa? Awali hawa waandishi walishikilia kueleweka kuliopo kwamba Yesu ana usawa na milele unao shirikisha baba yake/pamoja na baba yake. Tulifundisha mwelekeo huu kwa miaka ishirini. Tulijua kwa hakika kuwepo kwa mistari katika agano jipya ambayo ingeonekana kuunga mkono itikadi ya kale / kanuni ya utatu mtakatifu wa Mungu. Lakini utafiti wa maandiko matakatifu na historia ya kanuni za dini umetuelekeza kusadiki kwamba hoja ya utatu mtakatifu wa Mungu inahimiliwa msimamo wakuchukulia maandiko ya Bibilia katika njia inayo tia shaka, inapuuza ushuhuda mwingi wa kuunga mkono imani katika ibada ya Mungu mmoja:- imani katika Mungu mmoja kama nafsi moja, Baba Yesu Kristo:- na inategemea sana tafsiri za mistari michache teule. Inatenga vifungu fulani na kusahau kuwa muktadha wake (vifungu) ni maandiko matakatifu yote.

Itikadi/kanuni za kibibilia ni lazima vijengeke katika vifungu vilivyo wazi na vilivyo na uumbe wa moja kwa moja vinavyozingatia moja kwa moja maada inayoshugulikiwa. Msimamo wa kiimani na kibibilia ukichukuliwa katika maana ya moja kwa moja kuambatana na sheria za kawaida za lugha unawasilisha kanuni kuhusu Mungu ambayo haikubaliani na mifumo ya imani ya jadi. Tulipo chunguza swala la kanuni ya kibibilia tulitiwa moyo katika utafiti wetu na uchunguzi wa hivi punde wa watalamu wabibilia wajulikanao. Wasomi wengi wanakubali sasa kwamba itikadi ya nafsi tatu katika Mungu mmoja haiwezi kuthibitika katika bibilia. Huu ni upotoshaji wa Bibilia wa watu wasio wayahudi ulioanza baada ya uandishi wa Bibilia.

Huenda ikawa kuungama kuhusu jaribio la kutumia Bibilia ili kutetea utatu mtakatifu wa Mungu ni kwa mwanaelimu wa dini katika imani ya utatu mtakatifu wa mungu wa karne hii. Leonard Hodgson anatarifu ya kwamba katika mijadala ya karne ya kumi na saba na kumi na nane, kati ya walio mwamini Mungu aliye nafsi moja wa wale walio mwamini Mungu aliye nafsi tatu, pande zote mbili “ Zilikubali kwamba Bibilia inafumbua jambo hili katika hali ya pendekezo.” Anamalizia kwamba “kuambatana na hoja iliyobishaniwa na pande zote mbili, wanao mwamini Mungu katika nafsi moja walikuwa na hoja bora”¹. Mtazamo huu unastahili kufikiriwa kwa uangalifu na wanao mwamini Mungu katika nafsi tatu wote.

Ni mapenzi yetu kwamba msomaji atachunguza ithibati iliyo tolewa na mawazo yalio funguka. Tunatambua ya kwamba hili si jambo rahisi kwa mtu yeyote ambaye amelimishwa na labda aliyekita mizizi katika mtazamo mwigine wa elimu ya dini. Itikadi/kanuni ikisha kubaliwa kuwa kweli na kihizia, ushindani/upinzani wowote juu ya itikadi hii ambayo imekwisha zoewa haina budi kukataliwa pasipo maswali. Sisi sote kama binadamu huvutiwa kuiana na kundi ambalo limetulisha pamoja na mifumo ya mawazo katika maisha yetu yote. Tumejifunza kutoka kwa walimu wa kweli tulio waamini na kuwaheshimu na tunaweza kujenga kuta zinazo tusitiri dhidi ya pingamizi

¹ *The doctrine of the Trinity* (Nisbet, 1943) 220, 223, emphasis added. The Unitarian understanding of the nature of God which we propose in the following chapters should not be confused with the contemporary Unitarian Universalist theology.

zote na zinaweza kutupofua tusione ukweli ulio wazi kabisa. Hii imani tunayo shikilia kwa dhati ipingwapo bila shaka tunajihisi kutishwa na kujikinga. Mwandishi wa dini ya karne ya kumi na tisa kwa jina *Robert Hall* alikuwa na hili wazo la busara kwamba:

Chochote kinacho pinga roho ya udadisi, hatakiwe na wahisani gani ni rahisi kipotoke na kikose kufikia ukweli. Na inakubalika ya kwamba hakuna chochote kingependelea kupinga moyo wa udadisi kama hisia ya kuwa sehemu ya kundi. Punde tu kanuni / itikadi iwapo kama kitambulisho cha kundi fulani hata iwe na upungufu, inakita mizizi mara moja katika kuhusika na kushikamana na linakuwa jambo gumu sana kuing'oa hata kwa kutumia silaha ilio kuu².

Dhana zinazojengwa katika sura zifuatazo si mpya, ingawa zilifichwa katika karne hii. Zilikuwa jiwe la msingi la kanisa la mitume la Karne ya Kwanza na pia kanuni zisizopingika za hilo kundi lililo pambana na kubadilikabadilika. Huenda liwashangaze wengine, lakini wanahistoria wa kanisa wameandika ya kwamba waumini katika Mungu aliye nafsi moja: - Wakristo wenye imani katika Mungu kama nafsi moja: walikuwa bado sehemu kubwa katika mwanzo wa Karne ya Tatu.³

Imani katika nafsi moja, Mungu mmoja na muumba haujawahi kufutika kabisa, ingawa ulishambuliwa kwa haraka na falsafa shindani ya kiyunani na shauku ya kisiasa ya warumi na baadaye nafasi yake kuchukuliwa na Mungu aliye nafsi tatu. Imelazimika kushikilia kwa nguvu katika kingo za ukristo kama sauti ndogo isiyo zimwa, inayo sihi dhamiri ya wote watakaosikiliza.

Kutoelewa kwingi kunakoziua fikra razini kuhusu uungu huenda umetokana na sababu moja kuu. Hatujashikilia mabadiliko katika maana ya maneno yanayo sababishwa na wakati, lugha inapokuwa ikipandwa kutoka utamaduni moja hadi mwingine. Mfano wa kwanza wa hili wazo ni istilahi / neno "Mwana wa Mungu" ambalo leo hutafsirika pasipo kufikiria kama "Mungu aliye mwana", maana ambayo haiwezi shushikiwa katika maandishi ya kikristo ya mwanzoni. "Mwana wa Mungu" ndilo jina "Wadhifa" linalo tambua mhusika mkuu katika tamthilia ya kikristo, Yesu aliye masia. "Mwana wa Mungu" katika Biblia ni jina linalopewa wawakilishi wa Mungu, na hasa mfalme wake mteule. Kupotosha kwa maana ya jina hili kunaweza kuathiri vibaya jinsi tunavyoelewa imani/itikadi ya kwanza. Ukristo wa kweli ni lazima huundwa na dhana na fikra zilizozingira mazingira ya mitume wa karne ya kwanza, tunayoona sasa kutoka umbali wa miaka 1900. Tunatengwa na dunia ya fikra za mitume waandishi wa Biblia wakati unavyopita. Taswira tofauti kabisa ya mafundisho yao inajitokeza tukiangalia maandiko yetu matakatifu katika mtazamo wa lugha/isimu, utamaduni na dini wa waumini wa kihistoria ya Karne ya Kwanza.

Huenda ushawishike kama sisi kwamba kinaya cha mwisho cha ukristo, msingi wa karne hii, ambao unadai kwa dhati sana kwamba maandiko matakatifu hayana kosa, ni kwamba haujawahi kuamini usemi wa Yesu kwa ufupi kuhusu njia ya wokovu: "Huu ndio uzima wa milele kwamba wakujue wewe. . *Mungu wa kweli wa pekee*, ni Yesu kristo uliyemtuma" (Yohana 17:13). Je huenda kizazi chetu cha wakristo kimekosa kujali onyo lililotolewa na Yesu akisema, "Ibada yao kwangu ni bure, wakifundisha maono ya binadamu kama kanuni / imani"? (Mathayo 15:9) Je, huenda tulianguka chini ya mafundisho ya viongozi wa kidini, hasa wale wa dunia ambao hawakuwa na uyahudi kwenye dhana ya Mungu katika nafsi tatu? "Mwana wa Karne ya Pili hadi ya tano,

² "Terms of Communion," *Works*, 1:352, cited by John Wilson in *Unitarian Principles Confirmed by Trinitarian Testimonies* (Boston: American Unitarian Association, 1848), 156.

³ *Encyclopedia Britannica*, 11th ed, Vol. 23, 963.

ambao misingi yao ya falsafa ya kigiriki iliwaeleza kuchafua dhana na mafundisho ya dini ya kihebrania vilivyo kuwa msingi wa kanisa la mitume la kikristo?

Kufuatia hatua za wale ambao wametofautiana na mafundisho ya dini ya Mungu wa nafsi tatu, ni nia yetu kuonyesha kwamba hakuna ithibati kuu kuhusu itikadi ya utatu mtakatifu wa Mungu inayopatikana katika Agano la Kale wala katika Agano Jipya kama inavyoaminiwa na wengi. Tunaamini kwamba msomaji anaweza kuthibitisha hoja huu akichunguza maandiko matakatifu unachotangaza utatu mtakatifu wa Mungu. Hakuna mstari halisi wa Bibilia unaodai ya kwamba huyu Mungu mmoja ni nafsi tatu, Roho tatu, Uungu utatu, mawazo yasiyo kikomo, ama utatu wowote ule. Hakuna mstari wala neno la Bibilia linaloweza kuonyeshwa kuwa na maana “Mungu katika nafsi tatu.” Dai lolote kwamba kuna watatu wanao ungana kuunda Uungu unatokana na tafsiri wa semi/vifungu dhahiri. Dhana katika Mungu kama nafsi tatu unategemea urazini wa hali ya juu ambao umetezwa na ambao hauungwi mkono kikamilifu katika maandiko ya kikristo ya kale zaidi. Hisia zetu ni kwamba wengi wanaoamini katika nafsi tatu wanachukua Agano Jipya kama kwamba lingekuwa “maandiko yanayoelekeza kuwa Mungu ni nafsi tatu.” Hawakushikilia hoja iliyo msingi kwamba hakuna mwandishi wa Agano Jipya anayeweza kuonyeshwa kumaanisha “utatu mtakatifu wa Mungu”, wakati wowote anaposema “Mungu”. Kisha wanapekua maandishi kutafuta ithibati kwamba mitume uanatoa habari kuhusu kuumbwa baadaye kwa kanuni / itikadi ya utatu mtakatifu wa Mungu. Hawafi moyo ingawa hakuna mmoja wao anayefikia kuvumbua dhana ya utatu mtakatifu wa Mungu.

Kuna wakati fulani ambapo viongozi wa kidini walihitaji mtu akubali kwamba dunia ipo katikati ya mbingu na kwamba haikuwa duara kama ukweli wa kibibilia. Aliyeamini vingine alionekana kupotoka ingawa Copernicus alikuwa amekwisha fanya uvumbuzi wake wakimapenzi. Huenda hali ilivyo hivi leo kuhusu itikadi ya utatu mtakatifu wa Mungu ije kufanana na tukio hili la kihistoria.

Iwapo tumaini ya kwamba Mungu hujidhihirisha kupitia maneno ya bibilia, ni lazima iwe juu ya kila mtu anayedai kuwa mfuasi wa Yesu kuchunguza ushahidi katika maandiko matakatifu ili kuweza kuamua, Mungu wa Bibilia ni nani. Ni jukumu la kibinafsi la mkristo anayetafuta ukweli kupekua na kuchagua vifungu fulani kwa uangalifu kama walivyofanya watu waitwao kwa kiingereza *Bereans* kwa moyo mkubwa. Walisifika kwa mawazo yao yaliyohusisha na yaliyokuwa na ukuu nadra (Matendo 17:11). Walithubutu kuangalia “kama haya mambo yalikuwa hivyo”. Matokeo ni kwamba walikuja kuwa waumini wa kweli.

Wengi wetu huenda tukafikiri kwamba hizi kanuni/itikadi za utatu mtakatifu wa Mungu ni siri unaofumba, usioweza kueleweka, ambayo ungestahili kuachiwa mijadala ya wanaelimu wakuu wa dini. Lakini itakuwa ni salama kuwaachia swala muhimu kama hili, *Thomas Jefferson* (Rais wa tatu wa Marekani:- 1800 – 1809, aliyekuwa mdadisi mwangalifu/mwervevu na aliyekuwa mwanzilishi wa Marekani kujitangaza kuwa huru). Alisema kuwa utatu mtakatifu wa Mungu ni pendekezo lisilo na busara/fahamu kwa mafundisho ya kiashiki kuwa watatu ni mmoja na mmoja ni watatu *na hali mmoja si watatu na watatu si mmoja*”. Anaendelea kusema, “sijawahi kuwa na busara/ hisia za kutosha kufahamu utatu mtakatifu wa mungu na ilionekana kwangu kwamba fahamu lazima itangulie kukiri”⁴.

Hata hivyo si jambo lisilo la kawaida kwa viongozi wa kidini kusisitiza kwamba ni lazima uamini katika utatu mtakatifu wa Mungu ili uwe mkristo. Ama sivyo utangazwe kuwa mfuasi wa dhehebu lililopotoka. Kwa mfano kukubalika kuwa wanachama wa

⁴ C.B. Sanford, *The Religious Life of Thomas Jefferson* (University Press of Virginia, 1987), 88

baraza la makanisa za dunia wanahitajika kukiri itikadi /kanuni ya utatu mtakatifu wa mungu ili wawe wakristo.

Kufafanua usemi wa *Thomas Jefferson*, tunauliza swali hili: “Je itawezekanaje mtu kutarajiwa kukubaliana na jambo ambalo haliwezi kuelezeka wala kueleweka?. Je ni adili kutaka jamii ya kikristo ikubali itikadi/kanuni hii “kwa imani”:- kanunni ambayo haitajwi kwa jina, na kama wanavyokubali wengine wenye imani katika nafsi tatu za Mungu, haijawahi kujadiliwa katika kurasa za Agano Jipya? Tusingeweza kutarajia useme uliyowazi na sahihi katika maandiko kuhusu pendekezo hili geni la kwamba Mungu ni watatu katika mmoja?

Iwapo tuna sababu kamili za kushuku kile tunachokiita ukristo leo huenda kitofautiane na mafundisho ya mwanzilishi wa Yesu, aliye Masia. Inaonekana kwamba hii imani kama tunayojua ilichuku itikadi ya Mungu ambayo Yesu hangeweza kuitambua.

Historia ya kanisa inaonyesha ya kwamba, hata dhana ya nafsi mbili zilizo sawa katika Uungu Baba na Mwana haikukubalika rasmi katika jamii ya kikristo hadi miaka mia tatu baada ya huduma ya Yesu – katika baraza la ‘Nicea’ mnamo mwaka 325 - baada ya kristo, na hii ilitokea chini ya hali iliyochanganyika na msukumo wa sima. Lililokuwa kweli katika karne ya nne na ya tano lingelazimika kuwa kweli katika karne ya kwanza. Kwanini ilichukua muda mrefu hivi kwa kanisa kutangaza rasmi Mungu aliye nafsi mbili ya baadaye wa nafsi tatu – na kufanya hivyo chini ya msukumo mwingi wa kisima? Baada ya matokeo ya Nicea, maelfu ya wakristo waliuwawa na wakristo wengine kwa sababu waliamini kwa dhati kwamba Mungu alikuwa nafsi moja.

Mafundisho ya Mungu katika nafsi tatu ni moja wa mafumbo makuu ya utata ya wakati wetu. Ingawa haikubaliani na urazini unaojulikana wala maelezo ya busara, hili halijapunguza mapenzi ya waumini wa Mungu katika nafsi tatu kupigania kwa hali yoyote ile hii dhana ya kidini isiyoeleweka. Tunashangazwa panapokuwa na ubishi dhidi ya utatu wa Mungu. Hili linaonyesha ya kwamba hakuna uhakika katika jambo ambalo hudaiwa kuwa msimamo usiyoshukiwa na wahubiri karibu wote wakikristo.

Kuwatangaza wote wanaopinga na wasioamini, kama ilivyo kawaida, haisaidii. Kukubaliwa kwa dhana ya kidini na idadi kubwa haithibitishi wala kudhihirisha ukweli wake. Je dunia ni tembarare (si duara)? Je dunia ndio katikati ya jua na sayari zingine (mbingu)? Ukristo wote ulihitajika kuamini hivi wakati fulani kama msimamo wa imani na adhabu ya kutoamini ilikuwa kali. Hata hivyo lilizidi kuwa fundisho lisilo kweli.

Swali zaidi linahitaji kuulizwa: je kanisa la mitume lilikuwa na wasomi wa dini waliokuwa werevu na wenye mawazo ya hali ya juu? Isipokuwa mtume Paulo mwongozi wa kanisa la awali uliwakilisha sehemu kubwa ya jamii – wafanyikazi wa kawaida, wanabiashara na watumishi wa serikali. Je hawangeweza kubumbuzwa kabisa kama tulivyo na dhana ya kwamba Mungu alikuwa nafsi mbili ama tatu na hali akiwa bado mtu/kitu kimoja? Uvumbuzi kama ungehitaji kuelezwa kwa uangalifu na kwa kurejelewa kwa watu ambao walikuwa wamekolea/shikilia sana tangu kuzaliwa imani ya kuwa Mungu alikuwa nafsi moja pekee. Haiwezi kupingika kuwa dhana ya Mungu aliye mmoja na muumbaji wa pekee ndio fundisho teule zaidi la urithi wa kitaifa wa Israeli. Kiini cha imani yao katika Mungu mmoja kingeweza kufutiliwa mbali. Kusema kweli imani katika Mungu aliye nafsi tatu ingekuwa dhana ya kimapinduzi na yenye mshindo mkubwa na ambayo ingelitikisa kanisa la karne ya kwanza. Hata hivyo, hata kama mapinduzi haya yaliwahi kutokea Agano Jipya halidokezi kamwe.

Huenda watu wengi wasijue pasipo kunuia kwamba huu ubishi / uzushi kuhusu utatu mtakatifu wa Mungu ambao haujawahi kusuluhishwa umevuma kwa muda wa karibu miaka elfu mbili. Maelfu wameteswa na kuchinjwa wakiwa sehemu ya vikundi vilivyopinga. Hata hivyo hivi leo idadi inayozidi kuongezeka ya wasomi wa dini,

wakatoliki na waprotestanti wanaothamini sana maandiko matakatifu na ambao wanaweza kupoteza mengi iwapo wataacha njia kuu inayofuatwa na wakristo wengi wametaka ielezwe kama hii imani iliyomsingi sana-utatu mtakatifu wa Mungu – inaweza kupatikana katika Bibilia.

Kwa kufanya hivi wamehatarisha kupewa majina kama “wasioshikilia upande wowote” (wasio na msimamo kamili) wenye mafundisho ya uzushi wafuatao madhehebu yaliopotoka na kutengwa kwa lazima na madhehebu yaliokwisha “kustawi”.

Kuhusu hoja ya kueleza Mungu ni nani, mapokeo ya elimu ya dini yamegawa vikundi vitatu, imani imeelezwa katika Mungu aliye nafsi tatu (Baba, Mwana na Roho mtakatifu), Mungu aliye nafsi mbili (Baba na Mwana) na Mungu aliye nafsi moja, aliye Baba, ambaye hakuumbwa na ni wapekee katika mbingu zote (Mungu aliye nafsi moja).⁵ Kanuni/itakadi yoyote ambayo imezusha uhasama wa namna hii kati ya wote wanaokiri kuwa waumini ndani ya kristo inahitaji kuangaliwa kwa makini.

Katika kuchunguza utatu mtakatifu wa Mungu tumetumia Bibilia na historia iliyoandikwa. Hatujihusishi na uzushi unaojijusisha na swala linalo fuatilia kujua kama Bibilia ni neno la Mungu lililodhihinishwa na tunapuuza shtaka / msimamo ya kwamba Bibilia imezeeka na haina mchango wowote kwa jamii ya leo. Jambo tunalojali sana ni swali hili: je maneno yaliozungumzwa na Yesu na mitume yalimaanisha nini kwa wale wakristo waliokuwa wa kanisa la karne ya kwanza kama dini ya kikristo imestawika kwenye maandishi ya Bibilia, basi imani ya ukristo halisi inahitaji kutokana na Bibilia.

Kwa kweli hatupingi uhalisi wa imani katika nafsi tatu za Mungu hata hivyo tunasisitiza ya kwamba uhalisi haufanyi imani kuwa kweli. Hatudharau nguvu (uwezo) usio wa kawaida wa mapokeo katika kujenga imani ya kidini na uwezo wa waalimu wa dini ambao ni kama hauna mipaka, kuamini ya kwamba kile wanachofundisha kina uwezo/ mamlaka wa maandiko matakatifu kama ithibati.

Lengo la kitabu hiki nikusaidia kuvunja mipaka ambayo imejengwa na wakati, na mapokeo kati yetu na kanisa la karne ya kwanza lililoanzilishwa na Yesu. Tunaelekezwa kuamini ya kuwa dhana mpya ya Mungu ilijitokeza chini ya athari ya falsafa ya kiyunani na ghubika imani ya mwanzo. Tunatambua sana wasomi wengi ambao wamesaidia kufanya dhahiri maana ya maneno ya Bibilia katika mazingira yake ya asili.

Tumefaidika zaidi na uchunguzi wao katika swala hili muhimu na tumetiwa moyo wakati wote na wale wafasiri wanao huzuia kutuambia kile kinachosemwa na kifungu/maandiko wala si kile kingestahili kusemwa. Tumependezwa na njia Alexander Reeze anayoitumia, ambayo ni: hali akitafuta ukweli kuhusu jambo lililo tofauti ili alinukulu “wafasiri wakuu... ikisadikika ya kuwa msomaji mwenye elimu wastani ataona kwamba tafsiri halisi ikiungwa mkono na wasomi wakiwango cha juu ni bora kuliko moja iliyoduni/zushi ikiungwa mkono na fundisho la kanuni pamoja na mahitaji ya mfumo.”⁶

Tumeazima kutoka hazina ya mawazo ya waandishi wengi waliopo na wa kale pasipo kutua na kutambua kazi hizi katika hali zote. Kazi zao zinapatikana katika orodha za kazi tulizonakili mwishoni mwa kitabu hiki. Mahali kwingine tumeweka nukulu ndefu kutoka kwenye kazi za wataalamu wajulikanao katika uwanja wa utafiti wa kibibilia tulitaka nguvu kamili ya mawazo yao kujumuishwa katika mjadala.

Kwanza kabisa tungependa kuelezea shaka yetu kuhusu madai ya kawaida ya waumini wa Mungu katika nafsi tatu na katika nafsi mbili ya kwamba iwapo Yesu si Mungu kamili, hakuna ondoleo la dhambi halisi ulioifanyika kwa dhambi huu, na ukweli basi ungekuwa umeandikwa wapi katika Bibilia? Je Mungu hana uhuru wa kuiokoa dunia

⁵ Wale wa United Pentecostal Church wana amini kwamba Mungu na Yesu ni mtu mmoja

⁶ *The Approaching Advent of Christ* (Grand Rapids international Publications, rep. 1975), xii.

kupitia yeyote amchaguaye? Uvumbuzi wa kwamba huu ubishi wa imani ya Mungu katika nafsi tatu ambao umekubalika haujengeki katika maandiko matakatifu, unakanganya tu kama hoja ya kwamba neno “Mungu” katika Agano Jipya halielezei Mungu aliye nafsi tatu. Agano la Kale linamaanisha Baba anaposemwa kama Mungu karibu katika mistari yote, tunawaomba waumini wa Mungu katika nafsi tatu wapime tofauti kubwa uliopo kati ya Bibilia na msimamo wao.

Ni muhimu tuwaambie lile ambalo hatusemi katika kitabu hiki. Hatuamini ya kwamba Yesu alikuwa “tu mtu mzuri”, wala mmoja wa manabii wengi. Imani yetu iko ndani yake kama mtume mteule, wa pekee na asiye na dhambi, Mungu kwa ukombozi wa watu kila mahali. Hata hivyo, ikisemwa kwa kiingereza, kwamba yeye ni Mungu, kuna tafsiri isiyo maandiko matakatifu ya kikrisisto. Inatosha, na ni ukamilifu wa kibibilia kuamini ya kwamba yeye ni masia, mwana wa Mungu. Hatutishwi na ubishi unaosikika sana ya kwamba Yesu ni lazima awe mwendawazimu, mbaya (mtu ama) Mungu. “Tukilazimika kuchagua kati ya kumkubali yeye kama mwendawazimu, mdanganyifu ama Mungu mwenyewe, inatupotosha kutoka ukweli kuhusu kumtambua yeye katika uhalisi wake. Kuna chaguo jingine lile ambalo linatosheleza maelezo ya maandiko matakatifu kwa njia kikamilifu/kwa njia sahihi.

Kuhusu ufundi/(istilahi) wa uandishi tungependa kutangaza uamuzi wetu tulio ufikiria kwa kuongea kuhusu Mungu na Yesu kama nafsi (watu) pasipo kutumia herufi kubwa “N”. Tunafahamu ya kwamba waumini wa Mungu katika nafsi tatu waliofundishwa kikamilifu hutangaza imani yao katika “nafsi” tatu/watu, na kwamba kutumia “nafsi” hawamaanishi kile tunachoelewa kwa kawaida kwa neno hilo. Hata hivyo inaonekana wazi kwamba aliye Baba na Yesu wanawasilishwa kama nafsi / watu *nadi ya Bibilia*. Yaani nafsi tofauti katika kueleweka kwa leo tunapinga mfumo usioeleweka kwa kujaribu kuieleza bibilia kwa kutumia dhana isiyo ya kibibilia – “nafsi”. Waumini wa Mungu katika nafsi tatu walio na busara wameshindwa kufafanua wanachomaanisha na “nafsi” (mtu) katika Uungu. Dhana zisizo dhahiri za kupambanua/bainisha asili hazisaidii kupunguza mashaka yaliopo. Augustina, aliyekuwa Baba wa kanisa linalojulikana la kilatino aliomba msamaha kwa kutumia neno nafsi/mtu alipokuwa akizungumzia wahusika wa utatu mtakatifu wa Mungu. Kama alivyokubali ilikuwa nafuu zaidi mtu kuliko kunyamaza kabisa.⁷ Waandishi wa bibilia hata hivyo hawakuhitaji jina lolote mashuhuri kufafanua uhusiano wa Mungu na Yesu, mmoja alikuwa baba na mwingine mwanawe.

Kwa wale ambao wana jaribu kumfafanua Mungu kama “nani” watatu hapapatikani ushahidi wakibibilia wowote. Haiitaji mafira mengi kudhihirisha ya kwamba Mungu wa Israeli katika maandiko matakatifu hajawahi kuelezwa kama “nini” ama katika njia isiyo ya kinafsi/utu. Vijina katika umoja vina tuarifu huyu Mungu mmoja ni “nani” bila shaka. Kumfanya “nani” watatu ni kupinga dhahiri ushuhuda wa Bibilia ambao haujabadilika. Mtu yeyote anayekiri dhana ya imani katika nafsi tatu za Mungu kama watatu na mmoja, hawezi kueleweka. Tungependa kupendekeza ya kwamba kukiri huku kunaonyesha tu uhafifu wa dhana yote ya imani katika utatu mtakatifu wa Mungu.

Kumalizia, hatukatai kwamba yapo mafumbo/siri katika dini hatukatai kukubali kanuni/itikadi yoyote ambayo hatuwezi kuelezea kikamilifu, lakini fumbo/siri na kinyume /kukana mambo mawili tofauti kuna mengi tusioelewa kuhusu kurudi kwa Yesu lakini wakati kristo alipotangaza kwamba hakujua wakati wa kurudi kwake tena duniani, ni wazi kwamba itakuwa kukosea kusema kwamba alikuwa na fahamu ya mambo yote. Tunashusha hadhi ya lugha tunapokubaliana na *Charles Wesley* asemapo, “ni fumbo tupu; aishiye milele yuafa” Kuishiwa kimawazo hutokea maneno yanapokosa urazini.

⁷ Augustine, *On The Trinity*, Book V, ch. 9

Lalamiko letu kuhusu kanuni/itikadi wa utatu mtakatifu wa Mungu ni kupima msimamo na imani ya mtu pasipo maana kamili, pamoja na hoja kuu zinazopinga wazo hili ni kwamba haliwezi kuelezwa pasipo kutupilia mbali lugha ya kibibilia. Kuna pingamizi kuu moja zaidi: kwa wengi inaeleweka kwamba ni “Mungu” watatu waliosawa, maana hii ndiyo njia pekee wanavyoweza kufikiria nafsi tatu ambazo zote ni Mungu.

Tunaanza kwa kuangalia swali kuu kabisa na kujibiwa na mkristo yeyote, kama anadai kuamini kwamba Bibilia ndilo neno lenye mamlaka/uwezo la aliye mkuu zaidi: Je mwanzilishi wa ukristo alimaanisha nini, akiongea na aliye baba na kusema, “huu ni uzima wa milele kwamba wakujue wewe, Mungu wa kweli wa pekee na Yesu kristo ulientuma?” (Yohana 17:3).

I. MUNGU WA YAHUDI

“Tunamjua tunayeabudu kwa maana wokovu unatoka kwa Wayahudi.” – Yesu kristo.

Undani wa hisia ya kiyahudi kuhusu ibada ya Mungu mmoja ilijengeka kwa muda wa karne nyingi za maarifa wakati wowote taifa lile liliposhikilia imani kuu katika Mungu mmoja, lilinawiri. Punde walipopotoka katika ibada ya miungu wengi waliandamwa na adhabu kali. Hatima ya haya ilikuwa kifungu kilicho rejelewa sana. “Sikia, wewe Israeli bwana aliye Mungu wetu ni bwana mmoja” (Kumbukumbu, 6:4, RSV pia Mariko 12:29)⁸, kifungu hiki kilieleza imani ya taifa la Israeli na kilitajwa na kila Muisraeli mcha Mungu katika maisha yake yote hata kufikia kifo. Kuweza kuhisi juhudi iliyoandama imani ya Kiyahudi katika Mungu mmoja tungehitaji kufikiria shughuli zetu wenyewe tunazozishikilia kwa dhati; kwa mfano, mapenzi ya uhuru ni nchi kadhalika nyumbani kwetu na jamii zetu.

Ungelikuwa umezaliwa kama Myahudi na wazazi walioshikilia itikadi za kidini katika Palestina ya karne ya kwanza, ungeshikilia imani isiyotikizika kwamba kuna Mungu mmoja pekee aliye Mungu muumba mkuu astahiliye ibada katika mbingu. Itikadi/imani hii ilikuwa imesukika katika mwili wa maisha ya Kiyahudi – haingeweza kutengeka. Mambo mengi yaliimarika katika dhihirisho la Mungu aliye nafsi moja lililo katika kurasa za maandishi tunayoyaita agano la kale: Kwa mfano siku kuu za kitaifa, misimu ya kilimo, tumaini la ukombozi wa kitaifa kutoka kwa Warumi watezi na hata ahadi ya kuwa taifa kuu baadaye/siku zilizofuata. Maandishi ya kidini ya Wayahudi yalifafanua uhusiano wa waumini na huyu Mungu mmoja na yalitoa agizo kuhusu jinsi ambavyo angeweza kuwatendea binadamu wenzake. Sehemu kubwa ya agano la kale ni historia ambayo mara ilikuwa ya kupendeza na mara ilikuwa na mikasa mibaya. Pamoja na hayo, haya maandiko ya wokovu yalitabiriwa kwa hili taifa la Israeli na dunia, siku ambayo kila mmoja duniani atamtambua na kumtumikia huyu Mungu mmoja wa Israeli (Zak 14:9).

Yesu alizaliwa katika jamii hii ya kipekee ya kidini na iliyoshikilia misingi ya ndani. Chanzo cha kujitolea kiimani kwa jamii hii kwa ibada ya Mungu mmoja ilikuwa kukita mizizi katika agano alilofanya Abrahamu kama Mungu wa waumini. Muhimili wa kati wa dini ya Kiyahudi kwamba Mungu ni bwana mmoja ulihimizwa na kufundishwa kwa watu na Musa. Hatimaye Waisraeli fulani wapotovu walikuwa wameigeukia imani katika miungu ya majirani wao ambao hawakumuamini Mungu wao. Wakilishi wa hii miungu mkuu ya kale walikubali ukahaba hekaluni, kuteketezwa kwa watoto kwa Mungu aliyeitwa Molek na kukatwakatwa vipande vya miili – hii ni mifano michache ya tambiko / ibada yao kuu.

Hadithi iliyoandikwa katika vitabu vitano vya kwanza vya maandishi ya kale ya Israeli inaelezea taifa lililokuwa limechaguliwa na Mungu kutengana na dunia ya ibada ya miungu wengi. Mungu aliingilia kati kwa njia ya nguvu, kwanza wakati wa kuitwa kwa Abrahamu na baadaye wakati wa kutoka misri, taifa nzima lilijulishwa kwa kiumbe ambaye hakudai tu kuwa muumba wa pekee wa vyote viliyomo bali pia kuwa Mungu wa kweli wa pekee aliwepo. Ujumbe wake kwa watu wake Israeli haukuwa wakukanganya. Kupitia kwa Musa alinena haya “Lakini bwana amewachukua nyinyi na akawatoa kutoka Misri muwe watu walio mali yake hivi leo. . . kwenu nyinyi ilidhihirishwa ilimweze kujua kwamba bwana, yeye ni Mungu; hapana mwingine kuliko yeye” (Kumbukumbu 4:20, 35).

⁸ Ya NASH (The Nash Papyrus), ithibati ya zama kabisa ya maandishi ya bibilia katika ki heraiia, labda kutoka karne ya pili, inamalizia *Shema* na maneno “Bwana mmoja ni yeye”

Ni wazi kwamba taifa la Israeli ambalo lilipewa haya maelezo makuu kuhusu uungu/mungu halikujua chochote kuhusu uwili ama utatu mtakatifu wa nafsi katika uungu. Hakuna hoja ambayo inaweza kuelezeka zaidi (ya hii), iwapo maandishi ya kitaifa yatatumiwa kama uongozo na iwapo lugha ipo na maana isiyobadilika.

Jambo moja lisilo na ubishi ni kwamba mataifa yaliozunguka Israeli hayakuwa na tashwishi kuhusu imani ya Israeli katika Mungu mmoja. Imani hii ndio ilikuwa moja ya sababu za kuteswa kwa kizazi cha wayahudi walioshikilia dini, waliokataa kukubali ibada ya chombo chochote isipokuwa Mungu mmoja. Wapiganaji wa imani na mashuja wapiganaji wakristo walionea hamu jukumu la kuwafukuza “makafiri” Waislamu walioabudu Mungu mmoja kutoka nchi takatifu. Hii juhudi yao iliwapoleka vivyo hivyo kuwachinja wayahudi ambao hawakujihami kutoka jamii moja hadi nyingine huko ulaya / Uropa. Karne tatu baadaye hakuna aliyenusurika mateso ya uhispania pasipo kukana imani yake ya kidini na kukubali ukatoliki wa kirumi ama kutorokea sehemu zingine za dunia ambako hakukuwa na uadui: - Wote waliteswa, wawe wayahudi waliomwamini Mungu mmoja, au wakristo na hata wa protestanti waliomwamini Mungu katika nafsi tatu. Huenda liwe jambo la kutisha / kushangaza wengi kwamba maelfu ya wakristo ambao pia walikuwa na imani katika Mungu wa Wayahudi aliye nafsi moja, waliweza kuepuka kuteswa na kanisa (Wakristo) jinsi hii kwa kutoroka tu!

Imani katika Mungu aliye nafsi moja (kiungo kimoja) ilipatia Israeli mtazamo wa dunia ambao uliitenganisha na falsafa, dini, tamaduni zingine za mataifa ya dunia. Israeli inashikilia msimamo huu (kuelewa huku) wa kipekee kuhusu Mungu hadi leo. Dhidi ya msimamo huu upanifu wa ukristo unashikilia imani/dhana ya Mungu wa nafsi tatu katika utatu mtakatifu (Baba, mwana na Roho mtakatifu), wachache hudai kuamini katika Mungu aliye nafsi mbili (Baba na “neni”)⁹, nafsi zote mbili ziliwepo tangu milele. Dini za mashariki ya mbali hukubali kuwepo kwa zaidi ya Mungu mmoja ama sivyo kuwepo kwa nafsi simamizi kati ya Mungu mkuu na alivyoumba:- Imani iliyoshikiliwa na sehemu kubwa ya ugiriki / uyunani iliyoathiri kanisa la awali la kikristo ya punde baada ya kifo cha mwanzilishi wake, Yesu, aliye Masia. Idadi kubwa ya watu leo hupata mizizi yao ya kidini katika dhana ya mashariki ya mbali ya miungu mingi:- itakadi / imani ya kwamba sisi sote ni miungu wanaongojea kujivumbua (wenyewe) na kwamba, katika hali isiyo eleweka kwamba sote ni Mungu. Si vigumu basi kuona kwamba fujo ya kidini haina budi kutokezea kila mmoja awapo ni mungu pasipo kupingwa, akiamua imani yake na mwenendo (tabia).

Ili kuhimiza / kusisitiza umoja wa Mungu kwa Israeli kitaifa, kiasi kwamba kusingekuwa na nafasi ya makosa wala kutoelewa, Mungu alirudia kupitia kwa Musa. “jua basi hivi leo na ulishikilie moyoni kwamba bwana ni Mungu mbinguni juu na katika dunia na chini yake; “hakuna mwingine” (Kumbukumbu 4:39) kwa kuangalia uwezo (nguvu) wa kifungu hiki, na vingi vinavyofanana nacho, tunaweza kuelewa / kuhurumia kikamilifu kujitolea kwa wayahudi kuwa Mungu aliye nafsi / fungu moja. Maandishi haya yanaonekana kuwa ithibiti dhidi ya kuweko kokote kule kwa tafsiri isiyo kamili. Wayahudi walielewa “moja” kumanisha “moja”, na hawakuwa na tashwishi kuhusu usemi “hakuna mwingine.” Msemaji wa Wayahudi aliye mstari wa mbele hivi leo, Pinchas Lipide, anasisitiza uthabiti walionao wayahudi wanapokinga/tetea kiini cha imani yao:

Ili kukinga umoja wa Mungu dhidi ya kujumuishwa (Kuongezwa, kushukishwa hadhi ama kuunganishwa na itakadi za dunia inayowazunguka watu wa Israeli walijichagulia kifungu fulani cha bibilia kuwa kama msimamo, ambacho hadi hivi

⁹The Worldwide Church of God, ikiongozwa na Herbert Amstrong iliamini mwenendo hili la ‘binitarian’. Mabadilisho kwa ‘trinitarianism’ lilifanyika mwaka wa 1995

leo kinapatikana katika kanuni za sinagogi na husisitizwa kama mstari wa kwanza wa mafundisho kwa mtoto wa shule wa miaka mitano. Hili ni lile ungambo ambalo Yesu alilitambua kama “amri kuu kwa zote.”¹⁰

Kama Lapide anavyotambua, Yesu alipokua akieleza msingi wa imani yake, alirejelea maneno yaliyozungumzwa na Musa kwa taifa la Israeli: “Sikia wewe Israeli: Bwana aliye Mungu wetu ni Bwana mmoja: umpende bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote (Kumbukumbu 6:4,5; Mariko 12:29;30). Kutokana na kuthibitisha kwa Yesu kwa maneno ya Musa yaliyoandikwa katika kitabu cha kumbukumbu la torati, tunalazimika kusema kwamba ni lazima alielewa na kuamini chochote Musa alichuamini hayo maneno. Kumaanisha kama ingekuwa vingine, ama kama mabadiliko makali yangukuwa yametokea kukanusha maandishi ya hakika ya Musa kuhusu “Mungu mmoja”, maandishi wa agano jipya hawajafaulu kutoa hoja iliyosawa kimsimamo kugeuza ama kusahihisha huu muhimili wakati (uti wa mgongo) wa imani ya kiyahudi.

Ithibati ingine ya kuthibiti sehemu kuu ya imani ya dini ya kiyahudi inapatikana katika mazungumzo ya Yesu na mwanamke msamaria. Alimwambia pasipo kusita “Mnaabudu msiyemjua; sisi (wayahudi) humwabudu tunayemjua, kwa maana wokovu watokana na wayahudi. Lakini utafika wakati, na ndio huu, ambapo wanaoabudu kikweli watamwabudu baba ndani ya roho na ukweli” (Yohana 4: 22: 23). Si mara moja tunapomwona Yesu akikashifu wananchi wenzake kwa kutoelewa kikamilifu idadi ya nafsi zilizo katika Uungu. Wala hatumuoni Paulo akitambua Mungu mwingine yeyote isipokuwa Mungu wa Israeli. Alitarajia watu wasio wayahudi kuchukuliwa / kuchipukizwa katika Israeli na wamwabudu huyu Mungu. “Je Mungu ni Mungu wa Wayahudi pekee? Si yeye ni Mungu wa watu wasio wa Wayahudi pia?” (Warumi 3:29, 11: 17). Yule Mungu anayejulikana kwa Paulo myahudi anaelezea Mungu amjuaye kikamilifu katika Wagalatia 3:20, katika maneno ya “Amplified translation of the New Testament”, inayosomeka: “Mungu ni nafsi moja (pekee)”

Mapema katika huduma yake Yesu anadhihirisha kwa nguvu dhihirisho la kiungu lililopewa Musa: “Msifikirie kwamba nilikuja kupiga marufuku sheria ama mitume; sikuja kupiga marufuku, bali kutimiza (Mathayo 5: 17). Hoja kuu ya kwanza katika umuhimu wa jumla ya sheria ya Israeli iliyotolewa katika torati kupitia kwa Musa ilitoa kanuni ya kitaifa:” Msiwe na miungu mingine isipokuwa mimi (Kutoka 20:1-3).

Kama kungekuwa na kiumbe kimoja cha kipekee kisicho na mfano wenye uwezo wote katika mbingu ambacho kingependa kujidhihinisha kwa viumbe vyake kwamba ndicho Mungu pekee na kwamba hakukuwa na kingine: Hili lingeweza kuelezwaje pasipo uwezekano wakufanyika kosa? Nini lingeweza kusemwa kwa kuhakikisha kwamba hakukuwa na uwezekano wowote wakutoelewana? Mmoja wetu angewezaje kueleza hali ya kipekee ya Mungu kama ungekuwa wajibu wetu kufanya ujumbe huu kueleweka kwa taifa lote? Je tusingeweza kusema, kama anavyo arifu Musa kuhusu Mungu akisema, (“Angalia sasa kwamba mimi, niliye yeye, (ni yeye) na hakuna Mungu mwingine pasipo mimi? (kumbukumbu 32:39). Kulingana na semi huu dhamiri Israeli haikubali yeyote isipokuwa Mungu wa nafsi moja wa Musa hadi leo. Pasipokujali tofauti zozote zile za kidini umoja wa Mungu ndio uzi wa pekee unao unganisha jamii ya kiyahudi.

Bibilia ya Kihebrania na Agano Jipya kuna vijina katika umoja na vitenzi zaidi ya elfu ishirini na moja vinavyomfafanua / muelezea huyu Mungu mmoja. Lugha haina njia iliyo wazi zaidi ya kushuhudia imani katika Mungu wa nafsi moja na ibada katika Mungu mmoja wa Israeli na Yesu.

¹⁰ *Jewish Monotheism and Christian Trinitarian Doctrine* (Philadelphia: Fortress Press, 1981), 27.

Ile nafsi iliyo dhahirishwa katika Torati ya Israeli ilikuwa ni Mungu wa kutofautishwa dhahiri na miungu ya wamisri ambao hawakumwabudu Mungu mmoja. Alikuwa ameokoa taifa lililokuwa utumwani kwa kitendo chake cha nguvu. Alikuwa ni Mungu. Mwenye uwezo mkuu na hali akiwa na nafsi na uwezo wakukaribiwa: - Mungu wakupendwa aliyesemekana: “Bwana alikuwa akiongea na Musa uso kwa uso jinsi mtu aongevyo na rafiki yake” (Kutoka 33:11) Ni mtu ambaye Daudi aliwasiliana naye: “Umesema, tafuta uso wako ewe bwana.” (Zaburi 27:8). Wakati wakuondoka Misri wayahudi walijua ya kwamba, kwa mara ya kwanza katika historia taifa nzima liliweza kukutana karibu sana na muumbaji Mungu kupitia kwa mwakilishi aliyekuwa amemsimamisha. Tukio hili ambalo halina kifani lilipandika katika moyo wa taifa milele. Baada ya miungu ya mataifa yaliyowazunguka ilipigwa marufuku, ni jambo la kuhuzunisha kwamba kuogopa uchawi na tamaa ya kuwa kama mataifa mengine, yilishawishi Israeli kujiingiza katika ibada ya miungu mingi ya wasiyomjua Mungu kwa kweli. Hili liliwasababishia baa la mateso makubwa. Punde baada ya kukimbia Misri dhidi ya hali ya kuogofya sana walijijengea ndama wa dhahabu ili waweze kumuabudu.

Taifa lilihitaji kukumbushwa wakati wote kuhusu kanuni yake ya kipekee: “Sikiza wewe Israeli: Yehova Mungu wetu ni mmoja Yehova wa pekee” (Kumbukumbu 6:4, New Jerusalem Bible). Israeli ilijulishwa kwa mara nyingine kuhusu kujitambua kama taifa kupitia kwa nabii Isaya: “Nyinyi ni mashahidi wangu . . . na muelewe kwamba mimi ndiye. Kabla yangu hakukua Mungu yeyote, na hakutakuwa na yeyote baada yangu”. (Isaya 43:10). Elimu / kanuni za dini zinazowaahidi wafuasi wake kwamba watakuwa Mungu, zinaonekana kutoelewa wadhifa huu wa pekee unao daiwa na mmoja anayeshikilia kuwa *hakukua Mungu kabla yake na hakutakuwa na mwingine baada yake*.

Kuendelea kusesitiza kwa Isaya kuhusu umoja wa Mungu ni jambo lililo wazi na linaloashiria. Ananukuu Mungu akisema, “mimi ndio mwanzo, ndio wa mwisho na *hamna Mungu isipokua mimi / kando yangu*” (Isaya 44:6). Swali linarudiwa: “Je kuna Mungu mwingine isipokuwa mimi, ama kuna muumba yeyote mwingine? Simjui yeyote (muumba) (mwingine)” (Isaya 44:8). Hili dai la kipekee lilikuwa sehemu kamili ya mafundisho ya kidini ya mahali ambapo Yesu alilelewa. Ilikuwa ni kanuni iliyoshikiliwa na kila kijana wa kiyahudi. Kurudia kutaja nabii Isaya, na hana agano la kale lote katika huduma yake ya uma kunaonyesha jinsi elimu yake ya dini ilivyoadhiriwa na maandiko matakatifu ya Kihibrania. Mungu aliyetumikiwa na Yesu alijitangaza kuwa nafsi moja, wala si mmoja katika watatu.

Hatuhitaji kushangazwa na juhudi waliohifadhi wayahudi hii dhana ya umoja na upekee wa muumbaji Mungu. Uthabiti wao ulihimizwa na Isaya anapoendelea kurudia moja ya hoja zilizo muhimu sana kidini. Huyu nabii anaongea tena kuhusu Mungu wa Israeli: “Mimi bwana ndimi muumba wa vitu vyote, nilitandaza mbingu pekee yangu (pasipo msaada) na kutandika dunia pekee yangu. (Ama nani alikuwa pamoja nami?)” (Isaya 44:24). Vifungu vingi vingeweza kuandikwa namna hii kwa hila kupiga marufuku milele katika mawazo ya wayahudi hii dhana ya kwamba *zaidi ya mtu mmoja* alihusika na uumbaji (wa dunia na viumbe).

Mkazo unajitokeza wazi zaidi ambapo mwandishi huyu anaandika ifuatavyo katika mistari saba tofauti kwenye kifungu cha arubaini na tano cha kitabu chake: “mimi ndiye bwana, hakuna mwingine; hamna Mungu pasipo mimi (Isaya 45:5). Maandiko haya yalibuniwa ili kuimarisha milele katika akili / mawazo ya Israeli dhana ya kwamba Mungu ni mmoja. Huyu Mungu mmoja anaendelea kusema kupitia kwa Isaya: “Ni mimi niliyeifanya dunia na nikamuumba mwanadamu juu yake.” (Isaya 45:12).

Inafundishwa mahali kwingi ya kwamba yule ambaye alistahili kuwa Yesu, mwana wa Mungu wa agano jipya, ndiye aliyehusika na kazi ya uumbaji. Je wazo kama

hili lingeumbika aje? Kwa kigezo cha mwamba tulioyasoma? Je maandishi ya Isaya hayangeweza kuzuia dhana kama hiyo kuingia katika mawazo ya kiyahudi?” Hakika Mungu yu nawe, na hakuna mwingine, yeyote hakuna Mungu mwingine.” (Isaya 45:14) Na anaendelea, “Bwana anasema, aliyeifanya dunia na kuitengeza, alisimamisha na hakuiumba kama mahali pasipo na dhamani, bali aliifanya ile iishiwe / ikaliwe), “Mimi ndiye bwana na hakuna mwingine”. (Isaya 45:18).

Vifungu viwili zaidi vinaipa Israeli changamoto ya kujitua kwa uaminifu: “Nani aliyetangaza hili kutoka zamani ya kale? Nani aliyelitangaza kutoka kitambo? Je si mimi niliye bwana? *Na hakuna Mungu mwingine pasipo mimi*. Mungu wa haki na mwokozi, hakuna mwingine isipokuwa mimi. Nigeukieni muokolewe, pembe zote za dunia: Kwa maana mimi ni *Mungu* na *hakuna mwingine* (Isaya 45: 21,22). Wengine wamechanganya matumizi ya neno “mwokozi” katika kifungu, na matumizi ya mara kwa mara ya neno hili kumaanisha Yesu, aliye Masia. Niwazi kwamba anaitwa mwokozi pia katika Agano Jipya (kama wanavyoitwa waamuzi katika kitabu cha waamuzi kadhalika Josephus (Yusufu) aliyeitwa Vispasian).¹¹ Tunaona tofauti inayoletwa katika Juda 25, ambapo Yesu na Mungu wanatajwa mwishoni wa kitabu: “Kwa Mungu aliyepekee mwokozi wetu, kwa Yesu Kristo bwana wetu, iwe sifa, utukufu, mamlaka na uwezo kabla wakati wowote na sasa na milele” Ni wazi kwamba wazo la kiyahudi la Mungu aliye nafsi moja halipotoshwi na huyu mwandishi wa agano jipya. Kwa hakika hakuna kifungu kinachoweza kueleweka zaidi kuliko hiki:- kwamba kuna nafsi mmoja ‘pekee’ katika uungu / umungu. Wote wawili, Mungu baba na Yesu kristo wanatajwa katika mstari mmoja (si mstari tofauti), lakini Yesu anatofautishwa na “Mungu aliye pekee”. Waandishi wengine wa Agano Jipya wanaandika vifungu visivyokanganya vilevile. Baba ya Yesu ndiye aliye pekee mwokozi. Wengine isipokuwa yeye wanaweza kuchukua wadhifa wa mwokozi kwa njia ya kusaidia ama kutumwa.

Basi Yesu alizaliwa katika huu utamaduni wa kiyahudi na imani yake ilikita mizizi katika Mungu mmoja. Karne kumi na tisa baadaye muisraeli, myahudi anayeshikilia mafundisho ya kidini ya jadi, Pinchas Lapide, mwanachama katika chuo kikuu la Ar Ilan, Israeli (tuliye mtaja mapema), anaonyesha ya kwamba wayahudi walikatazwa kutoka kwenye imani ya umoja wa Mungu: “Kutokana na neno la (*echad*) Kumanisha moja) tunajifunza, sio kwamba tu, hakuna mwingine isipokuwa bwana, bali pia ya kwamba bwana ni mmoja na hivyo basi bwana hawezi kuonekana kwamba ni kitu kilicho wekwa pamoja (nafsi) ambacho kinaweza kugawika kwa sifa na miliki mbalimbali.”¹² Si ajabu basi kulingana na takwimu za bibilia kwamba Israeli ilipogeuka kuabudu miungu mingine, ghasia zilizuka, taifa iligawika na unabii wa kutisha wa Isaya ulitimiwa. Utumwa wa taifa ndio ulikuwa adhabu ya kupotokea kwenye ibada ya miungu wengi. Ingewezekana basi kuwa kuchanganyikiwa na kukatika tunakoshuhudia kwa historia ya ukristo unaweza kuelezeka kuhusiana na kupotoka kwa imani ya awali kwamba Mungu alikuwa nafsi moja.

Dhana ya Mungu aliye nafsi moja haikushikiliwa na nabii Isaya peke yake. Hosea anatoa hotuba ya Mungu wa Israeli akisema: “Hata hivyo nimekuwa bwana Mungu wenu kutoka nchi ya Misri; na hamkua mmjue Mungu mwingine, isipokuwa mimi, kwa maana hakuna mwokozi isipokuwa mimi” (Hosea 13: 4) zaidi za hayo upekee wa mamlaka / hadhi ya Mungu mmoja haukuonyeshwa hizo siku za kale. Tunapata maono yaliyowazi kutoka kwa nabii Joel akizungumzia Israeli ya siku zijazo ikishapata ukuu iliyo ahidiwa, kwamba taifa hili litakuwa bado limefunganishwa na huyu Mungu mmoja hata milele: “hivyo utajua kwamba niko kati ya Israeli na kwamba mimi ni bwana Mungu wako

¹¹ Waamuzi 3: 9,15 ambapo neno “mkombozi” kwingine lilimaanisha “mwokozi”

¹² Jewish Monotheism and Christian Trinitarian Doctrine, 31

hakuna mwingine” (Joel 2:27). Joel anatujulisha kwamba Mungu wa wayahudi katika agano la kale angeweza kuwa lolote lile ama yeyote yule lakini alikuwa abaki Mungu wao wa siku zote daima.

Akili ya kiyahudi ilikuwa imeisha sadiki kwamba huyu Mungu mmoja aliye muumba, alikuwa pia baba wa hilo taifa. Ndivyo anavyosema nabii Malaki: “Kwani sisi sote hatuna *Baba mmoja*? Kwani si *Mungu mmoja* aliyetuumba sisi? (Malaki 2:10)¹³ Hakuna jambo ambalo lingekuwa wazi zaidi kuliko kusema kwamba yule Mungu mmoja wa ibada ya Mungu mmoja wa kiyahudi, ambapo uridhi wa Yesu ulijengeka, alikuwa ndiye baba. Huu upekee (wa Mungu) huelezewa mara nyingi kama Mungu na Baba katika agano jipya, Naam yeye ndiye “Mungu na Baba wa bwana wetu Yesu Kristo”,¹⁴ mwanawe. La muhimu sana ni kwamba hata Yesu akiwa “bwana” bado yuko chini ya mamlaka ya Mungu wake. Cheo cha ‘bwana’ cha kimasia basi hakimaanishi Yesu ni Mungu.

Elohim, Neno la Kiebrania

Wanaoamini utatu mtakatifu wa Mungu na wale wanaoamini uwili wa Mungu wakati mwingine hutumia kifungu cha Mwanzo 1:26, bila ithibati kutoka kwa wale ambao wameisoma lugha ya kihibrania, kama ushuhuda kwamba nafsi nyingi katika uungu zilihusika na uumbaji (dhidi ya ushahidi wa maelfu ya vijina katika umoja vinavyoisharia Mungu mmoja). Basi/ndipo Mungu akasema, “natumuumba binadamu kwa mfano wetu na kulingana na umbo letu.” hii ni hatari. Wasomi wa siku wa leo hawachukulii huu usemi, “Natu”, ama neno *Elohim* (Mungu) kumaanisha wingi wa Mungu ki nafsi kama muumba. Kuna uwezekano kuwa wingi wa kijina unabeba maana ya huyu Mungu mmoja na kikao cha baraza la malaika,¹⁵ ambao wenyewe walikuwa wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wakashuhudia kuumbwa kwa mbingu (Job 38: 7) ni mzaha kuchukulia kwamba kifungu hiki kinaunga mkono dhana ile ya kwamba Mungu alikuwa akiongea na Mungu mwana na roho mtakatifu anaponena Mungu na Roho yake mwenyewe? Kifungu hiki cha maandishi hakisemi chochote kuhusu mwana wa milele wa Mungu, aliye nafsi ya pili katika utatu ulio sawa. Zaidi ya hayo “Natu” (sisi) katika kifungu cha maandishi haiwi ishara ya nafsi mbili shirikishi zenye usawa katika umungu. Ikawa / iwapo Mungu ni nafsi moja matumizi yake “Natu” (sisi) inamaana kwamba anazungumza na nafsi nyingine wala hajizungumzii mwenyewe: - wala / ila si Mungu.

Kamusi ya Bibilia ya Kihibrania inaweza kuhakikisha kwamba neno *Elohim* (Mungu) si neno la fungu la wingi, kumaanisha kwamba nafsi mbili ama zaidi zinashirikisha / jumuishia Umungu (Ama kama walivyofikiria wengine “jamii ya Mungu”). Upekee wa lugha yoyote lazima uzingatiwe kama tutaweza kupata udhahiri kamili wa maana. Tutagundua kwamba hili jambo ni muhimu na haliepukiki iwapo tutatafuta kuelewa kikweli.

Hoja zinazotambulika za lugha ya Kihibrania haziungi mkono dhana ya nafsi nyingi kwa Mungu. Tunaona inavyosema *Gesenius Hebrew Grammar*, maandishi wastani, kuhusu neno Elohim:

Wingi wa utukufu / enzi inajumuisha sifa kadha zinazohusiana na hii dhana kando na kuleta maana ya kiwango cha pili ya kutia mkazo wazo la awali.

¹³ Angalia pia 1 Mambo ya Nyakati 29:10, ambapo Mungu wa Israeli pia ni “baba yetu”

¹⁴ Warumi 15:6; 2 Wakorintho 1:3; 13:31 1 Petro 1:3

¹⁵ 1 Wafalme 22:19-23; Ayubu 15:8; Yereimia 23:18

Hii lugha imekataa kabisa dhana ya wingi wa kuhesabika katika Elohim (wakati wote inapoashiria Mungu mmoja) inathibitishwa hasa na kuunganishwa kwake na sifa iliyo katika hali ya umoja: - kubadilika ni adimu.¹⁶

Lazima tuheshimu hili wazo la kwamba ingawa wayahudi walikuwa na uzoefu wa lugha yao wenyewe, hili halikuwaelekeza kujumuisha / kukata kauli ya kwamba kifungu cha uumbaji katika kitabu cha Mwanzo kinadokezea hata kidogo wingi wa nafsi katika Ungu. Iwapo tutapata wayahudi walikosa kitu fulani kutoka kwenye Biblia yao, tunahitaji kuzingatia kwamba katika mistari ifuatayo (Mstari 27:31) hiki kijina kinachotumika kwa umoja kinaambatana wakati wote na neno Mungu. “Katika umbo Lake [si umbo lao] katika umbo la Mungu Aliwaumba [si Waliwaumba]” (Ms 27). Kungekuwa na jaribio kubwa la mtu kukataa kutokana na mistari huu ya kwamba wingi wa nafsi ilidokezwa katika sehemu ambazo vijina vinavyoeleza Mungu (Lake) viko katika umoja. Tazama tena: “Angalia nimekupatia [si Tume] kila mmea uzao mbegu kama chakula; na Mungu akaona vyote alivyounda [si wali. . .], Na ilikuwa vyema sana” (Ms 29-31)¹⁷

Uchunguzi wa neno Mungu katika kihebrania (Elohim) hauungi mkono kwa dhana inayorejelewa kwamba “Mungu Katika Mwanzo 1:1 anajumuisha wote wawili – Mungu Baba pamoja na mtoto wake na Roho. Hatuwezi kukosa kuona ugumu uliowazi wa tafsiri kama hii. Iwapo *Elohim* inamaanisha kwamba neno linalofanana na linamaanisha Musa.” Na Bwana akamwambia Musa, “tazama, nitakufanya kama Mungu kwa Farao, na Haruni ndugu yako atakua nabii yake” (Kutoka 7:1)? Kwa kweli hakuna mtu angeweza kudai wingi wa Musa aliye mtu mmoja. Mungu mmoja aitwaye Dagon, wa watu wasiomjua Mungu wa kweli pia anaitwa Elohim (Mungu): “Sanduku la sheria za Mungu (Elohim) wa Israeli haliwezi kubaki nasi, manake mkono wake umetuadhibu sisi na Dagon Mungu wetu (Elohim)” (I Sam 5:7). Vivyo hivyo neno (Elohim) linatumika kumuelezea mungu wa Amori: “je hamtamiliki kile ambacho Chemosh mungu wenu (Elohim) anawapatia mumiliki ? (Wamuzi 11:24), pamoja na hayo Masia mwenyewe anazungumziwa kama Elohim. (Zab 456 Waheb 1:8). Hakuna mtu anaweza kupingana kwamba Masia ni mtu zaidi ya mmoja.

Kutokana na dhibitiso hili tunaweza kuafikiana ya kuwa wayahudi ambao lugha yao imetumiwa kuliandika agano la kale, hawakutumia neno Elohim linalotumika kwa Mungu wa kweli, kumaanisha nafsi zaidi ya mmoja. Wale wanaotafsiri utatu mtakatifu wa Mungu au uwili wa Mungu katika Mwanzo 1:26 ama katika neno Elohim wanajihusisha katika tafsiri ya kulazimisha. Elohim iko katika hali ya wingi lakini iko na

¹⁶*Gesenius' Hebrew Grammar* toleo. E. Kautzsch (oxford: Clarendon Press, 1910), 398. 399. Angalia pia haya maandishi wastani, *Hebrew and Lexicon of the Old Testament* kilichoandikwa na: Brown, Driver and Briggs. (Oxford: claren Don Press, 1968) 43, 44. Gesenius anaorodhesha mifano mingi ya maneno ya kihibrania yaliyo katika hali ya wingi (vipengele vya mwisho wa maneno) ambavyo hayana *maana ya wingi*. Kwa mfano *Panim = Uso. Elohim ingeuzwa na sifa iliyo katika hali ya uchache katika Zaburi 7 – 10.*

¹⁷Mushkili wa kisarufi isiyotokea mara kwa mara hauwezi kufuta ushahidi wa maelfu ya matokeo ambapo jina la Mungu na vyeo vinachukuwa vitenzi katika hali ya uchache. Panapopatikana kitenzi katika hali ya wingi kikiwa na *Elohim* katika 2 Sam 7: 23, kifungu kilicho sambamba 1 Hesabu 17:21 kinatumia kitenzi cha hali ya umoja badala ya hicho cha hali ya wingi, hili linaonyesha ya kwamba matumizi ya kipekee ya hali ya wingi hayakuwa na maana kubwa. Elohim katika Mwanzo 31:24 inaweza kuchukuliwa kumaanisha malaika (kama alivyofikiria Calvin na wenzake, kwa mfano pia katika Zaburi 8:5 na nukulu / nukuu yake katika Hb 2:7. Yahweh na adonai aliye Bwana pasipo mabadiliko hutumia kitenzi katika hali ya umoja. Umoja wa *El* na *Eloah* (Mungu) unathibitisha kwamba Mungu ni nafsi moja. Ni ajabu kwamba watu wengi wanaendelea kutoa ili mistari minne ya “sisi” / tu kama dokezo kwamba Mungu ni fungu la utatu, ingawa kuna ithibati ya maelfu ya vifungu vilivyoandikwa ambako Mungu anaelezwa kwa vijina na vitenzi katika hali ya umoja!

maana ya umoja. Inapozungumzia Mungu mmoja, inafuatiliwa / ambatana na kitenzi katika hali ya umoja. Kabla ya karne ya kumi na mbili hakuna aliyechukulia kwamba hali ya wingi katika umungu / uungu ilidokezwa kwa jina la (cheo cha) Mungu katika kihebrania. Wengi wanaoamini katika nafsi tatu za Mungu waliacha kitambo kubishania utatu mtakatifu wa Mungu katika Mwanzo 1:1 ama Mwanzo 1:26.

Ni urazini kuwauliza wanaoamini nafsi tatu za Mungu ambao husema kwamba Elohim ni hali ya wingi kwa ukweli:” Kwa nini hawaanzi neno Mungu na Mi-Miungu ili kuonyesha kwamba liko katika hali ya wingi kama kijina kilichokatika hali ya wingi “Tu”/sisi katika Mwanzo 1:26 inaelezea uungu katika hali ya wingi, basi huu uungu/umungu ungekuwa kwa kawaida ukiiitwa “wale” ama “hao” (watendaji / watendewa. Wanaoamini katika nafsi tatu wapendeleo wazo hili ili kuonyesha kwamba fikra yao kuhusu umungu / uungu haiwahi na urazini sheria na za lugha. Kama Mungu angekuwa katika hali ya wingi basi kwa nini mstari unaofungua kitabu cha Mwanzo 1 usitafsiriwe: “Hapo mwanzo miungu . . . “? Hii dhana kubwa ya wanaoamini nafsi tatu za Mungu kuhusu ibada ya miungu mingi ingefanywa dhahiri.

***Echad* – neno la kihebrania lenye maana ya moja.**

Si kweli kusema kwamba neno la kihebrania *Echad* (moja) katika Kumbukumbu 6:4 linaashiria umoja ulioshikamana. Utetezi wa hivi punde wa utatu mtakatifu wa Mungu “unabisha ya kwamba ikiwa “moja” itabadili neno linalojumuisha kama “fungu” *Echad*; ubishi huu hauna ukweli. Kiini cha hali ya wingi kinachimbuka kutoka jina jumuishi (Kundi... sio kutoka kwa neno “moja”. *Echad* katika kihibrania ni neno la kuhesabu “moja”. “Abrahamu alikuwa mmoja (*Echad*)” (Ezekiel 33:24; “mtu/mwanaume mmoja pekee, NIV)”. Isaya 51:2 pia inamwelezea Abrahamu kama mmoja (*Echad*); “pekee yake,” KJV; “Yeye pekee / wa pekee, “ NJB), ambapo hakuna uwezekano wa kutoelewana kuhusu maana ya neno hili rahisi. *Echad* hutokeza katika tafsiri kama neno la kuhesabu “moja”, “pekee” “pekee yake” “yote isiyogawika”, “moja” (?)¹⁸ Maana yake ya kawaida ni “moja wala si mbili” (Muhubiri 4:8). “Mungu ni bwana mmoja (Kumbukumbu 6:4, ulinukuliwa na Yesu katika Mariko 12: 29, NASV), hivyo basi nafsi moja pekee na iliyotofauti na “Bwana Masia” inayotajwa katika kifungu hicho hicho (Marko 12:36) huyu Mungu mmoja anatambuliwa pamoja na baba katika Malaki 1:6 na 2:10 na katika agano jipya anatofautishwa mara nyingi na Yesu mwana wa Mungu, anaonyeshwa kama mtu / nafsi tofauti. Katika bibilia ya kihibrania “mteule wa bwana” (kamaanisha “Kristo”) ndiye mfalme wa Israeli. Huyu mtume wa bwana Mungu hajakuwa sawa na Mungu wakati wowote.

Dai la kwamba “moja” kwa kweli inamaanisha shirikisho la umoja ni mfano wa ubishi wa maneno matupu yasiohibitika kwa urazini. Robert Morey anashikilia ya kwamba *Echad* haimaanishi umoja usio umoja kamili bali umoja shirikishi.¹⁹ Ubishi (huu unashirikisha uongo wa kilugha / isimu unaovumbuliwa kwa urahisi. Neno *Echad* linajitokeza mara 960 katika Bibilia ya kihibrania na hakuna mahali linalodokeza wingi. Linamaanisha dhahiri “moja wa, si mbili ama zaidi.” *Echad* ni sifa / (kivumishi) ya kuhesabu. Pasipo tatizo, neno tosha hutumika kubadili jina shirikishi / jumuishi:- familia moja, kundi moja, fungu moja . . . ingefaa tuone kwa uangalifu kwamba dhana ya wingi ipo katika jina shirikishi / jumuishi wala si katika neno *Echad* (moja).

Mapema katika kitabu cha Mwanzo tunajifunza ya kwamba “hao wawili watakuwa mmoja / kiungo kimoja” (Mwanzo 2:24). Hili neno “moja’ hapa lina maana kamili ya moja wala si zaidi (kiungo kimoja wala si “viungo”! viwili / mwili mmoja wala

¹⁸ Robert Morey, *The Trinity: Evidence and Issues* (World Publishing, 1996)

¹⁹*Theological Dictionary of the Old Testament* (Grand Rapids: Eerdmans, 1974), 1:194

si “miili” (miwili) fungu moja la zabibu si zaidi fungu moja wala si fungu mbili. Hivyo basi Mungu anaposemekana kuwa Bwana mmoja” (Kumbukubu 6:4; Mariko 12:9; NASV) yeye ni bwana pekee na hamna zaidi.

Fikiria kwamba mtu angedai hili neno “moja” lingekuwa na maana ya “moja shirikishi/jumuishi” katika neno “kiweko kimoja” cha miguu mitatu “(tripod moja).” Ingekuwaje kama mtu angefikiria ya kwamba ule muungano mmoja wa majimbo ya marekani,” neno “mmoja” liwe na maana ya wingi. Katika mawazo ya upeo wa juu ni wazi kuwa dhana ya wingi ipo kwenye maneno “tripod / miguu” mitatu na “majimbo sio kwenye neno “moja”. Si sawa kuuipa neno “moja” dhana ya wingi ambao kwa kweli inahusishwa na jina linalofuatia pekee. Itakuwa sawa na kusema kwamba “moja” kwa kweli inamaanisha “mia moja” inapotokea kishirikisho / kusumuishwa katika “tandu mmoja!” (Mdudu mwenye “miguu mia moja” – inaaminika).

Hoja yetu inaweza kudhihirishwa katika kamusi yoyote ya kibibilia ya kihibrania. Kamusi ya Koehler na Baumgartner inatoa maana msingi ya *Echad*, “moja pekee”.²⁰ Wakati wajumbe waliporudi na ushahidi wa uzao wa matunda (ubora) katika nchi ya ahadi walibeba ‘fungu moja / pekee (Echad) la zabibu’ (Hesabu 13:23, NRSV). *Echad* huhesabika mara nyingi kama ‘pekee’ ama “moja tu.”²¹ Hivyo basi tunaposhughulikia hoja ya mambo ya imani ya Isareli, fungu hili linatuarifu kwamba bwana wa Israeli aliye mkuu ni “bwana aliye pekee”, bwana mmoja pekee”.

Imetubidi tuishughulikie sana hoja yetu kwa sababu utetezi wa hivi karibuni wa utatu mtakatifu wa Mungu unatumia hoja ya kushangaza na isiyothibitika, kwamba *Echad* inamaanisha “umoja jumuishi / ushirikishi.” Mwandishi anaelezea ubishi wake kuhusu Mungu aliye nafsi nyingi kuambatana na anachofikiria kwamba ni msingi imara katika bibilia ya kihibrania. Ukweli wa kilugha / kiisimu ni kwamba *Echad* haiwezi kumaanisha ‘moja jumuishi / shirikishi’ ila dhahini “moja pekee’ hoja ya kwamba maji mengi yalikusanyika mahali moja Echad (“Mwanzo 1:19) hatoi habari yoyote kuhusu dhana jumuishi / shirikishi kuhusu wingi wa uungu.”²²

Ubishi huu wenye uzushi kuhusu wanachoita wingi ulio ndani ya neno “moja” umetambaa sana na kukubaliwa pasipo kupimwa, tunaongeza maoni ya mmoja anayeamini katika nafsi tatu za Mungu aliye pia mhadhiri mkuu wa elimu ya dini. Anakubali kwamba hoja ya huu ubishi unaopendelewa kuhusu neno echad (moja) ni hafifu sana tu kama neno Elohim. Hakuna hoja ya kutetea dhana ya Mungu aliye nafsi nyingi inaweza kuimarika katika maoni ya kwamba neno moja” katika kihebrania na kiingereza linaweza kugeuza dhana ya mkusanyiko:

Hoja inayoshikilia kwamba neno la kihebrania la “moja” (*Echad*) linalotumika katika shema (sikia wewe Isreli Bwana aliye Mungu wetu ni Bwana mmoja”) inaashiria umoja wala si mmoja pekee ni hafifu hata kuliko dhana kuhusu umoja wa Elohim. Kwa sababu wengine wale wenye imani katika nafsi tatu za Mungu wametoa maoni kwamba agano la kale linadokeza kuhusu umungu ulioshikamana. Ni kweli kwamba ingewezekana kwamba maana ya neno hili katika mkutadha fulani lingeweza kuasharia wingi (kwa mfano mwanzo 2:24: “watakuwa mwili mmoja”) lakini hili halidhiirishi chochote. Uchunguzi wa matumizi katika agano la kale unaonyesha ya kwamba neno *Echad* lina uwezekano wa kuwa na maana kadhaa kama ilivyo neno “moja” katika

²⁰ *Hebrew and Aramaic lexicon of the Old Testament* (Leiden: E.J. Brill, 1967)

²¹ Angalia RSV, Kutoka 10:19 “nzige mmoja”; Kutoka 33:5 “dakika moja”; Kumbukumbu 19:15 “Shahidi mmoja” n.k.

²² Katika kitabu cha Mwanzo 1 na 2, inapatikana “siku moja”, “moja wetu” na kadhalika...

kiingereza. Muktadha ndio unaoamua kama maana inayotakikana ni ya hali ya umoja wa mkusanyiko²³.

Imekwishatolewa hoja mara kwa mara kwamba Mungu angeweza kuelezwa kama *Yachid*. Hivyo ni kusema peke yake, aliyetengwa, wa pekee kama ingekuwa nafsi moja katika uungu. Matumizi ya (Echad “mmoja pekee”), hata hivyo inatosha kudokeza kwamba hio nafsi moja ndio iliyo Mungu. *Yachid* nadra katika Kihebrania cha bibilia. Bibilia inakuwa na maana ya mpendwa wa pekee na aliye pweke na hivyo haingekuwa maelezo sawa kumhusu Mungu²⁴. Kuna neno jingine la kihebrania:- ‘Echad’, “pekee, peke yake aliyetengwa”, ambalo hasa linamuelezea vyema Mungu mmoja. Kumbukumbu 4:35 inaelezea kwamba hakuna mwingine pasipo yeye. Hii hali ya umoja wa Mungu mmoja iliyo dhahiri inasisitizwa kadhalika anapozungumziwa: “Wewe ni Yehovah pekee (Nehemia 9:6), “Wewe ni Mungu peke yako, Mungu wa wafalme wote wa dunia” (2 Wafalme 19:15), “Wewe peke yako ni Mungu (Zaburi 86:10). Mungu mmoja wa Israeli ni nafsi mmoja asiye mfano na aliye katika enzi / kiwango chake peke yake. Yeye ni mmoja katika maana rahisi ya kihesabu inayotolewa na neno hili²⁵.

Tukiwa na hoja hizi itakuwa ni vigumu kutokumhurumia myahudi wa karne ya kwanza aliyekuwa na agano la kale kama mwongozo, anapositiziwa kwa juhudi yote imani katika Mungu mmoja aliye nafsi moja. Ya dhahiri kama Yahweh ama Yahwe wa Majeshi jina lake hapakukutana na nafsi dhahiri ya Mungu”. Hakuna pendekezo hapa kwamba Mungu ni nafsi tatu. Utafiti wowote katika maandiko matakatifu ya Kihebrania kutafuta ishara yoyote ya uwili ama utatu wa nafsi tukufu zilizohusika katika uumbaji hazitafaulu. Kupendekeza uungu ulio zaidi ya nafsi moja utatuhitaji kutupilia mbali sheria za lugha na sarufi. Wanahistoria wazingatifu waumini na wasioamini wanakubaliana kwamba wayahudi wakati wa Yesu walishikilia kwa dhati imani katika Mungu ambaye hakuwa Mungu, ni kinaya kikuu cha historia kwamba Warumi wa dini ya kikristo wamewanyima wayahudi haki ya kuwaelezea maana ya Mungu katika maandiko matakatifu yao wenyewe. Sauti ya kiyahudi juu ya jambo hili inahitaji kusikizwa tena pasipo kupotezwa muda:

Ni dhahiri ya kwamba Agano la Kale linashikilia ibada ya Mungu mmoja. Mungu ni nafsi iliyo mtu mmoja. Wazo la kwamba utatu unaweza kupatikana hapo ama katika njia yoyote iliofichwa ni dhana ilioshikiliwa kwa muda mrefu lakini haina msingi wowote: Baada ya kuwa chini ya mafundisho kama haya wayahudi walipinga vikali mielekeo yote ya ibada ya miungu mingi na wamebaki kuabudu Mungu mmoja pasipo kulegea hadi leo. Katika hoja hii hakuna mwanya katikati ya maandiko ya Agano la Kale na Jipya. Hitikadi ya ibada ya Mungu mmoja inaendelezwa kwamba Yesu alikuwa myahudi, aliyefundishwa na wazazi wa kiyahudi kwa undani wote: injili mpya kwa kweli lakini si mafundisho mapya ya kidini.²⁶

Si kwamba dini ya kiyahudi haina kanuni za kufuatwa kama ambavyo watu wangepikiria ... mafundisho / vifungu ya kiyahudi yako ni itikadi zake ya mafundisho ya imani, kifungu cha *Shema* Israeli (Kumbukumbu 6:4) si cha kufuatiliwa tu kama cha ibada, na amri ni njia pia ya kukiri imani, na huchukuliwa kuwa muhimu zaidi kuliko kanuni za kihistoria za kiyahudi kama njia ya kukiri

²³ Gregory Boyd, *Oneness Pentecostals and the Trinity* (Baker book House, 1995), 47, 48

²⁴ *Yachid* is in fact found as a description of the One God in the Pseudepigrapha.

²⁵ Cp. the remarks of “the Old Testament name for God” (*In the Theological Dictionary of the Old Testament, Abridged in One Volume*, 489)

²⁶ L. L. Paine. *A Critical History of the Evolution of Trinitarianism* (Boston and New York: Houghton Mifflin and Co. ; 1902) 4.

imani. Hii *Shema* ni thibitisho la hali ya umoja na upekee wa Mungu inashikilia tangazo la hali ya juu kabisa kuhusu “ibada ya Mungu mmoja wa kiyahudi”: *Adonai*²⁷ ni Mungu wetu; *Adonai* ni mmoja . . . “Ishaara za imani ya kikristo: imani ya mitume, imani ya Nicea - constantinopole, Imani ya atansi, kutoa tu mifano michache:- zinachukuliwa na wayahudi kutokubaliana kabisa na msimamo huu ulio msingi wa ibada ya kiyahudi ya Mungu mmoja. Hili limesemwa kwa njia iliyo wazi zaidi na *Claude Montefiore*: “Kuhusu umbo la Mungu Wayahudi wote wanashikilia kwamba mafundisho ya kanuni za dini kuhusu uungu wa Kristo, kuhusu utatu, kuhusu Mwana wa (Mungu) wa milele na kuhusu nafsi ya Roho mtakatifu, ni sehemu za Uungu ulio kitu kimoja/ungana, na ni uwongo.”²⁸

Kuamini kwamba Mungu ni nafsi nyingi kama ilivyo imani ya kikristo katika utatu ni kutengana na (dhana) kueleweka kuliko wazi kwa umoja wa Mungu. Kizazi hadi kizazi Israeli ilikataa chochote kile ambacho kingezuia ama kuingiza giza dhana walioipatia dunia ya ibada ya Mungu mmoja isiyochanganyika; wayahudi wako tayari kutangatanga/kuambazwa, kutaabika, hata kufa, kuliko kukubali kuwa hafifu kwa hii imani yao.²⁹

Wasomi wa dini wanaoamini nafsi tatu za Mungu wamekumbana na shida hii iliyo wazi ya kuafikisha utatu na hoja ya kwamba muundo wa ukristo ni wa Mungu mmoja, msomi wa dini mwenye imani katika utatu mtakatifu wa Mungu, Leonard Hodgson anaandika:

Ukristo ulitokana na dini ya wayahudi na ibada ya Mungu mmoja katika dini ya wayahudi iliamini Mungu katika umoja, zama hizo na ndivyo ilivyo hadi leo. Je ingeweze kanaje kanisa la kikristo kuelezea / kutangaza fundisho jipya la kidini linalotosheleza kuelezea huu ufahamu mpya kuhusu Mungu ambao ulikuwa umelifikia kupitia Yesu? . . . je imani katika ibada ya Mungu mmoja ingeweza kubadilishwa ichukue / ishikilie haya maono mapya pasipo kubadilika na kutokuwa ibada ya Mungu mmoja?³⁰

Yesu ni Myahudi na alishikilia imani /kanuni ya Israeli (Mariko 12:28 kuendelea). Hoja hii pekee yake ingetushawishi kuelewa kwamba utengano umetokea mahali fulani katika historia ya hii imani kutoka kwa mafundisho ya Yesu katika kanuni za Kiyahudi / imani ya Yesu ya kiyahudi. Kwa hivi sasa lazima tuisitize kwamba dini ya Wayahudi ilikuwa na umoja wa Mungu, haijawahi kuwa ya utatu wake ilikuwa ni chini ya mafundisho ya dhana hii ya Kiyahudi, na kupata nguvu kwa kumwamini Mungu mmoja wa Israeli ambapo Masia aliyeahidiwa, alifikia utu uzima na akaingia huduma ya kipekee.

Je inawezekana kuthibitisha kwamba Yesu alishikilia na kufundisha imani katika huyu Mungu mmoja wa Wayahudi muda wote wa huduma yake? Kujibu swali hili ni jambo la busara. Tuangalie maneno yake mwenyewe, yalioandikwa kwa uaminifu na wale walioambatana naye katika Palestina, alipokuwa akitangaza, injili inayookoa ya Ufalme wa Mungu unaokuja (Mariko 1: 14, 15: Luka 4: 43 n.k.).

²⁷ Adonai “Inamaanisha aliye bwana” (mkuu), na ina patikana katika biblia ya kihibrania (mara 449) kadhalika jina la Uungu YHVH. Wayahudi leo hubadilisha *Adonai* na hili jina wakfu wanaposoma maandiko na wanapomba.

²⁸ *Lev Gillet, Communion in the Messiah: Studies in the Relationship between Judaism and Christianity.* (Lullerworth Press, 1968), 75, 76.

²⁹ J. H. Hertz Mwalimu mkuu wa dini ya Kiyahudi, *Pentateuch and Haftorahs* (London: Socino Press, 1960), 770.

³⁰ *Christian Faith and Practice, Seven Lectures* (Oxford: Blackwell, 1952), 72.

II. YESU NA MUNGU WA WA YAHUDI

“Wale wanaomuabudu Mungu ni lazima wamuabudu yeye ndani ya Roho na ukweli” – Yesu Kristo

Wale waliotetea msingi wa dini ya Kiyahudi wakiwa macho waliudhiwa sana na ushindani ulioendelea kukuwa pamoja na tisho lililokabidhi jamii ya kidini (Kiyahudi) na mgalilaya mzushi aitwaye Yesu. Wafuasi wake walioendelea kuwa wengi kwa kuvutiwa na miujiza yake, werevu wake ambao haukuchelea na kusema ukweli, mtazamo wake usio kifani iliofichua unafiki katika uongozi wa kidini vilisababisha hali ya uoga na uadui katika usimamizi wa mambo ya kidini.

Tangu mwanzo wa historia ya kuandikwa (andishi), kuogopa ushindani wa kidini, kwa kawaida kumesababisha vita vinavyojificha katika upande wa vyongozi wa kidini. Ni wazi kwamba viongozi wa kidini/watetezi wa imani katika hali kama hii huwa kuna nafasi ndogo ya kujadiliana wazi tofauti (zilizopo katika hali shauri). Ni jambo mwafaka kujiuliza wenyewe jinsi tunavyohisi tisho lolote lile lile (liwepo lisiwepo) dhidi ya imani tunazozishikilia kwa dhati;- liwepo lisiwepo. Jawabu mwafaka la changamoto/ushindani ni msimamo wa kunyenyekea na kutaka kujua unaovutiwa na kupima uzuri ama upungufu wa lolote tunalokabithiwa kuchunguza. Inahuzunisha kwamba mifumo ya dini ya jadi mara nyingi hupambana na vitisho dhidi ya msimamo wao kwa ukali na kutotaka kupatana upatanisho. Wamepambana pasipo huruma na watu (vikundi) wasiokubaliana na mifumo.

Kwa upande wa Yesu, inaonekana kwamba alikuwa mwalimu wa dini ambaye hakuwa na sabira. Alifichua uoga wao kwa kufanya hila ya kumaliza tisho lililosababishwa na athari waalimu wa dini katika mawazo ya umma uliomsikiza na uliopenda kutafuta ukweli. Injili ya Mariko inaandika hadithi/usimulizi wa vita vya mafundisho ya kidini vinavyoendelea, wawakilishi wa vikundi viwili vya kidini vinavyoshindana vilishirikiana kwa kutumia “mafarisayo na waherode kwa kusudi la kumtegemea katika usemi” (Mariko 12:13). Rai ya kwanza iliyokusudiwa kumtega Yesu: “mwalimu unajua ya kwamba wewe ni mwenye ukweli na umnyenyekee yeyote” (Mariko 12:14). Utangulizi huu uliwafuatwa na maswali yaliounuia kumkashifu Yesu mbele ya macho ya waliomsikiza. Hata hivyo majibu yake ya busara kwa maswali haya magumu yalimfanya kuvutia (kuajabiwa) angalao mmoja ama zaidi ya waandishi / waalimu waliokuwa na mawazo yaliyofunguka.

Yule mwandishi msoi wa kidini aliamua kuuliza swali lake mwenyewe. Mwelekeo wake ulikuwa wa moja kwa moja pasipo ujanja/ udanganyifu wala kuiga. Likitafsiriwa katika lugha ya leo ingesomeka hivi: “Je ni nini kiini, hoja kubwa unaloamini na kufundisha? Je ni nini itikadi / nguzo iliyo muhimu zaidi na ya kipekee ya mafundisho yako ya kidini?” Mariko analitoa hili swali kama ifuatavyo: Je ni amri gani iliyo ya kwanza?” ama kama wafasiri wengine wanavyoshikilia uhondo wa maulizano: Ni amri gani iliyo kuu kuliko zote / inayotangulia zote” (Mariko 12:28).

Jibu la Yesu halikulenga amri kumi, alinukulu moja kwa moja kutoka kwa usemi mtukufu wa baadaye, uitwao *shema*: “Sikia wewe Israeli! Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; mpende bwana Mungu wako na moyo wako wote, na roho yako yote, na akili zako zote na nguvu zako zote” (Kumbukumbu 6:4,5; Mariko 12:29,30). Wanafunzi wa Bibilia wanahitaji kujua kama wameelewa maana ya jibu lililo msingi wa ukristo wa Yesu. Anayaachilia maneno ya Musa ya Agano la Kale kama ghala la ukweli wa Uungu. Ufafanuzi wake kuhusu Mungu unapata hadhi/maana kutoka kwa Yesu na aliyohutubia walilijua kuwa dhihirisho msingi. Yesu alifasiri tu kwa njia ya kueleweka rahisi itikadi

iliyo msingi wa mfumo wa dini ya kiyahudi, akidhihirisha dhidi ya ubishi wowote kwamba aliye Mungu kweli ni bwana mmoja:- na *hivyo basi ni nafsi moja*.

Mazungumzo yanayofuata yanadhihirisha jinsi swali/swala hili lilivyozushi. Si kuuingiliana kwingi / malumbano mengi yangukuwa na jinsi hii ya kufumbua macho, kama tunavyomsikia Yesu mwenyewe akiuweka msingi wa imani yote ya ukweli na fahamu? Tunaona hapa wayahudi wawili waacha dini wakiongea kuhusu swala lililo muhimu zaidi kwa maisha ya kiroho. Jibu lisilo sahihi lingeweza kuharibu kuaminika kwa (jina) katika jamii ya kiyahudi. Jibu alilolitoa Yesu hata hivyo lilipata kueleweka mara moja na huyu mwalimu/msomi wa maandiko aliyekuwa na imani ya dhati katika ibada ya Mungu mmoja. Shauku yake kuhusu itikadi ya kihistoria ya Israeli inaonekana kutokana na jibu lake jema: “sahihi, mwalimu, umesema kweli kwamba yeye ni mmoja; na hakuna mwingine pasipo yeye” (Mariko 12:32).

Katika mawazo yake ama myahudi mwingine yeyote anaishikilia itikadi ya kifungu alichotoa Yesu kingeweza kuwa tu cha Mungu aliye nafsi moja wa agano la kale. Kifungu kinachopendwa sana *Shema* (“Sikia, wewe Israeli...”) kinatangaza kwamba Bwana aliye Mungu wetu ni Bwana ni mmoja (Kubukumbu 6:4).

Mungu ni mmoja, Yesu alidhihirisha ni Bwana mmoja (Mariko 12:29) kanuni/itikadi hii rahisi na inayoeleweka kabisa inakolea agano jipya: “kwani kuna Mungu mwingine isipokuwa Bwana? . . . hakuna aliye mtakatifu kama Bwana. Naam hakuna mwingine pasipo wewe, wala hakuna mwamba wowote kama Mungu wetu” (2 Sam. 22:32; I Sam 2:2).

Je Yesu angekuwa anashikilia kiwili chake dhana ya kwamba yeye mwenyewe alikuwa nafsi nyingine yenye usawa na Uungu, na hivyo basi kuwa Mungu kamili pia? Inazidi kuwa dhahiri kwetu kwamba fikira kama hii ingeweza kudadisika hapa ama katika taarifa nyingine yoyote ya Mariko kuhusu Yesu. Hakuna kutofautiana kokote kati ya wasomi wa elimu ya kiyahudi wa jadi na Yesu, aliye mwanzilishi wa imani ya kikristo. Mungu ni mmoja na mmoja pekee. Yeye ni Bwana mmoja, huu ndio usemi mkuu (hoja) kuhusu jinsi ya Uungu kulingana na Yesu. Kulingana na Yesu mwenyewe ni lazima usimame pasipo ubishi kama kanuni ya kuu ya ukristo.

Usemi ambao Yesu alitamataisha nao unadhihirisha kuuiana kwa mawazo yake na ya huyu mwandishi / mwalimu wa dini: “Na Yesu alipoona kwamba alikuwa amejibu kwa busara, akamwambia; wewe haupo mbali na ufalme wa Mungu” (Mariko 12:34). Kutokana na usemi huu tunaweza kusema kwamba bila hii imani yenye busara katika huyo Mungu mmoja wa wayahudi, mtu anaweza kuwa mbali na ufalme wa Mungu. Tangazo la Yesu la wazi kuhusu msingi na dini/ibada ya kweli linatuashiria kulinganisha kufikiria kwetu wenyewe na kwake, kuhusu jambo hili lililo msingi kuliko yote.

Ni muhimu kutambua kwamba mazungumzo haya yalitokea katika siku za baadaye za huduma ya Yesu. Kama angekuwa analeta mabadiliko hayakuharibika na wenye zushi katika dhana kuhusu Mungu katika dini ya kiyahudi, huu ungekuwa wakati mwafaka. Wengine kati ya wasomi wa dini wa leo, wamejaribu kuelezea sababu ya kutokuwa na kifungu kipya chochote kuhusu jinsi ya Mungu katika mafundisho ya Yesu. Msemi mmoja, anayeamini utatu mtakatifu wa Mungu, *Lorraine Boettner* alisema:

Jinsi fundisho/kanuni ya dini (ya utatu mtakatifu wa Mungu), iliyo ngumu sana kwetu sisi, ingechukua nafsi yake kwa kimya na pasipo kuhusishwa katika ukweli wa kikristo unaokubalika pasipo kujisukumiza wala uzushi:-hata katika mikono ya watu waliokuwa wakimwabudu Mungu mmoja kwa dhati kabisa, bila shaka hili ni moja ya matukio mashuhuri sana katika historia ya mawazo ya binadamu. . .

katika enzi ya vitabu ya Agano Jipya utu wa Mungu haungeweza kutenganishwa (ulikuwa mali ya wengi).³¹

Huu ni usemi unaoshtua na kutatiza. Kwanza kuna kutambua wazi kwamba wayahudi walishikilia ibada ya Mungu mmoja kwa dhati, na hili linajumuisha wale wanafunzi kumi na wawili wa kwanza, waliokuwa wayahudi wote: kuhusu usemi kwamba dhana ya utatu mtakatifu wa Mungu “ilichukuwa ukweli wa kikristo”, na huu usemi mwingine, “katika enzi ya vitabu vya agano jipya utatu mtakatifu wa Mungu ulikuwa hautengeki”. Kulingana na mafundisho dhahiri ya Yesu yaliyoandikwa na Mariko, je kuna ushahidi wowote kuhusu hizi semi? Ni wazi kwamba Yesu hajui chochote kuhusu hizi semi, ni wazi kwamba Yesu hajui chochote kuhusu utatu mtakatifu wa Mungu, haleti dhana mpya ya Mungu. Anakubaliana na agano la kale, mwandishi wa kiyahudi na mamilioni ya wayahudi wakati huo kwamba Mungu ni nafsi moja. Hii inamaanisha nini kuhusu ukristo wa jadi ambao umekuwa ukishikilia dhana *tofauti na ile iliosifiwa na Yesu kuhusu Uungu?*

Msimamo wa Boettner unaonekana kutozingatia ya kwamba injili ya Mariko inawakilisha imani ya kikristo kama ilivyoeleweka alipoandika, labda baadaye sana kitu kama miaka 80 baada ya kuzaliwa kwa Yesu. *Boettner* anahusisha kanuni/itikadi za Mungu ambazo hazikuwa zimeingia kikamilifu msimamo wake kwamba imani ya utatu mtakatifu wa Mungu ilikuwa imekubalika katika enzi ya wanafunzi wa Yesu. Hakutilia maanani hisia ya wingi wa Wayahudi ambao idadi yao ilikuwa kubwa katika kanisa la kwanza na ambao wangeiona dhana ya utatu mtakatifu wa Mungu kuwa ya kigeni na ikizidi.

Historia ya kanisa iliyoandikwa zamani kabisa, kitabu cha Matendo ya Mitume, inasimulia baraza zima lililokutana kuamua maswala kama kutahiriwa kwa watu ambao hawakuwa wayahudi, kula chakula kilicho na damu na kula nyama za wanyama walionyongwa. Kama mambo haya ya maumbile yalichukuliwa kuwa muhimu kiasi cha kufanyiwa mijadala rasmi, ingekuwa muhimu zaidi kwa baraza kuundwa lijadili swala zushi la kubadilisha imani kutoka Mungu aliye nafsi moja kwa Mungu aliye nafsi tatu. Walioamini kwa dhati ibada ya Mungu mmoja walikuwa viongozi wa jamii ya kikristo ya awali.

Jambo linaloonekana kutokuwa la kawaida sana tunapoangalia uzushi wa Yesu na waliomshambulia zaidi ni hili: kamwe hakukuwa na ishara yoyote kuwa ubishi ulihusu utatu mtakatifu wa Mungu. Hii sio kusema ya kwamba uzushi uliotokea kwa sababu ya Yesu kudai kuwa “Mwana wa Mungu” hauzingatiwi. Lakini dai hili lisikose kutofautishwa na msimamo wa baadaye sana wa kanisa kwamba alikuwa “Mungu Mwana” ni ukweli ambao haujabadilika kwamba kanuni/itikadi ya utatu mtakatifu wa Mungu haijawahi kutetewa katika agano jipya. Lote sababu, huenda ikawa hii dhana ilikuwa haijawahi, kusikika. Masia anaonekana katika maandishi ya agano jipya kama msimamizi na wa kipekee rasmi wa Mungu, wala sio nafsi ya pili ya utatu mtakatifu wa Mungu.

Maoni ya Boettner yanaonekana kutozingatia majadiliano ya karne ya pili na ya tatu kuhusu jinsi Mungu na Kristo na pingamizi ya mabavu iliyotokea wakati wa baraza la *Nicea*. Wakati wa Kristo walipolazimishwa kukubali imani katika nafsi ya pili ya Uungu iliyochukuliwa/ kudhaniwa kuwepo tangu zamani na iliyotambulika kama yesu. *Encyclopedia Amerikana* inapozungumzia kuhusu upinzani kati ya wanoamini Mungu kama nafsi moja, na wale wanaomwamini kama nafsi mbili na tatu, inatoa maana hizi muhimu:

³¹ *Studies In Theology*, (Grand Rapids: Eerdmans, 1957), 95

Umoja wa Uungu, kama dhana ya Elimu ya dini ulianza mapema katika historia; ni kweli kwamba ulitangulia utatu mtakatifu wa Mungu kwa miongo mingi. Ukristo ulitokana na dini ya Wayahudi, ambayo ilizingatia umoja wa Uungu kabisa. *Njia iliyotoka Jerusalemu kuenda Nicea (Baraza la) ilinyooka nadra. Utatu mtakatifu wa Uungu katika karne ya nne haukuzingatia kikamilifu mafundisho ya awali ya kikristo kuhusu jinsi ya Mungu; badiliko hili la ujasiri na maandiko matakatifu inapotosha vikali/kugeuza sana maneno tuliyopewa na Yesu.*

Yesu anaelezea nafsi yake mwenyewe kama Masia tofauti na Uungu ambao unajumuisha Baba (Mungu) pekee yake. Waumini wenye hekima watajipusha na udhalimu wa namna hii kwa bibilia. Kulazimisha maandiko namna hii kunaonyesha kwa urahisi jinsi Augustina alivyotamani sana kupata imani/kanuni yake kwenye maandiko matakatifu.

Dhana ya awali/ya kwanza ya Yesu haihitaji maelezo. Ni ya moja kwa moja na inaeleweka. Yesu ni nafsi iliyo kando na dhahiri kutokana na Baba yake, Mungu wa pekee aliye kweli/Mungu wa kweli wa pekee. Yesu hajajumuishwa katika Uungu. Umuhimu wa kanuni za yesu mwenyewe unatambulika. Neno “pekee” katika lugha ya Kigiriki ni *Monos*, dhana ambayo iko na maneno sawa / fanana katika kiingereza maana yake ni “pekee”, Peke yake”, bila mwingine” neno ukweli/kweli katika Kigiriki ni *alethinos*, likimaanisha ukweli katika maana ya halisi na hakika. Tunapoweka haya maneno mawili ya kigiriki pamoja *monos* na *alethinos* tunaona ya kwamba Yesu anamweleza baba yake kama Mungu aliye hakika na halisi pekee.

Angalia matumizi zaidi ya Yesu na neno “pekee.” Hakuna shaka kuhusu maana ya neno hili wala usahiliwa tafsiri wake katika Yohana 17:3. “Pekee” ni neno linaloweka mipaka nakutenga. Chochote kinachoelezwa kuwa “pekee” na huwa katika kundi/hadhi yake pekee yake – pekee kabisa. Mambo mengine yote yametengwa. Kama kitu ni cha “pekee” (. . . pekee) ni wazi hapawezi kuwa chochote.

III. JE, WAFUASI WA YESU WALIFIKIRIA KWAMBA YEYE [YESU] ALIKUA MUNGU?

Akizungumzia kuhusu neno “kwa hivyo” katika Luka 1:35, Raymond Brown anasema ya kwamba linahusisha jinsi fulani ya kusababisha kusababishi. Kuwa mwana wa Yesu kunatokana na kubebwa katika mimba ya kimiujiza. Brown anasema ya kwamba hili ni “jambo linalofedhehesha wasomi wengi wa dini wanaoshikilia imani ya jadi kwa sababu katika mapokeo ya elimu ya dini ya kutwaa utu, kutunga mimba kwa njia ya roho mtakatifu hokusababishi kuwepo kwa mwana wa mungu”. Baadaye Brown anataja wanaelimu wa dini ambao “wamejaribu kuepuka uhusiano wa kusababishwa, kwa kuepuka kutumia neno “kwa hivyo” katika Luka 1:35 - wakibishana ya kwamba kutungika kwa mtoto hakuleti/hokusababishi kuwepo kwa mwana wa Mungu”¹⁵. Brown anajikuta katika hali ya kutokubaliana nao. Kile Brown anachofichua ni ugumu aliyonayo mwanafunzi wa kawaida wa Biblia kukubali kwamba, katika jambo hili muhimu la mwanzo na jinsi ya Yesu, maandiko matakatifu hayakukubaliana na kile ambacho yeye amekikubali kuwa ukweli bila kuchunguza kwa uangalifu.

Kama misimamo ya mabaraza Nicene na baadaye Chalcedoni ilikuwa ni migumu kueleweka na ya kukanganya, maelezo ya Luka ni kinyume chake. Kulingana naye, Yesu alikuwa nafsi ya binadamu, aliyepata kuwepo kwake na utu wake/tabia yake kutoka kwa mama yake Mariamu ambaye alikuwa mzaliwa wa nyumba ya Daudi. Kama angekuwa binadamu kamili angekuaje Masiya aliye aidiwa, mbegu (wa kizazi cha) ya Abrahamu na Daudi? Je mtu (nafsi) ambaye amekuwapo tangu milele anawezaje kuwa mzaliwa wa nyumba ya Daudi katika maana yoyote ile? Maoni ya wenye imani katika utatu mtakatifu wa Mungu kuhusu yesu yanaonekana kutozingatia ya kwamba alikuwa mzaliwa wa nyumba ya Daudi, na ndipo akaweza kudai kua Masia.

Je, dhana ya nafsi ya pili katika uungu, ingeweza kuwa na maana yoyote kwa Luka ambapo nafsi tukufu iliokuwepo na ikafanyika mtoto katika tumbo la mamake, Maraimu, hali wakati wote huo ikishikilia uungu wake? Kama ufunuo wa kipekee kutoka kwa Mungu ungekuwa umeonyeshwa mtu yeyote, iwe Paulo, Petero ama Mariamu, wote ambao Luka alishauriana nao kikamilifu kabla ya kuandika masimulizi ya msingi wa imani ya awali/kwanza, si angekuwa ametaja tukio hili maalum angalao kidogo? Ni lazima tukumbuke kwamba mafundisho ya imani katika Mungu wa nafsi tatu yanashikilia rasmi kwamba, Yesu alikuwa na “hali ya ubinadamu ambayo haikuwa na unafsia” (kitaalamu kanuni/itikadi hii inajulikana kama “anhypostasia”), *lakini hakuwa nafsi ya binadamu*. Kukana huku kibusara kunatokana na msembo wa makosa kwamba Yesu ni Mungu, nafsi ya milele ya utatu mtakatifu wa uungu. Hivi ndivyo hoja ilivyo: kama nafsi (ubinafsi) ya Yesu ni Mungu - kiini cha kati cha pekee cha utu wake, ni lazima ieleweke kwamba kipengele cha ubinadamu kilicho ndani yake hakingeweza kuwa nafsi nyingine ama mtu mwingine. Kuhusu ubinadamu wake ni lazima isemwe ya kwamba ulikuwa hasa “ubinadamu usiokuwa na unafsia”. Kusema ya kwamba Yesu alikuwa na nafsi ya ubinadamu ya pili ni kumfanya nafsi mbili.

Kutoeleweka kusiko kwa kawaida hakujulikani na mwandishi yeyote wa maandiko matakatifu. Ni muhimu kwamba Gabrieli, Luka na Mathayo hawatambui kabisa kuwepo milele kunakosemwa kwa mwana wa Mungu, ambaye alikuwa mtu, wanapojihusisha na mwanzo/chimbuko la Yesu, na hawaonekani kujua kutoeleweka

kokote kuhusu ubinadamu wa mwokozi. Gabrieli, Luka na Mathayo wanaonekana kuwa hawakuzingatia itikadi ya imani kabisa na wanaweza hata kulaumiwa kwamba si wakristo, wakipimwa na kigezo cha kidini cha leo na maoni ya wataalam wengi wa dini.

Masiya katika kitabu cha Wahibrania

Mkazo wa kipekee unawekwa kuhusu utu wa yesu katika kitabu cha Wahebrania. Yesu anaonekana wazi kuwa sehemu ya binadamu kabisa:

Wahebrania 2:17. “Kwa hivyo ilibidi wafanywe kama ndugu zake katika Mambo yote” (ndugu zake wote walikuwa binadamu.)

Wahebrania 7:14. “Manaake ni dhahiri kwamba bwana wetu alikuwa mzaliwa Wanyumba ya Yuda” (kama mwana wa Daudi alikuwa sehemu ya ubinadamu.)

Wahebrania 5:8. “Ingawaje alikuwa Mwana, alijifunza kutii kutokana na mambo yaliyomtesa” (aliteseka kama binadamu mwingine yeyote. Mungu hajifunzi kutii.)

Wahebrania 2:18. “Yeye mwenyewe alijaribiwa katika mambo yaliyomtesa” (“Mungu hawezi kujaribiwa,” Yakobo 1:13).

Wahebrania 5:7. “[Yesu] alitoa maombi na haja kwa kilio kikuu na machozi kwa yule ambaye angeweza kumuokoa kutokana na mauti” (kama angalikuwa Mungu angaliweza kujiokoa mwenyewe.)

Wahebrania 4:15 “Manake hatuna kuhani mkuu ambaye hawezi kutuhurumia unyonge wetu, ila Mmoja ambaye alijaribiwa katika mambo *yote* kama tulivyo” (Mungu hawezi kujaribiwa.)

Wahebrania 4:4 Mungu, wala si Yesu alipumzika wakati wa kuumba; hii ni kusema ya kwamba Mungu ndiye alikuwa muumba.

Wahebrania 2:12 Yesu anajiunga na wakristo katika kumwabudu Mungu.

Dunn anatambua kwamba kitabu cha wahebrania kimefikiriwa mara nyingi kuwa kikiunga mkono kuwepo kimbele kwa kristo: “Mchango maalum wa Wahebrania ni kwamba kinaonekana kuwa maandishi ya kwanza katika agano jipya kushikilia wazo la kipekee la Uana wa utukufu uliokuwepo mbeleni.” Lakini angalia msimamo huo:

Ingekuwa kwa hakika inazidi ushahidi wetu kuufikia msimamo wa kuwa mwandishi amefikia kuelewa ya kuwa mwana wa Mungu alikuwa na nafsi iliyo kuwepo mbele kwa kweli. Kwa ufupi, dhana ya wana uliokuwepo kimbele, naam; lakini hukukuwepo kimbele kukiwa zaidi kama dhana na azimio katika mawazo ya Mungu kuliko kitu kilioko nafsi tukufu.³²

Wakati kitabu cha Wahebrania kinapoongea kuhusu Yesu (Wahebrania 2;6-8) kinazungumza kuhusu mstari ujulikanao katika Zaburi unaohusika na hatma ya mtu/binadamu: “Binadamu ni nani, kwamba unamkumbuka? Na mwana wa Adamu (ni nani), kwamba unamtunza? Hali umemfanya chini kidogo kuliko Mungu [ama Malaika],

³² *Christology in the making* (philadelphia:Westminister Press,1980),55,56,sisitizo yake/lake

na ukamvika kofia ya utukufu na enzi. Unamfanya atawale kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake” (Zaburi 8:4-6)

Je, kifungu hiki ambacho mwanzoni kinazungumzia binadamu, kingeweza kutumika kuhusu yesu kama kwa kweli angekuwa Mungu? Angeweza kuwa “chini ya Mungu [ama malaika]” na wakati huo huo, hata akiwa binadamu, awe Mungu kamili?

Kitabu cha Wahebrania kimetumiwa kuunga mkono kwamba Masia alikuwepo milele. Ushahidi kama huu unategemea sana udadisi uliofanyiwa mstari mmoja kwa mfano, “Mungu...katika hizi siku za mwisho ameongea na sisi katika Mwana, ambaye amemfanya mrithi wa vitu vyote na kupitia kwake alifanya dunia zote” (Wahebrania 1:2). Imependekezwa na wengine ya kwamba huu mstari ni ushahidi ya kwamba aliumba dunia. Tafsiri mwafaka wa mstari huu ni “*kupitia* [si kwa/na] kwake pia alizifanya *nyakati*”. Hakuna chochote hapa kinachoonyesha kwamba yesu aliumba mbingu na dunia. Kinachosemwa ni kwamba Mungu mmoja, ambaye kwa ushuhuda wake mwenyewe, kama ambavyo tumeona alikuwa peke yake katika kitendo cha uumbaji (Isaya 44:24), akastawisha nyakati za historia za binadamu ya kumfanya Yesu kuwa katikati/mkuu katika azimio lake, kabla ya kuongea kupitia kwa mwanawe peke yake “katika hizi siku za mwisho”. Si vigumu kuelewa kwamba maisha ya Masia, kifo, na utawala dunia ungeathiri vizazi vyote, vilivyopita vilivyomo na vijavyo. Taswira hii ya Yesu kuwa kati kati ya jinsi/hali ya Mungu kuumba dunia inapatikana katika Wakolosai 1:15-18. Katika Wahebrania ni muhimu sana kwamba Mungu *hakuzungumza* kupitia mwana katika nyakati za agano la kale ila tu “katika mwisho wa siku hizo” (Wahebrania 1:2). Inapendekezwa kwa mkazo hapa kwamba yule mwana si milele ila kuwepo kwake kunaanza kama Yesu wa kihistoria

Kinachojitokeza katika mistari miwili ya kwanza ya kitabu cha Wahebrania ni kwamba Yesu hakuwa mjumbe wa Mungu kwa Israeli katika nyakati za agano la kale. Mungu aliongea kupitia nafsi nyingine wakati uliopita ila si Yesu. Malaika mara nyingi walikuwa wajumbe wa Mungu. Hii haimaanishi ya kwamba yule “malaika wa Mungu”, aliyewakilisha Mungu wa Israeli alikuwa Mwana wa Mungu aliyekuwepo mbeleni kama inavyodaiwa mara kwa mara. Mwandishi wetu anaelezea hoja hasa ya kwamba Mungu hakumzungumzia malaika yeyote kwa kumuita “Mwana” (Wahebrania 1:5). Wadhifa huu ulitengewa Mwana wa Mungu wa pekee - Yesu. Hoja hii inazima dhana yoyote kwamba Yesu alikuwepo mbeleni kama malaika. Fikra ya kwamba angekuwa Mikaeli, malaika mkuu inatengwa dhahiri na kifungu cha kwanza cha Wahebrania. Huduma ya Mwana wa Mungu ni kuu zaidi ya ile ya malaika, ingawa walikuwa na sehemu kubwa katika kutoa amri huko Sinai, (Wagalatia 3:19).

Mwandishi wa Wahebrania anatuelekeza wakati mwingine tofauti anaposema “manake hakuwapatia malaika dunia ijayo ambayo imekaliwa, ambayo tunaizungumzia” (Waebrani 2:5), hazingatii katika mawazo yake matukio yaliopita bali wakati mpya hujao. Ukuu wa Masia kama kiongozi wa hii dunia mpya ijayo ni fundisho la agano jipya linalopotosha. Mwandishi wa Wahebrania anaipa kipao mbele hoja ya kwamba Yesu aliuja uridhi ulio mkuu kuliko ule wa malaika. Ndiye aliyekuwa uridhi wa haki wa Mwana mzaliwa wa kwanza: “Je, alimnenea malaika maneno haya, ‘wewe ni Mwana wangu, leo nimekupata/ kufanya wewe?’” (Waebrania 1:5). Yesu hangekuwa Mungu, alikuwa (nafsi) kiumbe kilichokuwa kimeumbwa na Baba. Kufanywa ama kuzaliwa kunamaanisha kuaanzia, na Mungu hana mwanzo. Yesu alikuwa mzaliwa wa kwanza wa uumbaji mpya wa Mungu. Mwanzo wake ulikuwa wa kipekee ukikusika na kutungika kimiujiza (Luka 1:35), lakini hakuwa Mungu wala haichukuliwi kwamba alikwisha kuwepo mbeleni. Wala hakuwa Melkizedek wa Mwanzo 14:18-20. Melkizedek hakuwa Mwana wa Mungu bali alikuwa kama yeye kama Wahebrania 7:3 inavyosema. Melkizedek alikuwa na nasaba kwa hakika ingawaje haijaandikwa katika maandiko

matakatifu. Huyu kuhani wakisiri/mafumbo na ambaye nasaba yake haiko katika maandiko matakatifu hakuwa mkuu kuliko Mungu! (Hata hivyo Mungu “si mtu” katika Bibilia ya kihebrania). Tafsiri ziko sahihi zinapomuonyesha Melkizedeki kama “mtu huyu” (Waebrania 7:4), ndiye pia mtu ambaye “nasaba yake haipatikani katika walawi”(Waebrania 7:6), lakini hoja ni kwamba inapatikana kwa mtu (mwingine) fulani. “Nasaba yake “ (mstari 6) inamaanisha ya kwamba alikuwa nayo kama kila mtu alivyo na yake. Inakubalika ya kwamba huu mjadala wa namna hii unaotegemea ukosefu wa ukoo wa kuhani mfalme si wa kawaida kwetu katika karne ya ishirini. Hii ndio sababu kuu ya kwamba Bibilia inahitaji kusomwa katika mtazamo wa muktadha wake na mara kwa mara pamoja na msaada wa hao ambao wanajishughulisha na kujua chanzo cha mambo.³³ Msimamo wa wale ambao husema, “Mimi husoma Bibilia tu, wala si maandishi kuihusu” huenda ukaelekeza katika uharibifu na kutojua.

Mwandishi kwa Wahebrania na Paulo walijaribu kuonyesha ukuu wa Yesu kwa njia dhahiri, kama “mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, ili aje kupata nafasi ya kwanza katika kila kitu”(Wakolosai 1:18). Kwa sheria ya kiyahudi mzaliwa wa kwanza alipata urithi mkubwa zaidi. Kitabu cha Wahebrania kinaeleza kupandishwa kwa cheo/hadhi ya huyo Mwana: “Na atakapomleta mzaliwa wa kwanza *tena* katika dunia [NASV], anasema, malaika wote na wamwabudu yeye”(Wahebrania 1:6). Waandishi wa agano jipya waliona kuwa ni jambo muhimu kuisitiza ukuu wa wadhifa wa Yesu kama Masia. Kwanini mwandishi hakusema wazi kwamba Yesu alikuwa yule Mungu Mmoja? Hili lingestawisha ukuu wake juu ya malaika, Musa na Yoshua pasipo shaka yoyote. Ambavyo mwandishi pamoja na Petero na mitume walijua ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Masia (Mathayo 16:16), ilimbidi adhihirish ukuu wake juu ya mamlaka yote yalioumbwa kutoka kwenye maandiko matakatifu. Tunaona pia ya kwamba ilikuwa ni Mungu aliyepumzika wakati wa kuumba, wala si Yesu Masia (Wahebrania 4:4). Hili halileti maana kamili ikiwa Mwana angekuwa anafanya kazi ya kuumba katika kitabu cha Mwanzo - jambo ambalo analipinga katika Mariko 10:6. Katika mtazamo wa Isaya 44:24, Yesu angekuwa amejifikiria kama kuwa pamoja katika Mwanzo 1.

Pasipo shaka ubinadamu wa Yesu kama kuhani mkuu ulikuwa swala jingine la kipekee la kuisitizwa katika kitabu cha Wahebrania. Hata hivyo hali ya kukanganya imetokea katika mstari wa nane wa sura kwanza: “Lakini kumhusu Mwana anasema, ‘Kiti chako cha enzi, Ee Mungu ni cha milele na milele.’” Brown anawakilisha maoni haya:

Vincent Taylor anakubali ya kwamba usemi “Ee Mungu” katika mstari wa nane una maana ya kusema na mtu na unahusiana na Yesu, lakini anasema ya kwamba mwandishi wa Wahebrania alikuwa akinakili Zaburi 2 na kutumia lugha/istilahi yake pasipo madhumuni ya kunuia kusema kwamba Yesu ni Mungu. Ni kweli kwamba hoja kuu ya kunakili Zaburi ilikuwa ni kuonyesha tofauti ya Mwana na malaika na kuonyesha ya kwamba Mwana alikuwa na ukuu wa milele hali malaika walikuwa watumishi tu. Kwa hivyo katika nuku hii haikufanywa hoja kuu kuhusu fikra ya kwamba Mwana anaweza kuzungumziwa kama Mungu. Pamoja na hayo hatuwezi kuchukulia ya kwamba mwandishi hakuona kuwa kugusia kwake kwa Zaburi kulikuwa na athari hii. Tunaweza kusema kwa ufupi kwamba mwandishi hakuwa na makosa yoyote ya kutumia majina haya, na tunaweza kuangalia hali iliyo sambamba na hii katika Wahebrania 1:10, ambapo matumizi ya Mwana katika Zaburi 102:25-27 iko na uzito wa kuzungumzia Yesu kama bwana. Kwa kweli hatuna njia ya kujua maana ya kifungu “Ee Mungu” cha Zaburi ambacho mwandishi wa Wahebrania anapokitumia kuhusu Yesu. Zaburi

Fafanuzi/maelezo ya kisasa yasaidia hasa kuelewa msingi wa lugha ya Wahebrania 7 kuhusu Melkizedeki

45 ni Zaburi ya ufalme; na kwa maelezo ya “Mungu Mkuu” katika Isaya 9:6, *neni* “Mungu” lingekuwa limeangaliwa kwa urahisi kama jina/cheo cha ufalme na hivyo basi kutumiwa kuhusu Yesu kama masiya aliyetokana na Daudi.³⁴

Raymond Brown anahisi kisawa nguvu ya umasia katika Wahebrania 1. Usemi wa “Mungu Mkuu” wa Isaya 9:6 unamaanisha hasa kama ulivyofafanuliwa na kamusi ya kihebrania, “shujaa mtukufu, likionyesha utukufu wa enzi.”³⁵ Ni hii maana ya kimasiasia ya neno “Mungu” inayomuidhinisha mwandishi wa Zaburi kumwita mfalme “Mungu” pasipo kunuia kutufanya tufikirie ya kwamba kumekuwa sasa na nafsi mbili za uungu. Kunakili kwa Zaburi 45:6 katika Wahebrania 1:8 kunaleta maana hio ya kimasiasia kwa neno Mungu katika agano jipya. Hatuhitaji kuelewa matumizi mabaya ya maneno ya kiyahudi ya haya majina/hivi vyeo. Ni kosa kubwa kufikiria ya kwamba Masiasia sasa ameingia nafasi iliyotengewa Mungu Mmoja aliye Baba. Ingawa nafasi ya Yesu ingeweza kuwa ya juu, na ingawa yuko na nafasi ya kumwakilisha Mungu, imani ya Israeli katika umoja wa nafsi kwa ibada ya Mungu Mmoja ya kipekee, haijawahi kupotoshwa na mwandishi yeyote wa Agano Jipya.

Mwandishi wa Wahebrania anajiunga na waandishi wengine wa Agano Jipya kwa kumtangaza Yesu kama Masiasia wa kifalme wa Mungu. Ila ahadi ya kuja kwa ufalme wa Masiasia kwa hakika inapatikana mara nyingi katika maandiko matakatifu. Paulo aliwaambia ulimwengu usio wa kiyahudi wazi kabisa kwamba Mungu “ametenga siku ambapo ataikumu dunia katika haki, kupitia kwa mtu ambaye amemweka baada ya kutoa ushahidi kwa watu wote kwa kumfufua kutoka kwa wafu.”³⁶

Yesu kama mwanadamu aliishi na akafa katika dunia hii na kwa utiifu wake akafaulu kuwa kiongozi wa kwanza wa dunia mwenye haki/mkamilifu kwa kufufuka kwake na uwezo aliyokabithiwa na baba yake, atarudi wakati uliowekwa kukaa katika kiti cha enzi cha baba yake Daudi, akiitawala na kuihukumu dunia. Hata hivyo anabaki “yule binadamu Yesu Masiasia”, hata baada ya kufufuka (1 Tim 2:5), kushuhudia jambo la ajabu ambalo Mungu amelifanyia mwanadamu kupitia kwa mwanadamu. Mtu akishikilia ya kwamba waandishi wa Wahebrania walikuwa wakijaribu kukabithi Mungu-binadamu aliyekuwepo mbeleni katika sura ya kwanza ya huu waraka, atakuwa hawafanyii haki hata kidogo.

Dhana inayorudiwa mara kwa mara kwamba hatuna mwokozi iwapo Yesu si Mungu, haina ithibati ya kibibilia. Kinyume na haya Bibilia inashuhudia mpango wa ajabu ambao Mungu anautenda kupitia kwa binadamu fulani mteule. Ni lazima tuelewe ya kwamba chanzo cha tumaini lote la kikristo kinapatikana katika huyu binadamu, Yesu ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Kama Yesu hangekuwa mmoja katika nyumba ya binadamu, kama tulivyo, basi hatuna uhakika kwamba binadamu wanaweza kufufuliwa kuingia uzima wa milele. Kufufuka kwa Yesu kulilidhihirishia kanisa kuwa Masiasia mwanadamu alistahili kwa kweli njia/cheo kikuu kilichowekewa yule masiasia katika agano la kale. Kufufuka kwake ndilo tumaini lililotia moyo lile kanisa la kwanza. Kwa vile hili lilifanyika kwa mtu mmoja, basi lingeweza kufanyika kwao.

³⁴ *Jesus, God and Man* (New York: Macmillan, 1967), 24, 25 mkazo umeongezwa

³⁵ Brown, Driver and Briggs, *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament* (Oxford: Clarendon Press 1968), 42 Cp. wingi wa *elim* “miungu”, ulitumiwa kwa nafsi zingine ila si yule Mungu Mmoja. Katika **Qumran** malaika waitwa “*elim*” pamoja na Mikaeli. *New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis* inasema “uwazi wa kutumia majina matukufu kwa malaika wakuu una maana rahisi katika ukristo wa agano jipya” (toleo Willem A. van Gemeren, Paternoster Press, 1996, 1:402).

³⁶ Matendo 17:31, ikilingana na Zaburi 96: 13, ambapo maandishi anasema kuwamba, Mungu anakuja “Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa kwa uaminifu wake.” Ni wakati wa kufurahi sana. Jambo hili kuhusu Ufalme wa Mungu ndilo Paulo anawaeleza watu wa *Athenia* (katika mstari wa 11, 12).

Yesu aliye binadamu

Wafuasi wa kale wa Yesu wanaonekana kufanya hoja ya kipekee ya kusisitiza ubinadamu wa Yesu. Hii ni kweli hasa katika waraka kwa Wahebrania. Tangu hapo watoto wanashirikiana katika nyama na damu, yeye mwenyewe pia alishiriki haya....Kwa hivyo 22 ilibidi afanywe kuwa *kama ndugu zake katika mambo yote*, ndipo angeweza kuwa kuhani mkuu mwenye huruma na mwaminifu.(Wahebrania 2:14,17). Ni vyema kuuliza: angewezaje kujaribiwa kama sisi, kushiriki katika nyama na damu, na kufanywa kama ndugu zake katika mambo yote, kama hakuwa binadamu wa kawaida kikamilifu kama sisi? Kiumbe aliye Mungu anayebewa na mwili wa kibinadamu, ama mmoja aliye Mungu na binadamu kikamilifu, si mwanadamu.

Thomas Hart, mwandishi wa kikatoliki anakumbana kwa ukweli na shida inayosababishwa na kanuni za baadaye za utatu mtakatifu wa mungu:

Ile dhana ya Chalcedonia [uwamuzi wa baraza kumtangaza Yesu kuwa Mungu na binadamu] inafanya ubinadamu halisi jambo lisilowezekana. Ufafanuzi wa upatanishi wa baraza huu unasema ya kwamba Yesu alikuwa binadamu kamili. Lakini iwapo jinsi mbili ndani yake, ambayo itatawala ni wazi. Na mara moja Yesu anakuwa tofauti kabisa na sisi. Anajua yote, anaweza yote na yupo mahali kote kwa mara moja. Anajua yaliyopita, yaliyomo na yajayo....Anajua kabisa kile kila mmoja anachofikiria na aendacho kutenda. Hii ni kando sana na hali ya ubinadamu wa kawaida. Yesu anajaribiwa lakini hawezi kutenda dhambi kwa sababu yeye ni Mungu. Hili ni jaribio la namna gani? Halina uhusiano mkubwa na mapambano tuliyoyazoea.³⁷

Kama kuhani mkuu, “huyo nabii”, na mzaliwa wa ukoo wa Abrahamu na Daudi, Yesu hakutamba mipaka yote ya binadamu ingawaje yuko na hali ya upekee ya kuwa Mwana wa Mungu. Paulo anatofautisha Yesu na mwanadamu wa kwanza, Adamu, ili kustawisha nafasi ya Yesu kama Masia. Aliwaandikia Wakorintho: “kwa sababu kifo kilikuja kupitia kwa mtu [Adamu], kadhalika ufufuo pia ulikuja kupitia kwa mtu[Yesu]...yule Adamu wa kwanza akawa roho inayoishi. Yule Adamu wa pili akawa roho wa kutoa uhai....Yule mtu wa kwanza anatoka duniani, udongo; yule mtu wa pili ni bwana kutoka mbinguni” (1 Wakorintho 15:21,45,47). Adamu alitengenezwa kutoka kwenye vumbi la mchanga. Yesu alitokana na roho wa uwezo wa Mungu akifanya kazi katika 23 Mariamu na atatokezea tena katika kuja kwake kwa pili kama nafsi inayotoa uhai, aliyobadilika akawa katika kufufuka kwake.

Hakuna ushahidi ya kwamba yeyote kati ya mitume ndiye alikuwa mvumbuzi wa mwelekeo mpya wa Yesu kama Mungu. Paulo anajua tu Masia aliye pia mwanadamu, Adamu wa mwisho. Anambainisha kikamilifu na baba yake katika waraka wake wa kwanza kwa Timotheo. Katika kifungu kijulikanacho kuhusu imani ya ukristo anasema, “maanake kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja pia katika Mungu na mwanadamu, yule binadamu/mtu Yesu Kristo” (1 Tim.2:5). Huu ni ufupisho mwema wa imani ya kikristo. Kuzima uwezekano wa kukanganya kokote kati ya Mungu na binadamu anatofautisha yule Mungu Mmoja na Masia aliye binadamu/mtu. Si hili pekee tu, anafanya imani katika huyu Mungu Mmoja na huyu Masia aliye mwanadamu kuwa msingi wa kujua ukweli unaoelekeza katika wokovu (1 Tim 2:4,5). Mtu asikose kupata kujihusisha kwa wokovu, kujua kwa ukweli na kuelewa kikamilifu kitambulisho cha Mungu na Yesu kulingana na Paulo.

Petero hamjui Masia mwingine baada ya ufufuo ila yule “Yesu binadamu/mtu”. Anamtambulisha Mwokozi kwa jamaa wa nchi yake kwa maneno: “watu wa Israeli,

³⁷ *Kumjua na Kumfuata Yesu [To know and Follow Jesus]* (Paulist Press, 1984), 46

nisikizeni. Yesu mnazareti, *mtu* aliyeshuhudiwa kwenu na Mungu...”(Matendo 2:22). Luka ananakili usemi wa Paulo kwa Wayunani kwamba “Mungu ametenga siku ambapo atahukumumu ulimwengu katika haki kupitia kwa *mtu/binadamu*”(Matendo 17:31). Petero na Paulo wanaeleza kuhusu mtu aliye Masia ambaye alikusudiwa kurudi kuhukumumu na kutawala. Yesu bado alizungumziwa kama mtu. Ni sehemu ya hekima ya Mungu isiyo kipimo kwamba anaweka hukumu yote kwenye mikono ya mtu ambaye amepitia maisha sawa na wanadamu.

Agano Jipya limejaa semi zilizo wazi kuhusu Yesu aliye binadamu ambaye alibidi kujaribiwa katika hali *zote* kama tulivyo (Wahebrania 4:15). Mtu/nafsi ambaye ni Mungu kikamilifu na mtu kikamilifu hawezi kuwa binadamu katika hali zote. Huu ndio msingi wa tatizo la imani katika nafsi tatu za Mungu. Haiwezekani kamwe kwa msimamo wa kibibilia kutotofautisha huyo Mungu Mmoja na mwanadamu. Hata ikiwa Mungu atampa binadamu aliye hafifu roho yake, na hata iwe Yesu aliyefufuliwa alikuwezwa kiasi gani, mtu/binadamu, kwa maoni ya Bibilia ni vumbi lililohusishwa na roho 24 wala si mwili na roho inayoweza kutengeka, ambayo ni dhana ya Kiyunani(*Kigiriki*).³⁸22. Binadamu, kwa ufafanuzi, ni neno linaloonyesha kutoweza kuishi milele, kupatikana na unyonge na kifo “imepangiwa mwanadamu kufa...”(Wahebrania 9:27). Yesu alipatwa na hatma ya mwisho ya binadamu wote.—si kwamba alihitaji kufa maanake hakufanya dhambi. Hata hivyo kwa kubeba adhabu ya dhambi za binadamu, alikufa. Mungu hawezi kufa. Lazima tuisitize hoja hii:*Mwokozi aliye Mungu hawezi kufa, na hivyo basi hakufa kwa ajili ya dhambi zetu. Hoja ya kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu ni dhahirisho ya kwamba hakuwa Mungu.* Ni ushindani wa ukuu wa mawazo kuisitiza kwamba Mungu wa milele (asiyeweza kufa) alikufa. Wale wanaobisha ya kwamba ni mwili wa Yesu uliokufa bado wanaangukia mtego wa kusema kwamba Yesu mwenyewe hakufa. Ubishi wote unaoshikilia huu mwelekeo wa njia mbili kwa vyovyote vile haumbatani na Bibilia. Hoja kuu inayounganisha imani yote ni kwamba Yesu *mwenyewe* alikufa.

Yesu aliishi maisha yake yote katika vizuizi vya ubinadamu. Alikasirika na kuchoka (Marko 5:3;Yohana 4:6) inagawa hakuwahi kufanya dhambi. Ilibidi ajifunze utiifu kwa mateso aliyopitia (Waebrania 5:8). Hangeweza kujiondoa na kujificha katika tembe ya utukufu kimawazo ili kuepuka ugumu na mapambano ya maisha ya kila siku. Anakubali mwenyewe kwamba hakuwa na maarifa ya kila kitu: hakujuu siku ya kurudi kwake, (Marko 13:32). Kama mtoto, alihitaji kukua katika hekima (Luka 2:52). Wakati fulani ilibidi awaulize wanafunzi wake: nani aliyenigusa? (Marko 5:30). Alilia (Yohana 11:35) na alijua kufa moyo/simanzi. Ni dhahiri kwamba hakuwa na sifa za maarifa yote (Marko 13:32), uwezo wa kuwepo mahali kote kwa wakati mmoja (Yohana 11:32) wala ya kutokufa , ambazo ni sifa zisizotengeka/achika za Uungu/utukufu.

Wayahudi na Wakristo wa karne ya kwanza walikuwa wakitafuta Masia aliye binadamu ili atawale hali mpya katika dunia kutoka kwenye nchi ya ahadi. Umuzi wa wasomi wa dini wa karne ya nne na ya tano ni kwamba huyu nafsi ya mwanadamu wa pekee aliyelitwa Yesu alikuwa “ Mungu halisi kutoka kwa Mungu halisi”³⁹ ungekuwa wa kutisha kwa jamii ya wakristo wa karne ya kwanza ambayo ilikuwa na fikra isiyo tashwishi kuhusu nasaba ya Masia: “kwa maana ni dhahiri kuwa Bwana wetu

³⁸ Cp. D.R.G. Owen “mwili na Roho” katika Agano Jipya” kwa *Readings in Christian Theology*, ed. M. J. Erickson (Baker Book House, 1967), 86: katika dhana ya Kiyunani, vile tumeona, maneno ‘roho’ imetafsiriwa kumaanisha ‘utu’ ama binaadamu, sio” roho inayoweza kutengeka.”

³⁹ 22 D .R .G Owen, “,mwili na roho katika agano jipya “katika readings in Christian Theology, toleo, M.J Erickson (Baker Book House, 1967), 86: “katika fikra ya kihebrania ,kama tulivyo ona, neon linalo tafsiriwa “roho” mara nyingi linasimamia kijina cha nafsi na umaanisha –enyewe (mwenyewe),na kifugu “ mwili na roho”kinasimamia dhana ya kihebrania kwamba mtu ni ‘ mwili uliohuishwa’na wala si maoni ya kiyunani kwamba ni “roho iliyojaliwa tena”....

alitoka/alizaliwa Yuda.” (Waebrania 7:14). Mathayo anaandika matarajio ya taifa ya kiyahudi na tisho lake kwa utawala ambao haukuwa wa kiyahudi (Mathayo 2:2-6). Herode, mtawala ambaye hakuwa wa kiyahudi alifadhaika kusikia ya kwamba watu wenye ujuzi kutoka mashariki walikuwa wakimtafuta aliyekuwa amezaliwa kama mfalme wa wayahudi. Nasaba yoyote ya ufalme ingeweza kutisha mamlaka yake. Herode aliuliza wakuu wa makuhani na waandishi kwamba huyu Masia alikuwa azaliwe wapi? Mathayo anaandika jibu lao: “katika Bethlehemu ya Yuda...“ Na wewe Bethlehemu nchi ya Yuda, umdogo kamwe katika watawala wa Yuda, manake mtawala atatoka kwako” (Mat 2:5,6). Haya yote ni mambo yaliyojulikana na kila mtu. Tafsiri inayopendelea pande moja katika King James Version kuhusu “chimbuko/mianza ya milele” ya huyu Masia katika Mika 5:2 (ikinakiliwa katika Mathayo 2:6) haistahili kutupotosha. Ahadi ya Masia ingeweza kupatikana katika “muda uliokuwa umepita kitambo.”⁴⁰ Ilikuwa ni kutoka kwa kabila la Yuda ambapo huyu Masia angesimama kurithi kiti cha enzi cha baba yake Daudi. Wayahudi walikuwa wakimtafuta mkombozi aliye mwanadamu, akiwa na nguvu zisizo za kawaida na busara yenye utukufu (Isaya 11:1-5), lakini hawakutaraji Mungu awe binadamu. Kuhusu hii dhana ya baadaye, Agano la Kale halikusema lolote.

Kufufuka kwa nafsi inayoishi milele kunadhoofisha mshangao wa hilo ambalo Mungu ametenda katika na kupitia kwa mwanadamu, na kwa ajili ya binadamu wote. Ambavyo Mungu amewafanyia wanadamu vema kwa kutoa mwanadamu angaziye njia ya wokovu, inamfanya kila mtu kufikia karibu kuishi milele (kutokufa). Wakristo leo wanasadiki katika tumaini lisilo kweli la zawadi isiyoeleweka huko mbinguni baada ya kifo. Tumaini la mitume lilishikilia kwamba mkombozi aliyeahidiwa, aishiye milele, alikuwa ameshinda kifo kwa kufufuka kutoka kaburini. Zaidi ya hayo aliahidi kurudi duniani kutunukia wanaoamini kwa mamlaka katika ufalme wake wakiimasia⁴¹ na kustawisha tena ukuu wa Israeli. Lile swali kuu ambalo wanafunzi walimuliza Yesu kabla hajapelekwa katika mkono wa kiume wa Baba lilikuwa wastani kabisa: “je utastawisha tena ufalme wa Israeli wakati huu?” (Matendo 1:6). Jibu lake lilikuwa ya kwamba haikuwa juu yao kujua ni lini tukio hili kubwa litakapotokea. Yesu alidhihirisha kwamba lingekuja kutokea kama mitume wote walivyokuwa wametabiri. Hoja ya wakati ilibaki kutojulikana.⁴²

Shujaa aliyejulikana kwa hawa wakristo wa kale kabisa hakuwa Mungu aliye binadamu. Alikuwa mwana stadi kabisa wa Israeli, mwana ya nyumba ya Daudi, mwana wa Yuda aliye bainika kuliko wote, na katika hali ya kipekee akiwa mwana wa Mungu kutoka kutungika kwake. Alikuwa amefundisha kati yao, akafa na akafufuka tena. Huduma yake iliwatia moyo kuwa na tumaini hilo pia la ufufuo. Picha mpya tofauti kabisa ya mwokozi ilikuwa ikijitokeza katika nyakati za baada ya kuaandikwa kwa Bibilia. Huyu Yesu wa baadaye wa mabaraza ya makanisa aliyeshikiliwa na waumini wa karne ya nne na ya tano alipotosha kwa njia kuajabiwa yule Yesu wa vitabu vya injili aliye binadamu halisi. Hata baada ya pingamizi kwamba haikuwa hivyo huyu Yesu wa imani rasmi mpya *alionekana* kama alikuwa mtu. Nafsi yake hasa, ilidaiwa, ilikuwa nafsi

⁴⁰ Angalia NEB na *The New International Commentary* kuhusu Mika 5:2 (Grand Rapids, Eerdmans, 1976), 343. Jambo hili Kihibrahia inapatikana tena katika Kumbukumbu 32:7 (*y'mot olam*). *Y'mot olam* inapatikana katika Mika 7:14; Amosi 9:11; Isaya 63:9, 11. *The Hastings Bible Dictionary* (*Kamusi ya Hastings*) (Edinburg: T & T Clark, 1912), extra vol., 696, translates the expression in Micah 5:2 as “remote antiquity”, adding that “days of eternity” wrongly suggests the eternal preexistence of the Messiah. See also the *Cambridge Bible For Schools and Colleges*: “More obvious and perfectly suitable to the context, [‘origins’ refers to] his descent from the ancient Davidic family – cp Amos 9:11, where the ‘days of old’ evidently refers to the reign of David.”

⁴¹ Ufunuo 2:26; 3:21; 5:10; 20:1-4; 1 Kor. 6:2; Mathayo 19:28; Luka 22:28-30; 2 Timotheo 2:12

⁴² Elezo sawa inapatikana katika Matendo 3:21

iishiyo milele, ya utatu mtakatifu wa uungu. Huyu Yesu wa mabaraza anaonekana kwamba alimmeza yule Masia-mwanadamu halisi wa kihistoria na aliye katika maandiko ya kikristo.⁴³

Yule seremala mnyenyekevu kutoka Nazareti angekuwa kiongozi bora kufikia ukweli kuliko maamuzi ya baraza lililokuwa likisimamiwa na kiongozi wa Kirumi ambaye hakuwa ametayarishwa kuamua jambo liliokuwa na uzito kuhusu kitambulisho cha Yesu. Hakuzingatia sana ya kwamba Yesu mwenyewe alikuwa hajadai kuwa Mungu. Mabaraza hayakufaulu kutuharifu ya kwamba Yesu hakufanya lolote kunyakua hayo mamlaka ya yule Mungu mmoja wa Israeli na kwamba alikubaliana na wayahudi wenzake kwamba Mungu alikuwa nafsi moja pekee (Yahana 5:44; 17:3; Marko 12:29).

Baada ya Masia kuvuliwa utu halisi na ubinadamu wake, ukweli wa kihistoria haukuzingatiwa. Dhana ya mashariki ya mbali ya kuzaliwa mara nyingi (kurudia maisha tena) ikajipenyeza katika imani ya kuzaliwa tena. Makisio ya Kiyunani na mafumbo yao yakaingia kwenye imani kiharamu yakiambatana na matokeo mabaya. Maoni ya Canon Goudge yanashuhudia marudio: “Wakati wazo la Kiyunani na la Kirumi lilipoingia kutawala kanisa badala ya wazo la Kiyahudi palitokea uharibifu katika kanuni na desturi na hatujawahi kujjepusha na hali hii”.⁴⁴

Wazo hili linahitaji uchunguzi zaidi. Je kupotea kwa kanuni za kibibilia za Mungu kunapatikana tu kutokana na kuingiliwa na falsafa ya kigeni ya Kiyunani?

Tomaso mwenye shaka

Na Tomaso mwenye shaka je? Wakati huyu mtu aliyekuwa na shaka zamani alipomuita Yesu baada ya kufufuka, “Bwana wangu na Mwokozi wangu” (Yohana 20:28), je katika mstari mmoja alistawisha kanuni ya dini ambayo ilimfanya Yesu sehemu ya utatu wa Mungu na hivyo basi “Mungu halisi kutoka kwa Mungu halisi”, kuamabтана na dhana za Nicene xxx na Chalcedonia? Na hii ilikuwa (kama wanavyokubali wenye imani katika Mungu aliye nafsi tatu) kabla wenzake hawajakuwa na mawazo yoyote kuhusu Uungu/utukufu wa Yesu. Je alimtangaza Yesu kuwa uungu wa nafsi mbili kama wengine wanavyodai? Ingawa Tomaso anatumia jina “Mungu” wazi kwa Yesu katika Yohana 20:28, Emil Brunner, mwanaelimu wa dini ajulikanaye sana anatoa maoni haya:

Historia ya elimu ya dini yakikristo na itikadi zinatufundisha kuichukua itikadi ya utatu mtakatifu wa Mungu kama kiini bayana katika dhana ya ukristo kuhusu Mungu...Kwa upande mwingine ni lazima tukubali kwa kweli kwamba kanuni ya utatu mtakatifu wa Mungu haikuwa sehemu ya ukristo wa kale wa agano jipya. Haikuwa nia ya mashahidi wa kwanza wa Kristo katika agano jipya kutuwasilishia tatizo la kiakili - hili la nafsi tatu tukufu - kisha watuambie kwa kimya tuabudu fumbo hili la watatu katika mmoja. Dhana hii haipatikani popote katika agano jipya. Hii “mysterium logicum”, dhana ya kwamba Mungu ni watatu hali akiwa mmoja, inapatikana yote nje ya ujumbe wa Bibilia. Mafumbo ambayo kanisa linawakabithi waumini katika mafundisho yake ya dini...lakini ambalo halina uhusiano na ujumbe wa Yesu na mitume. Hakuna mtume ambaye angeota kufikiria kwamba kuna nafsi tatu tukufu ambazo uhusiano wake--moja kwa wengine na umoja wake ulio kama fumbo vinapita kuelewa kwetu. Fumbo la

⁴³Cp. Martin Werner’s observation that “the dogma of Christ’s Deity turned Jesus into a Hellenistic redeemer-god, and thus was a myth propagated behind which the historical Jesus completely disappeared” (*Formation of Christian Dogma: An Historical Study of Its Problems*, A & C Black, 1957, 298).

⁴⁴ “Kuitwa kwa Wayehudi,” katika maandishi kuhusu *Dini ya Kiyahudi na Ukristo* (Shears and Sons, 1939), 139.

utatu mtakatifu wa Mungu...ni fumbo ambalo halipo, lililotokana na kupotosha urazini wa mawazo kutoka kwenye mistari iliyoandikwa katika Bibilia wala sio kutoka kanuni/itikadi za Bibilia zenyewe.⁴⁵

Maana ya maneno ni lazima itafutwe katika mazingira ambamo yaliandikwa. Bibilia haikutungwa katika karne ya ishirini wala waandishi wake hawakujua chochote kuhusu imani na mabaraza ambayo yalifuata. Mukstadha ni muhimu sana kwa kuamua nia ya mwandishi. Katika kurasa za injili ya Yohana Yesu hakuwahi kujiita Mungu. Ukweli ni kwamba agano jipya hutumia neno Mungu—katika hali yake ya kiyunani *ho theos*—kumaanisha Mungu, Baba wa pekee mara 1350. Maneno *ho theos* (kusema Mungu aliye mmoja), yakitumiwa kabisa (yote) hayaonekani kumzungumzia Yesu kwa hakika mahali popote. Neon Tomaso alilotumia kumueleza/kumuita Yesu katika Yohana 20:28. ilikuwa hasa *theos*. Lakini Yesu mwenyewe alikuwa amekwisha tambua ya kwamba agano jipya liliwaita waamuzi “miungu” anaponena katika Yohana 10:34 juu ya Zaburi 82:6: “je haijaandikwa katika sheria yenu, ‘nilisema, nyinyi ni miungu’?” *Theos* (hapa katika hali ya wingi, ambao ni *theoi*) ilitokea katika maandishi ya agano la kale kwa kiyunani kama jina/cheo cha watu waliomwakilisha huyo Mungu mmoja.

Hakuna wakati wowote ambapo Yesu alijiita Mungu katika hali kamili. Je Tomaso alikuwa na kielezo gani kumuita Yesu “Mungu wangu”? Bibilia shaka wakristo wa zamani walitumia neno “mungu” wakiwa na maana pana kuliko ilivyo desturi leo. “Mungu” ni jina (cheo) la kueleza lililotumiwa kwa mamlaka mbali mbali wakiwemo watawala wa kirumi. Halikupimiwa maana yake kamili peke yake kama jina la pekee la Mungu mkuu kama tunavyolitumia leo. Maneno ya kibibilia yanatujia kutoka kanisa la zamani na ni kutoka katika mazingira ya Agano Jipya ambapo inabidii tuvumbue maana yake.

Wazo la Martin Luther kwamba maandiko matakatifu huanza kwa unyenyekevu, na utuelekeza kwa Yesu kama mtu, kisha kwa yule aliye bwana wa viumbe wote, na baada ya hapo kwa yule aliye “Mungu”⁴⁶ halipati kuungwa mkono kokote katika Agano Jipya. Inaonyesha ugumu wa kusawazisha mapokeo tuliopata na maandiko ya Bibilia. Mafundisho yalioandikwa yanapinga kutengana kokote kutoka imani na ibada halisi ya Mungu aliye nafsi moja ya torati. Akithibitisha imani/kanuni ya Israeli Yesu alitangaza: “Sikia, ewe Israeli bwana Mungu wetu ni bwana mmoja” (Marko 12:29). Alieleza kushikilia imani yake kwa kifungu kilichosisitizwa sana katika imani ya Israeli. Maneno yake hayakunuiwa kamwe kuwaongoza mitume “kwa upole” kumwamini mwingine aliye Mungu. Dhana kama hii inakanganya zaidi. Ikisomwa katika bayana yake, hali maneno yakishikilia maana yao ya asilia, kuthibitisha kuwa Yesu kikamilifu kwa imani kuu ya dini ya kiyahudi kunahitaji kuonekana kama ithibati hakika ya kutambua kwake kwa imani na ibada katika Mungu aliye nafsi moja ya agano la kale.

Tomaso, ambaye hangeweza kuamini ufufuo ulikuwa umetokea pasipo kusikia ithibati iliyo dhahiri, alikuja kuelewa hatimaye wadhifa mkuu ambao Yesu aliupata kama masia aliyefufuka. Ukuu wa kitaifa wa Israeli ambao ulikuwa unangojewa ulionekana sasa kuwa uwezekano. Dai la yesu kuwa masia aliyeahidiwa lilikuwa limedhihirika kwa sasa. Yesu hatimaye anakuwa Bwana wa Tomaso na “Mungu” wa wakati ujao wa ufalme. Tomaso alikuwa amejua utabiri wa agano la kale kuhusu huo ufalme. Ahadi kwa Israeli ilikuwa “mtoto atazaliwa kwetu, tutapatiwa mwana, na mamlaka yatakuwa begani mwake; na jina lake litaitwa ajabu mshauri, Mungu mwenye enzi, Baba wa milele, mwana wa mfalme wa amani” (Isaya 9:6).

⁴⁵ *Christian Doctrine of God, Dogmatics* (Westminster Press, 1950), 1:205, 226, 238.

⁴⁶ Cited by Klaas Runia in *The Present Day Theological Debate*, 97

Hiki ni kifungu kilichokuwa dhahiri ambacho hakingeweza kutoeleweka kuhusu masia ambaye alikuwa anakuja. Lakini “Mungu mwenye enzi” wa Isaya 9:6 anafafanuliwa na kamusi ya kihebrania ya Agano la Kale inayoongoza kama shujaa mtukufu anayeonyesha utukufu wa enzi.”⁴⁷

Kuhusu usemi “Baba wa Milele”, jina (cheo) hili lilieleweka na wayahudi kumaanisha “baba wa enzi ijayo (ya kimasia)” Katika tafsiri ya agano la kale ya kiyunani neno “milele” haliitaji kutoa maana ya “ya wakati usio kipimo”, “kwa milele yote” wakati uliopita na ujao, kama tunavyoelewa kwa kawaida, lakini iko na dhana ya “kuhusiana na enzi (ijayo)” kwa kweli Yesu aliye Bwana Masia, ndiye atakuwa mzazi wa enzi ijayo ya ufalme wa Mungu katika dunia hadi “mambo yote yawekwe chini ya mamlaka yake. Kisha mwana mwenyewe atawekwa chini ya mamlaka ya huyo [Mungu, aliye Baba] aliyeweka vitu vyote chini ya mamlaka yake [Yesu] ili Mungu awe yote katika yote” (1 Wakorinto 15:28). Ilitambulika kwa upana na jamii ya kiyahudi kwamba kiongozi wa kisiasa aliye binadamu angeweza kuitwa baba. Isaya anasema kuhusu kiongozi wa Israeli: “nitamtwika mamlaka yako/yenu, na atakuwa Baba wa wakaazi wa Yuda na Yerusalemu” (Isaya 22:21).

Tomaso, bali na Judasi alikuwa amekwisha kutambua yule ambaye angekuwa “Mungu” wa Enzi ijayo, akichukua nafasi ya shetani, aliye “Mungu” wa enzi hii (2 Wakorintho 4:4). Tomaso hakuwa amefikia imani mpya ya kimapinduzi kwa ghafla kwamba Yesu alikuwa “Mungu halisi kutoka kwa Mungu halisi”. Hapakuwa na habari yoyote katika agano la kale kuhusu umasia wa Yesu ambayo ilitabiri ya kwamba kiumbe/nafsi iishiyo milele na isiyo na nafsi ya utu ilikuwa ichukue mwili wa mwanadamu na iwe mfalme wa Israeli aliyeahidiwa. Hata hivyo huyu mfalme aliye mwanadamu angeweza kuitwa Mungu “ingawa nadra sana, kama ilivyo katika Zaburi 45:6 ambapo pia anapewa jina/cheo “bwana” (mstari 11). Majina yote mawili, “Bwana” na “Mungu” ni ya Masia, na yanatumiwa na Yohana alipoandika kitabu chake chote ili kutusadikisha kwamba Yesu alikuwa ndiye Masia (Yohana 20:31).

Ukweli ulimdhahirikia Tomasi ambaye alikuwa na shaka alipotambua ya kwamba Mungu angeregesha ustawi wa Israeli kupitia huyu Yesu aliyekuwa amefufuka. Hivyo basi Yesu akawa Mungu kwa Tomaso mithili ya Musa alipofurahia wadhifa wa kuwa “Mungu” mbele ya Farao/Firauni: “Bwana” ali/akamwambia Musa, “Tazama na kufanya Mungu kwa Farao” (Kutoka 7:1). Matumizi ya hivi vyeo vya heshima kubwa kwa wajumbe wa Mungu walio wanadamu hauvunji kwa vyovyote uzingatifu wa ibada ya Mungu Mmoja wa agano la kale. Wala hayadokezi kupinduliwa kwa msingi wa kwanza wa Bibilia: Mungu ni nafsi moja, si mbili wala tatu (Marko 12:29). Yule malaika wa Mungu katika agano la kale angeweza kuitwa “Mungu” kwa hali ya kuwakilisha Mungu mmoja wa Israeli (Mwanzo 16:9, 10, 11, 13). Alipatiwa mamlaka ya Yahweh kwa sababu “jina la Mungu lilikuwa ndani yake” (Kutoka 23:20, 21). Katika wakati wa ulimwengu wao, neno “Mungu” halikuwa na maana lililolalo leo. Mandishi ya kuchonga ya mwaka ya 62 kabla ya Yesu yanamuita Mfalme Ptolemy X111 “aliye bwana mfalme mungu”. Wayahudi wa kale walimuita Daudi “Bwana wetu Daudi” na “Bwana wetu Masia” kama ilivyoandikwa katika Zaburi 110:1 (Luka 2:11).

⁴⁷ Brown, Driver and Briggs, *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament*, 42. This same authority records that the word “God” (*el*) used by Isaiah is applied elsewhere in scripture to “men of might and rank, as well as to angels.” (See Exodus 15:11, “among the gods”; Ezek. 31:11, “a god of the nations”, 32:21, “mighty gods”; 17:13, “gods of the land”; Job 41:25, “gods”, i.e., mighty men.) *El* refers to someone other than the One God in Ezekiel 28:2

Msomaji wa dini wa karne ya kumi na tisa anayeshikilia imani ya Mungu katika nafsi tatu anasema haya kuhusu maneno ya Tomaso kwa Yesu: “Tomaso alitumia neno “Mungu” katika jinsi ambayo linatumika kwa wafalme na waamuzi (wanaochukuliwa kuwa wawakilishi wa Uungu/utukufu) na kiheshima kwa Masia.”⁴⁸

⁴⁸C. G. Kuehnoel, cited by W. G. Eliot, *Discourses on the Doctrines of Christianity* (Boston: American Unitarian Society, 1886), 79

IV. PAULO NA UTATU WA MUNGU

“Ionekanavyo, Paulo hakumwita Yesu Mungu”

--Professor Sydney Cave

Hakuna adui aliyepinga kijeshi na kwa hasira kanisa la kwanza kama mtu aitwaye Sauli (Matendo 8:1-3). Wala hakuna msomi wa elimu ya dini anayemzidi Sauli aliyeingia katika kanisa la kale, baadaye alijulikana kama Paulo—mwandishi mashuhuri na msimaji/mtetezi wa ukristo wa karne ya kwanza. Wafumbuaji wa mafumbo wa leo wamemuita mtu asiyewezekana aliyekuwa na maono. Wengine wamemuita mtu aliyekuwa na matatizo ya kitabia/kimawazo aliyekuwa mtumizi wa madawa, lakini amezidi kuhimili hukumu kali za washambulizi wake na leo amebaki kama mtu mwenye mafkara wastani ya Ukristo.

Kwa sababu ya shauku ya hali ya juu ya imani yake, Paulo alijiunga na kundi ambalo Yesu alikuwa ameonya ya kwamba wakati utafika ambapo “yeyote atakayewaua nyinyi (Wakristo) atafikiria ya kwamba amemfanyia Mungu huduma” (Yohana 16:2). Juhudi ya Paulo ambayo haikuwa na mwelekeo ilimfanya kuchukua idhini hatari ya kutesa dhidi ya kundi geni potovu la wakristo lililokuwa limeundwa.

Si nia ya kitabu hiki kukadiria upana wote wa elimu ya dini ya Paulo. Hasa tunataka kuchunguza uiano ama kutouiana kwake agano jipya na maneno ya Yesu aliye Masia kuhusu hoja kuu ya Uungu.

Paulo alidai ufunuo wa kipekee kutoka kwa Yesu aliyefufuka. Ingawa wengi wanakubali ya kwamba busara na ufuno haviambatani, ni msimamo wetu kwamba havipingani. Paulo anaifanua hoja hii. Hakuna sehemu ya ufunuo aliyopewa Paulo na Yesu inashambulia busara. Tukiupatia nafasi ufunuo endelevi, ukristo wa Paulo haupingi mafundisho ya awali ya Yesu ya kihistoria wala yale ya waandishi wengine wa Agano Jipya. Hajatengana na kanuni/itikadi za Masia kuhusu Mungu.

Akiwa ameshikilia nafasi ya juu ya kidini, Paulo anasema ya kwamba “alitahiriwa siku ya nane, alikuwa wa taifa la Israeli, wahebrania, kisheria mfarisiyo;...mtesi wa kanisa na haki inayopatikana kwenye sheria, hakupatikana na kosa” (Wafilipi 3:5,6) bila shaka malezi haya yangemfanya kushikilia kwa dhati ibada ya Mungu mmoja---mtetezi aliyesadiki imani katika Mungu mmoja wa kweli *kama nafsi moja*.⁴⁹ Kama ambavyo tungetaraji kufundiswa kwa Paulo na walimu wa dini kulimweka kusadiki kwa nguvu kabisa kwamba kulikuwa na Mungu mmoja aliyeyumba vitu vyote. Ni wazi kwamba anakubaliana na Masia aliyesulubiwa karibuni kuhusu sheria ambayo Yesu alikuwa ameiita amri kuu ya zote. Kwa mwaandishi aliyeyuliza Masia alimwambia: “Sheria iliyo kuu ni hii, ‘sikia, wewe Israeli! Bwana aliye Mungu wetu ni bwana mmoja; na umpende bwana Mungu wako na moyo wako...’”(Marko 12:29, 30) kama mfarisiyo, Paulo angepitisha bila maswali shauku ya mwandishi kuhusu msimamo wa Yesu kwa ibada ya Mungu mmoja: “Ni sawa mwalimu, umesema kweli kwamba ni mmoja; na hakuna mwingine pasipo yeye” (Marko 12:32). Urithi wa Paulo wa kiyahudi ulikuwa umeweka Mungu aliye nafsi moja katika kilele cha imani yake. Kujitolea kwake kwa huyo Mungu

⁴⁹ This is clearly demonstrated by his declaration in 1 Cor. 8:4,6; Eph. 4:6 and 1 Timothy 2:5. In other areas of his theology, such as the relationship of the law to the new Jew/Gentile community, Paul expressly departs from his pharisaic point of view. As a Pharisee he could not have written Galatians 4 and 4. Under inspiration from the risen Jesus he there declares the law of Moses to have been temporary. Paul's indifference to Mosaic legislation about circumcision makes the same point loudly and clearly.

mmoja wa bibilia ya kihebrania kulibaki msukumo wake mkuu katika mambo yote ambayo alifanya hata baada ya kugeukia Ukristo.

Hakuna dokezo popote katika maandishi ya Paulo ya kwamba aliwahi kutofautiana na kanisa la kale kuhusu nafsi ya Mungu. Ukali wake kabla ya kugeuzwa ulikuwa umeelekezwa kwa dai la Yesu kwamba alikuwa Masia, jambo ambalo alifikiria lingekuwa kitisho kwa dini iliyostawika la taifa la Israeli. Wasomi wengi wanaotajika wa bibilia, baada ya kufanya uchunguzi wa ushahidi kwa uangalifu wafikirie kwamba Paulo alitingisha imani ya kiyahudi ya kwamba Mungu alikuwa nafsi moja. Sydney Cave anasema: “inaoneka Paulo hakumuita Yesu Mungu.”⁵⁰ C. J Cadoux anakubali: “Paulo kidehuri alibainisha kristo kutoka kwa Mungu.”⁵¹ Mtu anaweza kutafuta usemi dhahiri kwamba Yesu ni Mungu, kumaanisha “mwana aishiye milele” aliyekwisha kuwepo, nafsi ya pili ya usawa ya utatu mtakatifu wa Mungu katika maandishi ya Paulo pasipo kufaulu. Katika wahebrania 1:8 pekee yake (haijulikani kama ni Paulo aliyeandika hiki kitabu) inaweza kudaiwa kuwa kifungu ambacho *kwa njia fulani* Yesu anaitwa “Mungu” wazi. Idadi kadha ya vifungu vingine huenda iwe ama isiwe na sehemu zinazomtaja Yesu kuwa “Mungu”. Hii ithibati inabishiwa na wasomi kwa sababu ya kisarufi hii na muundo wa sentensi. Mistari hii kwa hakika haiwezi kutegemewa kuwa “vifungu vyenye ushahidi”. Tunajua kwamba katika Bibilia, neno “Mungu” halimaanishi wakati wote “yule Mungu aliye mkuu.” Haiwezekani kutofautisha imani ya utatu mtakatifu wa Mungu kutokana na vifungu vilivyotapakaa ambamo Yesu alitajwa ama hakutajwa kuwa “Mungu.”

Shida ya imani katika nafsi tatu za Mungu lazima ichunguzwe kuambatana na mwelekeo wa malezi ya kiyahudi katika ibada ya Mungu mmoja pekee ya Paulo. Luka anandika kuhusu huduma ya Paulo katika matendo ya mitume na pia nyaraka zilizoandikwa na Paulo mwenyewe. Swali moja ni muhimu: kama Paulo aliamini utatu ama uwili wa Mungu, hili lilitokea lini? Je alifundishwa utatu mtakatifu wa Mungu na wale mitume wengine ama ilikuwa ufunuo kutoka kwa Yesu aliye masia ama imani hii ilistawi katika maisha yake, ukweli ukijidhihirisha kwake, na kubadilisha vikali imani aliyokuwa nayo katika Mungu aliye nafsi moja? Hamna ushahidi wakushikika wakudhihirisha mambo haya. Tukizingatia mafundisho ya ndani ya akili ya kiyahudi kuhusiana na ibada ya Mungu mmoja na hasa inapomhusu huyu myahudi aliyeshikilia dini kwa dhati, ukuu wa dhana kama hii ungechukua kurasa nyingi za Bibilia.

Wakati msingi wa dini hasa unapobadilishwa ni lazima maelezo dhahiri yatolewe. Mapinduzi ya kanuni za dini ya nguvu ya namna hii yasingetokea pasipo kuhisiwa; angalia maandishi mengi na wakati mwingine uzushi uliomwaga damu ukisababishwa na wanaounga mkono utatu mtakatifu wa Mungu dhidi ya upinzani kutoka kwa watu walioshikilia imani katika Mungu aliye nafsi moja. Ufunuo ulio mtukufu/wa uungu ungekubalika ungekuwa wa busara ili kuanzisha imani katika Mungu aliye nafsi tatu. Lakini ambapo ufunuo haupo na busara inashambuliwa hamna kigezo chochote cha kumfanya mtu akubali dhana isiyo ya kawaida kama ya utatu mtakatifu wa Mungu. Katika maneno wa kiongozi wa kanisa wa Uingereza, yeye mwenyewe mfuasi wa Mungu aliye nafsi tatu, anasema “Busara inapingwa na imani” katika utatu mtakatifu wa Mungu.⁵²

Paulo alipokuwa katika kongamano huku Yerusalemu mjadala ulikuwa juu ya tohara na sheria nyingine za agano la kale. Je hizi zingelazimishwa kiasi gani kwa wakristo wasio wayahudi? (Matendo ya Mitume 15:5). Uanmuzi ulifanywa na Yakobo aliyekua

⁵⁰ *The Doctrine of the Person of Christ* (Duckworth, 1925), 48

⁵¹ *A Pilgrim's Further Progress: Dialogues on Christian Teaching* (Blackwell, 1943), 40-42.

⁵² Bishop Hurd, *Sermons Preached at Lincoln's Inn*, 2:287, cited by John Wilson in *Unitarian Principles Confirmed by Trinitarian Testimonies*, 321.

kiongozi wa kanisa la Yerusalemu. Ni huyu Yakobo aliyesema, alipokuwa kwa makanisa yaliyotawanyika “kama mataifa kumi na miwili yaliotawanywa mbali (Yakobo 1:1) ya kwamba “*Mnaamini kuwa Mungu ni mmoja?*” Mnafanya vyema; pepo wachafu pia huamini na kutetemeka” (Yakobo 2:19). Katika wakati huu wa historia ya kanisa, hakuna chochote kinachoonyesha mabadiliko yoyote ya nguvu kuelewa jinsi ya Mungu.

Ukosefu wa ufunuo unaofafanua utatu mtakatifu wa Mungu unamkabithi tatizo E. Calvin Beisner mwandishi wa utatu mtakatifu wa Mungu anapotetea msimamo wa jadi katika kitabu chake, *God in Three persons* (Mungu katika nafsi tatu) Tunachunguza kazi yake kwa sababu ananukuu mtume Paulo ili kuunga mkono insha yake/msimamo wake katika mjadala huu mapema. Katika sura ya kwanza inagusia imani/kanuni ya Nicene, kama ilivyotangazwa katika baraza la Constaninople katika mwaka wa 381 baada ya Yesu kuzaliwa: “Namwamini mungu mmoja baba wa enzi/utukufu, Muumba wa mbingu na inchi na vitu vyote vionekanavyo na visivyoonekana. Na katika bwana mmoja Yesu kristo aliyefanywa mwana wa pekee wa Mungu, mwanga kutoka mwanga, Mungu wa kweli kutoka kwa Mungu wa kweli....na katika roho matakatifu, bwana na mtoaji wa maisha....”

Beisner basi anauliza hili swali: “je Agano Jipya liko na kanuni/itakadi [utatu mtakatifu wa Mungu] kama hii, kwa njia iliyo wazi ama kwa njia iliyofumbwa? Na kama ipo, kivipi?”⁵³ Majibu ambayo wasomi hutoa kwa haya maswali mawili “ni tofauti sana, kwa kusema machache”⁵⁴. Anasisitiza hata hivyo ya kwamba utatu mtakatifu wa Mungu unapatikana katika Bibilia. Kiini cha hoja hii ni kama ifuatavyo: kuna Mungu mmoja, na mmoja tu aliye kweli; kuna nafsi aitwaye baba ambaye huitwa Mungu; kuna nafsi aitwaye mwana ambaye huitwa Mungu.⁵⁵

Katika kitengo cha maandishi yake anachokiita “Ibada ya Mungu moja aliye nafsi moja katika Agano Jipya”, Beisner anatoa hoja nzuri sana ya kwamba maoni ya ibada ya Mungu aliye nafsi moja. “Inakolea ya maoni yote ya Yesu,”⁵⁶ na ana nukulu Yohana 17:3 : “Basi huu ni uzima wa milele: kwamba wakujue wewe, Mungu wa pekee aliye kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.”

Kisha Beisner anaongeza ushahidi wa Paulo ambaye anajitokeza makusudi kujibu hili swali iwapo, kuna miungu zaidi ya mmoja. Maneno ya Paulo ni kama ifuatavyo: “Tunajua ya kwamba sanamu si kitu kabisa katika dunia na kwamba hakuna Mungu ila mmoja. Kwa maana hata kama wapo wanaoitwa miungu iwe katika mbingu ama duniani, (kwa maana ka kweli wako miungu wengi na mabwana wengi) lakini kwetu yuko Mungu mmoja tu, aliye baba na kuna Bwana mmoja, Yesu Kristo” (1 wakorintho 8:4-6).

Beisner anaonyesha kama ilivyo kweli kwamba jibu la Paulo kwa swali la ibada ya Mungu aliye nafsi moja lilikuwa “hakuna Mungu mwingine ila mmoja.” “Msimamo huu wa ibada wa Mungu aliye nafsi moja”, anaongeza, “unatawala agano jipya lote, na hakuna mahali popote limeelezwa kwa nguvu kuliko hapa katika maandishi ya Paulo.”⁵⁷

Tumefikia mahali muhimu sana katika hoja hii ambapo yalazimu tuchunguze kwa uangalifu Paulo anachosema. Wote wanakubaliana kuhusu imani ya Paulo ya kwamba kuna “Mungu mmoja pekee”, lakini kulingana na Paulo ni nani huyu aliye *Mungu mmoja?* Je kuna “Mungu mmoja—aliye Baba” (Imani ya Mungu aliye nafsi moja) ama “Mungu mmoja—aliye Baba, Mwana na Roho Mtakatifu” (Imani ya Mungu aliye nafsi tatu)? Beisner anaonekana kutozingatia ufafanuzi wa Paulo ulio muhimu sana kuhusu

⁵³ *God In Three Persons* (Tyndale House Publishers, 1984), 24.

⁵⁴ Ibid.

⁵⁵ Ibid., 26

⁵⁶ Ibid

⁵⁷ Ibid., 27

ibada ya Mungu aliye Mungu nafsi moja: “Kwetu sisi [Wakristo] kuna *Mungu mmoja tu, aliye Baba*” (1 wakorintho 8:6). Paulo anamuita huyu Mungu moja kuwa Baba na haongezi nafsi nyingine. Na anaendelea kusema, kwa hakika, kwamba kuna Bwana mmoja, Yesu Kristo, lakini hasemi (hapa ama pengine popote kwamba Yesu ndiye huyu “*Mungu mmoja.*” Huyu mungu mmoja wa ibada ya Mungu mmoja wa Paulo ikesemwa kwa njia ya moja kwa moja na katika huiano na mambo yote ambayo tumesoma katika Agano la Kale na mafundisho ya Yesu, ni yule aliye Baba pekee.

Kulingana na kanuni za kawaida za lugha tunapokuwa na idadi inayozidi moja kiungo “moja” (mono—kiyunani) hakitimiki. Kwa mfano kama mwanaume yuko na mabibi wawili hayupo tena na bibi **mmoja** bali wengi (mono—poly kwa kiyunani). Katika msimamo huu, pamoja na wayahudi na waislamu hatukubaliani ukweli wa kuongea juu ya imani ya Mungu aliye nafsi tatu kama ibada ya Mungu mmoja, kwa hakika si katika maana ya ibada ya mungu mmoja katika kihebrania na Agano la Kale. Ni vigumu kwetu kutokubali kukubaliana ya kwamba nafsi tatu kila moja ikiwa Mungu zinajumuisha Mungu watatu. Tunafahamu ya kwamba hili halikubaliwi na waumini wa Mungu aliye nafsi tatu; Hata hivyo tunafahamu ya kwamba wasomi wa dini fulani hulalamika ya kwamba waumini wa kawaida *hufikiria* Mungu wa utatu katika dini ya utatu—kama Mungu watatu. Inawezekana kumhurumia Hans Kung anayeonyesha “kujali halisi kwa Wakristo wengi na kukereka kuliko na haki kwa wayahudi na waislamu wanapojaribu kupata imani iliyo kamilifu katika Mungu mmoja kutoka dhana kama hii (Mungu aliye nafsi tatu).”⁵⁸

Kama Yesu ama Paulo angetumia lugha ya umoja wa Mungu mahali popote “kwamba wale watatu ni mmoja” ama “yule mmoja ni watatu”, ingetubidi tuelewe utatu mtakatifu wa Mungu kama sehemu ya kufunuliwa na kuikubali kama kanuni/itikadi ya Kikristo. Lakini historia haitambui mawazo haya kuhusu uungu hadi miaka mia tatu baada ya huduma ya Yesu. Kufikia wakati huo elimu ya dini ikilikua imeingia katika mikono ya watu waliokuwa hawafahamu ushirika wa karibu wa mitume na Yesu aliye Masia, na ambao walikuwa uzao wa kundi tofauti na elimu ya dini. Ni jambo moja kwa wakristo kushikilia ya kwamba kuna Mungu mmoja pekee anayezungumziwa katika Bibilia. Ni jambo tofauti kuwasadikisha wakristo kwamba kuna nafsi tatu katika huyu Mungu mmoja. Uwezo wa wanaelimu wa dini kuwarai waumini kwamba nafsi mbili ama tatu ni Mungu mmoja kwa kweli unaweza kuorodheshwa kama moja ya maajabu makuu zaidi katika historia ya ukristo. Tunashangaa jinsi watu wenye busara kwa kawaida wangeweza kukubali kwa urahisi jambo ambalo limekwisha pitishwa (hatma) kuwa fumbo lisiloleweka. Hili jambo linapata umashuhuri zaidi wakati vifungu ya imani vya Bibilia yenyewe havigusii/havidokezi majina kama hayo. Hakuna dokezo la fumbo katika hakikisho lilio dhahiri na rahisi kwamba “kuna Mungu mmoja aliye Baba” (1wakorintho 8:6).

Paulo hakutupilia mbali dhana ya kwamba moja, kuhusiana na Mungu, ilimaanisha moja kiidadi. Ni wazi kwamba alikuwa hajawacha ibada yake ya kiyahudi katika Mungu mmoja aliye nafsi moja alipotangaza katika barua yake kwa Timotheo: “Maana kuna Mungu mmoja, na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu *mtu* aitwaye Yesu Kristo” (1 Tim 2:5) hapa nafsi moja pekee aliye Baba, inatangazwa kuwa yule Mungu mmoja katika sentensi hiyo hiyo nafsi nyingine inaitwa *yule mtu* aitwaye Yesu Kristo. Hili linasababishia imani ya Mungu aliye nafsi tatu mzigo mzito zaidi. Paulo anashikilia imani hiyo hiyo katika waraka wake kwa kanisa la Efeso. Anaongea kuhusu “Mungu wa bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu” (Waefeso 1:17) na anaendelea kutangaza kwa mamlaka katika kifungu kimoja baada ya kwamba “kuna mwili mmoja na roho

⁵⁸ Cited By Pinchas Lapide , *Jewish Monotheism and Christian Trinitarian Doctrine*, 40.

moja...*Bwana mmoja* imani moja ubatizo mmoja *Mungu mmoja* na Baba wa wote” (Waefeso 4:4-6). Sote tunaelewa hiyo “roho moja”na hilo “tumaini moja” kuwa moja kiidadi. Lakini Mungu kwa Paulo ni mmoja pia katika maana ya kihesabu ndiye “aliye Baba wa bwana Yesu Masia.” Maoni ya Paulo hayabadiliki anapowaandikia Wagalatia: “Basi mpatanishi hawi kwa upande moja peke yake; *ingawa Mungu ni mmoja pekee*” (Wagalatia 3:20).

Paulo anaonekana kushikilia pasipo kubadili katika maandiko yake anapozungumza kuhusu Mungu kama nafsi moja (pekee), Baba wa Yesu. Kusema kwamba Paulo alifanya mabadiliko na akaamini katika kitu (uwezo) kilicho nafsi nyingi inazusha tashwishi kubwa. Misimamo yake ya kiimani ni bayana kwamba inaambatana na ibada ya Yesu ya Mungu mmoja bila vizuizi na urithi yote wa Kiyahudi ambao walishirikiana.

Wakati Paulo anaposisitiza kwamba “hakuna Mungu ila mmoja”, anaendelea kueleza, “ingawa si watu wote wanaojua hili (1Wakorintho 8:4, 7). Tunashawishika kufikiria ya kwamba hakujakuwa na mabadiliko makubwa tangu karne ya kwanza. Kuvichukuwa kwa ufupi vifungu vya Paulo vilivyo rahisi katika 1Wakorintho 8:4,6 tuko na himizo ya kwamba “hakuna Mungu isipokuwa Baba”. Imani katika mungu aliye nafsi tatu ni lazima inyenyekee (mbele) ya hii ibada halisi ya Mungu mmoja. Huenda ikawa ubishi wa Thomas Jefferson dhidi ya itikadi ya imani ya Mungu aliye nafsi tatu si mkali sana. Aliona imani hii kama kupotoka kutoka kwenye “dini/ibada ya kweli iliyoanzishwa na Yesu katika umoja wa Mungu na kuelekea katika ibada ya miungu wengi isiyo na busara.” Akimwandikia mchungaji rafiki yake, Jared Sparks hapendezwi na kukuwa kwa baadaye kwa itikadi hii ambayo aliita “kizuka kiinimacho cha Mungu kifananacho na mbwa mwenye vichwa vitatu katika masimulizi ya mafumbo ya Kiyunani aliyelinda milango ya jehanamu kwa kuwa na mwili mmoja na vichwa vitatu.”⁵⁹

Ni Paulo aliyeeleza kwa kanisa katika Korintho woga/kuchelea kwake “isiwe kama ambavyo kama nyoka alimdanganya Awa/Eva kwa werevu wake. Mawazo yenyu yaongozwe kando na kutokana na wepesi na usafi wa kujitolea kwa Yesu. Kwa maana kama mtu atakuja na kuhubiri Yesu mwengine ambaye hatujamhubiri...mnapendezwa na kushikamana na haya!”(2 Wakorintho 11:3, 4). Tunarithika kwamba hii dhana ya Mungu kama nafsi moja inawepesi wenyewe. Mungu aliye nafsi mbili ama tatu, hali akiwa nafsi moja ni mgumu kueleweka. Tatizo ambalo si dogo kuhusu utatu mtakatifu wa Mungu ni kwamba ni dhahiri kuwa Yesu na Mungu katika Biblia ni nafsi mbili bayana katika maana halisi ya kisasa ya neno hilo—watu wawili tofauti kama baba yeyote na mwana.

Si bure kuwa maneno ya Paulo yamekuwa rahisi kupingwa kwamba yanaendean kinyume wakati mwingine. Hili limeongezea kuni kwa moto wa uzushi wa imani ya utatu mtakatifu wa Mungu. Petero alionya kwamba katika maandishi ya Paulo “mambo fulani ni magumu kuelewa na hubadilishwa na wale ambao hawajafundishwa na ambao hawana msimamo thabiti, kama wanavyofanya pia na maandiko matakatifu mengine, kwa uharibifu wao wenyewe” (2 Petero 3:16). Kama hivi ni kweli, tuko na sababu kubwa ya kwamba kuelewa kwetu kwa imani ya Paulo kwa Mungu itegeme misimamo ya imani yake ya wazi. Tusiruhusu kwa vyovyote misitari mingine katika maandiko yake, isiyoeleweka kwa wepesi kama hii, izuie mapendekezo yake yaliyo rahisi na yasiyo na vizuizi anayatumia kufafanua Uungu.

⁵⁹ C.B. Sanford, *The Religious Life of Thomas Jefferson*, 88, 89.

Wafilipi 2.

Wengi wametazama usemi wa Paulo katika Wafilipi 2:5-8 kama ithibati ya kwamba aliamini katika Masia ambaye alikuwa amekwisha kuwepo na Mungu kikamilifu. Kifungu kinasomeka hivi:

Muwe na nia hii kati yenu uliokuwa pia katika Yesu, ambaye ingawa alikuwa katika hali ya Mungu, hakuona usawa wake na Mungu kuwa kitu cha kushikiliwa, bali alijitoa utukufu, akichukua mfano wa mtumishi asiye na uhuru na akafanywa katika mfano wa binadamu. Na akipatikana kiumbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza kwa kuwa mtiifu hadi kufikia kifo hata kwa kifo cha msalaba.

Semi kadha za Paulo zilizo msingi kuhusu huyu Mungu mmoja zinahitaji kurejelewa tunapoangalia kifungu hiki:

- (1) Kwa Mungu wa pekee mwenye hekima, kupitia kwa Yesu Kristo, iwe utukufu milele (Warumi 16:27).
- (2) Kwa maana yuko Mungu mmoja, na mwamuzi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, aliye Kristo Yesu/mtu aitwaye Yesu Kristo (1 Tim 2:5)
- (3) Kuna mwili mmoja...Bwana mmoja, imani moja...Mungu mmoja na Baba wa wote (Waefeso 4:4-6)
- (4) Hakuna Mungu ila mmoja...yuko mungu mmoja, aliye Baba...na Bwana mmoja, Yesu Kristo (1 Wakorintho 8:4,6).
- (5) Aliyebarikwa na mwenye enzi, mfalme wa wafalme na bwana wa mabwana, ambaye pekee ana uhai usio na mwisho na anaishi katika mwangaza usiokaribika, ambaye hajaonekana wala haonekani na mtu yeyote (1Tim 6:15, 16).

Kama Paulo alijua Yesu alikua nafsi ya Uungu yenye usawa na iliyokwishakuwa mbeleni angeweza kuandika vifungu vilivyonakiliwa hapo juu ambavyo ni wazi vinamzuilia yule Mungu mmoja katika nafsi moja, aliye Baba? Kama ni hivyo shtaka kwamba alikuwa amewakanganya wafuasi wake kuhusu jinsi ya Uungu lingeonekana kuwa sahihi. Ni muhimu ya kwamba Luka, aliyeiifuata/andika huduma ya Paulo katika kitabu cha Matendo ya Mitume, hataji hata kidogo ukweli mpya aliyopata Paulo baadaye kuhusu Utatu Mtakatifu. Paulo anafanya dai hili mwenyewe ya kwamba “hakuchelea kutangaza nia yote ya Mungu” (Matendo 20:27). Kwa hakika mahali fulani busara hii yenye umashuhuri kuhusu Uungu wenye nafsi ingejitokeza katika maandishi yake na mahubiri kama angekuwa ameiona kama sehemu muhimu ya mapokeo/kanuni ya kikristo.

Paulo alirejelea kumtaja huyu *Mungu mmoja* akimaanisha baba peke yake, hata katika mikutadha ambapo baba na mwana walitajwa pamoja na hapana kamwe kifungu chochote kisichoeleweka kinachoonyesha kuwa Yesu alikwishakuwepo mbeleni kama Mungu—mwanadamu, akiwa nafsi ya Uungu wa milele na akistahili kabisa neno/jina “Mungu” katika maana yake kamili. Paulo hatii giza bayana iliyopo kati ya yule *Mungu mmoja*, aliye baba na Yesu Mwana Wake, aliye bwana Masia. Na hata anaposisitiza ya kwamba hao wawili hufanya kazi kwa huiano, hasahau kamwe Baba ndiye yule Mungu Mmoja wa urithi wake katika ibada ya Mungu Mmoja. Inashangaza kufikiria kwamba Paulo akiwa katikati ya kuhimiza ya kwamba Mungu ni nafsi ya kipekee angeweza kutuuliza tuamini ya kwamba Yesu pia ni huyu Mungu Mmoja pasipo kueleza. Mapinduzi ya haraka namna hii katika muundo wa dini/imani ya kweli ungesababisha hasira ya sehemu ya wayahudi ya kanisa na ingekuwa sababu ya kuendeleza uzushi. Hakuna ushahidi wa mjadala kama huu.

Ni lazima tuepoke kwa vyovyote vile kuelewa tafsiri zetu za karne ya ishirini katika maandishi ya kanisa la karne ya kwanza. Maneno ni lazima yahidhinishwe kumaanisha kile yalichomaanisha katika muktadha wake. Mafikira ya Paulo hayabadiliki alijieleza kwingine na kueleweka kabisa alipofafanua nani aliyekuwa Mungu Mmoja. Tunauliza pamoja na wafasiri wa bibilia wa kale na waliopo kama kanisa la kale kwa kweli lilielewa kifungu kilicho katika Wafilipi kama utangulizi wa imani ya Nicene—kwamba Yesu alikuwa Mungu halisi kutoka kwa Mungu halisi, aliyekuwepo mbeleni hata milele na muumbaji?

James Dunn anaangalia kifungu hiki kwa kujaribu kutozingatia kuelewa mashauri ya ukristo wa baadaye katika dhana za Paulo: “Jukumu letu limekuwa muhimu lakini gumu la kujaribu kuleta huiano katika masikio yetu ya karne ya ishirini na dhana za miaka ya hamsini na sitini ya karne ya kwanza katika bahari kuu ya kati.”⁶⁰ Anamalizia ya kwamba “Tafsiri ya kuwepo mbeleni na kugeuka binadamu (Wafilipi 2:6-11) kadhalika, inahusika zaidi na hadithi ya mkombozi wa baadaye wa Gnostic kuliko vile inavyohusika na Wafilipi 2:6-11”. Anatuonya kuhusu hatari ya kuelewa maneno ya Paulo jinsi kizazi cha wasomi wa dini baadaye walivyoelewa, “Baba” kwa wingi wa kanisa la Kiyunani katika karne zilizofuata kumalizika kwa maandishi ya Agano Jipya.⁶¹

Inakubalika kwa upana kwamba tunachopata katika maandiko matakatiifu hasa ni kile ambacho tumekidhanika kuwemo, amabavyo hakuna moja wetu ambaye angekumbana kwa urahisi na uwezekano unaotisha kwamba kuelewa “tulikopokea” hakukubaliani na bibilia. (Hii shida huzidi kama tunahusika katika kufundisha bibilia ama kuhubiri) kanuni/itakida za kidini ambapo imekwisha kukubalika kibusara na kihisia haing’oleki.

Mkutadha wa maneno ya Paulo katika Wafilipi 2 unamuonyesha akiwasihi washiriki wa kundi lake kuwa wanyenyekevu. Imekwisha kuulizwa kama kuna uwezekano wowote ya kwamba Paulo angesukumiza hii dhana/somwa rahisi kwa kuwataka wasomaji wake wachukue taswira ya mmoja ambaye, baada ya kuwa Mungu wa milele, aliamua kuwa binadamu? Je kulinganisha kwa namna hii kuna uhusiano wowote na hali kibinadamu? Ni jambo la kushangaza pia kwa Paulo kumuita Yesu ambaye amekuwepo, kuwa Yesu aliye Masia na hivyo kuelewa hili kama jina la mamlaka aliyopata wakati wa kuzaliwa, kutokana na hali yake umilele.

Mahali pengine Paulo hasiti kumuita Yesu mtu/binadamu. Mara nyingi alifafanua wadhifa wa Masia kwa kumlinganisha Adamu na Yesu aliye binadamu. Hili linaonyeshwa dhahiri katika 1Wakorintho 15:45-47 ambapo Paulo anaandika: “kwahivyo imeandikwa, ‘Yule mtu wa kwanza, Adamu, akawa roho inayoishi,’ yule Adamu wa mwisho [Yesu] akawa roho itoayo uhai...Yule mtu wa kwanza anatoka duniani, ni udongo; Yule mtu wa pili anatoka mbinguni.” Paulo anasisitiza ya kwamba Yesu bado ni *mwanadamu*, kama alivyokuwa Adamu aliyeumbwa kutoka kwa mavumbi ya mchanga--hata atakaporudi mara ya pili. Paulo anasema katika Warumi 5:12-15:

Kupitia kwa mtu mmoja [Adamu] dhambi iliingia katika dunia...Hata hivyo, kutoka Adamu hadi Musa, kifo kiliwatawala wale ambao hawakuwa wamefanya dhambi kama ile ya Adamu, ambaye ni mfano wake [Yesu] huyo ajaye ...kwa maana kama kwa kufanya dhambi kwa mtu mmoja wale wengi walikufa, neema ya Mungu na karama ya huyo *mtu mmoja*, Yesu Kristo zilizidi kwa wengi.

Katika Wafilipi mbili Paulo anaeleza kuhusu wadhifa wa juu wa Yesu Kristo aliye mtu. Kama mfano wa Mungu, Baba yake, alikuwa katika “jinsi ya Mungu” (hiki kifungu

⁶⁰ *Christology In the making*, 125.

⁶¹ *Ibid.*, 128

hakisemi ya kuwa *alikuwa* Mungu), lakini hakuona huo “usawa wake na Mungu” kama nafasi ya kutumiwa kwa utukufu wake mwenyewe. Yesu, ambaye kama Masia alipewa usawa wa kutenda kama Mungu na ambaye alitayarishwa kuketi katika mkono wa kuume wa Baba, alijinyenyekeza kwa kuwa mtumishi wa wanadamu, hadi kufikia kujipeana kufa msalabani kama mhalifu. Yesu hakutaka kutumia nafsi yake ya kifalme kama mwakilishi wa haki wa Mungu ila alichukua sifa/tabia ya mtumwa. Kuna tofauti baina ya cheo cha Mungu—Yesu akiwa mwakilishi wa Mungu—na cheo cha mtumishi. Hii tofauti sio kama inavyofikiriwa mara nyingi kuwa baina ya Mungu katika hali ya milele na kuwa binadamu.⁶² Kwa kuacha haki yake ya kutawala na kukataa toleo la shetani la uwezo juu ya falme za dunia (Mat 4:8, 9), Yesu kwa kuwa mtiifu alifanya wadhifa wake wa mtumishi aliyekuwa tayari kuteseka katika mikono ya dunia ya uhasama. Paulo anazingatia/fikiria ni huduma ya Yesu Kristo aliye binadamu (1Tim 2:5), wala sio kufanywa mtu kwa nafsi iliyokuwepo ya Uungu. Unyenyekevu wa Yesu ni kinyume halisi cha kiburi cha Adamu. Yesu hakutumia vibaya wadhifa wake aliopewa na Mungu kuwa mfano wa Mungu baba yake, wala hakutumia uwezo wake kwa manufa yake mwenyewe ya uroho. Adamu chini ya athari ya shetani alijaribu kushikilia usawa wake na Mungu ambao haukuwa haki yake. Kwa kunyenyekea kikamilifu kwa Mungu Yesu aliweza kuonyesha mawazo na tabia ya yule Mungu mmoja, Baba yake.

Kwa kueleza maisha ya Masia yaliokuwa mfano mzuri duniani, Paulo hakunua kuitaja nafsi iliyokuwa mbeleni. Alikuwa anawasihi Wafilipi wawe wanyenyekevu kama Yesu. Yesu alikuwa ametoa mfano wa unyenyekevu na huduma. Ingawa alikuwa amezaliwa katika nyumba ya kifalme ya Daudi na akapata haki ya kuwa na mamlaka makuu ya kuwa mtawala wa dunia kwa kujinyima mwenyewe, kama Zaburi 2 ilivyotabiri karne nyingi kabla hajazaliwa. Alipoulizwa na pilato: “kwa hivyo wewe ni mfalme?” jibu lake lilikuwa, “umeongea sawa. Ni kwa sababu hii nilizaliwa, na kwa ajili ya hili nimekuja duniani” (Yohana 18:37). Yesu alishinda tamaa ya kawaida ya kuipiga/kuishinda dunia (ingawa atashinda nguvu za mtetezi wa Kristo kihaki atakaporudi mara ya pili). Mfano wake wa kujiweka chini ya mamlaka ya mapenzi ya Mungu ulimfanya kukwezwa kwenye mkono wa kuume wa aliye Baba. Hoja si kwamba nafsi ya utatu mtakatifu wa Mungu iliyokuwepo mbeleni ilikuwa imerudia wadhifa baada ya kuuwacha kwa muda mfupi, ila kwamba binadamu halisi aliye Masia, ambaye alikuwa mfano halisi (Wakolosai 1 :15), wa aliye Baba, alionyesha unyenyekevu na utiifu na alikuwa amekubalika/amethibitishwa katika ukuu na kuinuliwa na Mungu. Mahali pengine Paulo anaeleza huduma ya Yesu kuwa onyesho la unyenyekevu anaposema kwamba “ingawa [aliye masia] alikuwa tajiri, kwa ajili yenu akawa maskini, ili nyinyi, kwa umaskini wake, mweze kuwa tajiri” (2 Wakorintho 8:9). Ingawa Masia alikuwa amewekwa kama mfalme wa Israeli na dunia, alijitolea kwa wengine. Pasipo kutumia dai kama la Yesu, Paulo anatomia lugha inayolingana kuhusu huduma yake mwenyewe. “Alikuwa maskini, ingawa alitajirisha wengi, asiwe na chochote na hali akimiliki kila kitu” (2 Wakorintho 6:10) na “pasipo kutaka utukufu...kama tungeweza kuwa mzigo kama mitume wa Kristo” (1 Wathesolanike 2:6). Paulo alijiona mwenyewe na mitume wenzake kama watumishi waliotaabika wa kimasia alipochukua usemi wa Isaya “unabii wa mitume” kwa huduma yake mwenyewe (Matendo 13:47; Isaya 42:6; 49:6).

Kuelewa kifungu cha Wafilipi mbili kidesturi kwa wenye imani katika Mungu aliye nafsi tatu kunategemea, karibu kwa ujumla, kuelewa hali ya Yesu katika “umbo/jinsi ya Mungu”, kama kumzungumzia Mungu akiwa mbinguni katika maisha ya kuwepo mbeleni, badala ya kumuelewa katika kitambulisho chake rasmi akiwa na Mungu

⁶² Katika kitabu cha Wafilipo 2:7, hakuna maelezo ya kuzaliwa. Maneno *genomenos* inamaanisha “kukua”. Yesu alikua binadamu ya kawaida akijichukulia kama mfanyikazi

kama mwanadamu duniani. Inahuzunisha kwamba waliofanya tafsiri wamechangia kupanua wazo hili. Hiki kitendo “alikuwa” katika kufungu, “alikuwa katika jinsi ya Mungu” kinatokea mara nyingi katika Agano Jipya lakini hakichukui maana ya “kuishi/kuwepo milele”, ingawa tafsiri/toleo zingine hujaribu kukilazamishia maana hii. Katika 1 Wakorintho 11:7, Paulo alisema ya kwamba mwanaume astahili kufunika kichwa chake kwa maana yuko katika mfano na utukufu wa Mungu. Hiki kitendo “ni” hapa, ni jinsi nyingine ya hicho hicho kitendo kilichogeuzwa/tafsiriwa “alikuwa” kueleza Yesu kama “katika jinsi ya Mungu.” Nia ya Paulo haikuwa kuleta ile hoja kubwa ya nafsi ya pili ya utatu mtakatifu wa Mungu yenye utukufu wa milele iliyofanywa mwanadamu, ila kutoa funzo muhimu katika unyenyekevu, katika mfano wa Yesu wa kihistoria. Hakuna ushahidi ulio wazi katika kifungu hiki kwamba Paulo alikuwa na imani katika Mungu aliye nafsi tatu na aliamini katika mapokeo ya kanuni/itikadi ya kufanyika mtu/kuzaliwa tena.

Tunapendekeza tafsiri ifuatayo ya kifungu cha mwanzo/halisi cha Wafilipi mbili 2:5-8: “Chukueni nia moja na Masia Yesu: ambaye ingawa alikuwa na cheo cha utukufu, hakuona kwamba usawa wake na Mungu ulikuwa jambo la kuchukuliwa kumfaidi yeye mwenyewe, wala hakujifaidisha na cheo chake maana alichukua nafasi ya mtumwa na alikuwa kama binadamu wengine. Akaonekana kama mtu wa kawaida, alijinyenyekeza kwa kuwa mtiifu hadi kufikia kifo cha kusulubishwa”. Hakuna chochote katika kifungu kinachotuhitaji kufikiria kuhusu nafsi aliyekuwepo mbeleni.

Kuinuliwa/kukwezwa kwa Masia kwa mkono wa kuume wa Mungu ni kutumia kwa Zaburi 110:1. Kumekuwa na ubishi sahihi kwamba hiki kifungu kinahitaji kusomeka, “katika jina la Yesu kila goti litapigwa”, sio “kwa/penye jina la Yesu...” (Wafilipi 2:10). Kwa hivyo kuinuliwa kwa Yesu katika ukuu na kuwekwa katika mkono wa kuume wa aliye Baba, hakubadilishi hoja ya kwamba yote yale aliyofanya Yesu yalikuwa ni kwa utukufu wa Mungu. Bwana aliye katika mkono wa kulia wa mungu ni lazima ikumbukwe, ni *adonai* (“bwana”), ambalo si jina la Mungu.

Wakolosai 1:15-17

Kuhimiza cheo kilicho inuliwa cha Masiya aliye fufuka, uwezo wake juu ya maadui wote na cheo/nafasi yake kikuu katika mpango wa Mungu, Paulo aliwaandikia watu katika kolosai:

Na yeye ni mfano wa mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa maumbile yote. Kwa sababu vitu vyote viliumbwa na yeye, vilivyo binguni na duniani, vionekanavyo na visivyoonekana, iwe viti vya enzi ama falme ama watawala ama mamlaka—yote haya imeumbwa na yeye na kwake yeye. Na yeye ametangulia vitu vyote na ndani yake vitu vyote hushikamana pamoja (Wakolosai 1:16).

Wengine wamechukulia kwamba hiki kifungu ni ithibati ya kutosha kutupilia mbali yote yale ambao Paulo aliyosema mahali pengine kuhusu kanuni ya kikristo kama imani katika “Mungu mmoja, aliya Baba.” Hoja kadhaa zinahitaji kuangaliwa. James Dunn, aliyekuwa msomi katika Mungu aliye nafsi tatu anatoa haya maoni muhimu kuhusu hiki kifungu cha Wakolosai 1:15-20 :

Ni lazima tuelewe ya kwamba Paulo hakuwa akinuia kuwabadilisha watu ili waamini katika nafsi iliyokwisha kuwepo. Hakuitaji kueleza uwezekano wa kuongea kuhusu hekikma iliyokwisha kuwepo. Lugha kama hiyo ilikuwa ikitumika kama kawaida, na hakuna shaka kwamba haikuwa geni kwa walio soma nyaraka zake. Wala hawakushikilia ya kwamba Yesu alikua nafsi Fulani ya kipekee iliyokwisha kuwepo... Alichokuwa akisema ni kwamba, hekima kwa

maana yoyote kamilifu kwa wasomaji wa nyaraka zake, inaelezwa sasa kikamilifu katika Yesu. – Yesu ndiye anayewakilisha hekima yote ya utukufu pasipo kikomo; Utukufu wote uliomkamilifu uliishi ndani yake. Kosa unalofanywa na wengi (pasipo kujua) ni kugeuza hoja ya Paulo na kuelekeza upande usio. Kwa sababu lugha inayoshikilia wazo wa kuwepo kimbele kwa viumbe watukufu ni geni kwa wanaosikiza hivi leo, ni rahisi kushikilia (kwa kufasiri isivyo halali mawazo ya karne ya ishirini katika hali ya Karne ya Kwanza) kwamba hii lugha ilitumiwa kwa sababu hii (kuendeleza imani katika wawakilishi wavitukufu walivyokwisha kuwepo) na kwamba Paulo alijaribu kumtambulisha Yesu na hawa wawakilishi, ama kama Mmoja wao.⁶³

Tunamnukulu profesa Dunn kwa urefu kwa sababu ya kifungu chake muhimu kuhusu hatari ya kumuelewa Paulo kana kwamba alikuwa anajua uwamuzi wa mabaraza ya makanisa baadaye. Paulo anahitaji kueleweka katika muktadha wake mwenyewe wakihebrania. Dunn haandiki kama mpingaji wa imani ya Mungu aliye nafsi tatu. Lakini hapati ithibati ya utatu wa Mungu wa kifungu hiki. Anaendelea kusema:

Lakini usemi wa Paulo ni wazi ulikuwa umeathirika na utamaduni na dhana za kimjini katika siku zake. Kwa hivyo hakuwa akitetea kuwepo kwa nafsi tukufu zilizokwisha kuwepo mbeleni...na maana iliyopo ni kwamba, tukizingatia hii lugha katika ibada ya Mungu mmoja ya kiyahudi, Yesu anahitajika kuonekana kama kitendo cha hekima cha Mungu, kama hekima na Mmoja anayewakilisha hekima ya Mungu kikamilifu zaidi kuliko mwakilishi yeyote yule aliyekwisha mtangulia wa hekima hii iwapo ni katika maumbile/kuumba ama katika agano.⁶⁴

Mchanganuo wa Dunn, unatosha kuonyesha ya kwamba kifungu hiki cha maandiko matakatifu hakidumishi imani katika Uungu/utukufu wa nafsi mbili ama tatu. Hoja zingine kadhaa zinahitaji kuzingatiwa. Kwa njia ya kipekee Paulo amuita Yesu mzaliwa wa kwanza wa viumbe wote. Usemi huu ukichunguliwa kwa uhalisi wake hajumuishi ile dhana ya nafsi ambayo haikuumbwa na ina dumu milele. Kitendo cha kuzaliwa kinahitaji kuwepo kwa mwana fulani. Mzawliwa wa kwanza wa Mungu “ndiye aliye juu zaidi katika wafalme wa dunia” (Zab 89:27). Paulo anatumiya jina la kimasiya linalojulikana sana katika mawazo ya Paulo Yesu si Mungu lakini ndiye Masiya na kunatofauti iyo kubwa sana.

Katika tafsiri nyingi Paulo anasema kwamba “vitu vyote viliumbwa na yeye [Yule Masiya] viambishi vinavyotumika katika Wakolosai 1:16 vinahitaji kutafsiriwa sawa kabisa (kama inayoonekana katika matoleo asili ya biblia wastani (standard Bibles) Alichokandika Paulo hasa ilikuwa kwamba “vitu vyote”—hapa akimaanisha “viti vya enzi, falme, watawala wa mamlaka “—viliumbwa “katika” Yesu “kupitia” kwake na “kwa ajili”yake, haikuwa ya kwamba Yesu alikuwa/ndiye muumba katika msitari unaofunguwa wa kitabu cha Mwanzo ila ilikuwa kwamba alikuwa ndiye kiini (katikati) cha serekali (tabaka) ya Mungu katika mbingu. Mamlaka yote yalikuwa yawe chini ya Mwana ambaye angerudisha kwa Baba yake aliye mkuu (mwenye yote) na aliye mtii, kwamba “Mungu [aliye Baba] aweze kuwa yote katika yote” (1 Wakorintho 15:28).⁶⁵

⁶³ Christology in the Making, 195

⁶⁴ Ibid., (kama ukurasa unaotangulia, 195, 196).

⁶⁵ Tunaona kuamba kulingana na J. H. Moulton, ed., *Grammar of New Testament Greek* (T & T Clark, 1963), Wakolosai 1:16 ina maanisha, “kwa sababu yake I [Yesu]...”(3:253). Hi ina tofauti kubwa na “na yeye...” Angalia pia the *Expositor's Greek Commentary* (ed. W. Robertson Nicoll, Grand Rapids: Eerdmans, 1967) kulingana na hi ukurasa: *en auto*: haimaanishi “na yeye” (504). Watafsiri hawakuchunga ukurasa huu kwa makini.

18Itastajabisha kusema ya kwamba Yesu aliuumba vitu vyote kwa ajili yake mwenywe (Wakolosai 1:16). Hoja kamili ni kwamba Mungu alifanya vitu vyote akifikiria Yesu (kwa ajili ya Yesu), kwa kumuona yeye kama sababu ya uumbaji, na kwa hivyo kwa ajili yake, kama mzaliwa wa kwanza Yesu nu mrithii wa mbingu zilizofanywa na Mungu kwa mpango wa kwamba Mwana wake alihaidiwa ndiye angerithii vilivyoumbwa katika kifungu hiki Paulo natatazama uumbaji mpya ulioanzishwa na kufufuka kwa Yesu, aliyemzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu (Wakolosai 1:18) kugusia uumbaji wa mamlaka ya kimalaika haimaanishi kuwepo kwa Yesu wakati wa uumbaji wa kwanza. kama ilivyo kawaida muktadha ndilo jambo kuu katika tafsiri. Katika kifungu hiki Paulo anazingatia “urithi,” “ufalme na mamlaka” (Wakolosai 1:12, 13, 16). Hili linapendekezwa kwa uthabiti ya kwamba aliufikiria uwongozi wa Masiya juu ya viumbe wote kama mpangilio mpya alioufikiria Mungu kutoka mwanzoni na ambao Yesu kama mzaliwa wa kwanza aliteuliwa kuuongoza.

Misemo ambayo, kama anavyosema Dunn, huonekana kutengana mbali na wasikilizaji wa karne ya ishirini, na ambao huitaji kuthibitiwa kwa uangalifu, haitowi sababu yoyote ya kuamini katika kuwepo kwa yesu mbeleni. Paulo aliamini ya kwamba Mungu alikuwa amepanga ya kuwa Masiya awe na ukuu juu ya vyote vilivyoumbwa, vionekavyo na visivyoonekana, vilivyo mbinguni ama duniani, iwe ni vitu vya nzi, falme watawala ama mamlaka. Yesu ndiye alikuwa mahali pakuanzia uumbaji wote wa Mungu—ndiye alikuwa kiini cha sababu yote ya Mungu ya kuumba vilevile mfano wa hekima ya Mungu. Hata hivyo Masiya hakuwa kiumbe cha milele bali nafsi ya binadamu ya kudhirishwa wakati wake ufikapo na ambaye amefaulu hivi sasa, kama mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, “kuongoza” mpangilio ulio mpya. (Waefeso 1:10)

1 Wakorintho 10:4

Waumini wengi katika kuwepo mbeleni kinafsi kwa Yesu wametumia maneno ya mtume katika 1 Wakorintho 10:4 anaposema akizungumzia waisraeli jangwani kwamba wote walikunywa “kinywaji kilicho sawa cha roho; maana walikunywa kutoka kwa mwamba wa kiroho uliowafuata; na huo mwamba ulikuwa kristo” kama alivyosema John Cunningham:

Inasisitizwa katika kifungu hiki ya kwamba Kristo binafsi aliandamana na watu wa Israeli walipo tembea jangwani kwenda katika inchi ya ahadi. Kuunga mkono hoja hii vifungu vya Kumbukumbu 32:4 na Zab 18:2 udondolewa kwa sababu Yahweh (Mungu) anaelezwa hapa kama mwamba .Imefikiriwa ya kwamba ambavyo Mungu ndiye huo mwamba ulioambatana na Israeli, basi ni lazima Kristo awe Yahweh ama yule Mungu wa Agano la Kale.⁶⁶

Mandishi yanaochunguza vitendo vya Mungu kupitia vizazi vingi, “Mungu alinena zamani na baba zao kupitia kwa mitume katika vifungu vingi na njia nyingi, lakini [kwa kinyume] katika siku hizi za mwisho ameongea nasi katika Mwana wake. (Waebraia 1:1-2). Hili linaonekana kuthibitisha ya kwamba hadi kuzaliwa kwake kama binadamu Yesu hakuwa Mwana wa Mungu wala mjumbe wa Mungu kwa watu. kitabu hiki hiki cha Waebraia kinadokeza y akwamba Neno lilisemwa kupitia malaika katika zama za agano la kale (Waebraia 2:2) kama ujumbe wa Israeli alikuwa kupitia huyu huyu Yesu aliyekuwepo mbeleni na ambaye alibadilika kuwa mwanadamu, huyu mwandishi wa hiki kitabu cha agano jipya anaonekana kutokuwa na habari yoyote kama hii. Ujumbe ulipeanwa kupitia manabii na malaika kwa hakika, lakini haikuwahii

⁶⁶ “Yule Mwamba ni Yesu”, *Restoration Fellowship*, 1981

kudokezwa kwamba ujumbe wa agano la kale ulipitishwa kwa yule ambaye alikuja kutambuliwa kama Mwana baadaye.

Kifungu hiki kinapozingatiwa pekee yake pasipo kuzingatia muktadha wake ama matumizi ya Paulo ya jinsi ya kufikiria ya wahebrania/kihebrania, kinaweza kupendekeza dhana ya kwamba Kristo alikuwa hai kabla kuzaliwa. Kuna vifungu vingine vingi ambamo malaika ndio vyombo vilivyotumiwa kupitisha ujumbe wa Mungu kwa Israeli. Stefano anaongea kuhusu Musa akitoa sheria/amri: “Huyu andiye alikuwa ushirika jangwani pamoja na yule malaika ambaye alikuwa akiongea naye katika Mlima Sinai...Alichukuwa usia iliawapitishie” (Matendo 7:38) Matendo 7:53 inasema ya kwamba walikuwa wameipokea sheria kama ilivyo tawazwa na malaika na bado hawakushikilia. Paulo pia anazungumzia kuhusu nafasi malaika dhidi ya mdhihirishaji wa baadaye anayeitwa “mbingu” (aliye Masiya): “Basi kwanini iwepo sheria? Ilongezwa kwa sababu ya utendaji wa dhambi, baada ya kwamba ilikuwa imetawazwa kupitia kwa malaika...mpaka ambapo “mbingu” [Yesu] angekuja ambaye alikuwa amewekewa ahadi” (Wagalatia 3:19). Punde anaendelea kudhihirisha umoja wa Mungu: “Mpatanishi hausiki na upande mmoja tu, ingawa Mungu ni mmoja pekee.” (Wagalatia 3:20). Ni wai katika kila kimoja katika vifungu hivi kwamba kutolewa kwa sheria kupitia malaika ni moja ya sehemu muhimu za hoja hii. Lakini hoja muhimu inayohitaji kuzingatiwa hapa ni kwamba injili ni kuu kuliko sheria. Upatanishi wa sheria ulifanywa na malaika pekee lakini habari njema (injili) ililetwa na Mwana wa Mungu na hivyo basi ni kuu zaidi. Kwa hakika Paulo hakuamini kwamba Yesu ni malaika aliye kwisha kuwepo.

Kristo hangeweza kuwa na nafasi yoyote ama kwa kutoa sheria kwa wa Israeli ama kwa kuwahubiria/kufundisha wa Israeli jangwani. Matumizi ya Paulo ya neno “mbingu” ama mzaliwa wa kwanza, lina udhahiri mkubwa. Yule “mbingu”— anayetambuliwa kama Kristo— ilikuwa bado haijafika/tokea na hakuwa katika huduma halisi ya Mungu.

Ni wazi kwamba kwa Paulo hiyo “mbingu” ulitajwa hapa na katika sehemu zingine – mbingu ya Abrahamu (Mwanzo 22:18), mbingu ya Yuda (Mwanzo 49:10), na mbingu ya Daudi⁶⁷, ina maana hasa ya Yesu aliye Kristo, mzaliwa wa baba aliye Israeli wengi na Daudi aliyeahidiwa. Warumi 1:13 inazungumzia moja kwa moja kuhusu mwanzo/chimbuko la Kristo kama Mwana wa Mungu. Injili inahusika na “Mwana wake ambaye alizaliwa na mmoja aliyewauzao (mbingu) wa Daudi kimwili.” Hatuwezi na kuepuka na kurudia kusisitiza kuhusu mwana aliyezaliwa na mwanamke na aliyekuwa mzaliwa wa binadamu. Masiya alikuwa atokane na uzao wa binadamu. Hivi ndivyo hasa wayahudi wa siku hizo na kanisa la kale walivyo amini na kutarajia kama Paulo angefundisha kwamba Masiya alikuwa kwa hakika na kibanafsi pamoja na Israeli jangwani, akiwa tayari Mwana wa Mungu, ingekuwa ni kinyume kikubwa cha maneno ya manabii.

Tunahitaji kuepuka kuelewa 1 Wakorintho 10:4 katika maana ya moja kwa moja, tukitia maanani matumizi ya taswira katika kihebrania na njia ya mazungumzo ya kiyahudi. Si jambo lisilo la kawaida kwa maandiko matakatifu kutumia kitendo “kuwa” katika maana isiyo ya moja kwa moja. Yesu alisema “kikombe hiki ni damu yangu ya Agano Jipya (Luka 22:20). Kitendo “Ni” hakimaanishi kutambulisha moja kwa nyingine; hii ni lugha taswira: hiki “kikombe kinawakilisha damu yangu.”

Muktadha wa karibu wa Wakorintho 10:4 unadokeza jinsi Paulo anavyo fikiria. Paulo anaona mambo yaliowapata wa Israeli jangwani kama mifano – aina ama kielelezo ya maisha ya leo ya kikristo. Kama anavyosema Paulo, “haya mambo yaliwapata ‘dhahiri’” (1 Wakorintho 10:11) kupitia kwa wa Israeli katika bahari ya shamu ilikuwa ni

⁶⁷ 2 Sam 7:12-14 pamoja na Isaya 11:1; Warumi 1:3; 2 Tim 2:8.

“mfano/taswira” ya ubatizo ya kikristo. Chakula cha kiroho kinachotajwa katika mstitari wa tatu ni wazo kwamba ni ile maana ya kimiujiza iliopatiwa Israeli kila siku kwa muda wa miaka arubaini. Walikunywa pia kutoka kwa “mwamba wakiroho.”

Kuchukuwa matumizi ya mara moja kuhusu mwamba ulifuata Israeli kama ithibati ya kuwepo kwa Yesu kabla hajukuwa binadamu ni kukosea hoja ya funzo la Paulo. Pia ni kutozingatia ya kwamba wayahudi hawakutarajia Masiya asiwe lolote lingine ila nafsi ya binadamu. Tukiangalia kwa karibu hio hadithi ya agano la kale anayofikiria Paulo tutaona ya kwamba kuna visa viwili vinavyohusisha Mwamba vilivyoandikwa wakati wa Israeli walipo tanga tanga jangwani. Ni muhimu kuona tofauti iliyopo katika visa hivi/miamba hii.

Kisa cha kwanza kinatokea pundu tu baada ya muijiza wa kutoa mana. Israeli ilifika katika Refidim na wakaanza kulalamika mara moja kuhusu kukosa maji, ambapo Mungu alimuamuru Musa kugonga mwamba. Maji yalibubujika kutoka kwa mwamba na kiu yao ikatulizwa (Kutoka 17:1-6). Kugonwa kwa mwamba kulikuwa ishaya kwamba Kristo, mwamba wetu, alikuwa ateswe/apigwe kwa ajili ya dhambi za binadamu. Na hayo maji yalikuwa kama kivuli cha kutolewa kwa roho mtakatifu kimuijiza, yale maji ya uzima yanayo elezwa na Yesu : “anayeona kiu, na aje kwangu na ayanywe” (Yaohana 7:37). Ulemwamba katika jangwa uliwakilisha Masiya ambaye alikuwa anakuja kutoa roho mtakatifu.

Kisa cha “Mwamba” cha pili kilitokea karibu na mwisho wa kutanga tanga katika jangwa. Kwa mara nyingine Israeli ililalamika kuhusu ukosefu wa maji na kwa mara nyingine Mungu akawakamilishia mahitaji yao. Mara hii alimwambia Musa azungumze na jiwe, lakini katika hasira yake Musa akakosa kutii na akaugonga mwamba mara mbili (Hesabu 20:1-12). Kwa kugonga mwamba badala y a kusema na wao Musa alifanya kosa kuharibu maana ya “aina” Huu mwamba katika kitabu cha kutoka ulikuwa ishara ya Kristo katika mwili aliyepigwa kutupatia maji ya uzima, hali ule mwamba katika kitabu cha Hesabu ni ishara ya Kristo aliye kuhani mkuu wetu ambaye si wa kupigwa mara mbili bali kuzungumziwa ili atowe maji ya uzima.

Kisa cha kwanza kilitokea mwanzoni wa kutanga tanga na cha pili mwishoni; visa vyote viwili vinatoa mfano wa kuwepo kwa Yesu wakati wa wote pamoja na watu wake hivi sasa katika “kutanga tanga jangwani,” ile safari ya Wakristo kuelekea nchi ya “ahadi” ya ufalme wa Mungu.

Hivi visa viwili tulivyoangalia vilitokea katika sehemu zinazo tofautiana kabisa na kuna neno tofauti lakihebrania linawakilisha “mwamba” katika hizi sehemu tofauti. Katika kitabu cha Kutoka 17 neno linalotumika ni *Tsur*, na katika kitabu cha 20 neno linalo tumika ni *Sela*. Basi Paulo anamaanisha nini anapo sema ya kwamba “walikunywa kutoka kwa mwamba wakiroho uliowafuata”? Ni wazi kwamba Mwamba halisi wa (kawaida) haukuambatana na Israeli katika jangwa. Jibu lilosahii zaidi ni kwamba Paulo anatumia ile lugha ya mambo yanayowapata wakristo na kuilinganisha na aina yake katika Agano la Kale. Hili linaloonekana dhahiri anapozungumzia ubatizo katika mwanzo wa mjadala wake. WaIsraeli hawakupata ubatizo halisi. Kwa hakika tunaambiwa ya kwamba maji hayakuwakaribia; walipita pasipo kutota kokote katika Bahari ya shamu. Lakini lililowapata ni mfano uliokaribu sana kwamba Paulo anasema “walibatizwa kwa Musa.” Kadhalika ule mwamba haukuwafuata katika maana halisi. Ilikuwa ni kielelezo ama aina ya Kristo kuambatana na Kristo katika maisha. Hili hasa ndilo Paulo mwenyewe analolisisitiza; “haya mambo yote yalitokea kwao kihalisi” (1 Wakorintho 10:11).

Huu ushaidi ni mcache mno kuunga mkono dhana ya kwamba Paulo alikuwa anjaribu kuanzisha itikadi kuhusu Mungu/mwanadamu aliyekwisha kuwepo. Hili lingeweza kugongana na usemi wake mwenyewe kwingineko kuhusu kuwepo kwa Kristo

kama angekuwa anapendekeza ya kwamba Masiya alikuwa nafsi yenye usawa na Mungu, mapenduzi ya nguvu namna hii kutoka kwenye urithi wake wakiyahudi yangehitaji maelezo zaidi.

Tunahitaji kuepuka kuhusisha kosa la mapokeo/desturi ya imani ya Mungu aliye nafsi tatu na maandishi ya Kiebrania ya karne ya kwanza. Ukweli kuhusu kitambulisho cha Yesu ni chimbuko lake ni lazima utokane kikamilifu na habari inayopatikana katika maandishi ya kanisa la kale kama yanavyopatikana katika maandishi matakatifu. Ni rahisi sana kuanguka katika mtego wa kusoma maandiko matakatifu kutumia miwani iliyotiwa rangi ya itikadi/kanuni zilizoanzishwa kutoka karne ya pili hadi ya tano.

Kuna unabii uliodhahiri kuhusu Yesu katika Agano la Kale, lakini hakuna hata mmoja unamtenga kutoka katika upeo wa jamii ya wanadamu. Wengi watakubali ya kwamba unabii wa kwanza kuhusu mwokozi anayekuja inatokea katika kitabu cha Mwanzo ambapo Mungu alimwambia nyoka, “nitaweka uwadui kati yako na yule mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; utamkwaruza kwenye kisigino na ata kukwaruza kwenye kichwa” (Mwanzo 3:15). Ilikuwa wazi ya kwamba ni mzaliwa wa Eva aliyemwanadamu ambaye hatimaye angemshinda yule nyoka ama shetani. Wayahudi na Wakristo wote huamini kwamba huu unabii ulitamilika katika Masiya; lakini hakuna kundi katika haya linalopata chochote katika kifungu hiki kwamba Masiya alikuwa tayari hai.

Tunapomsikia Paulo akihubiria ulimwengu usio wakiyahudi ukiwakilishwa na watu wa adhina, maneno yake yanafanana na yale ya nabii wa agano kale. Akizungumza kuhusu yule Mungu Mmoja wa Israeli anasema; “yule mungu aliye umbwa ulimungu na vyote vilivyomo, ambaye bwana wa mbingu na dunia hawezi kuishi katika hekalu zilizotengezwa kwa mikono” (Matendo 17:24). Huu ni sawa na usemi wa Isaya; “mimi, niliye Bwana ndiye muumba wa vyote niliozianika mbingu pekee yangu na nikaitandaza dunia, nani alikuw na mimi?” (Isaya 44:24). Kuharibu hii imani katika Mungu iliyomsingi ya Kiyahudi na kuleta nafsi nyingine ambayo haijaumbwa kama mmoja wahusika watendaji katika uumbaji ulio katika kitabu cha Mwanzo ni adha kwa imani ya Paulo ambayo ni wazi ipo katika misingi inayoshikilia elimu ya dini ya kiyahudi hasa katika imani katika Mungu aliye nafsi moja na ibada aliye Mungu mmoja isiyo badilika.

Haikutokea hadi Karne ya Nne, zaidi ya miaka mia tatu baada ya kifo cha mwanzilishi wa Ukristo ambapo wasimamizi wa kanisa waliona kama jambo muhimu kuanzisha kanuni ya imani katika Mungu aliye nafsi tatu na kuilazimisha kwa waumini kama sharti rasmi la wanachama katika kanisa la uwokovu.

Ni lazima tuulize ni vipi, ni kwanini hili lilitokea. Waumini wengi wa leo hawajapata kujua undani wa maelezo ya kustawi kwa itikadi/kanuni ya imani katika Mungu aliye nafsi tatu. Je kama Yesu na Paulo hawakuachilia imani katika dhana ya Mungu kama nafsi moja kama ilivyo katika Agano la Kale, ilwezekanaje imani katika umungu (uungu) aliye nafsi mbili ama tatu kutokea? Hadithi ya kutokea kwa mufumo wa imani uliyo mpya wa kigeni na unayo athiri kwa upana na ya ajabu.

V. KUTOKA ULIMWENGU WA KIEBRANIA WA BIBLIA KUFIKIA KARNE YA ISHIRINI KUPITIA FALSAFA YA KIYUNANI

“Maandishi yaliotokea baada ya mitume yamechanganyika na dhana zilizo geni kwa Ukristo wa enzi ya mitume. Huu Ukristo wa mitume umepotoshwa pasipo kunuia na kuakilishwa isivyo”—G T Purves.

Kuisoma/kuichunguza fani inayo julikana kama falsafa, haitoshi kujifunza tu, kilicho aminiwa ni watu waliokuwa na fikra kuu. Lazima ujifunze kujifikiria mwenyewe kubali kitu tu, kama kinacho onekana kuwa sahihi kwako, baada ya kufikiria. Na hapo utakuwa unafanya falsafa si kujifunza tu kuihusu; utakuwa mwana falsafa.⁶⁸

Huu usia ulio sahihi unaweza kutumika pia katika mafunzo/utafiti wa elimu ya dini. Unatufanya kufikiria kuhusu jambo muhimu linalohusika na mabadiliko yalioupata Wakristo wa mitume ambapo katika mwanzo wa karne ya pili, hio imani ilishikiliwa katika mazingira ya kiyunani na Kirumi. Ukristo wa kibiblia wenyewe unatoa “falsafa”, ingawa zipo tofauti za mkazo katika kanuni za agano jipya. Unadai kufafanua kile kilicho na dhamani kamili (kwa mfano “tafuteni kwanza ufalme wa Mungu”, Mat 6:33; “kuna Mungu mmoja aliye Baba na Bwana Yesu Masiya wa pekee,” 1 Wakorintho 8:6 kadhalika); unatoa maelezo ya maana ya kuwepo kuishi na sababu kuu ilyotukufu ambayo imekuwa ikitayarishwa katika historia. hata hivyo sisi tunahusika na kuelewa swali linalo husu mabadiliko yalioupata “imani ya mwanzo iliyopatiwa mitume”, ambayo Yuda aliwasihii watu wa enzi yake wasije wakaacha (Yuda 3), tupatekujua vile ambavyo ilipata kubadilishwa pole pole na pasipo kuhusiwa chini ya falsafa za kigeni. Iwapo jambo kama hili limetokea ingekuwa ni kuambatana na falsafa inayotafuta ukweli kwamba tujitahidi kupata kilichopotea ama kufunikwa/kufichwa.

Wasiamini katika nafsi tatu zilizo Mungu wamekuwa mara nyingi wakihesabiwa kuwa kundi moja wapotovu, nao kwa upande wa pili wanawalaumu walio na imani sahihi kwa kubadilisha mwelekeo/kitambulisho chao. Hata hivyo waandhishi fulani kutoka upande wanaoshikilia imani halisi wameonya ya kwamba huenda hali isiwe nzuri sana katika hali ambapo “wakristo walijiungana na kitamaduni ya kiyunani ili wanusurike na katika juhudi ya kujipatia wafuasi.”⁶⁹ Katika muhadhara wake wa kielemu juu ya “ukristo na ubinadamu” ilitolewa mnamo 1938 Eberhard Griesebach alisema ya kwamba “katika kukumbana na falsafa ya Kiyunani, Ukristo uligeuka na kuwa elimu ya dini. Hapo ndipo Ukristo ulianguka.”⁷⁰

Tatizo linajitikeza hapa inatokana na sababu ya kwamba ingawa desturi ya imani halisi ina dai kuwa na misingi katika maandiko matakatifu. Inashikilia dhana/vipengele vinvyotokana na mchanganyiko wa maandiko matakatifu na mchango wa mawazo/falsafa ya kisasa.⁷¹ Huku kuchanganyika kwa mafikira ya kiyunani na Kiebrania kulianzishwa katika Karne ya Kwanza na ya Pili na kufuatia kwa dhana za Kiyunani kupitia kwa mapadri/makasisi wa kanisa, ambao elimu yao dini ilikuwa imeathiriwa na waliofuata

⁶⁸ Rodgers na Baird *Introduction to Philosophy* (Harper and Row, 1981), 21

⁶⁹ *Ibid.*, 5.

⁷⁰ Cited by Robert Friedmann in *The Theology of Anabaptism* (Herald Press, 1973), 50

⁷¹ Rogers and Baird, *Introduction to Philosophy*, 5.

falsafa ya Plato, ya Platinus na Poryphyry.⁷² Matokeo ya athari za Kiyanuni zinafumbuliwa kwa upana na wanaelimu, ingawa hazitambuliwi na waumini wengi: G.A.T Knight anasema:

Watu wengi leo hata wenye imani, wako mbali sana kujua msingi wa imani yao...Pasipo kujua wanategemea falsafa ya Wayunani badala ya neno la Mungu ilikuelewa dunia wanamoishi. Mfano moja wa haya ni imani inayo vuma katika Wakristo kuhusu kutokufa kwa kiroho. Waumini huchoka na hii dunia. Wamekufa moyo kuhusu maana yoyote katika maisha katika dunia ambamo kuteseka na kuudhika ndio mambo yanayotawala. Na hivyo basi hutafuta kufunguliwa kwa roho zaokutoka kwenye uzito wa mwili na hutumai kuingia katika “ulimwengu wa pepo” kama wanavyo uita, mahali ambapo roho zao zitapata baraka zisizoweza kupatikana katika mwili. Agano la Kale, ambalo ndilolilikuwa maandiko matakatifu ya kanisa la kale kwa hakika halina neno lolote la dhana ya leo kuhusu “roho” (ama ya Uyunani wa kale). Hatuna haki la kulielewa hili neno la leo katika mazingira ya “mafikira” ya enzi ya Paulo, maanake hakulitumia kuelezea alichotaka kusema Plato kwa kutumia neno hilo; alikuwa akieleza alichoeleza Isaya na alichotuma Yesu kwa kulitumia... Kuna jambo moja la hakika ambalo tunaweza kulisema hapa tilipofikia nalo ni kwamba kanuni/itakadi inayojulikana sana ya kutokufa kwa roho haiwezi kupatikana katika mafundisho ya Biblia.⁷³

Ingawa kuna maonyo haya, hata hivyo mahubiri yapendwayo sana, yanayodai jina la Kristo yanazidi kustawisha hiyo kanuni ya kuhepukia mbinguni wakati wa kifo kama roho isiyo na mwili.

Hili lalamiko ya kwamba maandiko matakatifu husomwa mara nyingi kwa miwani iliyo athiriwa na mawazo mapya ya ki-platolilifanywa pia na Niell Hamillton, ambaye alijali athari ya dhana za kiyanuni kwa kuelewa kwetu maisha yajao kibiblia (kanuni kuhusu siku zijazo: “Maoni yangu ni kwamba msimamo wa maoni katika kanisa bado unatawaliwa sana na dhana ambayo si ya Kikristo ya kutokufa kwa roho kuliko kutawaliwa na dhana uliotokana na kuwasikiza mashahidi wa Agano Jipya pasipo shaka.”⁷⁴

Ushahidi huu unatuonya kwamba tabaka mpya za kimaana zimekwisha chimbiwa katika maandishi ya kibiblia. Matukio haya ni lazima yawe na hatma ya kufunguwa kilichotunganisha na nia ya awali wa Biblia. Ni wazi kama tutatafsiri dhana mpya wa ki-ismu/lugha. Kuna hatari kubwa kwamba maana yake huenda itapotea. Kwa kweli hiyo “hadithi” ya Biblia huenda ibadilike kiasi cha kutotambulika tena. Swali linajitikeza kuhusu jinsi tunavyoipata/sikia ile sauti ya mitume, hasa hatujuwi tahamaki inayo sababishwa na urithi wetu ulio jaa athari za kiyunani katika kusoma kwetu kwa maandiko matakatifu.

Kutafsiri kwa Biblia katika lugha ya mwazo mapya ya ki-plato inaonekana kua athiri zingeni katika dhana msingi zinazohusika na maoni ya Biblia kuhusu binadamu imechangia pia kuzuia maoni ya kibiblia ya Kristo na hivyo basi ya uungu wenyewe. Hili ni jambo lililo muhimu sana maanake kanuni zinazo fafana utatu wa Mungu kuhusu mamboi yajayo baadaye, zilitokezea kutokana na jamii ya kiyanuni na kirumi.

⁷² Ibid.

⁷³ *Law and Grace* (Philadelphia: Westminster Press, 1962), 78, 79.

⁷⁴ “The Last Things in the Last Decade,” *Interpretation* 71 (April, 1960): 136.

Maswala Mapana Zaidi Kuhusiana na Ukristo.

Nguvu ya utafiti huu wa kutafuta picha ya Yesu katika Biblia na uhusiano wake na Mungu inatokana na fikra za siku nyingi kuhusu historia yenye matatizo ya Ukristo. Utafiti wa wasomi wengi wanao tazama ustawi wa kanuni/mafundisho ya Yesu kabla ya enzi ya Nicene huonyesha mara nyingi ya kwamba athari ya kupotosha iliingilia imani ya Kikristo ilipotoka kutoka kwa uvuli wa mazingira yake asilia ya kihebrania na kuingia katika mazingira yenye uharibifu ya falsafa ya Kiyanuni. Haya mageuzi yalikusisha mambo zaidi—hayakuelezea tu, uhalisi wa ukweli wa Kikristo kwa waumini ambao hawakuwa wa Yahudi. Yule Kristo wa baraza la kanisa la Karne la Nne na la Tano. Alijitokeza kama picha iliyokuwa tofauti hasa na yule yesu aliyetangazwa na maandishi wa agano jipya—ambaye angekuwa na ushahidi uliougana, ili-awe Masiya aliye ahidiwa na kupitia kwake shauri la Mungu katika dunia lingeweza kufanyika.

Dondoo fulani zilizo dhahiri zinaweza kuonyesha hoja ya kwamba imani haikuendelea vizuri ilipoanguka katika jaribu la kuazima dhana za kidini kutoka kwa mazingira yake ambayo hayakumuamini Mungu. L.W Grensted akiandika mnamo 1933 alikuwa na maoni yafuatayo kuhusu ustawi wa Kikristo:

Urithi/desturi kutoka kwa falsafa ilianguka katika njia hadaa katika karne ya pili tunamuona Justin Martyr na wengine wakitangaza Ukristo kama falsafa ya kusomwa/vyuo....Dhana ya funzo (logos) la Stowick inatambulika pamoja na dhan ya funzo (logos) la Yohana....Mtandao wa kushangaza unao endelea kukuwa ...ulikuwa ni hatari,na unabaki kuwa hatari hadi leo....Wakati huo huo lililo hatari kuliko yote ni kwamba kukanganya kukubwa ilikuwa kumeingilia itikadi/kanuni ya Mungu wa kibanafusi wa dini ya kiyahudi alikuwa amechanganywa visivyo na Mungu ambao wajakamilika wa dini ya kiyunani iliyojulikana kadhalika pamoja na dhana zilizo roho ambapo wanafalsafa wamenuia kuifanya dhana ya Mungu toshelezi kama msingi wa mafikira na kuwepo.⁷⁵

Dhana ya ukristo haikuachwa bila kuguswa wakati itikadi/kanuni ya Mungu ilipokuwa ikiumbwa upya: lakini je Agano Jipya kiwa na urithi/desturi yake katika manabii wa Israeli, inaweza kuingiliwa na falsafa ya Kiyunani pasipo kupoteza vipengele yake muhimu? Kujali kwa Filson kuna dhihirika katika usemi huu:

Chimbuku asili ya Agano Jipya halihusiani na mazingira yasiyo Kiyahudi bali na yale ya Kiyahudi na urithi wake ambayo tumeyazungumzia katika husu ya kwanza ya mhathara huu. Kanuni zetu za jadi na elimu ya dini hutuelekeza mara nyingi kufikiri katika jinsi ambayo inaongozwa na dhana zisizo za kiyahudi na hasa za Kiyunani. Tunajua ya kwamba mnamo Karne ya Pili wa *Apologists* (walinzi wa imani) walifanya juhudi kwa mfumo fulani kuonyesha ya kwamba imani ya Kikristo iliboresha kilichokuwa chema zaidi katika falsafa ya Kigiriki....Agano Jipya halijawahi kukubaliana na madhehebu ya Kigiriki na limekwisha ya pinga pamoja na falsafa zake linakubaliana hasa na mashtaka ya Wayahudi dhidi ya dunia isiyomuamini Mungu.⁷⁶

Kutorithika na hali ambavyo falsafa ya kigiriki imeharibu imani ni kwingi kiasi.Kukanya kwa Norma Snaith kunajulikana na wengi....

Kumekuwa na wayahudi wakati wote ambao walinuia kukubalina na dunia isiyoyahudi, na kadri wakati ulivyo pita hili limekuwa dini ya kiyahudi kwa wengi kama hao. Kumekuwa na wakristo tangu mwanzo walionuia hili pia. Mara nyingi

⁷⁵ *The person of Christ* (London: Nisbet and Co. Ltd., 1933), 122

⁷⁶ F. Filson, *The New Testament Against its Environment* (London: SCM Press, 1950), 26, 27

imekuwa pasipo kujuwa, lakini iwe walijua ama hawakujua, swali linahitaji kuangaliwa ni kama hili lilikuwa sawa. Msimamo wetu ni kwamba kufasiriwa mara nyingi kwa elimu ya dini ya kibiblia kwa kutumia dhana za wanafalsafa wa kiyunani kulitapakaa kwa karne nyingi na kila mahali kulihariribu kiini cha imani cha kikristo....Biblia yote imijengeka katika msimamo na mwelekeo wakihebrania; iwe Agano Jipya ama Agano la Kale. Msimamo wetu imara ni kwamba lile jambo lingehitaji kutambuliwa kwa upana na wote wanaohusika. Ni wazi kwetu, na tunamaoni ya kwamba tumewadhirishia wengine katika kurasa hizi ya kwamba kuna kuwa na tofauti kubwa mara kwa mara kati ya elimu ya dini ya kikristo na elimu ya dini ya kibiblia....Ukweli ni kwamba *elimu ya dini ya kikatoliki na ile ya kiprotestanti hazijajengeka katika misingi ya elimu ya dini ya kibiblia*. Katika zote mbili dhana ya kiyunani imefunika elimu ya dini ya Kikristo.... Tunashikilia ya kwamba haiwezekani kuwa na jibu sahihi [Kuhusu swali, Ukristo ni Nini?]. Hadi tufikie maoni yalio wazi kuhusu dhana za kipekee za Agano Jipya na la Kale na tofauti za dhana hizi na zile za watu wasiomuamini Mungu ambazo zilitawala kwa upana dhana za Kikristo.⁷⁷

Waandsihi wanaoandika juu ya Ukristo wanaweza kupatikana katika vikundi viwili. Kundi la kwanza linashikilia kwa vyovyote vile msimamo wa imani wa jadi kuhusu nafsi ya Kristo pasipo kujali fumbo la mtu (nafsi) wanayejaribu kumuelezea: Yesu....angeweza kuwa “yule mwana wa pekee” (“aliyezaliwa pekee” inamaanisha wa kipekee) na mwakilishi wa binadamu wa kweli, “Mungu aliyekamilika na binadamu mkamilifu”, akiwa na “hali” mbili katika “nafsi” moja, pasipo kukanganya kubadilika, kugawika ama kukatika (Nukuu kutoka katika uwamuzi wa kiimani/itikadi wa kikao cha Chalcedon) [451AD]. Yesu alikuwa “mtu/nafsi” sio “mtu fulani/nafsi fulani”, nafsi ya utu wake, na ubinafsi wake vilikuwa na utukufu, vilikuwa vimekwisha kuwepo na vilichukuwa umbo na kutumika katika mwili wa biadamu; “alikuja katika historia wala hakutokana na historia”, alikuwa Mungu katika binadamu na akifanya kazi katika binadamu wala hakuwa mwanadamu aliye pandishwa kwa kiwango cha utukufu utu/uume wake haukupungua kwa vyovyote alikuwa, amehusika katika “maingiliano” kikamilifu, hata kama alikiri mipaka ya myahudi wa wakati wake na mahali alipoishi....Mwelekeo huu tunmaweza kuona kama uliokauka wa kiusomi na mgumu kufanyika (wa kifumbo). Hili linatokana na mwelekeo wetu, ule wa dhana ya kiyunani....Yesu na wanafaunzi wake hawakukubali tu ibada ya Mungu mmoja wa kiyahudi pasipo kuuliza bali pia alithibitisha kwa kunena (Marko 12:29 ff) Imani katika Mungu mmoja aliye muumba ndio msingi wa imani ya Kikristo, na inatubidi tuzingatia, kutoka mwanzoni, dhana yoyote ya kwamba itikadi/kanuni ya utatu wa Mungu haishikili ama inabadilisha.⁷⁸

Kwa upande mwingine wengi, kufuatia historia ya Kikristo, wameshangaa kama fafanuzi hizi za kiitikadi ya jadi kuhusu nafsi Kristo zinaweza kuingizwa kwa urahisi katika imani ya Yesu ilio ya ibada ya Mungu mmoja kama inavyonakiliwa na Marko (12:29 ff). Thomas Hart, msomi wa kanisa ya kikatoliki wa wakati wetu/uliopo ana hariri ukristo wa imani ya jadi kwa kukumbusha ya kwamba:

⁷⁷ *The Distinctive Ideas of the Old Testament* (London: Epworth Press, 1944), 187, 185, 188, emphasis added

⁷⁸ R. J. W. Bevan, *Steps to Christian Understanding* (Oxford University Press, 1958), 140, 167.

Yesu anaitwa mwanadamu katika jinsi ya kuhusishwa, si kwamba alikuwa mtu. Yuko na jinsi ya binadamu lakini si nafsi ya kibadamu. Ile jinsi iliondani yake ni ile nafsi ya pili ya utatu uliobarikiwa. Hivi ndivo baraza [Chalcedon] linavyozunguka utata kuhusu nafsi iliogawika.

Anaendelea kuchunguza:

Upungufuambao wanaelimu ya dini wanaupata katika ule muundo wa Chalcedon...1. Jinsi ilio tukufu na jinsi ya kibadamu haziwezi kusmamishwa pamoja na kuhesabiwa kana kwamba zingekuwa takrimu zilizo sawa. 2. Mtazamo wa Chalcedon unafanya uhalisi ubinadamu usiwezekane. [Huu ugumu] unatokana na kugubikwa kwa ubinadamu na utukufu na pia unatokana na Yesu kutokuwa na kiini kisicho kuwa nafsi ya binadamu...3. Mwelekeo wa Chalcedon unamsingi duni katika maandiko matakatifu. Hilo baraza linamuita Yesu Mungu wa kweli. Agano Jipya lilichelea kumuita Yesu Mungu.⁷⁹

Tatizo la Lugha

Matatizo mengi hutokea kutokana na pendekezo la kidesturi/mapokeo kwamba Yesu ni “Mungu” katika ile hali inayohitajika na imani/itikadi za jadi. Kwa kweli Agano Jipya linatupatia huu ufafanuzi wa mwokozi, ama ni kwamba tulielea vibaya hio habari na hivyo basi kuupotosha ujumbe wa ukristo katika agano jipya? Huenda labda kuna kizuizi cha mawasiliano kimaana kati kati ya desturi ya usomaji wetu na maneno muhimu katika Agano Jipya na ile nia ya awali ya wale waandishi wa maandiko matakatifu?

Muingereza anayetembelea Marikani na kusema ya kwamba “Mad about his flat” (Amekasirishwa na nyumba yake/ameipenda kupita kiasi nyumba yake asitegemee kueleweka. Hisa kama hiki kinaweza kuwa mfano mzuri wa usemi wa Shaw kwamba Uingereza na Marikani ni nchi mbili zinazotenganishwa na lugha moja zinazoitumia zote mbili. Katika Uingereza muingereza atakuwa anawasilisha wazo la kwamba “anaipenda kupindukia nyumba yake.” Katika upande w apili wa nahari ya Atlantiki itafikirika ya kwamba “amekasirishwa na tairi ilioisha pumzi.” Hali nyingine kama ya kutowasiliana hutokea iwapo muingereza atatangaza huko kwamba Tom na Jane “have broken up” wamerekani watafikiria ya kwamba hao wawili wametamatisha uhusiano wao. Huko uingereza haya maneno inatuarifu ya kwamba mhula wa shule yao imekwisha.

Mwamerika/Mmarekani aliulizwa huko uingereza: “Do you want a pie?” Hili swali lilitoka kwa mtu anayepelekea maziwa ambaye huko uingereza hujulikana kama Milk Man, ingawa hili neno halitakuwa na maana kubwa huko Marekani ambapo maziwa hununuliwa katika maduka makubwa. Huyu mwamerika/mmerekani alishangaa kwamba muuzaji maziwa angekuwa akiuza mkate ulioshindiliwa nyama hadi alipotambua ya kwamba alichu maanisha muingereza katika kugubikwa kwa usemi wake la fudhi ya kicockney ilikuwa “Do you want to pay?” Hapa tena kutooleanwa kukuu kukatokea kwa sababu ya matumizi ya upande mmoja ya maneno yalikuwa ni mageni kwa yule aliyemzungumzia.

Hali ilio sawa ya kutooleanwa/kutoelewa hutokea wasomaji wa Biblia wanapokuwa hawaielwi vilivyo lugha ya waandishi wa Agano Jipya. Hili halimanishi ya kwamba kila mmoja anahitaji kujifunza Kiyunani. Hata hivyo wanahitaji kuelewa ya kwamba Wakristo Waebrania wa Agano Jipya hawatumie maneno kama vile tunavyotumia katika Karne ya Ishirini (sote tunatambua ya kwamba kutoka tafsiri ya “King James”, ama Authorised Version ilipofanyika mnamo mwaka wa 1611, maneno mengine yamebadilika kabisa kimaana) ili kuisoma Biblia kwa hekima tunahitaji kuingia

⁷⁹ *To know and Follow Jesus*, 44-48

kimawazo katika ule ulimwengu wa Karne ya Kwanza. Tunahitaji kuyaelea maneno kama walivyoyaelewa. Kama hili halifanyiki huenda tuelewe visivyo ili imani ambayo mitume waliniuia kutuwazilishia.⁸⁰

Neno/Istilahi “Mungu” na Swala la Utatu wa Mungu Katika Yohana

Waandishi wa Biblia wanamaanisha nini kwa mfano wanapotumia “Mungu” neno muhimu sana? Je wanamaanisha, kama sisi pia nafsi tukufu ambao haijaumbwa na ambayo ilikwisha kuwepo wakati wote? Mara nyingi Mungu ndilo jina la ile nafsi ilio kuu.⁸¹ Lakini je neno “Mungu” liko na maana nyingine katika Biblia?

Iwapo tutatoa taarifa ya kwamba tulijulishwa kwa “Rais” ingeweza kufikiriwa ya kwamba tulikutana na Raisi wa Marikani. Hata hivyo inawezekana kwamba muktadha wa usemi wetu unawezeshe wanao tusikiza kuelewa tunachosema kwa mfano awe ni Rais wa Banki. Kwa bahati nzuri hapana nafasi kubwa ya kutooleanwa sote tunaolewa ya kwamba neno Rais inaweza kutumika katika viwango mbali mbali. Hatusemi hii neno linalo maana pana (inayopanuka) lenye na uwezekano wa kuzungumzia (watu) nafsi zilizo katika nyadhifa mbali mbali. Neno lenyewe halina maana maalum. Maana yake inaamuliwa na muktadha. Hatuta mchukulia mtu yeyote kuwa mwenye akili nyingi iwapo atasisitiza ya kwamba “Rais” wakati wote na pasipo mabadiliko humaanisha “Rais wa Marekani.”

Ikiwa tutasoma Biblia tuliwa na msimamo wetu wa karne ya ishirini ya kwamba neno “Mungu” pasipo mabadiliko humaanisha nafsi aishiye milele na ambaye haukuumbwa, tutaingia taabani kuhusu 2 Wakorintho 4:4, ambapo shetani anaitwa “Mungu” inahitaji kusawazishwa ili kuidhinisha maana ya pili ya Mungu, ambayo haitachanganyika na matumizi ya Mungu kama nafsi ilio kuu kuliko zote. Katika Yohana 10:34 tunapata “miungu” katika hali ya wingi. Tukichunguza muktadha tutatambua kwamba Yesu hapo alikuwa akizungumzia viongozi wa Israeli kama “miungu” walikuwa wawakilishi wa Mungu na Mungu alinena neno lake nao, na hivyo basi walipatiwa

⁸⁰ Mtu aliyekwisha kuwa kiongozi wa kanisa la “Church of England” alitoa hoja hii kwa njia ya kipekee alipojisikia ya kwamba hangeweza kumudu maandiko aliwajibika kutafsiri. David Watson aliandika : “Uchunguzi unaozingatia pande moja wa dini wa jadi ya kiyahudi umeweza kudhihirisha kiasi ambacho mukristo muingireza wa hivi leo huyapatia maana maneno ya Agano Jipya *Yaliotofauti na ile iliyokuwa katika mawazo ya waandishi wakiyahudi* walitumia lugha ya kiyunani kuwasilisha ujumbe wa Kristo kwa wote. Lakini mwelekeo wao wakimawazo ulikuwa wakihebrania kwa sehemu kubwa. Ili kuelewa kikamilifu ni muhimu kwa mkristo wa leo kusoma maandishi ya kigiriki na hilo pekee halitoshi anahitaji kutambua dhana ya kihebrania walionuia kuwasilisha hawa waandishi wa kiyahudi katika maneno ya kiyunani. Siwezi kudai kuwa nimekuwa mjuzi sana katika hili jambo, lakini nimepiga hatua hadi. *Nikatambua nilikuwa nimeifasiri biblia zamani visivyo kabisa* kama wahubiri wengine wowote wakikristonilizungumza kwa kufuata kanuni na mamlaka nikiwakwenye madhabawa ambapo mtu hawezi kusimama pasipo idhini ya Askofu; na mengi ya yaleniliokuwa nimesema yalikuwa ya kupotosha kwa sababu akili yangu haingiweza kutafsiri sahihi kitabunilichokuwa nimeidhinishwa kufafanua. Kwangu mimi kutambua jambo hili kulifanya nione kama mzaha tofauti iliopo katika viongozi wa kanisa wa wafuasi ambao hawajaelimika kidini, na ndio hasa na ndiko kuliko nielekeza kujiuzulu kutoka kwa kazi yangu. Kwa kuelezea upungufu wa hekima yangu mwenyewe na jinsi nilivyotambua ambavyo singeweza kuelewa maana ya biblia kwa sababu ya mwanya mkubwa ulionitenga na waandishi wake wa kiyahudi, naweza kudai kwa hakika ya kwamba nina andika kwa ushahidi usio wa kushuhudiwa kulingana na yale ninayo jua kuhusu viongozi wa makinisa/wahubiri kwa jumla sione sababu ya kuchukuliwa ya kwamba nilikuwa peke yangu katika huuukosefu wa hekima. Kwa kuema kweli mamlaka ya huduma ya kiprotestanti kwa jumla—liledai la kuelewa biblia na kuifafanua kama neno la mungu kwa maoni yangu ni ujanja mkuu wa kuonyesha uhakika. Si walaumu viongozi wa dini kuwa Wadanganyifu ama wanafiki. Huu ujanja wa kuonyesha uhakika unawahusisha walio wengi; kibanafsi wanohusika hudanganyika na huo ujanja kama mimi tu nilipoanza kufafanua biblia kwenye madhabau, nilikuwa na hakika kabisa kwamba ningeweza kutoa tafsiri iliyo sahihi.

⁸¹ “*Ho theos*”, kwa mfano, yule Mungu mmoja linamzungumzia aliye baba katika Agano Jipya mara 1325.

jina/wadhifa wa utukufu (Zaburi 82:6). Lakini hakuna mtu angewafikiria kuwa “miungu” katika ile maanaya mungu aliye mmoja. Mwandishi wa kiyahudi wa karne ya kwanza kwa jina Philo anaongea kuhusu Musa kama “mungu na mfalme”: “Si Musa pia alifurahia ushirika mkubwa wa aliye Baba na muumba wa mbingu, akichuliwa kustajili jina (wadhifa) hili hili? Kwa maana alitwa mungu na mfalme [*theos kai basileus*] wa taifa lote.”⁸²

Maneno ya Tomaso akizungunza na Yesu katika Yohana 20:28 yanosomeka: “Bwana wangu na Mungu wangu” Kwa maana wasomaji wengi wa Biblia wamefanywa kuamini ya kwamba Yesu ni “Mungu” katika jinsi ambayo tunatumia hili neno katika karne ya ishirini wanakimbilia kumaliza ya kwamba hivi ndivyo Tomaso alivyo maanisha. Kwa hivyo Yesu ni lazima awe ni nafsi iliyokwisha kuwepo ishio milele. Lakini iwapo Yesu ni “Mungu” aliye nafsi kuu kuliko zote kwa nini amuite Baba yake “Mungu wangu” katika msitari michache iliyotangulia na hali wakati huo huo akisema “Mungu wenu”... Mungu wa wanafunzi wake. Yesu alipokuwa akimuita aliye Baba “Mungu wangu” (Yohana 20:17) alitambua ya kwamba alikuwa mdogo/chini ya mamlaka ya Mungu, aliye Baba. Yesu kwa hivyo si mungu aliye nafsi kuu kuliko zote. Kwa Tomaso pia Yesu ni Mungu katika njia ya kuidhinishwa kama Masiya, aliye mjumbe mkuu wa kisheria wa yule Mungu mmoja. Yule aliyeitwa Mungu wa Tomaso ni mdogo wa yule Mungu mmoja aliyeitwa na Yesu Mungu wake. Hivyo basi ikieleweka vizuri Yesu anabaki katika kiwango cha Masiya mwana wa Mungu, kiwango ambacho Yohana anakiweka wazi katika kitabu chake chote kuna hoja mbili kuu zilizo msingi wa mtazamo wote wa Yohana kuhusu ukristo: Yesu anaaminiwa kama “Masiya, Mwana wa Mungu”, hali wadhifa wa babake wa kipekee ukihifadhiwa kama “Mungu aliye kweli pekee” (Yohana 17:3) na yule ambaye ni Mungu pekee yake (Yohana 5:44).

Ni muhimu sana kwamba yule Masiya aliye ahidiwa alipatiwa jina/wadhifa Mungu katika Zab 45:6: “Kiti chako cha enzi, ewe Mungu, ni cha milele na milele” katika msitari unaofuatia inadhihirishwa kwamba huyu “Mungu Masiya” amekwisha kubarikiwa na Mungu wako amekupaka mafuta (amekuweka wakfu)...⁸³ Heshima iliyokubwa kabisa Yesu alipatiwa na Tomaso alipoongea akitumia majina (nyadhifa) ya kifalme ya Masiya “Bwana” na “Mungu”, yanatokana katika zaburi 45:6,11. Ushahidi wa Agano Jipya ya kwamba Yesu ni Mungu katika maana iliyo sawa na Mungu aliye Baba ni nadra sana ikiwa tutazingatia sehemu za Biblia zinazotumia jina Mungu. Tutaona ya kwamba liketumika kuhusu Mungu aliye Baba zaidi ya mara 1325 katika Agano Jipya, ambapo “Mungu” linatumika kuhusiana na Yesu mara mbili tu. Kwa uhakika kamili (kwingineko kuna shaka kama jina Mungu limetumika kuhusiana na Yesu, na hili ni dhahiri kwa sababu za kisarafu na mpangilio wa maandishi). Hoja hizi zinapendekeza ya kwamba matumizi machache la jina “Mungu” kuhusiana na Yesu yamekuwa matumizi maalum. Ni wazi basi ya kwamba huenda litakuwa jambo lakupotosha kusema kwamba “Yesu ni Mungu” katika karne ya ishirini, isipokuwa tuelewe kwanza Yohana analitumia neno hili katika maana gani (na Tomaso anaye mnakili). Matumizi yetu ya maneno haya kwenye Biblia hatuitaji kutegemea tu matumizi ya neno pasipo kuzingatia maana yake. Na zaidi ya hayo ni lazima tuwe tayari kutoshikilia imani ya kisisitiza kukubali itikadi/kanuni pasipo kuuliza. Hii jinsi ya kushikilia imani katika njia fulani ambayo tumejifunza kwa muda mrefu pasipo kupinda huzuia kutafuta ukweli na hivi ndivyo ukristo unavyo kuwa ulivyo (Matendo 17:11)

⁸² *Life of Moses*, 1:155-158.

⁸³ Wahebrania 1:8 inakili Zab 45:6 inatumia jina Mungu kuhusu Yesu likitumika kwa njia inayo kubalika.

Maoni ya Wasomi Kuhusu Athari Mbaya Za Falsafa.

Falsafa ya mawazo huru ya karne ya kumi na tisa ilizusha swala la athari zisizofaa za falsafa ya kiyunani katika imani ya mwanzo. Ardolf Harnack anayependwa sana alihimiza ya kwamba injili iligubikwa na kuingizwa uyunani mwingi ambao ulisababisha fikra za kimila kuhusu Kristo. Shauku ya kumtenga Yesu na mafundisho yake kutokana na nyongeza za falsafa ya kigiriki ilichangia uhuru mzuri wa kutafuta mawazo mapya. Kwa bahati mbaya falsafa ya mawazo huru ilitawisha dhana zake yenyewe. Huenda tushuku ya kwamba elimu yake ya dini (falsafa ya kigiriki) wakati mwingine ilikuwa hasa jaribio la kujihakikishia kwamba imani yake ya wakati wake ilikuwa imegusiwa katika mafundisho ya Yesu wala haikuwa kurejea vilivyo kwenye imani ya mitume. Inaonekana ya kwamba wazo la dunia ya kihebrania kuhusu biblia lilibaki bila kupendwa.

Roho ya ukweli na roho ya kustahimili haziwezi kuwa sawa hata hivyo stahimili inapowezesha kuuliza kwa uhuru na kutenga kando misimamo ya kiesturi ukweli unaweza kujitokeza. Msimamo ya “kiuhuru” ulitengeneza mazingira ambamo itikadi/imani ya kiesturi zingeweza kuzungumziwa/kurekebishwa hali ya kupima upya kila sehemu ya imani iliwezesha kuzingatia jinsi ambavyo mambo ya kiroho ya kiyunani ya enzi iliyofuata baada ya kuandikwa kwa biblia yalisababisha kupotea kwa Kristo wakibibilia. Kulegezwa kwa kamba iliyoshikiliwa na kanuni za jadi/kiesturi kumedhihilisha matokeo mema ya mafundisho ya ndini ya enzi iliyofuata enzi ya uwongofu/mwangaza (Post elightment). Kutorithika na fafanuzi ya Yesu iliyotolewa Nicean/Chalcedon kunmekuwa kukijitokeza mara kwa mara. Kutafuatwa kwa Yesu wa historia kumeendelea hadi wakati wetu wenyewe. Kulipata nguvu mpya wakati katibu kiitwacho “*Myth of God Incarnate*” kilipochapishwa mnamo 1977.⁸⁴

Harnack hakukosea alipoonyesha tatizo la kutia uyunani katika imani ya mwanzo iliyo husika na kihebrania kinacho sababisha vikundi vingi vya kisasa niya ‘kiinjili’ (Protestanti) kuona ya kwamba kupingwa kwa kanuni ya utukufu wa Yesu unao dumu milele pamoja na Mungu ni sawa kushambulia maandiko matakatifu yenyewe, ni kutoweza kubainisha kati ya kilicho kweli kulingana na maandiko matakatifu na kilicho desturi/mapokeo. Ingawa vikundi vya kiinjili (Protestanti) vinasimama chini ya mwito wa *Sola Scriptura*, wakati mwingine haviwezi kubainisha maandiko matakatifu na tafsiri za maandiko matakatifu za kiesturi. Lindbeck anatoa onyo anapoonyesha ya kwamba “waprotestanti wengi wanaoshikilia Biblia wanafuata mafundisho ya utatu wa Mungu ya enzi iliofuata baada ya kuandikwa kwa Biblia, lakini wanafanya kana kwamba mafundisho haya yanaudhahiri ya kibiblia.”⁸⁵ Maoni ya F. F. Bruce yenye ujanja yanahitaji kuzingatiwa kwa karibu : “watu wanaoshikilia imani katika Biblia pekee (kama wanavyo sadiki) huwa mara nyingi kwa kweli wanaskiwa mfumo wa tafsiri wa kiesturi wa *Sola Scriptura*. Waprotestanti wa kiinjili wanaweza kutumikia desturi kama vile wakatoliki, au kama wafuasi wa Greek Orthodox, ni vile tu hawatambui kwamba ni desturi.”⁸⁶

Kwa Michael Servetus na yule mholanzi Annabaptist akiongozwa na Adam Pastor pamoja na jamii yote ya Annabaptist wa Kipoland, utstu wa Mungu ulikuwa ni potevu kutoka kwa ibada ya Mungu mmoja ya kibiblia, jaribio liliokuwa kosa la kutafsiri imani ya mitume katika Mungu mmoja, aliye Baba,⁸⁷ katika lugha ya kiroho ya kiyunani.

⁸⁴ Toleo John Hick (London: SCM Press, 1977).

⁸⁵ *The nature of Doctrine and Religion: Theology in Postliberal Age* (Philadelphia :Westminster Press 1984), 74.

⁸⁶ Kutoka kwenye nyaraka tarehe kumi na tatu mwezi wa sita, 1981.

⁸⁷ 1 Wakorintho 8:6;1 Timotheo 2:5;Yahana 17:3;Waefeso 4:6.

Isitoshe itikadi/imani ya mabaraza ya Nicean na Chalcedon yalitumiwa katika njia ya kusukumiza na kuharibu ili kulazimisha imani katika kanuni hizi. Hili ni jambo lenye majuto kwa sababu maneno yanayotumika katika mjadala kuhusu ukristo ni mchanganyiko yasio na maana sahihi—jambo lillilo kinyume na imani/itikadi ya Biblia ili dhahiri kuhusu ibada ya Mungu aliye nafsi moja.

Ijapokuwa kulikuwa na “uwongozi wa mabavu” wakikanuni (ukiwakilishwa kwa mfano na itikadi ya Athanasia iliyotishia kuuwa mtu yeyote ambaye hakukubaliana na kanuni/imani ya utatu wa Mungu). Uhuru wa kutafuta ukweli ulielekeza kutambulika tena kwa kipengele kimoja kinacho sahalika mara kwa mara katika jinsi ambavyo kanisa huwasilisha Yesu—binadamu wake. Lilikubalika kwa upana ya kwamba kueleweka kwa Yesu kulingana na desturi kulikumbwa na shida ya “docetism” iliyofichika (imani ya kwamba alionekana kana kwamba alikuwa mwanadamu) jambo ambalo kwa mtume Yohana, liliashiria sana “mpingaji wa Kristo” (1 Yahana 4:2; 2 Yohana 7). Zaidi ya hayo maoni ya kidehuri kuhusu Yesu yalionyesha kupendelea fasiri fulani ya Yohana 1:1, isiyoshikilia picha ya kibadamu ya Yesu iwasilishwayo na Mathayo, Mariko, Luka na Matendo ya mitume. Kusema kweli injili ya Yohana imeruhusiwa sehemu kubwa kuliko inavyostahili katika kuadhiri mwanzo wa ukristo. Je hili lingekuwa limesababishwa na mtindo wa maandishiwa Yohana, ambao ingawa ilikuwa wakihebrania kweli ulivutia mawazo ya kukisia ya kiyunani na ungeweza kutoeleweka kwa urahisi pamoja na kupotoshwa na watu ambao hawakuwa wayahudi?

Tunaonelea ya kwamba huu mwelekeo wa kuficha hoja ya kwamba Kristo alikuwa mwanadamu ulitokea katika kupinga thibitisho lililo msingi na rahisi la Agano Jipya la Yesu “kama Masiya”, Adamu wa pili aliyemzaliwa kwa njia isiyo ya kawaida na hali akiumbika katika tumbo la mamake. Haya maoni kuhusu chimbuko la Yesu tunaweza kuyaita “chimbuko la ukristo” katika namna ya matumizi kwa kukubaliana na Raymond Brown.⁸⁸ Brown anasisitiza ya kwamba Mathayo na Luka hawakujua chochote kuhusu kuwepo kimbeleni kwa Masiya.⁸⁹ Hivyo basi hawangeweza kuamini katika nafsi tatu zilizo Mungu katika njia ya desturi. Kuwepo kulianza alipoumbika katika tumbo la mama yake. kiini kibaya cha baadaye cha elimu ya dini ya utatu wa Mungu kingehitaji kutafutwa mahali pengine wala si ndani ya haya maelezo ya kiinjili. Je kihusishwe na Yohana ama Paulo? Ama kihusishwe na kupotoshwa kwa maandishi yao kuliko sababishwa na hali ya kukisia ya falsafa ya kiyunani? Athari hii ilikuwa imekwisha kuwepo wakati wa Yohana, akiandika mwishoni mwa karne ya kwanza anapositiza ubinadamu wa Yesu dhidi ya Gnostic dhana ya kwamba Yesu alionekana kana kwamba alikuwa mwanadamu (1 Yohana 4:2; 2 Yohana 7). Alikuwa *en Sarki*, “kama nafsi ya binadamu” wala hakuingia katika mwili wa binadamu” ambayo ni mambo mawili yalio tofauti sana. Katika waraka wake wa kwanza inaonekana kana kwamba Yohana anakosowa kutoeleweka kunako jitokeza katika “mafundisho” yake (“*logos*”) ya kanuni katika injili (Yahana 1:1-3). Ni nafsi isiyo husika (impersonal) “uzima wa milele” ilio kuwa “na aliye Baba” (1 Yohana 1:2) kabla kuzaliwa kwake Yesu, wala si mwana mwenyewe akiwepo mbeleni. Kwa kunena vingine Yohana alinua tuelewe ya kwamba Neno lilipokuwa mwili (Yohana 1:14) haya mabadiliko *hayakuwa nafsi tukufu kuwa nafsi ya biadamu, ila ya kwamba ambacho hakikuwa nafsi kilichokuwa hali ya nafsi (cp hekima katika Methali 8:12,30)—“Neno” la Mungu—likibadilika na kuchukuliwa/kubebwa katika hali ya binadamu/kama mwanadamu.*

Kustawi kwa fikra ya utatu wa Mungu kuliko fuatia kuliitwa nguvu na kutoelewa kwa ili dhana ya kihebrania ya “Neno” ya Justin Martyr. Kwa Yohana, *Logos*

⁸⁸ The Birth of the Messiah, 150 fn 52

⁸⁹ Kama hapo juu, 31 fn 17

haikumanisha nafsi ya pili katika uungu bali kitendo cha Mungu akijielezea mwenyewe. Justin, ambaye alishikilia falsafa ya kiplato (platonogist) alikuwa ameshikilia desturi ya kufikiria logos kama mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu. Si ajabu kwamba kwa kulingana na dhana ya logos anamfikiria Yesu kuwa Mwana aliyekuwapo nafsi iliyotofauti na Mungu kitakwimu na iliyochini ya Mungu aliye mmoja, kisha Justin anaendelea kumtafuta Yesu katika Agano la Kale, hata kufikia kumtambua kama malaika wa bwana kabla hajachukuwa utu wa binadamu. Hata hivyo mafikira ya Justin bado yako mbali msimamo wa kiimani/kanuni wa mwisho wa baraza la Chalcedon. Hoja muhimu ya kuchukuliwa hapa ni kwamba imani ya utatu wa Mungu iliyokwisha stawi haiwezi kupatikana katika Agano Jipya kupitia kwa viongozi wa kale kabisa wa kanisa. Hawa viongozi walifikiria wakati wote kwamba alikuwa mdogo wa yule Mungu mmoja. Wengine waliamini kwamba yule mwana alikuwa na mwanzo.

Falsafa ya kiyunani uliweza kuingilia mafundisho ya kibiblia katika injili ya Yohana kulielekeza katika kumpanua Yesu na kumuingiza nyuma katika huyu “logos” aliyekwisha kuwepo. Hivyo basi ukristo wa kimasiya uliyo rahisi wa vitabu vya injili vitatu vya kwanza na pia ule wa Yohana (iwapo hasomwi katika mwelekeo wa makisio ya kiyunani) ulikuwa umefunikwa. Imekuwa wajibu wa wanaelimu wa dini wa Cambridge katika maandishi *Myth of God Incarnate* kuzusha swali kama “mazungumzo ya kuwepo mbeleni kwa Yesu kunahitaji labda katika hali zote kueleweka katika maelezo ya kuweko mbeleni kwa torati ilikuonyesha lengo la milele la utukufu ambalo linafikiwa kumpitia yeye [cp 1 Petero 1:20], wala si kuonyesha kuwepo mbeleni kwa mmoja aliyekuwa nafsi kamili”⁹⁰

Kama huku ndiko kuliko sahihi basi maoni ya John Robinson kuhusu jinsi Yohana anavyomchukulia aliye Baba:

Elimu ya dini ya watu wa kale katika vikundi vyote ilitumia vibaya haya maandishi ya [Yohana] kwa kuyachukuwa nchi ya muktadha na *kuyapatia maana ambayo Yohana hakuyanua*. Wajibu wa lugha kuhusu mwana na roho wakitumwa na baba katika ulimwengu uligeuzwa na kuwa ule wa uhusiano wandani wa milele katika nafsi zilizo katika uungu na maneno kama “kizazi” na “maandamano” ya kufanywa kuwa istilahi ambazo matumizi yake katika Agano Jipya hayawezi kuelezeka.⁹¹

Malalamiko kuhusu jinsi Yohana anvyotumia vibaya dhana ya “Neno” yamekuwa yakisukumwiwa mafichoni. Wakati umefika wa sauti kuu kusikika. Mnamo mwaka wa 1907 Profesa wa mfumo wa elimu wa dini Jena huko Jerumani alitoa maandishi yake *System der christlichen lehre*, yalio kilele cha mafikira yake katika maisha yake yote kuhusu jinsi ya imani ya kikristo. Pamoja na maandishi wajulikanao wengi waliokuja baadaye huyu Profesa alionyesha shida ya imani katika Mungu aliye nafsi tatu inayotokea wakati “Neno” katika Yohana moja inapotumiwa katika maana ya nafsi ama kiumbe cha pili badala ya kuwa neno la kunafsisha la hekima na uumbaji wenye lengo wa huyu Mungu mmoja. Hakuna nafsi tatu za Mungu zinazo patikana katika utangulizi wa Yohana iwapo “Neno” linaandikwa katika herufi ndogo “n” na iwapo litafikiwa kuwa kama njia ya kueleza nia ama mpango wa Mungu wala sio aliye mwana wa Mungu (katika kiwango hicho).

⁹⁰ Maurice Wiles, *the Remaking of Christian Doctrine* (London: SCM Press, 1974), 53. Cp Wiles observation in *The Myth of God Incarnate*.

⁹¹ “Kitabu cha injili cha nne na kanuni ya kanisa ya utatu ya Mungu” *Twelve More New Testament Studies* (London: SCM Press, 1984), 172, kuongeza mkazo.

Hans Wendt wa Jena analitia swali hili katika ufafanuzi wa ndani. Anaonyesha ya kwamba wakati neno linaeleweka katika maana ya Kiebrania kama kitendo cha uumbaji cha Mungu—kwa kutegemea linavyotokea katika maana hii pasipo kubadilika katika agano la kale—Hakuna sababu yoyote ya kufikiria ya kwamba Yohana alimaanisha kusema : “Hapo mwanzoni palikuwa na Mwangu wa Mungu wa milele pamoja na Mungu na huyu Mwana alikuwa na Baba na Mwana alikuwa Mungu.” Tafsiri kama hii inakanganya dhana kuu na inayoshikilia zote ya ufunuo/uvumbuzi wote kwamba Mungu ni nafsi iliyo moja. Iwapo Neno ni Mwana katika hali yake kabla hajakuwa binadamu, basi Baba na Mwana wanastahili kufikiriwa kwa usawa kuwa Mungu mkuu. Hata hivyo mwelekeo huu uliharibu sana imani katika Mungu mmoja ya Biblia ya Kiebrania, hio imani katika Mungu mmoja ambayo Yesu alikuwa amedhibitisha mbele ya watu (Mariko 12:28, 29) wakiwepo wanafunzi wake mwenyewe na msomi wa dini aliyeuliza Kama “neno” katika Yohana moja itachuliwa kumaanisha “neno la Mungu”, ni dhahiri kwamba Yohana anafiriria neno la kuumba katika mwanzo moja 1:23, Zab 33:6, 9: 19:103—105. Hatua hatari ilichukuliwa, anasema profesa Wendt, wakati “neno” katika utangulizi wa Yohana lilipoeleweka katika maana ya kialexandria na kiphiloni kama mpatinishi kati ya Mungu na mwanadamu, wala si katika maana la msingi wake wakihebrania.

Msitari wa kwanza wa injili ya Yohana ambao ungefanana kama falsafa ungeweza kueleweka na myahudi ama mkristo aliye elemika pasipo kuhusishwa kokote na Philo. Kwa hivyo hatuitaji kubishana katika maana ya Philo ya “neno” kama hypostasis kwamba Yohana alimaanisha pia Mtu/nafsi iliyokwisha kuwepo alipotumia “neno” katika sehemu iliyo salia ya hio injili na katika 1 Yohana, “neno” si kueleweka katika maana ya ubinafsi...Linamaanisha hasa kuvumbuliwa kwa Mungu ambako ilikuwa kumepatiwa Israeli (10:35) ilikuwa kumewajiwa wayahudi katika maandiko matakatifu (5:38) na ambao ilikuwa umepatiwa Yesu na akaupitisha kwa wanafunzi wake 8:55; 12:48; 17:6, 8, 14, 17; 1 Yohana 1:1) na ambao ilikuwa huifadhiwe nao (1 Yohana 1:10; 2:5,14). Neno linazungumziwa kwamba linakuja katika ulimwengu katika njia yenye kunafsisha kidogo (1:9-14). Huu mteno wa kunafsisha unaoatikana sana katika Agano la Kale linayozungumzia neno (Isaya 55:11; Zab 107:20; 147:15; c.p 2 Wathesolonike 3:1) haiwezi kuthibitishwa kwamba mwandishi wa utangulizi alifikiria neno kuwa nafsi/mtu hasa. Ni yule Yesu wakihistoria tu anayesemekana kuwa mwana wa la si neno la mwanzo (asilia) (Yohana 1:14, 18). Lakini katika huyu mwana ulidumu uvumbuzi/ufunuo wa Mungu na kufanya kazi.⁹²

Profesa Wednt anaendelea kuonyesha ya kwamba kuunganishwa kwa Yohana na Philo kama inavyoonekana hakuwezi kuelezwa kwa matumizi yake ya dhana ya falsafa ya Philo kuhusu neno. Ukweli ni kwamba huyu mtume anajaribu kukataa kuingizwa kwa falsafa ya Philo na wawakilishi wa fikra za kialexandria ambao mapema zaidi walikuwa wapinga ukweli kwa kusia kwao (c.p Matendo 18:24-28). Yohana aliuelekeza utangulizi wake kwao. Kinaya cha historia ni kwamba kanuni ya dini za jadi ziliangukia makisio haya haya ya kifalsafa, na kupendekeza “Mungu wa pili” aliyekwisha kuwepo, na akatumia Yohana kuunga mkono huu msimamo tofauti na ibada ya Mungu mmoja! Tafsiri za kisiasa za huu utangulizi zinazo andika neno kwa herufi kubwa na matumizi ya vijini vya logos katika jinsi ya kiume. Ni ushuhuda uliobaki wa falsafa ya kiphiloni ya kigiriki ambayo imeikanganya imani ya kihebrania ya agano jipya. Kitabu cha Yohana

⁹² *System der Christlichen Lehre* (Göttingen: Vandenhoeck und Ruprecht, 1907), Pt. 2, ch. 4, 353, 354. Utafsiri kutokea kwa Ujeremani ni wangu.

kimepindwa na kutoeleweka na kilicho umia ni imani ya ibada ya katika Mungu aliye mmoja ya Yesu na waguasi wake (Yohana 45:44; 17:3).

Maelezo ya Profesa Wendt ya kihisia yanastahili kusikizwa na wote:

Kutoka wakati wa Justin elimu ya ukristo ya logos ulitawala katika elimu ya dini ya kikristo...haya mafundisho ya logos yaliwasiliana na kukubaliana na falsafa ya jadi ya baadaye (Late antiquity). Shida kuu ya hii ya falsafa ilikuwa jinsi ya kuweka uhusiano wa dunia isiyo roho na iliyo chini na dunia ya Mungu na roho inayopita fahamu. Kutatua shida hiikuwepo kwa viumbe/nafsi za kati kuliwekwa. Hivi nafsi (viumbe) vilikuwa vimetokana na uungu/utukufu na viliwakilisha njia ya hatua ambayo ingeweza kutumika kuziba ufa uliopo katika Mungu na binadamu. Kukisia kwa Kristo kuhusu huyu logos akiwa kama mpatanishi katika uumbaji kuumba kulihusika moja kwa moja na huku kukisia kwa falsafa ya kiyunani kwa maana ilitoa suluhisho la kufafanua na hilo kwa tatizo la kiroho/kimbingu kama hilo.... Lakini nia zote zinazohusika zilipoungana—za kimbingu na kifalsafa zikiungana na zakidini na soteriological zili leta kukanganya kwa kidini kama mafundisho ya logos yangeweza kutoa suluhisho linalotosha kwa matatizo ya kimbingu, huyu logos angewasilisha kama mwanadamu mpatanishi (nafsi) aliye halisi, akitoka kwa Mungu lakini akiwa mdogo kuliko Mungu, ili huyu logos amuunganishe Mungu na binadamu kama mpatanishi. Katika upande mwingine kama huyu mpatanishi alikuwa alikuwa alite uwokovo basi nafsi yake ilikuwa ni lazima iwe na thamani iliyosawa na wokovu ambao angelete kwa wanadamu....Ni lazima afikiriwe “kama Mungu” (2 Clem 1:1). Ambavyo mwelekeo wa kimbingu cosmological ama ule maoni ya soteriological ulivuma kadhalika mwanya kati kati ya logos na Mungu ama kufanana kwake na Mungu vilisisitizwa.⁹³

Ukinzani ulipo katika makisio ya logos unawakilishwa na mabishano yanayo pingana na wafuasi wa Arius na Athanasius. Pande zote mbili ziliamini ya kwamba alikuwa nafsi iliyo kwisha kuwepo. Lakini kama profesa wednt anavyosema hukumuelewa logos kama nafsi ilio mwanadamu kulisababisha tatizo. Ambavyo si tu kuwepo mbeleni kwa kinafsia na kimbingu pamoja na Baba kulikohusishwa na Mwana bali pia kuwepo naye milele na kwa pamoja pasipo na uwezekano wa kutengana, hivyo basi dhana ya umoja Mungu ilipotea. Hili ndilo lililokuwa lalamiko kubwa la munaki wote (munarchians) [wanaounga mkono kwa dhati umoja wa Mungu].⁹⁴

Wendt anamalizia kifungu chake kuhusu “utatu (matatizo) wa kanuni za elimu za kikristo za awali”: “ibada ya Mungu mmoja ambayo kwa maoni ya mkristo kuhusu Mungu si jambo lisilo uhimu iliharibika/vunjika....Iwapo logos ambaye anamilikiwa na Mungu ni nafsi na Baba ni lazima kutokee wingi katika Mungu na hivyo ibada ya Mungu mmoja iliyohalisi uharibiwa.”⁹⁵ Hii ndio shida inayosababishwa na imani katika imani ya Mungu aliye nafsi tatu ya jadi.

Kuhusishwa kwa karibu kwa Yesu na huyu Mungu mmoja wa Israeli hakuelekezi kwenye misimamo ya elimu ya kikristo ya imani/kanuni. Mambo yaliofikia kilele katika Nicean na Chalcedon yanaweza kuonekana katika viwango vitatu vikuu. Kwanzo “logos” ya falsafa ya kigiriki ilitambuliwa pamoja na Kristo aliyekwisha kuwepo na wanaelimu

⁹³ Kama hapo juu. 357, 358

⁹⁴ Kama hapo juu. 359

⁹⁵ Kama hapo juu., 368

wa dini wakialexandria. Pili, Origen alibashiri itikadi/kanuni isio ya kibiblia ya kizazi cha milele cha mwana kwa Baba na ikapunguza tofauti zilizopo katika uungu kufikia kiwango ambapo haiwezekani tena kusema ni vipi hawa watatu watawezi kuelezwa.

Inaonekana ya kwamba uzushi usio rahisi wa enzi iliofuata baada ya kuandikwa kwa Biblia kuhusu jinsi ya kufafanua mwana kwa kuhusiana na Baba ungeweza kuepukwa kama maneno ya kitalaam ya maneno ya kihebrania katika Biblia yangehifadhiwa. Geoffrey Lalpe katika maelezo yake (yenye hisiya) ya elimu ya Ukristo ya zamani analalamika kwamba:

Dhana ya elimu ya ukristo kuhusu mwana aliyekwisha kuwepo inabadili nafsi ya Yesu iliyohalisi kijamii na kitamaduni kuwa hali ya binadamu isiyo shikika ya kiroho. Mwana alichukuwa uwanadamu ulio kawaida popote na akijifanyia wake mwenyewe... Lakini uwanadamu wa kawaida ni dhana isio shikika... Kulingana na elimu ya ukristo, Mwana aliye milele anachukuwa jinsi ya ubinadamu isio na kipimo cha wakati ama anaifanya kutokuwa na kipimo cha wakati kwa kufanya iwe yake mwenyewe; ni jinsi ya ubinadamu ambayo haizingatii hali za kimaumbile (Geographia); hailingani na chochote katika dunia halisi ya maumbile. Yesu kristo “hakuja kama inavyoaminika, katika mwili”⁹⁶.

Mosheim alisema ya kwamba “uzushi kuhusiana na utatu wa Mungu uliongezeka katika karne ya pili baada ya kuingizwa kwa falsafa ya kigiriki katika kanisa.”⁹⁷ Utafiti wa elimu ya dini ya kibiblia umeleta ithibati ambayo inatulazimisha kufikiria vilivyo huku kugeuzwa kwa imani kulikotokea wakati falsafa ya kiyunani ilipoingizwa/ongeza katika mfumo wa kihebrania wa biblia aliokuwarahisi. Tunamalizia na dondoo zingine tatu hizi inatufanya tufanye upya uchunguzi wa historia ya imani katika kutafuta kwa imani kuliopo. H. Constable aliandika manamo 1893:

Wakristo wanauliza kama maoni yanakubalika kuhusu jinsi ya binadamu na adhabu ijiao yanatokana na falsafa pamoja na desturi ama yanatokana na matakatifu. Wanaanza kushuku ya kwamba kiasi kikubwa cha elimu ya dini iliopo kinatokana na falsafa ya binadamu. Wahusika katika uwanja wa dhana ya kidini waliofikiria kuwa wahusika wakristo, manabii na mitume wake wameanza kuwashuku kuwa wahusika wa pepo chafu, wahusika wa plato na viongozi wa kanisa wa zamani ambao sehemu kubwa ya elimu yao ya dini ilitokana naye.⁹⁸

Alfred Voucher anaitua turegelee imani ya kibiblia:

Maji masafi ya ukweli uliodhirishwa yana pita katika kurusa za Agano la kale na lile Jipya kama mto mkubwa. Ni Mungu pekee ambaye huishi milele huwapo binadamu na uwahasilishia maisha yakeya utukufu yasioweza kuharibika. Lakini sambamba na hiki kijitoupo mto wenye matope wa falsafa ya wasiomuamini Mungu ambao unahusika na roho ya mwanadamu, mwanzo wenye utukufu roho iishio milele ikitangulia uwepo kwa mwili na kunusurika mwili. Baada ya kifo cha mitume hii mito miwili iliungana ikafanya umoja wa maji yaliochafuka. Polepole makisio ya falsafa ya kibinadamu yakachanganyika na mafundisho yenye utukufu. Hivi sasa jukumu ya elimu ya dini ya kiinjili ni kutenganisha hivi vipengele viwili visivyo kuenenda pamoja, kuvifanya visishiriane na kuondoa kikipengele cha wasio mcha Mungu ambacho kimejiingiza/jisimamisha kama mnyakuzi katikati ya elimu ya dini ya

⁹⁶ *God as Spirit [Mungu kama roho]* (London: SCM Press, 1977), 144.

⁹⁷ *Institute of Ecclesiastical History* (New York: Harper, 1839)

⁹⁸ *Hades or the Intermediate State* (n.p., 1893), 278

kidesturi. Ilikuhifadhi thamani ya kipengele cha kibiblia kilicho pekee cha ukweli, na ambacho kinauhuina na jinsi ya Mungu na ile ya mwanadamu, kiumbe chake.⁹⁹

Kinachojitokeza kutokana na hii hali ya kukanganya ya awali kuhusu jinsi ya Mungu na mwanadamu ni ibada ya Mungu mmoja ya zamani ya manabii, Yesu na mitume. Mungu atahisiwa tena kama nafsi moja, Baba ya Yesu, Mwana wake aliyezaliwa katika njia pekee aliye Masiya. Ubinadamu kamili wa Yesu uliofunikwa na elimu ya dini ya kukisia na isioshikika ya viongozi wa kanisa wa kale/waanzisha, Ni lazima urudishwe kama sababu ya imani/kanuni ya Agano Jipya kwamba Yesu ndiye Masiya,¹⁰⁰ Mjumbe wa ufalme wa Mungu ujao duniani.

Wasomi wenye msingi tofauti hukubaliana katika ushuhuda wao kuhusu kuharibiwa kwa imani ya kikristo tangu karne ya pili kuendelea matumaini ya kimasiya yalisahulika polepole. Ile dhana ya ufalme wa Mungu katika dunia ilitokea. Kutopatikana na mauti kulichukuwa nafasi ya kufufuka:

Sawa na dhana zingine maana y amaneno ya kidini linabadilika, jinsi maisha yanavyobadilika na mabadiliko wa mwelekeo wa dunia. Kutafsiriwa katika mwelekeo wa dunia wa kiyunani hapana shaka kuligeuza mafundisho ya kikristo—kwa hakika kuliyabadili. maswali ambayo yalikuwa hayajawahi kuulizwa yakapata kipao mbele na asili ya kiyahudi inaonekana kutoweka. Hasa matumaini ya kimasiya yalisahulika ama yakahamisishiwa dunia ya kifumbo kupita kifo. Wakati hii maya ilipobadilika na kuwa kikristo katika kaene ya nne, dhana ya ufalme ya Kristo duniani ambao ungeanzishwa na mapambano makubwa ilipotea, ikabaki tu kama ya imani ya vikundi vilivyofichika. Kutokufa—dhana ya kifalsafa—kilichukuwa nafasi ya kufufuka kwa mwili. Hata hivyo hili jambo la pili linandelea kwa sababu ya kuwepo kwake katika mianzo iliyo msingi, lakini tena sio kigezo kiamuzi kwa sababu mwanzo wake—ule ufalme wa kimasiya duniani umefichika. Hivyo basi msingi umebadilika kutoka kiyahudi na kuwa kiyunani, kadhalika nazo dhana msingi za kidini... Hivyo basi tuko na muangano wa kipekee—*itikadi/kanuni za kidini na za kibiblia zikitumikishwa katika jinsi/njia ya falsafa ya kigeni.*¹⁰¹

1 Yohana 4:2

Majaribio ya zamani ya vikundi mbali mbali ya kutia shaka katika wanadamu halisi wa Yesu yalikumbwa na maonyo makali ya Yohana kwa wanafunzi wake kwamba “wadanganyifu wengi wameenda katika dunia, wale wasio utambua kuja kwa Yesu kwatika mwili¹⁰² huyu ndiye yule mdanganyifu na mpinzani wa Kristo.” (2 Yohana 7; cp. 1 Yohana 4:2).

*Translators New Testament*¹⁰³ inatokana na huu msitari katika njia ambaye inaondoa shaka kuhusu uneni “kuja katika mwili” Wahadaji wengi wameenda katika dunia ambao hawakubali ukweli ya kwamba Yesu alikuja kama mwanadamu. Huyu ndiye mhadaji na yule mpingaji wakristo.” Msimamamo dhahiri wa Yohana akisamamia upande wa uwanadamu wa Yesu alikuwa na madhumuni ya kifichua mfumo wowote ambao unashuku kwamba Yesu alikuwa mwanadamu halisi kama mfumo unaopinga ukristo. Tumeona katika sura moja iliotangulia kwamba msimamo rasmi wa ibada ya

⁹⁹ *Le probleme de l'immortalite* (n.p., 1957), 6

¹⁰⁰ Mat 6:16; Yohana 9:22; 20:31; Mat 5:42; 9:22 n.k

¹⁰¹ G.W Knocks, D D, LLD, Profesa wa falsafa na historia ya dini, Union Theological Seminary, New York, *Encyclopedia Britanica*, toleo la kumi na moja awamu ya sita, 284

¹⁰³ Shirika la wingireza na kigeni la Biblia, 1973.

Mungu aliye nafsi tatu ni kwamba mwokozi alimilki jinsi ya uwanadamu isio na nafsi, lakini hakuwa nafsi ya mwanadamu.

Kiombe/nafsi ambaye alikuwa Mungu na pia mwanadamu haingeweza kuwa mwanadamu halisi, akijaribiwa jkatika mambo yote kama sisi. Kama wakinzani wengi wa utatu wa Mungu walivyokwisha kulalamika, mafundisho ya desturi kwamba Yesu alikuwa Mungu hayakubaliani na imani ya kwamba alikuwa mwanadamu halisi. Yule mungu mwanadamu wa mabaraza mengi ya enzi ya baada ya kuandikwa kwa Biblia anaonekana kuwa kama “Yesu mwingine”, jambo lililo hatari, Paulo anaonya katika waraka wake wa pili kwa wakristo kuhusu jambo hili (2Wakorintho 11:4).

Kinaya cha uzushi huu mbaya wa kizazi kizima ni kwamba vikundi vyote hudai kuabudu Mungu mmoja pekee—vile vya ibada ya Mungu aliye nafsi moja, nafsi mbili na nafsi tatu. Wale wanaosisitiza ya kuwa Yesu ni Mungu hubishana ya kwamba anastahili kuabudiwa/ibada, kitendo ambacho hutolewa kwa Mungu pekee yake. Iwapo haya maoni yangeshikiliwa basi tungeweza kutia tamati kwamba nafsi mbili zinastahili ibada kama Mungu. Kupendekeza uungu ulio nafsi mbili ama tatu kunapinga vifungu vingi vya kibiblia kwamba Mungu ni nafsi moja. Ni bure kuepuka msimamo huu kwa kushikilia ya kwamba hizi kanuni/imani hazi maanishi kwa kutumia neno nafsi kile ambacho tunamaanisha leo na matumizi ya neno nafsi. Katika Biblia Baba na Yesu ni wazi kwamba ni nafsi katika maana yake ya kisasa—watu wawili tofauti.

Suluhisho la utatu huu ni kwamba ibada katika maandiko matakatifu haitolewi tu kwa Mungu pekee lakini pia kwa nafsi zilizowanadamu bali pia kwa nafsi zilizo wanadamu wanaoshikilia nafasi ya heshima. Neno la kiyunani *Proskuneo* linatumika kumaanisha ibada kwa Mungu na pia kusujudu nafsi. Si hivyo kwa mfano mfalme wa Israeli anaabudiwa kwa kuhusiana na Mungu (1 Hesabu 29:20, KJV; neno lililotumika ni *Proskuneo* katika LXX). Danieli alihabudiwa (Dan 2:46). Mitume walihabudiwa (Ufunuo 3:9, KJV). Yesu anaabudiwa kama Masiya, lakini ni nafsi moja pekee, ilio Baba, nayostahili ibada kama Mungu. Ni muhimu sana neno lingine la kigiriki *latreuo* linalotumika katika ibada ya dini pekee yake, limetumika mara zote ishirini na moja linapotokea kuhusiana na yule aliye Baba katika Agano Jipya.

Wasomaji wa King James Version wanapatiwa maneno wambayo sio ya kweli kwamba Yesu ni Mungu kwa sababu “anaabudiwa.” Ubishii huu huu ungeweza kutumika kudhihirisha kuwa Daudi na mitume walikuwa pia Mungu! Ni katika matumizi ya kisasa ya neno ibada ambapo wasomaji wanaelekezwa kudhani Yesu aliabudiwa kama Mungu.

Mungu na watumishi wake walio wanadamu wanashirikiana kwa karibu mara nyingi. “Na watu wakamuogopa Bwana na wakamuamini Bwana na mtumishi wake Musa” (Kutoka 14:31). “Na watu wote wakamuogopa sana bwana na Samweli” (1Sam 12:8). “Na wote walioshiriki ibada wakamubariki bwana Mungu wa baba zao, na wakamuabudu bwana na aliyekuwa mfalme” (1 Hesabu 29:20). “Hezekeya na mwana wa mfalme wakamubariki bwana na watu wake Israeli (2 Hesabu 31:8).

Tafsiri za kisasa zimesaidia kulifanya wazi hili swala “kumuabudu Yesu.” Katika Mathayo 8:2, kwa mfano, tunasoma kuhusu mtu mwenye ukoma aliye kuja na “kuanguka mbele ya Yesu” (*Translators New Testament*).

Haya yote hayanuui kupinga kwamba Yesu ndiye anayezungumziwa inaposemwa “Anastahili yule mwana kondoo ambaye alichinjwa kupata uwezo, utajiri na hekima na uwezo na heshima na utukufa na Baraka.” Kama Masiya, Yesu aliyemwakilishi halali wa muumba anaheshimwa kuhusiana na yule Mungu mmoja Baba yake (Ufunuo 5:12, 13). Lakini anajiunga na mitume katika wimbo wa mwana kondoo wa kumsifu Baba (Ufunuo 15:3; cp. Waeb 2:12, ambapo Masiya anamsifu Mungu. Yesu ndiye mwanzo na mwisho wa mpango mkuu wa Mungu wa uwokovu (Ufunuo 1:17). Na hali alikufa (Ufunuo 1:18), jambo ambalo linamaanisha wazi ya kwamba hawezi kuwa Mungu kwa sababu Mungu

hafi. Ni yule mwenye uiwezo wote pekee aliye Mungu mkuu. Katika Ufunuo 1:8 (cp 1:4) Baba ndiye Alfa na Omega na bwana Mungu mwenye uwezo “ambaye anakuja.” Cheo (jina) cha pili, *pantokrator*, halipatiwi Yesu ingawa Biblia zinazotumia herufi nyekundu kuhusisha msitari huu na mwana zilijaribu kufanya hivyo, hivyo zikaendelea kukanganya ambako kumekuwapo kwa muda mrefu kwa Masiya – na Mungu. Yesu aliyefufuka kwa kweli anapata ufunuo kutoka kwa Baba (Ufunuo 1:1), kudhihirisha kwa mara nyingine kwamba huyu mwana siye mungu anayejua yote!

Katika Ufunuo 22:12 yanawezekana ya kwamba yule malaika (“Yule” katika msitari wa) anaongea, kama katika Agano la Kale, kama Mungu akimwakilisha. Yule Alfa na Omega wa msitari wa kumi na tatu huenda anazungumzia aliye Baba ambaye anazungumziwa na yule malaika, kama ilivyokatika Ufunuo 1:8 na 21:6, kwake huenda kutaelezwa pia katika Ufunuo 22:12, ukifuatiwa na jina tukufu katika msitari wa kumi na tatu. Yesu ndiye anayezungumza tena kutoka msitari wa kumi na sita.

Ni kitendawili kinachoshangaza kwamba Yohana, ambaye anashuku kubwa ya kushikilia ya kwamba Yesu alikuwa mwanadamu halisi, aliyechoka na kupatwa na njaa, Yohana ameeleweka visivyo eti alitoa funzo la kwamba Yesu alikuwa Mungu kamili katika maana ya mungu aliye nafsi tatu. Injili ya Yohana inaregelea kumuita “Mungu” Baba. Na hali katika waraka wa Yohana wa baadaye tunahisi wengine wakati huo walijaribu kulazimisha fafanuzi ya Yesu katika maandishi yake ambayo hakuinua. Ithibati ni hii: katika injili ya Yohana ile *logos* (Neno), ilikiwa neno lisiloeleweka kikamilifu kwa kiasi fulani linaweza kuelekea kutoeleweka. Huenda ifikiriwe ya kwamba Yohana alimaanisha kwamba nafsi ya pili iishiyo milele ilikuwepo sambamba na Baba. Lakini hivi sivyo Yohana alivyo fikiria na chukuwa nafasi katika mwanzo wa waraka wake wa kwanza kujieleza kikamilifu. Anasema ilikuwa “uzima wa milele” uliokuwa na Baba (Yohana 1:2).¹⁰⁴ Ilikuwa hilo “neno la uzima” ama “uzima” lisilo na nafsi (1 Yohana 1:1, 2) ambalo lilikuwa limedhihirika wakati huo katika nafsi iliyo mwanadamu, Yesu. Kilichokwisha kuwepo sio mwana wa Mungu ila ni hilo neno ama ujumbe ama ahadi ya uzima. Hio ahadi ya uzima ilielezwa katika mmoja aliyekuwa binadamu, yule Masiya wa Israeli. Kupata uhai tena katika Biblia haimaanishi ya kwamba yule nafsi ya pili katika utatu wa Mungu alibadilika na kuwa mwanadamu, bali sababu ya Mungu kuwapatia viumbe vyake kutokufa ilidhihirishwa, ikaonyeshwa na ikawekwa katika mwili wa binadamu wa pekee.

¹⁰⁴ Cp “na hilo neno lilikuwa na Mungu (Yohana 1:1)

VI. UTATU WA MUNGU NA SIASA

“Basi hajuwe, rafiki yangu, kwamba utatu wa Mungu ulianzishwa zaidi ya miaka mia tatu baada ya kutangazwa kwa injili ya kale; ilizaliwa katika kutojua, ikastawishwa na kushikiliwa kwa mabavu.”—William Penn.

Mwanahistoria fulani alikuwa na msemo huu sahihi:

Ukristo ukihusisha ukweli na imani, ni lazima ufundishe,—na ikielewekwa vizuri huwa unafundishwa ya kwamba ukweli unapoingwa si jambo adilifu. Mkristo mwenye imani haitaji kuogopa chochote katika hoja zilizokweli; mkristo mwana historia anyeweke mpaka katika uwanja wa utafiti popote pale atakuwa anakubali mpaka/upeo wa imani yake.¹⁰⁵

Muamini anayeogopa huwa anazuia lengo kuu la shuguli ya kikristo ambayo inanuia kutafuta kuendelezwa kwa kuelewa kwa kweli.

Kwa bahati mbaya, historia mara nyingi huonekana kupitia kwa jina la muhusika hasa kama swala kisiasa linaangaliwa kutoka kwa mwelekeo ulio mwebamba wa kidini ama usio wa kidini. Chunguza maisha wa waanzilishi wa kundi lolote la kidini; soma maelezo katika vitabu, majarida, na magazeti yalioandikwa na waandishi wasio wafuasi wa dini. Kisha yasome maisha hayo hayo katika maandishi ya mtu aliyeandika kuhusu maisha yake mwenyewe ama katika kazi ya waumini walio jitolea. Kuna uhiano mchache sana isipokuwa katika hoja chache za ukweli na habari ndogo za kitakwimu zisizoweza kufutika. Wakati unaopita na umbali kuongezeka mwanya mkubwa ufanyika kati ya uhalisi/ukweli wa kihistoria na jinsi habari hio hio itakuwa imeingizwa katika maandishi/kanuni za kanisa. Ustadi mwingi umetumika kuficha sehemu za maisha zisizopendeza za waanzilishi wa vikundi vya kidini kama kwa mfano *Church of Jesus Christ of Latter Days Saints (Joseph Smith)* na wa *Presbeteri (John Calvin)*.

Kinyume na haya kufichua kwa wazi kuhusu maisha ya mashuja wa Biblia kunapatikana katika maandiko matakatifu (takwimu takatifu)—pasipo kuficha chochote hadi ulevi na maisha ya ngono yasio na uwadilifu. Tunalionga kuwa jambo muhimu kunadhifisha maisha ya viongozi wa dini ya baadaye. Ingawa huenda wengi wasipende na walione kuwa jambo lililo katili, tunasikia na maandishi ya kibiblia yalio neno la Yesu: “mtu ulio mbaya haiwezi kuzaa tunda zuri (Mat 7:8). Je, huenda ikawa kwamba kufichua wazi huenda kukaonyesha mbegu za uharibifu zinazochukiza? Juhudi za uangalifu zinafanywa ili kuwasilisha maisha ya viongozi wanaojulikana wakidini katika hali ya kimitume kadri inavyowezekana. Inatumainiwa ya kwamba hili hupatia mafundisho yao maana na mfumo wa imani waliopitisha kufikia vizazi vijavyo.

Kadhalika tunaposoma maelezo mbali mbali kuhusu mwanzo wa utatu wa Mungu tunashangazwa na vile ambavyo chimbuko mbali mbali zinaeleza swala hili. Waandishi fulani wakristo wanashikilia kwamba utatu wa Mungu ulikuwa umekwisha kita mizizi katika tabaka za kikristo wakati Agano Jipya lilipotungwa. Kwa hivyo waandishi wa Agano Jipya hawakuwa na hoja kuutaja utatu wa Mungu ila katika njia ambayo haikuwa ya moja kwa moja. Ilichukuliwa kuwa sehemu ya desturi ya kanisa iliokubaliwa sana hivyo basi hawakujali sana kuandika kile ambacho kingekuwa badliko kubwa zaidi la wakati wote kuingilia jamii ya kidini ya karne ya kwanza. Waandishi wengine wakiandika kisa hiki hiki cha elimu ya dini hawakubaliani kabisa. Wanaonyesha vita iliyo mwaga damu kati ya wakristo iliyochukuwa karne nyingi, na ambamo maelfu walilipia

¹⁰⁵ Paul Johnson, *A history of Christianity* (New York: Atheneum, 1976), Viii.

kwa maisha yao kabla utatu wa Mungu haujawekwa wakfu kama kanuni/itikadi ya kikristo—zaidi ya karne tatu baada ya kifo cha mwanzilishi wa ukristo.

Kanisa imekuwa tayari kuwaunga mkono viongozi wakuu wakisia iwapo wanaendeleza jukumu la Kristo na kutetea usimamizi wa mahubiri yake. Katika sheria ya Milan mnamo 313 baada ya kuzaliwa kwa Yesu mtawala Konstantine alijipatia heshima ya kizazi kutoka kwa kanisa la kikristo kwa kuruhusu dini zingine potovu. Miaka michache baadaye alichukuwa msimamo mgumo ulioelekeza kusuluhisha matatizo kuhusu kanuni/imani katika vikundi mbali mbali. Matokeo yalikuwa ile hatuaya kwanza muhimu kuelekea kuingizwa rasmi kwa imani ya Mungu aliye nafsi tatu katika imani ya kikristo.

Wakristo wengi huenda watahangazwa na matokeo/maana ya maoni ya msomi wa kikatoliki. W. E. Addhis anapozungumzia kuhusu ile fufu ya kidini iliyosababishwa jarabio la kuanzisha ile dhana ya kwamba Mungu alikuwa zaidi ya nafsi moja, alisema: Idadi kubwa ya wakristo kama wangeachiwa wangeridhika na imani ya zamani katika Mungu mmoja, aliye Baba na wangekosa kuamini “*dispensation*” kama ilivyokwisha itwa, ambamo utukufu/uungu wa aliye Mwana “Watu wote wa kawaida,” Tertullian aliaandika, “wasi itwe wasiojua na ambao hawajaelimika ...hutoroka huu mgawo (*dispensation*). Wataelewa ya kwamba tunatangaza miungu wawili ama watatu.”¹⁰⁶

Wale wanomuamini katika nafsi tatu za Mungu na ambao huu sadiki ya kwamba dhana ya utatu wa Mungu ilikuwa ukweli ulio stwawi kiasi cha kwamba haikuonekana kuwa ya muhimu kuzungumziwa wakati wa Agano Jipya lilipoandikwa. Wanapatiwa changa moto na husemi wa mwandishi mwingene Harold Brown:

Ni hoja iliyo rahisi na ukweli wa kihistoria usioweza /kukataliwa kwamba kanuni kadhaa zilizokubwa na ambazo zinaonekana leo kushikilia sehemu ya kati/muhimu ya imani ya kikristo—hazikuwepo kikiamilifu na katika njia y ajuwa na fafanuzi ya wazi kwa jumla hadi karne ya nne na tano—kwa mfano kanuni ama imani ya utatu wa mungu vilevile imani/kanuni ya ujinsia wa Kristo. Kama hizi ni muhimu leo – kama imani/kanuni zote za kidesturi na pamoja na imani zinavyosisitiza—ni lazima iwe ya kwamba ni za kweli.kama ni za kweli basi ni lazima iwe zimekuwa kweli wakati wote;hazingekuwa zimegeuka na kuwa kweli katika karne ya nne na ya tano. Lakini ikiwa ni za kweli ni muhimu ingeweze kanaje kuwa kanisa la awali lilichukuwa karne nyingi kuzitoa/kuziandika?¹⁰⁷

Mahali pengine anasema: “mafundisho ya kupotosha yanajitokeza katika maandiko/takwimu za kihistoria mapema zaidi, na imeandikwa vizuri kuliko kile ambacho kanisa lilikuja kukiita imani barabara.”¹⁰⁸ Huku kukubali kunakotisha ya kwamba jamii ya kidini ilibadilisha mafundisho asili na wengine mapya na kanuni za ukristo hazijapita pasipo kuonekana na wahusika wengine/watafiti wa mambo ya ukristo. Mwandishi wa kiyahudi Pinchas Lapide, katika mazungumzo yake na msomi wa kiprotestanti, Jurgen Moltmann, anatoa maoni haya kuhusu imani/kanuni ya Mungu aliye nafsi tatu:

Yeyote anayejua jinsi historia ya mafundisho ya kanuni za imani/kanisa ilivyokuwa anajua kwamba mfano/umbo la mungu katika kanisa la mwanzo

¹⁰⁶ *Christianity and the Roman Empire* (New York WW Norton, 1967), 174.

¹⁰⁷ *Heresies* (Doubleday, 1984), 20.

¹⁰⁸ Kama hapo juu, 4

ulikuwa katika hali ya nafsi moja. Ni katika karne ya pili ambapo ulichukuwa umboi la nafsi mbili pole pole dhidi ya mafundisho ya kukaliwa/kuwekwa chini. Kwa waanzilishi wa makanisa kama Justin martyr, Irenaeus na Testullian Yesu alikuwa mdogo/chini ya aliye Baba katika mambo yote, na hata Origen alisita kuelekeza maombi yake kwa Kristo kwa maana kama alivyoandika, maombi yalistahili kuelekezwa kwa Baba pekee.¹⁰⁹

Picha/Taswira kamili inayojitokeza kutoka kwa historia (ya kanisa) ni karibu kuwa sawa na mfuatano (njia) wa kihesabu: “Katika karne ya kwanza Mungu bado akali wa nafsi moja katika mtindo wakiyahudi uliosafi. Katika karne ya pili Mungu chukua umbo la wawili katika mmoja; katika karne ya tatu yule Mungu mmoja wanakuwa watatu taratibu.”¹¹⁰

Lapide anaongea kuhusu “vita vya baina ya wakristo katika karne ya nne na ya tano ambapo maelfu ya wakristo waliwaua wakristo wengine kwa ajili ya utatu wa mtakatifu.”¹¹¹

Je mzozo huu wa kuhuzinisha ulitatuviwa vipi? Mtu mmoja aliyebadilisha maendeleo ya historia ya ukristo ni mfalme Konstantino ndiye aliyekuwa wa kwanza kuunganisha wakristo wasio muamini Mungu na serekali chini ya paa/uvuli wa serekali ya kirumi. kama Johnson anavyoonyesha bila shaka Konstantine alishiriki maoni yaliovuma wakati huo kwamba vikundi vyote vya kidini vinastahili kuheshimiwa katika kufanya amani na miungu ya taifa zao. Alisema pia kwamba Konstantino:

anaonekana kuwa alikuwa akiabudu jua mmoja katika vikundi vya baadaye ambavyo havikumuamini Mungu lakini ambavyo vilikuwa na desturi sawa na wakristo. Ibada ya miungu kama hawa haikuwa dhana muafaka. Kila muyunani ama mrumi alitarajia ya kwamba kufaulu kisiasa kulitokana na uchaji wa kidini. Ukristo ndio ulikuwa dini ya baba ya Konstantine. Ingawa Konstane alidai kuwa mtume wa kumi na tatu badiliko lake halikuwa la haraka kama la Paulo/la (kidamasiku). Kwa hakika ni vigumu kuamini kwamba hakuendelea kuabudu jua. Baada ya kukiri kukubali ukristo alijenga tao la ushindi wa Mungu wa jua na kusimamisha sanamu ya kuchongwa katika mji wa Constantinople kwa huyu Mungu wa jua ikuwa na sura kama yake. Mwishone alifanywa kuwa Mungu baada ya kifo chake kupitia amri rasmi katika ufalme kama walivyokuwa watawala wengi wa kirumi.¹¹²

Katika Konstantino, aliye kuwa askari halisi ukristo, ulimpata shujaa asiye ya kwaida. Ndiye aliyekuwa mfalme wa kwanza wa kidunia mwenye uwezo zaidi wa kutoka kizazi chochote kuhesabika katika mashujaa wa kanisa. Ingestahili kuuliza jinsi maisha yake yalivyo karibiana na yale mwanzilishi wa ukristo aliyepewa jina la “mwana mfalme wa amani.” Ni Konstantino ambaye aliufanya ukristo katika amri rasmi kuamini katikakugawinyika rasmi kwa Mungu katika sehemu mbili—Mungu aliye Baba na Mungu aliye Mwana. Ilibaki jukumu la kizazi cha baadaye kuleta imani katika Mungu aliye nafsi tatu katika ukristo.

Ni huyu huyu Konstantino aliyeingia katika mji wa Rom akiwa na kichwa cha mpinzani wake (hemeki yake) alilicho kuwa amekikata huku mkuki wake ukiwa na damu. Alieleza kwamba ushindi wake ulitokana na oni ambapo anaamini kuwa aliona

¹⁰⁹ *Jewish Monotheism and Christian Trinitarian Doctrine*, 39.

¹¹⁰ Kama hapo juu.

¹¹¹ Kama hapo juu, 40.

¹¹² *A History of Christianity*, 67.

herufi za kiyunani *Chi-Rho*, herufi mbili za mwanzo za jina Kristo. Hii hadithi huwa tofauti kulingana na hii simulai lakini kabla uchinjaji huu wa kihistoria alihamrisha kwamba hizi herufi zichorwe katika ngao za askari wake Miaka sita tu, kabla kuingia kwake huko Rom kwa ushindi alihamrisha kwamba ma mia ya askari wa Kifrank waliokuwa waasi wakatwe katwe vipande katika uwanja mkubwa. Aliuunga mkono pia wakati mifumo isio ya Kikristo ya diokletia (*Diocletian*) iliposababishwa kuchomwa kwa maandiko matakatifu (wakfu) ya Kikristo kukifuatiwa na kukatwa katwa kwa waumini walio kataa kuabudu miungu ya dunia.

Miaka kumi na moja baada ya ushindi huu uliotoka mbinguni historia inaeleza ya kwamba huyu bwana anaye kisiwa kuwa mfuasi wa Yesu aliua mpinzani wake aliyekuwa amekwisha kumshinda, akaua bibi yake kwa kumchemsha akiwa hai katika berika lake mwenyewe (bibi)—na akaamua mwana wake adui ambaye hakuwa na makosa. “Maisha yake nje ya uma yaliendelea kuchafuka kadri alivyozeeka. Alinenepa na akaanza kujulikana kama “shingo ya ndume”....Uwezo wake ulikuwa siku zote katika usimamizi/uwongoziAlikuwa fundi wamapatano yaliokuwa yameandikwa kwa maneno matamu.”¹¹³ Hata hivyo alikuwa “mdalimu mwenye ubinafsi aliyedai kuwa mwenye haki na asiye kuwa na huruma.”¹¹⁴ Katika miaka ya baadaye “alionyesha kuvutiwa na kusifiwa, mavazi ya sare yaliokuwa ya kuvutia na kusifiwa, mavazi ya sare yaliokuwa ya kuvutia kujipendekeza mwenyewe na majina makuu. Mpwa wake, Julian anasema ya kwamba alijifanya kudhihakiwa kutokana na alivyoonekana kuwa – [mavazi] Mavazi ya kutisha ya kutoka mashariki yaliokauka. Johari katika mikono yake, na taji katika kichwa chake lilikuwa limewekwa kwa njia ya kuchekesha juu ya nywele isio halisi iliokuwa imetiwa rangi.” Eusebius, aliyetoka Caesarea, aliyeonekana kuomba msamaha kwa niaba yakeanaeleza ya kwamba huyu mtawala mkristo alivalia ili kuwapendeza watazamaji wake wengi; akiwa pekee yake aalikuwa akichekelea. “Lakini hili ushahidi mwingi mwingine, ukiwepo ule wa Eusebius mwenyewe. Huenda aliukubali ukristo katika hali yake ya ushirikina na upumbavu wake kwa sababu viliuhiana na matakwa yake mwenyewe na tamaa yake ya ukuu (kiwazimu) iliokuwa ikikuwa/ikizidi.” Huenda wenye mzaha/madharau waulizi ni vipi ambavyo maisha ya Konstantino yalikuwa mfano wa maisha ya yule seremala mnyenyekevu wa Nazareti. Ingawa alibatizwa punde kabla ya kifo chake imekuwa ikikisiwa ya kwamba nia ya ndani kabisa ya Konstantino zaidi ya ushirika wa kawaida wapiganaji siku hizo, ilikuwa ya kisiasa. Nia yake ya kuleta uhiano/shuari katika ufalme uliokuwa umegawika ulihibitaji ustadi wa kisiasa. Wanasisia wa siku za baadaye wanao lazimika kutia viungo (vya kuonja) vilivyo sehemu kubwa za vikundi vya kidini vinavyoshindana na vinavyoshikilia siasa, wangetamani ustadi wa Konstantino. Wakati mwingine hili uhusisha kudai kuzaliwa mara ya pili katika kampeni/mapambano ya kisiasa yanapo pamba moto.¹¹⁵

Mabishano /Uzushi wa elimu ya Ukristo

Katika ufalme wa Kirumi tofauti kubwa ya elimu ya kidini ilitokea baina ya wakristo wa Alexandria na wale wa Antiokia. Hivi vikundi vilivyopigana vilisababisha tisho kwa muungano wa huu ufalme. Kwa sababu ya uwezo wa kisiasa wa hivi vikundi vilivyo pingana ilibidi hizi tofauti zisuluhishwe. Wakristo huko Alexandria waliamini ya kwamba Yesu alikuwa amekwisha kuwepo milele kama nafsi tukufu na kwamba alikuwa mwanadamu kwa kuonekana/kwa kuchukuwa umbo la mtu. Huyu Yesu wa elimu hii ya dini alihatarisha “kuonekana” tu kama mwanadamu halisi. Katika lugha

¹¹³ Kama hapo juu 114, 68.

¹¹⁴ Kama hapo juu.

¹¹⁵ Kama hapo juu.

ya ki istilahi ya elimu ya ukristo huyu Yesu wa wakristo wa Alexandria alikuwa wa kidoceti (“*docetic*”) [kutokana na kitendo katika kigiriki kumaanisha “kuonekana kama]. Ukweli ni kwamba uungu wake ulikuwa zaidi ya uwanadamu wake. Mwokozi mwenyewe alikuwa Mungu kwa kweli akiishi katika mwili wa binadamu na akiwa na “jinsi ya mwanadamu isio nafsi” (maneno maalum yalio tumika baada ya kustawisha wa kufuatia kamati ya baadaye ya Chalcedon mnamo 451 baada ya Kristo). Yesu mwenyewe ilivyoshikiliwa kulingana na mafundisho ya dini ya awali alikuwa “mtu” wala si “mwanaume”.

Kwa wale ambao walikulua karibu na Antiokia, sehemu ambayo ilijumuisha sehemu iliyokuwa nyumbni kwa Yesu. Maoni tofauti yalishikiliwa. Hapa ibada ya Mungu mmoja ya asili ya wayahudi ikihimiza umoja wa Mungu ilikuwa na matokeo ya imani katika mwana aliye umbwa. Kigezo cha pekee cha hii elimu ya ukristo ya “Arian” kilikuwa ya kwamba Yesu kama mwana wa Mungu ni lazima alikuwa na mwanzo na ingawa alikwisha kuwepo hangeweza kuwa pamoja na aliye Baba milele na pamoja aliye Baba katika usawa. Kiini cha ubishi/uzushi huu ulio imarika baina hivi vikundi viwili kilikuwa kuhani aliyeitwa Arius, aliyekuwa na wafuasi wengi kati ya wale wa Askofu wa Alexandria na himaya ya Alexandria juhudi ya Arius za kuendeleza elimu yake ya ukristo katika Misri zilimueleza kutolewa mara moja katika ushirika wa kanisa.

Tofauti za kidhana zilijulikana baina ya Rom, Alexandria na Antiokia zilikuwa jambo ya kushugulikiwa na utawala wa kirumi. Uwezo wa dini ulikuwa na sehemu maalum katika kuimarisha utawala wa kirumi yua karne ya nne kiasi cha kwamba mzozo wa kidini ilikuwa ni lazima uzimwi na serekali lau sivyo ungechafua umoja wa kisiasa. Konstantino alijitolea kusuluhisha huo mzozo kwa njia ya hizi barua zinazo fanana za kupatanisha zilizotumiwa kila vikundi, zikihimiza kupatanisha tofauti zilizopo:

Konstantino aliye mshindi, Augusto mkuu kwa Alexanda na Arius...Ni kidonda kilicho cha ndani sana kilicho pata masikio yangu na moyo wangu kutokana na taarifa ya kwamba zipotofauti kati yenu...Baada ya kupeleleza kwa uwangalifu kuhusu chanzo chake na msingi wa tofauti hizi haoni chanzo chake kuwa mambo yasio muhimu, yasiostahili kabisa shindano kali namna hii.¹¹⁶

Konstantino ni wazi hakujua undani wa maswala ya elimu ya dini yaliohusika katika mabishano haya (uzushi). Baada ya juhudi yake ya mwanzo kutofaulu kusuluhisha ugomvi huu, aliita baraza la kidini la viongozi wote lililowahi kuwa na uwezo mkubwa zaidi katika historia ya kanisa ya kikristo. Uwamuzi wa kisadfa na uliokuwa na athari mkubwa ulifikwa kuhusu hili swala la mgawanyiko kuhusu jinsi ya ukristo na uungu. “Tarehe iliowekwa ilikuwa ni mapema katika msimu wa joto mnamo mwaka wa 325 baada ya Kristo, na mahali pa mkutano ilikuwa ni mji wa kuvutia wa Nicea ulio kando wa ziwa...Katika kaskazini magharibi ya uturuki, ambapo Konstantino alikuwa na makao ya kifalme yenye nafsi kubwa kama yalivyo tarajiwa.”¹¹⁷

Ambavyo ukristo ulikuwa umesambaa na kufikia sehemu za mbali kama uingereza katika magharibi na India katika mashariki wajumbe wengine walihitaji muda wa wiki nyingi kama si miezi kusafiri...Yule mtawala Yakobo kutoka nisibis alifika akiwa ameivalia ngozi za mbuzi akiwa ameambatana na wadudu kama mbuu waliokuwa wengi na ambao hawakuwa wanataka kumuacha. Mjumbe mwingine alikuwa yule Nicholas aliye kuwa kama mtumwa na aliyeigwa baadaye akiitwa Santa Claus wa siku kuu ya Krisimasi. Konstantino aliketi katika kiti chake kilichokuwa chini na mkutano huu ambao lilikuwa haujawahii kuwepo.

¹¹⁶ Imenakiliwa na Ian Wilson, *Jesus: The Evidence* (Harpa and Row, 1984), 165

¹¹⁷ Kama hapo juu.

Alikuwa amevalia joho lililometameta akiwa amejaa dhahabu na johari, uharibifu ambazo watawala wa zamani wangezisujudu.¹¹⁸

Mwana historia wa kanisa aitwaye Schaff akimnakili Eusebius wa Caesarea anazidi kueleza tokeo hili: “Wakati kufika kwa mfalme kulipotangazwa kwa kutumia ishara fulani wote walisimama kutoka kwa viti vyao na mfalme alitokea kama mjumbe wa mbinguni na wa Mungu akiwa amefunikwa na dhahabu na johari, kuwepo kwa kimungu, akiwa mrefu na mwebamba aiyejaa urembo, nguvu na utukufu.”¹¹⁹

“Ilikuwa ni wakati huu katika historia na mbele wa mkutano huu ambapo uwamuzi ulikuwa ufanyike ambao ungekuwa na matokeo makuu kwa wanao amini ndani ya Kristo hadi leo.”¹²⁰ Kwa sababu anazojijua yeye mwenyewe huyu kiongozi ambaye hakuelewa biblia na ambaye hakuelewa kikamilifu maswala ya elimu ya dini yaliozungumziwa alisimamia mjadala wenye maana sana ambao umekwisha wahiikufanywa na kanisa. Msimamo uliochukuliwa na hili baraza ungekuwa na athari muhimu za muda mrefu zenye mageuzi kwa jundi lote la wanao amini. Uwamuzi wa Konstantino ulipendelea maoni ya walio wachache katika baraza hilo. Uwamuzi uliofanywa unakubaliwa na wingi wa Wakristo hadi leo—kwamba Yesu alikuwa na usawa na jinsi ya kuishi milele na Mungu, “Mungu mwenyewe wa Mungu mwenyewe.” Hivyo basi mkondo wa pili wa ile pembe tatu ya utatu wa Mungu ikiwa mafundisho ya kanuni ya imani. Ilikuwa imalizwe katika karne iliofuata kwa tangazo la kwamba roho mtakatifu ndiye nafsi ya tatu ya uungu.

Wale wanaelimu ya dini wakialexandria walio na mawazo ya kifalsafa ndio walioshinda wakiongozwa na Athanasios. Wale waliokuwa chini ya athari ya ibada ya Mungu mmoja walishindwa, wale ambao hawakukubali wala kuitikia kutia sahihi makubaliano haya walifukuziliwa mbali. Hapo ikiwa kanisa limechukuliwa na kuongozwa kiimla na wanaelimu ya dini waliokuwa na mawazo yenye athari kuuya kigiriki (athirika na mawazo ya kigiriki). Hivyo basi muundo wa mafundisho yake ya dini ilikuwa kwa karne kumi na saba. Maoni ya H. L. Goudge ni muafaka: “Wakati mawazo ya kiyani na kirumi, badala ya mawazo ya kiyahudi yalipotawala kanisa lilitokea janga ambalo kanisa halijaepuka (pona) katika mafundisho ya kidini na katika kutenda.”¹²¹ Kumilikiwa huku kuliendelea kutoka karne ya nne pasipo mabadiliko, Konstantino alifikia nia yake ya kuleta utawala wake katika umoja wa kisiasa. Huu ni ukweli wa historia, lakini umegharimu nini ukweli? Kanisa la ukristo hadi leo linajiinamisha mbele ya kiti cha enzi cha Konstantino kilicho chini na kilichofungwa na dhahabu.

Kwa kuelewa sana wengine katika waantiokia waliotia sahihi walimwandikia Konstantino kupinga kwa kusema “walifanya jambo lisilo la kiungu, wewe mfalme kwa kukubaliana na kukufuru/ubatili kwa kuogopa wewe.”¹²² Hivi ndivyo alivyoandika Eusebius Mwenyeji wa Nicodemia. Hata hivyo, tendo lilitendwa mfumo mpya kabisa wa elimu ya kidini iliingiziwa kanisani kuanzia wakati huo, wakristo halisi walio pinga sheria za utawala wame kabiliwa na utesaji mkali na mauaji yaliyo tekelezwa na utawala na mara nyingi wakristo wengine. Hapana haja ya kushangazwa na ukabalifu wa Constantine na wanazuoni wagiriki juu ya uwili wa Mungu ukubalifu wa wingi na miungu ulikuwa kawaida tena kwa mapana. Himaya za Roma na Ugiriki zilisheshani miungu. Wazo la Mungu kuwa binadamu na wala binadamu kutawazwa kuwa Mungu

¹¹⁸ Kama hapo juu. 165, 166

¹¹⁹ History of the Christian Church (Grand Rapid: Eerdmans, 1907-1910), 3: 625.

¹²⁰ Ian Wilson, *Jesus: The Evidence*, 1968.

¹²¹ “The Calling of the Jews,” in the collected essays on *Judaism and Christianity*. [’Kkuitwa kwa Wayahudi,’ katika tungo zilizo kusanywa juu ya dini na desturi za kiyahudi na ukristo].

¹²² Ian Wilson, *Jesus: The Evidence*, 168.

halingefikirika (cp Matendo 14:11). Constantine alikuwa ame amuru kufanywa kwa babake na yeye mwenyewe kufanyiwa vivyo hivyo afapo babake. Wakati wa mazishi yake alitambuliwa kama mtume wa kumi na tatu.

Leo, uamuzi huo wa ajabu wa Constantine umeathiri ukristo wa karne ya ishirini uliogawanyika bila upingamizi yenye maana. Athari ya Constantine yaonekana kuendelea bila kupingwa kwa njia yoyote ile. Kama ilivyo hali ya Napoleon, aliyekuja kuwa muuaji wa binadamu Europa; Luther; Calvin; au kiongozi wa kidini wa kisasa kama vile Joseph Smith, kuwa wafuasi waminifu hawaruhusu viongozi wao kutia aibu ila kusafisha majina yao yapate kung'aa.

Ukweli wa historia huenda ikawa hukumu vikali, lakini ni nadra kwa vizazi vyao vyenye imani ya kiroho kuvumilia yeyote ambaye angethubutu kutia kosa. Kwa karne mbili baada ya enzi ya Constantine, mauaji baada ya mauaji yalifuatia huku mkristo akipamabana na mkristo katika kukurukakara za kupigania kilichotokea kuwa imani imara ya kidini. Ilihitajika kuwa mtu akubali imani katika uwili wa Mungu (baadaye kupanuliwa kwa Mungu mwenye utatu) au akabiliwe na kufukuzwa, kuteswa na kuuawa hasa kwa ajili ya maslahi ya kisiasa yanayofaa na hifadhi ya kanuni zilizotangazwa kuwa ukweli usiopingika.¹²³

Baada ya Constantine, fujo ilikuja kukubaliwa kama njia ya kusuluhisha migogoro katika ukristo. Katika sehemu ya mapema ya karne ya II baada ya kristo, waenezi wa ukristo waliegemea uwezekano wa kuweka huru eneo takatifu (taifa takatifu) kwa nguvu za silaha. Baada ya kuchinja wayahudi wa Europa waliendelea kupatilia mwenye imani katika Mungu mmoja, Muislamu, “Kafiri” aliyedhibiti mji mtakatifu wa yerusalemu, maangamizi makubwa. Mauaji haya yalichochea na ukatili wa imani katika utatu wa Mungu. Baadhi wamependekeza kuwa uislamu kamwe haungepata nafasi duniani kama Mungu mmoja wa wayahudi, angebaki kuwa Mungu wa Wakristo.

Katika maendeleo haya yote, nivigumu kupata chochote kinachooana na maisha ya mwanzilishi wa ukristo aliyesema “siasa uovu” “geuza shavu jingine” (Mathayo 5:39), “heri wapatanishi” (Mathayo 5:9) na aliyeahidi kuwa wanyenyekevu wataridhi ardhi (Mathayo 5:5) mjumbe yuyo huyo alipinga kwa kusema “ufalme wangu si wa dunia hii [yaani, asili yake si ya mifumo miovu ya ulimwengu huu ingawa utakuwamo ulimwenguni wakati ujao] kama ingekuwa hivyo basi watumishi wangu wangepigana” (Yohana 18:36).¹²⁴ Uamuzi usio wa kidini ulipotolewa, ukristo ulijifunga kwao na hivyo basi ukabilifu wa ujuba ukaimarishwa kanisani. Kanisa lilikuwa limefanya mapatano mabaya na dunia uamuzi unao liacha likitapatapa katika hali ya kutokuwa na hakika, na kuchanganyikiwa kiimani, likiwa tayari pia wakati wa vita kuu maadui na vilevile wafuasi wao waliomo katika maeneo ya maadui zao. Kanisa katoliki lilipotishwa na imani isiyo kweli lilichukulia kuwa ni wajibu wa waumini kuvunja upinzani wote kupitia kwa baraza kuu la kuhukumia wazushi wa dini, liliona wafuasi wake waasi katika ulimwengu wa uprotestanti wakitumia mbinu sawa na hiyo. Waasi wa mageuzi ya uprotestanti walipokea adhabu kali kutoka kwa viongozi wa protestanti wenye nguvu wakishirikiana na serikali isiyo ya kidini.

¹²³ Maelezo yaliyofanyiwa utafiti mzuri juu ya athari za kisiasa zenye nguvu katika utayarishaji wa kanuni kikristo yametolewa na R.E. Rubenstein Katika kitabu kinachoitwa “ Wakati Yesu alikua Mungu (when Jesus became God)”; Ugumu wa kueleza ukristo katika wakaati wa mwisho wa Urumi (Harcourt, 1999).”

¹²⁴ Aya nyingi za Biblia zinatambua kuwa ufalme wa Mungu utaimarishwa duniani (Mathayo.5:5, 19:28, 25:31, Ufunuo:5:10, Isa:2:1-4, n.k.) Yesu akirudi.

Calvin Dhidi Ya Servetus

Mfano mzuri wa jinsi uongozi wa kikristo hukabiliana na tisho la imani yake ya jadi ya utatu mtakatifu kwa dai la kuwa Mungu ni mmoja, unaonyeshwa na kiongozi wa mageuzi ya ki protestanti anayetambuliwa sana, Yohana Calvin. Mhasiriwa asiye na bahati wa ukatili wa Calvin ni Michael Servetus, mpinzani wa utatu wa Mungu.

Servetus, aliyepata elimu ya kikatoloki alisomea sheria kuhusu watu na utabibu, alichukizwa na enzi aliyopewa kuhani mkuu aliyekuwa Roma, baada ya kuadhiriwa na mageuzi ya mapema/awali, Servetus aliendeleza usomaji wake wa Biblia kwa dhati akaja kuwa mprotestanti wa kwanza kuipiga vita imani ya utatu wa Mungu. Maelezo yake yanaondoa shaka kwamba alikuwa msomi wa kipekee aliyejua kiebrania na kigiriki. Alitangaza katika hali inayokwaruza kwamba kanuni ya kidini ya kanisa katoliki juu ya utatu mtakatifu wa Mungu ilikuwa zao la kimawazo, zimwi lililoshirikisha sehemu mbalimbali zisizofaa miungu ya kiulimwengu na mambo yaliyo magumu kufahamika.¹²⁵ Shtaka liliteka makini ya Calvin aliyesema kuwa Servetus alistahili kuondolewa kwa matumbo yake, na kuraruliwa vipande vipande.¹²⁶

Ajabu ni kwamba ingawa Servetus alikubaliana na upande wa kiprotestanti, alijikuta kageukwa na waprotestanti wajerumani na waswisi, hata hivyo, aliweza kupata hifadhi katika jumba la kifalme la askofu mkuu wa ki katoliki ufaransa aliyeenzi wasomi. Wakati huo Servetus alikuwa ametokea kuwa tabibu mahiri na wa kwanza kuandika maelezo juu ya mwendo wa damu kutoka sehemu ya juu ya kulia hadi ya chini ya kushoto ya moyo. Mapana ya aliyoyafahamu yalimtambulisha kama aliye sawa na wanamageuzi wengine. Hata hivyo mawasiliano ya mara kwa mara kati yake na calvin kuhusu wazo la utatu wa Mungu, hayakumrai na mamlaka yaliyotungwa ya Geneva, ambapo Calvin alikuja kudhibiti mfumo wenye nguvu wa mamlaka yanayoendeshwa na imani katika Mungu. Aliambia Calvin, “Injili yako haina Mungu mmoja, imani ya kikweli, matendo mema. Badala ya Mungu mmoja unaye Cerberus mwenye vichwa vitatu”¹²⁷ (mbwa anayesimuliwa mwenye vichwa vitatu wa ugiriki aliyelinda milango ya jehanamu). Aliendelea kumuambia Calvin, “badala ya imani ya kikweli unayo maono hatari ya uongo; na unadai kuwa matendo mema ni maonyesho matupu.”¹²⁸ Kwa maneno haya Servetus hastahili umaarufu, hata hivyo tusitilie shaka uadilifu wake au ujasiri wa msimamo wake.

Calvin, aliapa kumuua alipopata nafasi ya kufanya hivyo, kama ambavyo angelitaka Constantine. Servetus alinuia kuchapisha kazi moja zaidi, kwa lengo la kurejesha Ukristo katika hali yake ya kiasili iliyo safi na kuiweka huru kutoka kwenye dosari zilizokuwa zimeichafua imani. Calvin alipokea nakala kamili ya Servetus akiipiga vita kanuni ya imani ya utatu wa Mungu. Kupitia kwa mpatanishi/mwamuzi aliifanya kanisa katoliki kumtia Servetus nguvuni. Wakati wa kifungo chake alionyeshwa heshima na baada ya siku tatu alipewa ufunguo na msimamizi wa gereza na wafungwa ili apate kutembea bustanini. Alitoroka na kujiweka huru; lakini ilitokea kuwa matembezi ya mauti.

Uhuru wake ulikuwa wa muda mfupi tu. Kwa nia yake kuu ya kwenda “Naples”, “Italy”, kuendelea na kazi yake kama tabibu, alifanya maamuzi wa maafa wa kusafiri kupitia geneva. Hili lilikuwa eneo la Calvin. Kwa kutawala kiimla, alikuwa amejiimarisha mfumo wa utawala unaongozwa na kanuni za kidini. Servetus bila shaka

¹²⁵ Bohari la kawaida na maandiko yenye maoni ed. Andrews Norton (Cambridge, MA: William Hilliard, Oct., 1813), 4:37.

¹²⁶ Ibid. [Kama hapo juu].

¹²⁷ Ibid., 47

¹²⁸ Ibid.

na Wagalatia walijitetea kwamba kama angeshikwa angeonyeshwa huruma na wa protestanti wenzake kuliko ambavyo angetendewa iwapo angeshikwa na wakatoliki wenye mamlaka. Baada ya kutoroka kwake, alifanyiwa kesi bila kuwapo kwake na kanisa katoliki na kumhukumu “kuvutwa katika rikwama lenye sadi hadi mahali pa adhabu na pia kuchomwa na vitabu vyake akiwa hai (*tout vif*) kwa moto unaowaka polepole.”¹²⁹

Cha kusikitisha ni kuwa Servetus hakukubaliana na hali ya adui wake mprotestanti aliyekuwa amesema “akija na ikiwa katika hali yoyote ile kwa mamlaka niliyo nayo sitamuacha aondoke huru akiwa hai.”¹³⁰ Calvin baadaye alikiri, “Sifichi kuwa kwa amri zangu alitupwa gerezani.”¹³¹ Calvin angewatumikia waliomuomba msamaha wa kisasa vyema kama angaliandika aliyoyatenda na Servetus. Lakini si nadra kwa wafuasi wa kiongozi yeyote yule kujitia upofu na kuondoa kutoka machoni mwa umma hali nzuri za hulka za shujaa wao, bila kujali ukweli uliopo.

Servetus alipitia ukatili kamili wa Calvin. Baada ya kuteswa kwa kufedheheshwa, alifungwa kwenye kikingi kilicho na myororo wa chuma huku kitabu chake cha mwisho kikiwa kimefungiwa kwenye paja lake. Baada ya kumuomba mtesaji kutoendelea kumtesa zaidi, moto uliwashwa kwenye matawi machache ya mpingo. Alikawia katika utesaji kwa muda mrefu akilia kwa sauti iliyopenyeza, “Yesu, Mwana wa Mungu wa milele, nihurumie!” Mwishowe baadhi ya walioshuhudia, kutokana na huruma walimrushia vijiti vinavyowaka moto ili kukomesha mateso yake.¹³²

Hivyo maisha ya mtu mwadhimu ambaye kutalii kwake bililia kulimtia katika upinzani dhidi ya mprotestanti mgeusi mwenye ushawishi mkuu wa karne ya kumi na sita. Ijapokuwa kulikuwapo na kutoelewana kwa kihistoria kwokwote juu ya umaarufu na udhaifu wa hao wapinzani wawili katika matukio haya ya kimaafa ukweli ulio wazi ni kuwa, Servetus aliteketezwa kikingini kwa sababu ya kupingana na kanuni ya kidini-utatu wa Mungu. Alikufa kifo cha kikatili kwa kuthubutu kuchapisha kutokubaliana kwake kwa dhati na desturi iliyotukuzwa kutokubaliana alikokufanyia utafiti mzuri ambako muungaji mkono wake alihisi kuwa anatishwa. Kupita kwa wakati hakujafulu kufuta aibu hii inayotisha kutoka katika rekodi imarishi za kikristo.

Ingekuwa kosa kuamini kuwa upinzani wa kidini au usio wa kidini dhidi ya imani juu ya umoja wa miungu umejikita tu katika wakati wa zama za kale. Kupitia mbinu moja au nyingine, iliyo fiche au iliyo wazi, dhana ya Bibilia ya Mungu mmoja, baba, wa imani ya utatu ya paulo (1 wakorintho 8:6) imepata kufichwa chini ya maneno yanayokinzana, kauli na mazungumzo yaliyobanwa.

Shaka inatiliwa juu ya kanuni ya imani ya utatu wa uMungu kwa jinsi imani hiyo ilivyolindwa kwa njia ya fujo. Pana jambo lisilo sahihi juu ya funzo linalotolewa huku likichochea matukio ya kimaafa katika historia ya kanisa. Hilo fundisho la kanuni ya kidini ambalo hata wanaliunga wanasema halielezeki na ambalo maana yake inafahamika kidogo tu kwa akili yenye busara lilikuwa zao la njia ya kufikiri kigiriki. Ilikinzana na elimu ya sifa za Mungu na dini ya kihebrania ambamo Yesu na mitume wake walilelewa. Mungu wa Musa, Isaiah, Yesu na mitume alikuwa nafsi moja, baba. Moja haiwezi ikafanywa ikawa sawa na mbili ama tatu. Kinachoweza kufanyiwa moja ni kuivunja katika sehemu. Ivunje katika vijisehemu vidogo zaidi na haiwi moja tena. Ipanue, na hata kwa sarakasi kubwa za wanaokiri utatu wa uMungu, haiwezi ikafanywa mbili au tatu na ibaki kuwa moja. (Hivi si kusema Mungu hawezi akatumia maajenti kueneza ukuu wake. Lakini huu ni uhusiano wa kiamana). Mungu hatakubali uvunjaji au ugawanyishaji.

¹²⁹ Ibid., 56

¹³⁰ Ibid., 48

¹³¹ Ibid., 58

¹³² Ibid., 72

Ukristo ulipochukua hatua ya kwanza rasmi kulazimisha ugawaji wa Mungu katika vipande viwili (Baba na Mwana) ulijigawa wenyewe, si Mungu. Ndivyo ulimwengu wa Ukristo ulivyo hadi sasa; hauja ungana vile Yesu alivyoomba, ila umegawanyika katika madhehebu yanayopingana. Ukweli huu unapaswa kutufanya kuwazia swali la: ikiwa Yesu aliomba kuwa kanisa lake lingekuwa moja (Yohana 17: 20, 21), ombi hilo halikujibiwa? Yawezekana kuwa jamii ya kidini iliyogawanyika na kuchanganyikiwa ni Ukristo kijina tu? Yawezekana kuwa mwito wake wa kimsingi unatokana na kwenda kinyume na Biblia ambayo inadai kuwa sauti kuu kuwa ndicho kigezo chake?

Tukiweka kando mawazo ya kidhahamia ya wasomi wagiriki tukiacha ubishi kutokana na ufahamu tunaopata kutokana na utafiti wa kutaka utafiti wa kutegemea matangazo ya amri za misahafu, Biblia inatambua kuwa Yesu ndiye aliyekuwa Masiya, mwana wa Mungu. Hili ndilo funzo kuu la Agano Jipya. Hili ndilo tangazo la imani ya wakristo wa awali zaidi na hakuna haja ya kugeuza wanavyo chukulia mwokozi kwa kumuonyesha kama malaika wa kipekee aliyekuwapo kabla au kama Mungu aliyebadilika na kuwa binadamu.

Ni jambo la busara kuelezea sababu ya kubadilika mawazo kunako zua ugumu kwa wasomaji wa Biblia kutofautisha kati ya athari za desturi kutoka kwa mafunzo aili ya Yesu na mitume. Mkristo anayetafuta ukweli uliopo hataweza kuchanganyikiwa au kuogopa ukweli ya Biblia.

VII. HALI YA KUWAPO-KABLA KATIKA AGANO JIPYA

“Roho mtakatifu atakuja juu yako.... kwa ajili hiyo aliyemtakatifu atazaliwa na ataitwa mwana wa Mungu- Gabriel.

Katika desturi ya Ukristo, Agano Jipya limekuwa likisomwa kupitia matangazo ya awali ya upatanishi.. yaliomtaja Yesu kama mwana wa Mungu yalikuwa na maana tofauti katika karne ya kwanza na ile iliyokuwa nayo tangu kongamano la Nicea (325AD). Uzungumzi juu ya kuwapo kabla kwake kunadhamira kuashiria kupatikana kwa kusudio la kiungu kupitia kwake zaidi ya kuwepo kabla kwa aina ya kibinafsi.¹³³

Waumini wa makanisa maarufu ni waminifu kwa imani Fulani kuhusu Yesu, lakini wajuzi wa maoni ya kiawali ya ukristo wanashuku maamuzi ambayo kwayo funzo hilo la imani lilifikiwa. Wasomi wa agano jipya huuliza ikiwa agano jipya hufunza imani hiyo kwa vyovyote vile, nao wana historia hushangazwa na umbali uliopo kati ya Yesu mwenyewe na ukristo uliokomazwa kikamilifu. Maswali haya hayatulizi kwani yana ashiria kuwa ukristo waweza kuwa katika hali mbaya zaidi ya ilivyodhaniwa. Labda siyo ujenzi wa kimsingi tu unaohitajika kufanyiwa usasa, ila labda ujenzi upya wa kimageuzi. Agano jipya kamwe halipendekezi kuwa kauli “mwana wa Mungu” ina maana tu ya “Mungu”¹³⁴

Ilhali wanaoshikilia wokovu kama njia ya pekee ya kufanya mama hung’ang’ania kisawazishaji hicho kama kigezo cha kuchukuliwa kama kristo.

“Myahudi alipotaka kusema kuwa kitu kimepangiwa mwisho wake, alidai kuwa kilikuwapo tayari mbinguni.”¹³⁵ Hivyo kauli za kuwepo kabla”katika agano jipya zinahusiana na mipango ya awali ya kikomo cha mja. Wagiriki ndio walioelewa vingine mienendo ya kufikiria kwa wayahudi na kuishia duniani kutoka anga za juu. Yesu kama huyo ni binadamu lakini? Yeye ni Masiya kweli wa Israeli?

Wakristo wengi hivi sasa wanajizoea juu ya mambo ya kisiri yanayoathiri kanisa. Lakini wengi hawana habari kuwa mambo ya kidunia, mawazo ya kisiri yaliingia kanisa kwanzia Karne ya Pili kuendelea kupitia “baba wa kanisa” ambao walizama katika mambo ya ukafiri na waliojenga misingi ya matangazo ya imani ambayo kwa sasa yanaitwa “orthodox”(-enye imani sahihi). Mbegu ya imani katika utatu wa Mungu ilipandwa katika fikira ya Justin Martyr, mkristo wa Karne ya Pili aliyeona mfumo wa Plato kuwa ndio unaokaribiana na ukristo na akahisi kwamba hakukuwa na haja kuuacha ndipo kupata ufunuo mkuu zaidi wa Ukristo. Makundi yaliyopania kubadilisha kanuni za mitume yalitokana na ukafiri. Mazoea ya kimawazo yalitolewa na wasio katika kanisa yanatosha kuelezea uchafuzi wa kanuni za mitume ulioanza baada ya enzi ya mitume.”¹³⁶

Wakristo wenye busara wanapaswa kufahamishwa juu ya uchafuzi huu jinsi “unavyoenziwa” kama maandishi matakatifu na wengi . Utambulizi unamaanisha kujifunza tofauti kati ya ukweli uliofunuliwa na urafiki, mafunzo ya ulimwengu yaliyotoka nje ya Bibilia ilhali yaliadhiri kinachoitwa ‘orthodoxy’ sasa.

¹³³ Maurice Wiles, *Utenzi Upya wa Mafundisho ya Dini ya Ukristo*.

¹³⁴ Don Cupitt, *The Debate About Christ* (London: SCM Press, 1979), vii, 4.

¹³⁵ E.G. Selwyn, *First Epistle of St. Peter* (Baker Book House, 1983), 124.

¹³⁶ G. T. Purves, *The Testimony of Justin Martyr to Early Christianity* (New York: Randolph and Co., 1889) 167.

Tungemuomba msomaji awazie athari za maafa za kutotia maanani mienedo ya kufikiri kwa wayahudi inayopatikana katika Bibilia, iliyoandikwa nao (isipokuwa Luka). Ikiwa wayahudi hawamaanishi tunachoelewa kuwa 'kuwapo-kabla', basi twaweza kuwaelewa vingine juu ya mambo ya kimsingi kuhusu kuwa Yesu ni nani. Kuna tofauti kubwa kati ya kupangiwa mwisho na kuwapo kabla. Elimu ya mambo ya kigiriki iliaminisha kuwapo kwa 'Mungu wa pili', mpatanishi asiye binadamu. Kati ya muumba na ulimwengu. Yesu aliye kweli, hata hivyo ni 'Masiya binadamu' mpatanishi mmoja kati ya Mungu na binadamu (Tim 2:5). "Kwetu sisi wakristo kunaye Mungu mmoja baba... Na mfalme mmoja Masiya" (1 Wakorintho 8:6). Zingatia kwa makini fasili ya Paulo ya Mungu mmoja.

Agano jipya ni kitabu cha kiyahudi kweli kweli. Waandishi wake wote walikuwa wayahudi ila labda Luka (amabaye hata hivyo ni myahudi kama waandishi wengine katika hali yake iliyo wazi ya kuchangamkia wokovu wa kiyahudi) [Yohana 4:22] unaotolewa kuwa wote, wayahudi na wasio wayahudi). Wasomaji wa Bibilia wa kisasa wakizungushia handaki maswala yake ya kimsingi kwa mtazamo wa kigiriki wa maisha. Wameyarithi haya kutoka kwa makanisa na pia imani za kiBibilia za baadaye zilizopuuza ukweli kuwa Yesu alikuwa myahudi aliyefikiria na kufunza katika misingi ya kiyahudi.

Kunao mwelekeo usio wa kiyahudi katika Ukristo ambao kitamaduni, kiimani ambao lazima utambuliwe na pia upuuziliwe. Umeathiri vikubwa mafunzo ya imani ya kikristo. Umeathiri jinsi tunavyo elezea Yesu, amabaye ni Masiya.

Wazo kuwa roho hujitenga na mwili na kuendelea kuwepo katika hali ya kufahamu mbali na mwili ni wazo lisilo la kiyahudi kabisa (Hili limejikita katika Agano la Kale-na funzo la Agano Jipya juu ya hali ya binadamu lina misingi yake katika Agano la Kale). Wasomaji wa kisasa wa Bibilia hushangaa wagunduapo kutoka katika Bibilia kuwa binadamu mzima kufa na kuingia katika 'usingizi' na hurudishwa katika uhai kwa ufufuko pekee wa mtu mzima. Ukristo wa kitamaduni hung'ang'ania kimakosa kuwa binadamu anayo "roho inayodumu milele" baada ya kifo. Wasomaji wengi wa Bibilia hawajazingatia kauli ya "*Interpreter's Dictionary of the Bible*:" hakuna maelezo yoyote ya Bibilia yanayo kubali kauli hii kwamba 'roho' imetenganishwa kutoka kwa mwili wakati wa kifo."¹³⁷

Wazo kuwa Yesu alikuwa hai kabla ya kuzaliwa kwake bethlehemu pia ni wazo lisilo la kiyahudi kabisa. Binadamu hawi kabla ya kuzaliwa kwao kuligana na wayahudi. Kuwepo kabla kwa roho ni kwa ulimwengu wa mawazo ya kigiriki na kushikiliwa na baadhi ya uongozi wa kanisa (hasa Origen aliye na mtazamo katika usini wa mambo ya kiulimwengu.) Lakini hawakulitoa wazo hili kutoka kwa Bibilia.

Kuwa radhi kukubali kuwa tumehadaiwa na kwamba hatujapata kuwa na habari za kutosha kutuwezesha kufanya maamuzi mazuri juu ya maswala ya Bibilia, ni sehemu ya kukua kikristo.

Ukweli mmoja muhimu sana tunaapaswa kujua kabla ya kujaribu kuelewa kuwa Yesu alikuwa nani ni:

Myahudi aliposema kuwa kitu kilikuwa kimepangiwa mwisho alikuwa amekidhania kwamba tayari 'kilikuwapo' katika kiwango cha juu cha uhai. Historia ya dunia hivyo basi imepangiwa mwisho kwa kuwa tayari imekuwapo kabla na kwa hivyo imekitwa, katika hali fulani. Imani hii ya kipekee kwa

¹³⁷ Ed. G.A. Buttrick (Nashville: Abingdon Press, 1962), 1:802. See further our article, "Do Souls Go to Heaven?"

wayahudi inaweza kutofautishwa na ile ya wagiriki ya kuwapo kabla ikitawaliwa kabla na wazo la *'kuwapo kabla' katika kusudi la kiungu.*¹³⁸

Msomu wetu anaendelea hatua zaidi kuambia kuwa jinsi hii ya kipekee ya kiyahudi imeelezwa vyema katika 1 Petro. Hili mara moja latukumbusha kwamba peter hakuacha mienendo yake ya kiyahudi ya kufikiri (kurejelea Bibilia ya kiebrania) alipokuwa mkristo. Barua ya Petro imeanwaniwa kwa *'wateule kulingana na ujuzi kabla ya Mungu babu (1 Petro.1:2)'* Peter aliamini kuwa wakristo wote walijulikana kabla, lakini hilo halikumaanisha kuwa sote tulikuwepo kabla!

Mafunzo ya Petro juu ya mustakabali wa vitu yameingiliwa na wazo sawa la kwamba yote yamepangwa kabla katika mpango mkuu wa Mungu. Mungu anayaona yote yakiwa yamepangwa mbele yake. Wote walio na vipaji vya roho watashiriki mtazamo wa Mungu na katika imani kutambua kuwa uhalisi katika mipango ya Mungu katika mustakabali itakuja kwa uhalisi duniani. Kwa maoni ya Petro Masiya mwenyewe *alijulikana kabla, si kifo chake tu kwa ajili ya dhambi zetu, lakini pia Masiya mwenyewe (1 Petro 20) Petro anatumia neno lilo hilo kuelezea 'kuwapo' kwa mwana wa Mungu katika mpango wa Mungu alivyofanya kueleza 'kuwepo kwa' kanisa la kikristo (v.2).*

Ijapokuwa Masiya alijulikana kabla (kama Jeremiah alivyokubaliana kabla kuzaliwa kwake, Jer 1:5), aloinyeshwa kwa kuzaliwa kihalisi (Luka 1:35) hii ni njia ya kipekee ya kiyahudi ya kuelewa kusudi la Mungu kwa binadamu. Mungu hutimiza mpango wake kwa wakati unaofaa.

Aina ya *'kuwapo kabla'* anakowazia Petro ni aina inayopatikana na mazingira ya kiyahudi, si ile ya kigiriki ya Ukristo wa aina ya baada ya kuwapo kwa Bibilia. Hatuna haki ya kusema kwamba peter alikuwa na uzoovu wa wazo la kuwapo kabla kwa kristo pamoja na Mungu kabla ya kutwaa utu [kwa hivyo hatuna haki ya kudai kuwa Petero aliamini katika utatu wa uMungu] wazo hili halidokezwi anapoelezea kristo kama *"aliyejulikana kabla ya kuanzishwa kwa dunia"*, kwani wakristo pia ni vyombo vya kujua kabla kwa Mungu. Tunachoweza kusema ni kwamba kauli *'pro kataboles kosmou'* [kabla ya kuanzishwa kwa dunia] inathibitisha jukumu la Yesu na umuhimu wake mpana Petro hajaeneza imani yake katika uMungu wa kristo kwa uthibitisho wa kuwapo kabla kwake: Ukristo wake ni kama ule wa sura za awali matendo ya mitume kuliko ulivyo wa Yohana na Paulo.¹³⁹

Peter, kama mtume anayeongoza (Mathayo 10:2) hangehurumia aliyeamini utatu wa uMungu au aliyekana uungu wa Yesu (cp. modern Jehova 's Witness).

Kwake Peter pia tunatambua kuwa uokovu wa siku zijazo wa wakristo, ufalme watakaorithi Yesu arudipo, wasubiri huko mbinguni tayari kufunuliwa *'wakati wa mwisho'* (1Pet.1:5) hivyo basi kuja kwake kwa pili kutakuwa kufunuliwa kwa hali iliopo sasa lakini iliyofichwa kutoka machoni mwetu. Kwa hivyo imesemekana kuwa Yesu *'alijulikana kabla'* anasubiri kufunuliwa kwa wakati mwafaka wa Mungu. (1 Petro. 1:20) Ufalme wala Yesu vilikuwepo kabla. Vilipangwa kabla ya kuanzishwa kwa dunia. Paulo anatumia wazo la lugha hiyo hiyo kuhusu mustakabali wa ufufuko na kuishi milele kwa watakatifu. Anasema kuwa tayari tunalo jengo kutoka kwa Mungu, nyumba inayofaa kwa

¹³⁸ E.C. Dewick, Primitive Christian Eschatology, The Hulsean Prize Essay for 1908 (Cambridge University Press, 1912), 253, 254, emphasis added.

¹³⁹ E.G. Selwyn, First Epistle of St. Peter, 248, 250. Tunakataa kwamba wazo la Petro la Yesu ni tofauti na ile ya Paulo na Yohana. Huenda ikawa kuwa Mitume awakusikizana kwa wazo linalomtambua Yesu ni nani.

enzi ijayo (2 Wakorintho 5:1).¹⁴⁰ Mwili wetu utakaofufuka baadaye tayari upo katika makusudio ya Mungu na huweza kufikiriwa kuwa halisi kwa kuwa ni hakika utaonyesha katika siku zijazo. Katika hali hiyo ‘tunao’ ijapokuwa bila shaka hatunao kwa kweli. Ndivyo ilivyo kwa hazina tuliyo nayo mbinguni. Imeahidiwa kwa mustakabali wetu. Tutapokea tuzo la urithi (Wakolosai 3:24) Kristo atakapokuja siku zijazo.

Mpango Baada Badala ya Hakika ya Kuwepo Kabla

Baada Ya Kufahamu Ukweli Huu Wa Kimsingi Wa Kimawazo na elimu ya kidini ya kiyahudi (na kiBibilia), itakuwa vigumu kugeuza kidogo kuelewa kwetu kwa mafungu mengine ambamo mawazo sawa ya ‘kuwapo’ yanayofuatwa na kudhihirika kwa hakika kunapatikana. Yesu anasema katika Yohana 17:5: nitukuze mimi (sasa) kwa utukufu niliokuwa nao nikiwa nawe kabla ya kuanzishwa kwa dunia” kwa kurejelea 2 kor.5:1 Mkristo katika siku zijazo, baada ya ufufuko wakati wa kurudi kwake Yesu, atakuwa na uwezo wa kusema kuwa sasa amepokea kile “alichokuwa nacho” tayari, yaani, alichotayarisha katika mpango wa Mungu. Wakristo husema kuwa wanayo hazina mbinguni (Marko.10:21), yaani tuzo iliyohifadhiwa na Mungu sasa iliyopangwa kutolewa siku zijazo. Hivi ni kusema tu kuwa siku moja katika siku zijazo watarithi ufalme waliotayarishiwa tangu kuanzishwa kwa dunia (Mathayo 25:34).

Yesu anaposema kuwa ‘alikuwa na’ utukufu aliofahamu kuwa alitayarishiwa na Mungu tangu mwanzo (Yohana 17:5),¹⁴¹ utukufu huo upo katika mpango wa Mungu, na katika hali hiyo Yesu alikuwa tayari anao. Tunazingatia kuwa Yesu hakusema “nirudishe” au “rejesha kwangu utukufu niliokuwa nao nilipokuwa nawe kabla ya kuzaliwa kwangu.” wazo hili lingekuwa geni kabisa kwa dini na desturi za kiyahudi. Hapana haja na pia ni kosa kusoma mawazo ya wasio wayahudi ndani ya maandishi ya misahafu ilhali tunaweza kuyaelewa vizuri jinsi yalivyo katika mazingira ya kayahudi. Ni wajibu wa wanaoamini kuwapo kabla kihakika kuonyesha kuwa maandishi hayo hayawezi kuelezwa katika hali yao yenyewe ya kiyahudi. Na lazima ikumbukwe kuwa Bibilia ya kihebrania, iliyo na mengi ya kusema juu ya mtarajiwa, mwana wa Mungu, haitoi kauli inayodokeza kuwa Masiya alikuwa Mungu aliyepangiwa kuwasili kutoka mbinguni alikokuwa tayari kutokana na kuzaliwa kabla. Wazo kuwa Mungu anaweza kuzaliwa kama binadamu ni geni katika mazingira ya wayahudi ambamo Yesu alielimshwa. Mageuzi ya Wagalatia inahitajika kwa waanzilishi wa wazo jipya kama hili.

Kinachoitwa “kuwepo kabla” kwa Yesu katika Yohana hurejelea 'kuwepo' kwake katika mpango wa Mungu. Kanisa limeadhiriwa na kuingizwa kwa lugha isiyo ya kiini. Kuna neno zuri kabisa lenye maana chalisu 'ya kuwepo kabla' katika lugha ya kigiriki (*pro uparchon*). Ni wazi kuwa halitokei popote katika maandishi matakatifu likirejelea Yesu, lakini linatokea katika maandishi ya akina baba wa makanisa wa karne ya pili. Wafafanuzi hawa wagiriki wa maandishi matakatifu walikosa kuelewa viwango vya kufikiri vya kiuibraniya ambamo Agano Jipya limeandikwa.

Maoni ya kiBibilia juu ya Yesu kabla ya kuzaliwa kwake yana husiana na “kuwepo” kwake katika mipango ya Mungu. Kuwepo kabla katika Bibilia haina maana. Sawa na iliyotokea katika imani za baadaye: kuwepo kunakojulikana kwa mawana wa Mungu kabla ya kuzaliwa kwake ni wakati ambapo alikuja ulimwenguni na hali yake ya kibinadamu kupitia kwa uzazi wa mamake. Katika maandiko matakatifu, Yesu anazaliwa

¹⁴⁰ Huu ndio tafsiri sahihi wa aionios, i.e., mali ya kuja kwa umri ya nchi, sio “ya milele.” Hii haimaanishi kuwa mwili wa wakati ujao ni wa wakati. Inatia maisha ya milele na inaishi milele. Pato la mwili ni tukio kuu ka kuja kwa umri iliyotangazwa na ufufuko.

¹⁴¹ Muhtasari wa kueleza wazo sawa ni kuzungumza juu ya nchi ya ufalme “iliyotayarishwa kabla ya ujenzi wa dunia” (Mathayo 25:34)

kutoka kwa Maria (Mathayo 1:16). Kiajabu, katika Karne ya Pili, Justin Martyr anaanza kuzungumzia kuja kwa Yesu kupitia kwa mamake.

Maana inayopewa dhana ya kuwepo kabla na wayahudi na Biblia ni muhimu sana kwake Yesu kwa ajili ya kujielewa kama mwana na binadamu. Mwana wa binadamu anapatikana katika kitabu cha Danieli. Yuko katika kuwepo kabla ila tu katika hali ya kuwa Mungu anatupa kumwona-binadamu-katika mpango wake wa siku zijazo. Mwana wa binadamu ni binadamu-maneno yanamaanisha hivyo. Hivyo tu kile ambacho Yohana anataka tuelewe ni kuwa Masiya aliyepata binadamu alikuwa mbinguni kabla ya kuzaliwa kwake (Katika mpango wa Mungu) na alionekana katika maono ya danieli ya siku zijazo (Dan. 7; Yohana 6:62). Wakati wa kupaa kwake, Yesu alienda juu katika mahali/nafasi aliyokuwako ametayarishiwa mbeleni na Mungu katika mpango wake. Hakuna habari inayosema kuwa Yesu alirudi (*upostrepho*) kwa Mungu, ingawa wazo hili limeingizwa kimakosa katika baadhi ya tafsiri za kisasa za kiingereza ili kutetea imani halisi kutafsiri huku kubaya kwa kigiriki “kwenda kwa Mungu” kuwa “kurudi kwa Mungu” kunatia maana tofauti.¹⁴² Tafsiri za Biblia hupendelea desturi za enzi ya baada ya kufungwa kwa Biblia kuhusu Yesu.

Mwana wa binadamu sio malaika. Hakuna malaika aliyepata kuitwa 'Mwana wa binadamu' (= mmoja wa jamii ya binadamu- nemsu aliyependwa sana Yesu wa sababu nzuri). Kumsema Masiya kuwa ni malaika kungekuwa kuvuruga viwango. Hivyo basi wasomi wanaoripoti kuwa wazo la kuwepo kabla kwa Masiya “antecedent kwa kuzaliwa kwake Bethlehemu kunajulikana kama uyahudi.” Kulingana na yote yaliyotabiriwa kumuhusu katika agano la kale anatokana mwanzo wake katika wanadamu: Uyahudi haujawahi kutambua jambo lolote la kuhusu kuwepo kabla kwa Masiya antecedent ya kuzaliwa kama mwanadamu (Dalman, *Words of Jesus*, pp. 128-32, 248, 252). Kujitokeza sana kwa wazo hili katika mambo ya wayahudi hakuwezi kuchukuliwa kuwa jambo la dharura. Wayahudi hawakujua lolote kuhusu kuwepo kabla [kawaida bila maana ya kindani] Kwa Mwanaume (mtu).¹⁴³

Kudai “kuwa kabla Abrahamu” (Yohana 8:58) hakumaanishi unakumbuka kuwa hai kabla ya kuzaliwa. Hivyo ni kufikiri kama Mgiriki anayeamini kuwepo kabla kwa roho ya binadamu. Kwa mafikira ya waebania katika Agano Jipya mtu anaweza “kuwepo” kwa mpango wa Mungu kama ilivyokuwa madhabau, hekalu, toba na misingi mingine ya maana ya utakatifu. Hata Musa alikuwepo kabla kwa jinsi hiyo kulingana na msemo tutakaotumia baadaye. Mtume Yohana angeweza pia kusema kuwa Kristo “alisulubiwa kabla ya uanzilishi wa dunia” (Ufunuo 13:8). Hii inaonyesha ono muhimu, jinsi waandishi wa Agano Jipya walivyoelewa “kuwepo kabla”.

Kuna mifano mingi sana ya muda uliopita katika Biblia ya Kihebrania inayoashiria matukio ya wakati ujao. Ni ya wakati “uliopita” kwa sababu inaelezea matukio yaliyodhibitiwa kwa shauri ya Mungu na hivyo basi yatakayotokea kwa hakika. Wasomaji wa Biblia wanapuuza jinsi wayahudi walivyofikiria wanaporukia kuamini kuwa Yesu aliposema huwa “alikuwa nao” utukufu na Baba kutoka mwanzoni mwa ulimwengu (Yohana 17:5), alimaanisha kuwa alikuwa hai wakati huo. Kwa hakika katika dhana ya kimagharibi maelezo ya kiasili yana maana kiasi. Lakini si tusimfanyie Masiya heshima aje, kwa kujaribu kuyaelewa maneno yake katika mazingira ya kihebrania? Biblia haiwezi kutafsiriwa kwa mwanga wa maana yake halisi na wala si ile ya maandishi ya baadaye?

¹⁴² Ona NIV Yohana 16:28 na 20:17.

¹⁴³ Charles Gore, *Belief in Christ* (London: Yohana Murray, 1923), 31.

Kutokuwapo Kwa Kuwapo Kwa Yesu Katika Mathayo, Marko na Luka

Kuna kimya kikuu katika Mathayo, Marko, Luka, Matendo ya Mitume na Petero na Agano Jipya nzima juu ya kuwapo kabla halisi kwa Kristo. Licha ya kutodokezea, Mwana binadamu wa Mungu aliyekuwapo kabla, wanakinza wazo hilo kwa kuzungumzia asili ufunguo (mwanzo) wa Yesu (Mathayo 1:18) na kuzaliwa kwake kama mwana (Mathayo 1:20) katika tumbo la uzazi la Maria huku kungekuwa kuzaliwa kwa pili kwa wanaopinga, kwa vile wanafikiria kuwa Yesu alizaliwa milele hata kabla ya kutungwa katika tumbo la uzazi la Maria.¹⁴⁴ Tazama kwamba wale wafuasi wa Arian, na wale walioamini dokeo la Mungu katika nafsi tatu waliamini kwamba Yesu alikuwapo kabla ya kuzaliwa kwake. Hii ni kama kuzaliwa kwa Yesu mara mbili.¹⁴⁵ Luka hajui lolote kuhusu wazo hili. Wasomaji wasio na chuki bila sababu watamuona Yesu aliye katika Mathayo, Mariko, Luka, Matendo ya Mitume na Petero ni binadamu anayetokeza wakati wa kutungwa kwake katika tumbo la uzazi na kuzaliwa kama binadamu wengine wowote; hayakuwapo kabla. Mathayo anazungumzia hata mwanzo wa Yesu katika Mathayo 1:18.

Yohana anafunza, kwa kulazimisha, aina tofauti ya maelezo ya Yesu katika injili mbali na wawazavyo Mathayo, Mariko na Luka-mmoja ambaye ni malaika haswa au Mungu anayeonekana kama binadamu. Aina hii ya Masiya asiye binadamu ni wazo geni sio tu kwa Agano Jipya, lakini pia kwa ufunuo wa Mungu katika Agano la Kale katika kurejelea fasili yake ya Masiya mtarajiwa. Kumbukumbu la Torati 18:15-18 inajulisha kwamba Masiya atatokea kutoka familia mojawapo za Israeli. Masiya anaelezewa katika maandishi hasa kuwa si Mungu ila mwakilishi wa Mungu aliyezaliwa katika familia mojawapo za Israeli. Wayahudi wote waliotazamia kuja kwa Masiya walitarajia binadamu, si malaika, wala Mungu mwenyewe! Ingawa wayahudi hawakuwa wameelewa kuwa Masiya angezaliwa kimaajabu, hata kuzaliwa huko kimiujiza kulitabiriwa (Isaya 7:14; Mathayo 1:23).

Hata hivyo hakuna pendekezo la Masiya binadamu aliyekuwapo mbeleni, kulingana na Isaya 44:24 Mungu hakuwa na mshiriki wakati asili wa kuumba. Yesu katika injili anahusisha uumbaji na Mungu Baba na hana kumbukumbu yake kuwa mwakilishi katika mwanzo wa uumbaji (Mariko 10:6, Mathayo 6:30, 16:4 Luka 12:28). Ikiwa Yesu ndiye aliyekuwa muumbaji wa mbingu na dunia mwazoni, kwa nini hana kumbukumbu hiyo? Mbona anasema moja kwa moja kuwa Mungu ndiye muumba? Jibu ni kwamba Yesu alielekezwa na misingi ya maandishi matakatifu ya kibibilia aliyopata na ambayo hakuyavunja.

Roho wa Mungu yupo kwa wanaoamini. Wanapojifunza kufikiria jinsi anavyofikiria Mungu, watahiriki wazo kuwa "Mungu huzungumza vitu visivyokuwapo kama kwamba vilikuwapo" (Warumi.4:17). Ni kosa kuchanganya 'kuwapo' katika mpango wa Mungu na kuwapo halisi kabla halisi, hivyo kuumba Yesu ambaye si binadamu kamili. Yesu aliyetarajiwa kibibilia ni binadamu, aliyetungwa kimaajabu.

¹⁴⁴ Kumbuka makosa ya kutafsiri katika nakala zetu: maandishi hayana maana ya kutungwa mimba bali "kutwaliwa" na Baba kupitia kwa roho mtakatifu. Ni matendo ya Baba yanayofanya kuwapo kwa mwana. Mwana wa Mungu Masiya ni mtu ambaye ameumbwa kwa njia isiyo ya kawaida, Adamu wa pili. Kumbuka pia katika Matendo ya Mitume 13:33 maelekezo ya "Kuamshwa" kwa Yesu, kulio na maana ya Mungu kumfanya awe. Aya ya 34 inataja ufufuko wake uliofuata. *King James Version* inapoteza tofauti hii muhimu.

¹⁴⁵ Justin Martyr ndiye pengine baba wa kwanza wa kanisa kuongea kuhusu kutwaliwa kwa mwana kabla ya mwanzo (kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu). Lakini hajapeana maandishi matakatifu yanayoshikilia maoni hayo ya kutwaliwa kwa mwana. Kulingana na Bibilia kama wanadamu, wakati wa kutungwa kwake katika tumbo la mamake. Justin anatofautiana na mathayo kwa kusema kuwa mwana alikuja "kupitia" Maria. Mathayo anashikilia kuwa alikuja kutoka Maria. Hii inaashiria ule mtazamo au mafikiria yaliyotokea kufikia 150AD, Mtazamo mpya uliokuwa mbegu ya Uanzilishi wa Utatu.

Utukufu mkuu wa manufaa anayoleta alijaribiwa lakini Mungu hawezi kujaribiwa (Yakobo 1:13).

Mtume 'Mwamba' ambaye Yesu aliteuwa “Kulisha Kondoo wangu” amepata funzo nzuri ajabu juu ya jinsi ya kuelewa maana ya kuwepo kabla kama ufahamu wa awali na kupingiwa mwisho mwanzoni. Utambuzi wa Petero wa Yesu kama Masiya ulikubaliwa kwa bashasha na Yesu (Mathayo 16:16-18) Petero na Yohana walielewa utukufu aliokuwa nao Yesu tayari ni sawa na utukufu waliokuwa wamepeleka waumini wa wakati wa Yesu. (Yohana 17:22). Hili linamaanisha kuwa vitu katika mipango ya Mungu 'huwapo' kwa dhana na wala si kuwapo kiasili. Lazima tuchague iwapo tutaelewa lugha ya Agano Jipya kama Wamerikani au Wayuroa au tunahurumia Yesu na desturi yake ya Kiyahudi. Mstari katika kitabu cha Ufunuo unazungumzia vitu 'Kuwapo' kabla kuumbwa kwao,” vilikuwa na vikaumbwa” (Ufunuo 4:11).¹⁴⁶ 14 Kuumbwa kwao kulitokana na mpango asili wa Mungu kuvileta katika hali ya kuwa.

Ufahamu wa misingi ya Agano Jipya unafunua kuwa wayahudi waliamini kuwa Musa 'alikuwapo kabla' katika mipango ya Mungu na sio kama binadamu aliyepo hasa

Kwa kuwa hiki ndicho alichuamuru mfalme wa dunia: Aliumba dunia kwa niaba ya watu wake, lakini hakufanya kusudi la uumbaji kujulikana tangu mwanzo wa dunia ili kuniwazia mimi [Musa], niliyetayarishwa tangu mwanzo wa dunia kuwa mpatanishi wa agano (Ushuhuda wa Musa, 1:13,14).

Ikiwa Musa aliamriwa katika mpango wa Mungu, ni jambo lenye maana wazi kuwa Masiya mwenyewe alikuwa ndiye sababu ya Mungu kuumba vitu vyote. Hivyo basi yawezekana kusema kuwa vitu vyote viliumbwa kwa niaba ya Yesu. Kwa ajili ya heshima kwa mpango wa Mungu uliofunuliwa na ya mwokozi binadamu, inabidi tutafute kuelewa hali yake katika muktadha wake wa kiebrania.

Kauli safi ya jinsi wayahudi wanavyochukulia “Kuwepo kabla” imetolewa na msomi mnowejia Mowinckd katika kitabu chake kiitwacho “*He that cometh*”.

Kwamba onyesho lolote la mpango wa Mungu kwa ulimwengu, na nia yake ya wokovu, vilikuwa katika mawazo yake au katika 'neni' lake kuanzia mwanzo ni njia halisi ya kusema kuwa si kibahati ila kudhihirika na uonyesho wa kuwepo kwa Mungu mwenyewe. [Cp Yohana Neno lilikuwa na Mungu na lilikuwa Mungu”]. Dhana hii inayopewa kuwepo kabla inaonyesha umuhimu wa kidini wa hali ya juu zaidi. Mafunzo ya kidini ya kirabi yanaongea juu ya sharia, juu ya kiti cha enzi chenye utukufu cha Mungu, juu ya Israeli na vyombo vingine muhimu vya imani kama vitu vilivyokuwa vimeumbwa na Mungu, na vilikuwapo tayari naye kabla ya kuumbwa kwa dunia. Hiyo ndiyo hali ilivyo hata kwake Masiya. Inasemekana jina lake lilikuwapo naye Mungu mbeleni mbinguni, kwamba liliumbwa kabla ya dunia na kwamba linadumu milele.

Urejeo hapa basi si kwa kuwapo kabla halisi. Hivi ni wazi kutokana na hali ya kuwa Israeli imejumuishwa miongoni mwa vilivyokuwapo kabla. Hili halimaanishi kuwa Israeli kama taifa au mzimu wake ulikuwepo mbinguni zamani, ila kwamba jamii ya Israeli, watu wa Mungu, walikuwapo tangu milele katika mawazo ya Mungu, kama dhana

¹⁴⁶ Utumizi wa kitenzi “kuwa” kunavutia ukitazama maandiko badala katika Yohana 17:5 yanayosema “Utukufu uliokuwa nao”. Hii ni taarifa kuhusu kuwepo kabla kwa utukufu (wala sio Yesu kabla kuwa binadamu) ambao Yesu aliomba uwekwe ndani yake (Yohana 17:5) na pia kwa wafuasi wake (Yohana 17:22). Tazama Raymond Brown *The Gospel According to John, Anchor Bible (New York: Doubleday, 1966)*, 743. Kumbuka pia kwamba Augustino na wapekuzi wengine wengi hawajapata ushahidi wa kuwepo kabla kiasili katika Yohana 17:5

kubwa katika nia yake. Hili rejeleo ni la kweli kuhusu kuwepo kabla kwa Masiya. Ni jina lake, na wala si Masiya mwenyewe, anayesemwa kuwa aliyekuwapo pamoja na Mungu kabla ya uumbaji. Katika *Pesikta Rabbati 152b*, wanasema kuwa “kuanzia mwanzo wa uumbaji wa dunia mfalme Masiya alizaliwa, kwani alizuka mawazoni mwa Mungu kabla ya kuumbwa kwa dunia.” Hii inamaanisha kuwa tangu milele ilikuwa mapenzi ya Mungu kwamba Masiya anapaswa kuja katika uwepo, kutimiza lengo la milele la Mungu la wokovu.¹⁴⁷

Madai yaliyoanzishwa na (Gentile) Mataifa, wenye mafikira ya kifilosofia ama "wababa wa kanisa" kuwa Yesu alikuwa pengine "Mwanachama" wa Mungu Msimamizi (kiasili) ama malaika aliyeumbwa. Pendekezo linalotolewa na wasio wayahudi kwamba Yesu alikuwa nafsi ya pili ya Mungu mkuu au malaika aliyeumbwa, lilianzisha tatizo kuu la hali ya Yesu kuhusishwa na Mungu mkuu na kuweka ukungu ukweli kuhusu Masiya wake na injili juu ya uMasiya kuhusu ufalme. Yesu Wanazareti alitokea kuwa neno linalotajwa katika Yohana 1:1 (Yohana 1:14).¹⁴⁸ Ndiye onyesho la kipekee, kama binadamu, wa busara ya Mungu. Ndiyo busara ya Mungu iliyokuwapo tangu mwanzo na busara iligeuka kuwa binadamu alipotungwa Yesu kazini. Elezo hili linadumisha imani kuu kwamba Mungu aliye mmoja ndiye baba na kwamba Yesu ni mflame Masiya, si mfalme Mungu.¹⁴⁹ Wagiriki waanzilishi, mababa wa kanisa, ndio walio vuruga imani ya wayahudi/wakristo juu ya imani katika Mungu mmoja kwa kuingiza dhana ya “Mungu wa pili kihesabu.”¹⁵⁰

Ni muhimu kuwa Paulo anaeleza kwamba injili ilikuwa imefichwa katika mipango ya Mungu.¹⁵¹ Alikuwa kuwapo kutokana na mwanamke kutoka katika ukoo wa Daudi (Wakolosai 4:4; Warumi 1:3) Ni jambo lisilofikirika kuwa Paulo angeamini kuwapo kabla kwa mwana. Ingekuwa uongo kusema kuwa mwana alipata kuwa pale alipozaliwa, kama kweli tayari alikuwapo daima. Ni jambo la kibusara zaidi kudukulia kwamba Paulo alikubaliana na Petero kwamba Masiya alifichwa katika mpango ya kiungu kisha kufumuliwa wakati mwafaka uliokamilika.¹⁵² Paulo aliamini kuwa katika Yesu “vitu vyote vimeumbwa” (Wakolosai 1:16). Hakusema kuwa viliumbwa “naye.”

Kumaliza, ni jambo lisilo la busara kudai kuwa “hekima” katika ‘Methali’ (yaani, “*Lady Wisdom*”) ilikuwa Yesu, mwana, akiwapo kabla. Lisiwe jambo gumu kuelewa kuwa busara/hekima hapa ni uhuishi wa sifa ya uungu, si mtu. Thibitisho la hili halipatikani tu katika tahariri kuu ila wazi kabisa katika andishi lenyewe. “Mimi hekima, ninaishi kwa uwekevu” (Methali.8:12). Kama hekima ni (mume) mwana wa Mungu, hekima ni nani basi?

Malengo ya kuwapo kabla na uhuishi wote ni sehemu za fasihi ya kiyahudi lakini kuwapo kabla, na Masiya asiye binadamu siyo. Masiya asiye binadamu ni dhana inayokaribiana na dhana ya kirafiki ya kuwapo kabla kwa roho. Kuingilia mapema kwa urafiki ndiko kulikoanzisha, kwa bahati mbaya, uchafuzi wa imani, vile walivyoonya Petro na Paulo. (2 Petero 2; Matendo ya Mitume 20:29-31).

¹⁴⁷ Transl. G.W. Anderson (Nashville: Abingdon, 1954), 334, masisitizo yanaongezwa.

¹⁴⁸ Yesu anachukua umbo la Hekima ya Mungu na pia umbo la "wokovu" wa Mungu (Luka 2:30)

¹⁴⁹ Kumbukumbu la Torati. 6:4; Mariko. 12:29ff.; 1 Wakorintho. 8:4-6; 1 Timotheo. 2:5; Yohana 17:3; 5:44.

¹⁵⁰ Justin Martyr, Dialogue, 56, 62, 128, 129. Justin aliamini kuwa Mwana alitwaliwa kabla kuumbwa kama ilivyo katika Mwanzo.

¹⁵¹ Waefeso 3:9; Wakolosai. 1:26; 2 Timotheo. 1:9; Tito. 1:2; cp. 1 Petero. 1:20; Ufunuo. 13:8.

¹⁵² Tunakumbuka kuwa James Dunns anapinga kwa haki matamshi ya Cranfield kuhusu Warumi 1:13 "bila kushughulikia utumizi wake wa vitengo visivyofuata mpangilio, Cranfield anaendelea kuhoji kwamba Paulo alidhamiria kudhibiti utumizi wa "nani alikuja kuwepo" kwa ubinadamu ambao yule mmoja (Mwana wa Mungu, v.3) aliouchukua." (Warumi 1-8).

Matokeo ya kuingiliwa kwa ukafiri ni taarifa za ajabu kuhusu Yesu. Kuwapo kwake kabla kiutu kunaashiria ukweli kuwa yeye si binadamu halisi. Amekuwapo kama malaika kabla ya kuzaliwa. Hii ni dhana inayokaribiana na “kuja kwa miungu kwa mfano.” (Matendo ya Mitume 14:11). Yesu wa aina hii ni mfano wa mwokozi kafiri. Kulikuwa na waokozi wengine aina hii wa kiduma katika maeneo ya Ugiriki na Roma. Lakini Masiya aliyekuwapo ni mmoja tu, ambaye utambulisho wake ulitolewa kitambo kabla ya kuzaliwa kwake. Alijulikana kabla (Petero 1:20) na angechipuka kutoka nyumba ya Israeli kama muisraeli wa kabila la Judah. (Kumbukumbu la Torati 18:15-18; Matendo ya Mitume 3:22; 7:37). Andiko hilo maalumu la Kumbukumbu la Torati kwa hakika linasema kuwa mwakilishi wa Mungu aliyeahidiwa hangekuwa mfalme Mungu, ila msemaji wake. Wakristo wanapaswa kuwa makini kudai kuwa waaminifu kwa mwokozi huyo. Kuabudu mwokozi kwa dhana zenye makosa kumhusu kunazua hatari ya kuabudu mwokozi mwingine. *Imani ya Yesu ndiyo imani sahihi kwa Wakristo* (Mariko 12:29).¹⁵³ Kuna wasomaji wengi wanavyojua imani hiyo si ya aina ile ya utatu wa uMungu. Mungu, mmoja wa Israeli na wa Yesu ndiye baba,¹⁵⁴ ”Mungu mmoja na pekee” (Yohana. 5:44) ”Mungu pekee wa kweli” (Yohana 17:3).

Yohana 1:1

Usomaji kuhusu kuwa Kristu ni nani, unahusiana na kauli juu ya uhisiano wa Yesu na Mungu mmoja wa Israeli. Hapana shaka kwamba kwa wakristo watangulizi Yesu alikuwa na thamani na uhalisi wa Mungu. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa walimdhania “kuwa alikuwa Mungu.” Imechukuliwa na baadhi kwamba Yohana anamwonyesha Yesu katika hali ya uungu ambao ungevutia watu katika ulimwengu wa Ugiriki waliowazia dhana katika hali isiyoeleweka iliyozelewa nao. Imani thabiti inam dai Yohana kama kiunganishi kati yake na ulimwengu wa uungu wa kigiriki-uungu uliosadia kufinyanga Yesu wa mabaraza ya kanisa.

Tunapendekeza kwamba inatupasa kwanza kuona ikiwa Yohana anaweza kueleweka katika hali yake ya mtazamo wake ambao kwa vyovyote vile ni wa kiyahudi. Mbona tujaribu kumsoma Yohana kana kwamba alikuwa mwanafunzi wa myahudi Philo au wa dini isiyofahamika ya asiye myahudi? Mbona Yohana adaiwe kuwa muungaji mkono mafunzo ya kidini ya mabaraza ya kanisa ya baadaye? Si inatupasa kumuelewa kutoka ulimwengu wa dhana za Agano la Kale? Tunachojua ni kwamba Yohana alifundishwa sana katika mambo ya Agano Jipya asema msomi mmoja wa Bibilia. Tukitaka kuelewa historia ya chimbuko la Yohana la dhana ya neno kama alivyolielewa, inatubidi kurejelea maandishi hayo matakatifu.¹⁵⁵

Ni kosa linalopaswa kutiwa maanani ikiwa usomaji wa Yohana 1:1 utachukuliwa kwamba una maana ya “mwanzoni alikuwapo mwana wa Mungu, naye mwana alikuwa na baba na mwana ndiye aliyekuwa Mungu.”¹⁵⁶ Hili silo aliloandika Yohana mshairi mjerumani Goethe alijitahidi kupata tafsiri iliyo sahihi. “Mwanzo lilikuwapo neno, wazo, nguvu au tendo.” Aliamua kuchagua “tendo” anakaribiana kufikia nia ya Yohana. Alichotaka kusema mwanidishi wa injili ni kuwa “wazo la Mungu la uumbaji limekuwa likitenda kazi tangu milele.”

Ufafanuzi, Dallas: Word Books, 1988, 15). Cranfield anapambana kuhalalisha "orthodoxy" kutoka kwa Paulo. Lakini Paulo Hakuwa "orthodox", Wa-Utatu (Trinitarian) wala "asiyekuwa Orthodox" Arian.

¹⁵⁴ Yohana 17:3; Yohana 5:44; 1 Timotheo. 2:5; 1 Wakorintho. 8:4-6.

¹⁵⁵ C.J. Wright, Jesus: Ufunuo wa Mungu, Kitabu cha 3 (Book 3 of The Mission and Message of Jesus: An Exposition of the Gospels in the Light of Modern Research (New York: E.P. Dutton and Co., 1938), 677.

¹⁵⁶ Cp. Maandishi ya Bibilia iishiyo yanayopotosha yaliyogezwa “kabla ya kuwepo kwa chochote alikuwepo Kristo akiwa na Mungu. Amekuwa siku zote hai na yeye mwenyewe ni Mungu. Aliumba kila kitu kiliopo- hakuna chochote kichoko ambacho hakuunda (Yohana 1:1-2).

Jinsi alivyoandika msomi mwingereza msifika:

Yohana anaposawiri neno la milele hakuwa akiwazia kiumbe kilichotengwa na Mungu. Tofauti katika imani za utatu wa Mungu za baadaye hazipaswi kuonekana katika mwanzo ya Yohana... kwa mtazamo wa imani ambayo haikuwa yake ...Tuisome Yohana kwa misingi ya historia ya imani za kidini za karne tatu baada ya maandishi ya mwandishi wa injili.¹⁵⁷

Ili kumuelewa Yohana (na Agano Jipya lote) lazima tuzingatie urithi wake wa kitamaduni ambao sio wa mafunzo ya kigiriki ambamo mafunzo ya kidini yaliundwa yapata miaka tatu baadaye. Yohana anaposomwa katika misingi ya chimbuliko lake la kiebrania hatupi uungaji mkono wa imani ya Yesu ambaye ni “Mwana wa Mungu”, binadamu asiyeumbwa katika ushiriki wa utatu ulio Mungu mkuu:

Lugha ya mwandishi itatuchanganya, ila labda tusikilizane mwanzo yake. Muinjilisti Yohana anachukua neno linalojulikana “*logos*”; alitafsiri, lakini anafafanua anachomaanisha yeye kwalo... wazo lilikuwa la Agano la Kale na linahusiana imani nzima ya kidini na tajriba ya maandishi matakatifu ya kiebrania. Ndilo neno linalofaa zaidi kuwasilisha ujumbe wake. Kwani ‘neni’ la mtu ndilo wasilisho la mawazo yake, nayo mawazo yake ndiyo hulka yake iliyo muhimu. Kila wazo lazima lijieleze, kwani utendaji ndio hali halisi ya wazo... hivyo Yohana anazungumzia ‘neni’ lililokuwa na Mungu, na lilikuwa na Mungu, na lilikuwa la kiungu, ili kuwasilisha imani yake kuwa Mungu amekuwa mtendaji akifunua mawazo yake. Mungu, kwa hali yake halisi, hawezi akakaa mbinguni na asitende chochote. Baadaye katika injili Yesu anaposema, “Baba yangu hufanya kazi hadi sasa” anasema anachosema muinjilisti katika mstari wa kwanza wa utangulizi.

Lugha anayotumia Yohana si lugha ya maelezo ya kiuchunguzi. Yohana ana akili thabiti na yenye taswira. Kutofaulu kumuelewa Yohana[katika matangulizi yake] kumeelekeza wengi kuamua kwamba yeye ndiye mkuu wa ‘ukristo wa utatu wa uungu’ na hivyo basi anawajibika kwa kufumbika kwa baadaye usisitizi wa Yesu wa kimaadili na kiroho. Muinjilisti hakuwazia katika hali ya aina ya vitu vyote”-aina ilipendeza sana kwa ya Ugiriki.¹⁵⁸

Kwenye makala yanayoangaza katika *Bible Review*, J. Harold Ellens anaashiria kuwa nemi kama vile mwana wa Mungu jinsi zilivyotumiwa wakati ambapo Agano Jipya liliandikwa:

hazikukusudiwa kuvipa viumbe ambavyo kwavyo zilitumiwa kama viumbe vya kiungu ila zilimaanisha kuwa viumbe hivyo vilijazwa roho ya kiungu au neno. Nemi hizo ziliashiria utendaji wao na sifa zao kama watu wa Mungu ila si kwa wao kuwa Mungu. Kuwazia binadamu kama kuwa Mungu lilikuwa wazo la kigiriki tu. Hivyo mijadala ya mafunzo ya kidini ya mapema kuanzia katikati ya karne ya pili kuendelea, kwa mapana yalikuwa kati ya Antiokia, kituo cha ukristo wa kiyahudi, kwa upande mmoja, na ule wa kialeksandria, ulioadhiriwa vikubwa na mawazo mamboleo. Kukisia ya kipilato kwa wingi, ubishi wa wakristo wayahudi

¹⁵⁷ C.J. Wright, *Yesu: Ufunuo wa Mungu*, 707.

¹⁵⁸ *Ibid.*, (kama hapo juu), 707, 711.

ulielekea kwamba walikuwa binadamu, mwalimu mahiri aliyejazwa roho ya kiungu... lakini kwamba yeye hakuwa wa kiungu katika hali iliyoshikiliwa na waaleksandria. Mabishano yalidumu katika hali moja au nyingine hadi pale kundi la Cyril wa Aleksandria liliposhinda kwa kushikilia dhana ya Cyril alikuwa na uwezo wa kuwauwa maaskofu wenzake ili apate mradi wake.

Kufikia wakati baraza la Nicea mwaka wa 325CE, mtazamo wa ukristo wa hali ya juu wa kialeksandria ulikuwa wenye nguvu. Lakini haukukosa upinzani kutoka kwa mtazamo wa ukristo wa hali ya chini ya kiantiokia. Kutoka Nicea hadi chalcedon mtazamo mamboleo wa kipilato wa kukisia ulipata mashiko zaidi na ukaja kuwa mafunzo asili ya dini ya kikristu mwaka wa 451 CE. Kwa bahati mbaya, walichomaanisha wasomi wa dini kwa nemi kama mwana wa Mungu *kilikuwa mbali na maana za nemi zizo hizo katika injili*. Maelezo ya imani yalielezwa kwa misingi ya elimu ya kigiriki ya malimwengu: injili ilikuwa ikieleza katika misingi ya kiyahudi... maaskofu wa mabaraza walipaswa kutambua kwamba walikuwa wamehama kutoka jazanda za Kiebrania na kuhamia kwenye mawazo ya Kigiriki na hiyo basi walimsaliti Yesu Kristo halisi.¹⁵⁹26

Ni vigumu kuelewa kwamba Bibilia imetengwa wakati mambo ya kimsingi kama vile mwana wa Mungu yanapopewa maana mpya na isiyo ya kibibilia chini ya ushawishi wa mtazamo mamboleo wa kipilato wa kukisia wa kigiriki, mabaraza ya kanisa, yaligeuza mahali pa mwana wa Mungu aliyetungwa kwa mawazo ya kiulimwengu. Maana mpya ya nemi ukichukua mahali pa maana yake asili, imani mpya inaumbwa. Imani hiyo mpya ilikuja kuwa dini kamili ilishikilia sheria zake za kidini, juu ya uchungu wa kutengwa katika ushirika mtakatifu na adhabu ya kutengwa na Mungu (imani ya athanasia) sheria za kidini za Nicea za chini kamili zilimuinua Yesu kutoka nje ya mazingira yake ya kiebrania na kupinda injili ya Yohana kwa juhudi ya kumfanya afae katika ufinyanzi na ulimwengu wa dini kamili. Na hivyo ndivyo ilivyobaki kuwa mpaka sasa.

Mageuzi yatakayobadilisha hali ya maangamizi yanahitajika yatatokea pale ambapo wakristo watawajibika kibinafsi kurudia Bibilia na kuichunguza kwa mbinu zote tulizo nazo. Jambo kubwa ili kuelewa Bibilia vyema ni kutambua kuwa Bibilia ni maktaba ya kiyahudi ya vitabu na kwamba Yesu alikuwa muiyahudi aliyefunzwa kwa Bibilia ya Kiebrania (Agano Jipya).

Ukafiri wa ukristo uliofichika wapaswa kufichiliwa. Historia ya dini kamili inaonyesha ishara za roho iliyo mbali sana na roho ya Yesu. Wale ambao wametia shaka "dini kamili" mara kwa mara wamedhulumiwa.¹⁶⁰ Mfafanuzi mmoja auliza:

Imetokeaje kwamba dini ya upendo imesimamia kutekelezwa kwa baadhi ya ukatili mbaya zaidi na ukosefu wa haki ambazo umetia ubinadamu aibu...? Kanisa limedhulumu kwa ukatili zaidi kupitia dini nyingine yoyote... imani zetu za kidini zimeegemezwa juu ya imani za kitamaduni, na wengi wetu huudhika sana kama utulivu wa imani hii itatiwa shaka.

¹⁵⁹ Tazama "The Ancient Library of Alexandria," *Bible Review* (Feb. 1997), 19-29 na maelezo mengine kutoka "From Logos to Christ" ("Readers Reply"), *BR* (June 1997), 4-7, emphasis added.

¹⁶⁰ Kwa mfano unaoangaza udini mpotovu wa dhali na wa ukatili tazama taarifa ya Calvin inayokariri mateso makali na utekelezaji wa daktari na msomi wa kihispania aliyetoa maswali wa mafundisho ya Utatu, kwa Marian Hillar, *The Case of Michael Servetus (1511-1553) — The Turning Point in the Struggle for Freedom of Conscience* (Edwin Mellen Press, 1997).

Mkatoliki wa wastani [na vile vile kwa waprotesanti wengi] hutegemea uhakika wa kanisa lake, ambao kwa kawaida hukubali pasi na kuchunguza. Kukiri kuwa kanisa lake limekuwa likikosa na kwamba limeruhusu uhalifu wa kuchukiza, ni jambo asiloweza kutenda.¹⁶¹28

IMANI KATIKA MUNGU MMOJA

Sio Paulo wala mwandishi mwingine wa Bibilia aliyesema kwa hakika kuwa “kuna Mungu mmoja; baba, mwana na roho mtakatifu.” Miongoni mwa matukio maelfu ya Yaweh na Mungu hakuna mfano unaoweza kuonyeshwa kumaanisha “Mungu katika utatu mtakatifu.” Mungu wa utatu ni dhana geni kwa Bibilia. Maneno ya Paulo yanahitaji kufikiriwa kwa makini. “Hakuna Mungu ila mmoja ... kwetu sisi kuna *Mungu mmoja, baba*” (1.Wakorintho 8:4, 6). Pia kunaye mfalme Masiya mmoja, Yesu (1.Wakorintho 8:6), lakini yeye ni Kristo mfalme (Luka 2:11; Zaburi 110:1), *mwana* wa Mungu aliye mmoja, baba yake.

Watendaji wakuu wawili katika Bibilia wanaelezewa katika utabiri wenye uungu na thamani zaidi katika Agano Jipya kuliko kwingineko kutoka Bibilia ya Kiebrania. Zaburi 110:1. Pale Mungu aliye mmoja “Yaweh” anazungumza na bwana wa Daudi, anayetajwa kama adoni (“bwana wangu”). (Neno) Adoni linapotajwa mara 195 halitupi maana ya Mungu aliye mmoja kama tulivyoona. Linarejelea daima binadamu au kwa nadra aliye na ukuu wa kimalaika, *badala ya Mungu*. Yesu ndiye bwana wa Daudi amabaye Zaburi 110:1 inazungumzia. *Anateuliwa* bwana na Masiya- uteuzi ulofanywa na Mungu, baba yake (Matendo 2:34-36).

Kwa ajili ya heshima yetu kwake Yesu Masiya, wakristo wanafaa kufuata imani yake ya kiyahudi katika Mariko 12:29. “Sikia, Israeli, bwana Mungu wetu *ni bwana mmoja*.” Mungu ni *bwana mmoja*. Yesu ni bwana mwingine. Hilo linaunda mabwana wawili, lakini imani inamjua bwana mmoja tu ambaye ni Mungu. (Kumbukumbu la Torati 6:4; Mariko 12:29). Hiyo ndiyo imani ya Yesu na hivyo basi ndiyo iliyo asili na yenye uhakika wa kikristo. Ndiyo pia imani ya Paulo. Sote tunaweza kuikumbatia kwa furaha na kufuatana na Yesu Masiya wa historia.

¹⁶¹ Dean W.R. Inge, *A Pacifist in Trouble* (London: Putnam, 1939), 180, 181.

VIII. YOHANA, KUWAPO-KABLA, NA UTATU

“Ushahidi wa Yohana ulio wazi ni kuwa Yesu alikataa kudai kuwa yeye ni Mungu” - professor J.A.T Robinson

Mtu fulani amewazia kuwa viwakilishi vya umoja vinaelezea Mungu katika Bibilia ya Kiibraniya mara elfu kumi.¹⁶² kabla kila moja ya maraajelo hayo ni ushuhuda kuwa Mungu ni nafsi moja, wala si wingi wa nafsi. Ni ukweli wastani wa lugha usiopingika kuwa kiwakilishi cha umoja kinasimamia nafsi moja.

Utaratibu uliofanya Mungu wa Israeli kuwa wa utatu mtakatifu unaelezea kutofaulu kwa wasio wayahudi kuingilia undani wa umoja wa Mungu wa wayahudi na mtindo wa kujaribu kuchanganya ukafiri kiasi na maandishi ya kidini. Juhudi za kupotosha zimetendwa kugeuza Mungu wa Israeli katika zaidi ya nafsi moja. Vidokezi vinavyoashiria utatu mtakatifu vimepatikana pasipotarajiwa kabisa, kwa mfano, “mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu” ya maono ya Isaya (Isaya 6:3). Waumini wengi wa utatu mtakatifu sasa wameasi harakati zao za kutafuta imani yao katika Bibilia ya Kiebrania. Kazi nyingi ya sulubu isiyo na maana inatakikana kuepukwa iwapo kauli za imani za Yesu na Paulo zingesikilizwa. Unabaki ukweli usiopingika kuwa Yesu alikubaliana na imani ya umoja ya Israeli (Mariko 12:29) na Paulo alifasiri Mungu aliye mmoja kama nafsi moja. Katika aya inayolingana kimakusudi Ukristo na ukafiri, Paulo anafasiri Mungu aliye mmoja kama mmoja kihesabu, tofauti na miungu mingi ya walio makafiri. Tukifupisha habari inayotolewa na Paulo katika mistari ya nne na sita ya 1.Wakorintho.8, tunapata kanuni ya imani ifuatayo: “Hakuna Mungu ila Mungu aliye mmoja, baba.” Hii ndiyo imani ya kipaulo juu ya wasioamini katika Utatu Mtakatifu.

Ufafanuzi wa John Milton, mshairi mwingereza, msomi wa dini na mpinzani mkuu wa utatu mtakatifu, anathibitisha tulisemalo:” hapa [1Wakorintho.8:4,6] hakuna Mungu mwingine ila mmoja”, anatenga nafsi zozote zile; kwa kusemwa kihakika katika mstari wa sita, “kwamba baba ndiye yule Mungu mmoja; kwa hivyo hakuna nafsi nyingine ila moja.”¹⁶³

Ni ajabu kwamba imani katika utatu mtakatifu haitosheki kwa fasiri hizi zilizo wazi kumhusu Mungu. Yaonekana imepania kutupilia mbali imani iliyoshikiliwa sio tu na maandishi wa Agano la Kale lakini pia na Yesu mwenyewe. Mageuzi katika mawazo yanafaa. Wasomi maarufu wa dini wametambua kuwa adhari za kigeni zimefunika imani ya asili. C.H. Dood alitamka kuwa “Wayahudi wamehifadhi mambo mazuri” ya kimitume yaliyokuwa ya kikristu awali katika utamaduni lakini yalipata kulemewa na malimwengu ya kigiriki na sheria za Roma.¹⁶⁴

Tatizo lilo hilo lilitajwa na Albert Schweitzer aliposema kuwa “Kazi kubwa inayobaki kwa wanaochunguza ukristo wa kale kihistoria ni kueleza jinsi funzo la Yesu lilivyokua likawa mafunzo ya awali ya kigiriki.”¹⁶⁵

¹⁶² James Yates, Thibitisho la kuonyesha kuwa Mungu ni mmoja, hamna nafsi tatu. (Boston: Wells and Lilly, 1816), 66 153.

¹⁶³ *Treatise on Christian Doctrine* (republished by the British and Foreign Unitarian Association, 1908), 16, 17.

¹⁶⁴ *Epistle of Paul to the Romans*, cited by Hugh Schonfield, *The Politics of God* (London: Hutchinson, 1970), 105.

¹⁶⁵ *Paul and His Interpreters* (London, 1912), v.

Kuingilia Injili Ya Yohana

Tafsiri yetu ya Yohana.1:1-4 inaelekea kuweka ugumu katika wepesi wa ukuu wa Mungu mmoja wa imani ya Israeli, ikiweka kizuizi kisichotakikana kati ya Ukristo, Uyahudi na Uislamu. Mtafsiri maarufu wa Bibilia ya kiingereza, William Tyndale, hakuwa na hakika kuwa “Neno” lake Yohana lilikuwa sawa na kuwepo kabla kwa Kristo moja kwa moja. Anaeleza mistari maarufu ifuatayo: “mwazoni lilikuwapo neno nalo neno lilikuwa na Mungu, nalo neno lilikuwa Mungu... vitu vyote viliumbwa nalo. Uhai ulikuwamo ndani yalo”¹⁶⁶ Yaonekana ajabu kuwa Yohana.1:1-4, mistari kadhaa katika injili ya Yohana, na aya kadha nyingine za Agano Jipya ziachiliwe kubadilisha ushaidi mwingi wa kiBibilia unaodhihirisha imani katika Mungu. Umoja wa Mungu ulitetewa kwa juhudi na kasisi, mtume na Yesu, aliyekuwa mwelezaji mwenye bidii wa sehemu hii ya urithi wa kiyahudi kama wenzake walivyokuwa.

Sura hii imetolewa kwa ajili ya mazungumzo juu ya maswali yaliyozuka kutokana na maelezo yake Yohana juu ya nafsi ya Yesu. Jinsi anavyomsawiri Yesu haijumuishi taarifa kuwa mwana na Mungu ni nafsi ya kiungu iliyokuwapo kabla na mojawapo wa nafsi katika utatu. Yesu anavyochululiwa kuwa njia inayoenziwa kuwa hakuumbuwa na kuwa anashiriki usawa na baba haitoki kwenye maandishi matakatifu; ila impeokezewa kupitia utamaduni wa baada ya kuandikwa kwa Bibilia majaribio ya kuingiza kuwapo kabla katika injili ya Yohana yanahusu kuharibu nia ya Yohana, maandishi ya mtume mpendwa yanapatana na maandishi tangulizi yanayosawiri Yesu kama binadamu wa kipekee amabaye anaipata asili yake kutokana na utungaji upitao akili ya binadamu.

Yohana anamshawishi Yesu kama utumizaji wa mpango wa Mungu wa mwisho wa kumleta Masiya katika hali ya kuwa na wala siyo kama mojawapo wa nafsi katika utatu wa kudumu milele. Hivyo kwa Yohana, na Paulo vile vile Yesu alikuwapo kabla katika akili na nia ya Mungu na wala siyo kijalisi kama kiumbe chenye wakati usio kadirika. Njia hio isiyo ya kidini kamili ya kumsawiri Yesu ilikuwa na washikilizi wake katika karne zilizofuata uandishi wa Agano Jipya. Inajitokeza sehemu muhimu kwote katika historia ya kanisa, hasa miongoni mwa Wenyeji wa Poland wa Karne ya 16. Mazungumzo ya kisasa juu ya ukristo yamejikita katika jambo hili la hali ya kuwapo Kabla. Linalojulikana kitamaduni juu ya kuwapo kabla ni uharibifu wa ukweli wa ubinadamu wa Yesu na hudunisha hadhi ya maajabu ya ufanisi wake kwa niaba yetu. Hii pia huunda tatizo zima la utatu ambalo wengi uamini tu kwa kuwa wanatarajiwa kufanya hivyo. Kurudisha Ukristo wa kiBibilia kutamaanisha kupatikana kwa uMasiya wa Yesu, uliofunikwa na kuumbuliwa kwa uMasiya wa Yesu, uliofunikwa na kuumbuliwa kwa muda mrefu na maendeleo ya baadaye ya Ukristo wa kiBibilia.

Matatizo Juu Ya Dhana Ya Kuwapo Kabla Kihisili

Wazo la kawaida linaloshikiliwa kwamba Yesu alikuwa hai kabla ya kutungwa kwake linazua maswali mengi kuhusu hali yake. Yawezekana mtu kuwa binadamu katika hali yoyote ile yenye maana ikiwa chimbuko lake si tumbo la uzazi wa mamake? Wasomi watambulika kadha hivi karibuni. “Wamewaza kuwa haiwezekani ubinadamu wa Yesu anaweza kuwapo bila kuwapo kabla na pia kuwa kabla ya bila ubinadamu. Hakuna uwezekano wa kuwapo kwa hali zote mbili.”¹⁶⁷ Malaika ni wa kikundi tofauti na cha kibinadamu kwa ajili ya asili yao kuwa nje ya mfumo wa kuzaliwa kwa kibinadamu. Kama mwana wa Mungu alikuwa kiumbe aliyejigeza (au aliyegeuzwa na Mungu) ili aje

¹⁶⁶ Tyndale's *New Testament: A Translation from the Greek by William Tyndale in 1534*, ed. David Daniell (New Haven: Yale University Press, 1989), emphasis added.

¹⁶⁷ Yohana Knox, *The Humanity and Divinity of Jesus* (Cambridge University Press, 1967), 106.

kuingia katika jamii ya binadamu kupitia kwa Maria bila shaka yenye ni wa kikundi cha vivumbe tofauti vikubwa binadamu wengine.

Kuna mengi yanayoweza kwazimwa Masiya kulingana na maandiko matakatifu alitarajiwa kuwa kizazi cha Daudi,¹⁶⁸ cha Abrahamu (Wagalatia 3:16), na mbegu ya mwanamke (Mwanzo 3:15). Mara kwa mara Paul humfikiria Yesu kama Adam wa mwisho(Mtu). Ikiwa alikuwapo kama nafsi kabla ya kutungwa kwake, yeye ni nafsi halisi katika hali hii, binadamu, kizazi cha Daudi na Abrahamu? Kweli maandiko matakatifu yanamuweka Yesu katika kikundi cha kiume kilichoko nje ya tumbo la uzazi la kibinadamu? Pendekezo letu ni kuwa ushahidi ambao mara nyingi hutolewa kutoka Bibilia sana sana kutoka injili ya Yohana, juu ya imani katika kuwepo kabla kwa Masiya hakujitokeza kiasi cha kuweza kutazamwa kwa makini. Tunashikilia kwamba wazo lenyewe lazima kudumishwa kabla ya uchunguzi wa ushahidi wa maandishi matakatifu kisha yaingizwe katika Bibilia. Pia kuna upendeleo unaotambulika katika tafsiri zetu za wastani kwa sababu ya taarifa za awali za imani halisi ya kidini, zinazotuhimiza kusoma Agano Jipya kwa ukengeushi unaotokana na mafunzo ya kanuni .Upendeleo huo huo husababisha wasomi wa dini kuwakilisha mitume,hata baada ya pentekosti kama waumini wasiostaarabika,wanaotapatapa kuelekea katika imani ya utatu ya enzi ya mabaraza ya kanisa baada ya kutungwa kwa Bibilia.

Je, Yohana alitofautiana na Mathayo, Marko, na Luka juu ya swala la Kuwepo Kabla?

Ni muhimu kurejea injili tangulizi za (Mathayo, Marko na Luka) tukizingatia ukweli kuhusu chimbuko la Yesu tunapochunguza injili ya Yohana.Luka alipanga kuweka mbele ya mkristu maarufu Theophilis ambaye (Theophilis) alikuwa amejifunza kama muumini: 'Ukweli hasa juu ya vitu ambavyo umefunzwa'. (Luka 1:4)Wachache wamejaribu kubisha kuwa luka alijumuisha katika uwasiri wake wa Yesu neno moja linalopendekezwa kwa Yesu alitungwa kimiujiza ila si kibinadamu, na kwamba aliingia katika hali ya kuwa kwa mara ya kwanza wakati wa kutungwa kwake. Lilo hilo laweza kusemwa kuhusu uneni wa Mathayo na Marko na uwasiri wa Yesu katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Wasomi wa dini na wana historia wote wanaafikiana kuwa hivyo ndivyo ilivyo. Katika injili zinazo tangulia, hakuna kauli ya moja kwa moja ya kuwapo kabla kwa kristo....hazitangazi popote kuwapo kabla kwake.”¹⁶⁹

Kwanza tunayo mambo ya Ukristo ya injili zinzotangulia na hapo haiwezi ikadaiwa katika njia toshelezi kuwa zinatupa hata chembe ya uhalili wa kuendeleza zaidi ya dhana ya Masiya ambaye ni binadamu.Dhana ya kuwapo kabla ipo nje kabisa ya maneno ya injili tangulizi.Hakuna kinachoweza kuonyesha hili wazi zaidi kuliko usimulizi wa uzazi wa kiajabu wa Yesu. Kinachomuina juu zaidi ya ubinadamu kinapaswa kurejelewa tu kwa *pneuma hagion* (roho mtakatifu) aliyesabiabisha kutungwa kwake.....mambo ya Ukristo katika injili tangulizi yanayo msingi mkubwa kiasi wa wazo la Masiya aliyepewa mamlaka na kutungwa kaa *hvis theou*(mwana wa Mungu): na vidokezi vyote vya kujulia taarifa hiyo vinaegemea dhana iyo hiyo ya ubinadamu kwa vyovyote vile.¹⁷⁰

¹⁶⁸ Ps. 132:11; Matendo 2:30; 2 Sam. 7:14-16; Matt. 1:1.

¹⁶⁹ B. F. Westcott, *The Gospel of John* (Grand Rapids: Eerdmans, 1981), lxxxiv, lxxxvii.

¹⁷⁰ F.C. Baur, *Historia ya Kanisa ya Karne Tatu za Kwanza* (London: Williams and Norgate's, 1878), 65.

Kuwapo kabla si kwa data (taarifa) za imani ya ukristo katika Yesu aliye tukuzwa kihistoria. Hili ni kiashiria muhimu cha imani hiyo. Haya Hayaundi lolote katika sura funguzi za matendo ya mitume. (Katika matendo ya mitume), haitokei wazo kubwa chimbuko lake lazima liwe bora sana kama ulivyo mwisho wake-hakuna kidokezi cha kuwapo kabla. *Mahali pa Kristo milele papo katika ufahamu wa awali na kusudi la Baba.*¹⁷¹

Jambo muhimu, msimamo kuwa Yesu alikuwapo tu katika mpango wa Mungu kabla ya kuzaliwa kwake ndio unaendelezwa na Petro katika waraka wake wa kwanza. Mwisho mwa taaluma yake hajabadili msimamo wake kama alivyoonyesha katika hotuba zake za mapema katika matendo ya mitume: 'Yesu' Alijulikana kabla ya siku za mwisho kwa ajili yenu' (1 Petro 1:2). E.G.Selwyn anasema kisahih;wala hatuna haki ya kusema kuwa (Petro) alifahamu wazo la kuwapo kabla kwa kristo ...kwani wazo hili haliashiriwi katika fasiri yake ya kristo kama 'aliyejulikana kabla kuanzishwa kwa dunia',kwani wakristo pia ni viumbe vya ujuzi wa awali wa Mungu."¹⁷²

Waumini wote walijulikana kabla kwake, vivyo hivyo (1 Petro 1:2), lakini hili bila shaka halimaanishi kuwa walikuwapo kabla. Kama Petro hakufikiria kuwa Yesu alikuwapo kabla ya kuzaliwa kwake, huyu mtume mashuhuri bila shaka hangekuwa na imani katika utatu.

Profesa wa historia ya mambo ya makanisa aliyetazama wazo hilo kwa makini hakupata ushahidi kwa ajili injili za mathayo, Marko na luka;

Kwamba Yesu, aliyefunzwa yanayohusu manabii, alipata mtazamo wake wa kiMasiya kutoka kwa asili ya kawaida ya kiebraniya ni muhimu ... wakati ambapo utume wake wa kiMasiya umejikita katika unabii, ambao kwao Yesu mwenyewe anataja katika ushuhuda wake, haitokei kuwa alijipa sifa ya kuwapo kabla kwa muda... kuligana na kile mathayo na luka wanaeleza juu ya asili yake, alianzishwa kiungu. Ila hajakuwapo kabla ameonyeshwa kama aliyekuja katika hali ya kuwa katika tumbo la uzazi la bikira kwa mwanzo wa roho mtakatifu... hakuna anayeweza kushikilia kimaarifa kuwa Yesu alikuwepo kabla ya tendo hili la kiungu... wala hakuna ishara yoyote iliyo wazi katika matamshi yake kwamba yeye mwenyewe alikuwa na ufahamu wa kuwapo kwake kabla. Hivyo basi hatushughulikii kiumbe aliyekuwapo kabla katika injili tangulizi, ila na aliye wekezewa kiungu wajibu na mwisho uliotukuka na aliyepitia hali zote za kuwepo kibinadamu tangu kuzaliwa hadi kufa.¹⁷³

Hakuna atakayetia shaka uchunguzi unadhifu wa Raymond Brown juu ya simulizi za kuzaliwa kwa Masiya. Yeye pia anagundua kuwa mathayo wala Luka hawakuamini kwamba Yesu alikuwapo kabla ya kutungwa kwake:

Kwamba Mathayo anasema Yesu kama "mzaliwa" katika 1:16, 20, kwake yeye kunapendekeza kuwa utungaji kupitia kwa uwakala wa roho mtakatifu ndiko kuja kwa mwana wa Mungu... ni wazi hapa kuwa *uwana*

¹⁷¹ Kamusi ya Kanisa ya Mitume (T & T Clark, 1916), 2:264, Mkazo unaongezwa.

¹⁷² First Epistle of St. Peter, 248.

¹⁷³ James MacKinnon, *The Historic Jesus* (Longmans, Green and Co., 1931), 375-379, emphasis added.

*wa kiungu si ule wa kupanga ila hakuna pendekezo la utwaji utu ambapo aliyekuwa mbeleni na Mungu anatawaa nyama.*¹⁷⁴

Katika kazi iyo hiyo anasema:”nitasisitiza katika mafafanuzi kuwa mathayo na Luka hawaonyeshi kuwa wanao ufahamu juu ya kuwapo kabla; yaelekea kuwa kwa maoni yao kuwa utungaji ndio uliokuwa uzaaji wa mwana wa Mungu.”¹⁷⁵

Kukiri kwa ajabu kwa msomi mheshimika wa kiBibilia kunadhihirika ukweli kuwa kanuni ya utwaji wa utu haipatikani katika injili ya mathayo na Luka. Hivyo ndivyo ilivyo pia katika injili ya Mariko. Brown anataja kwamba hizi ni kweli zinazotatiza wasomi wa dini walioelimishwa katika imani za kitamaduni juu ya Mwana aliyekuwapo mbeleni na amabaye kuwapa kwake kulikuwa kusiko na mwisho:

Lyonnet, L’Annoiation,¹⁷⁶ anataja kuwa huku kutorejelea kuwapo kabla katika injili ya Luka kumefedhehesha wasomi wa dini kamili wengi, kwani katika mambo ya kikristo yanayohusu kuwapo kabla, utungaji kwa njia ya roho mtakatifu katika tumbo la uzazi la Maria hakusababishi kuwapo kwa mwana wa Mungu. Yaelekea Luka hana habari juu ya mambo ya ukristo ya aina hii. Kwake yeye *utungaji unasababishwa kuhusika uwana wa kiungu.*¹⁷⁷

Hata hivyo ukristo wa kiutamaduni umeshikilia vikubwa kuwa Yesu alikuwapo kabla ya kutungwa umeshikiliwa vikubwa kuwa Yesu alikuwapo kabla ya kutungwa kwake kama mwana wa Mungu nafsi ya pili ya utatu mtakatifu. Hata hivyo dhana hii haiwezekani kupatikana misingi yake katika injili ya mathayo au Luka. Wote wawili wanatusawiria Yesu aliyeanza kuwapo maria alipotunga mimba kwa uwezo wa roho mtakatifu. Ujumbe wa luka u wazi: ilikuwa ni tendo la ajabu la Mungu lilioathiri maria lilioleta mwana wa Mungu kuwepo. Hakuna yeyote anayesoma maneno ya Luka angefikiri huyu mtu amekuwa mwana wa Mungu kabla muujiza Mungu alioufanyia Maria. Yesu wa Luka anatumungwa kama mwana damu mwingine yeyote katika tumbo la mamaye.”Utatumungwa mimba na umpate mwana...roho mtakatifu atakujaza na uwezo wa aliye juu zaidi na hivyo basi mwanao ataitwa mwana wa Mungu (Luka 1:31, 35).”

Mandishi haya muhimu hayaonyeshi ushahidi wowote wa kufikiria kuwa Yesu alikuwepo kabla ya kutungwa mamba. Kwa luka, mwana wa Mungu anatokezea katika mwaka wa 3BC na wala sio Milele. Mathayo anakubaliana kabisa na Luka. Anamtangaza Yesu”mwana wa Daudi na mwana wa Abrahamu” (Mathayo 1:1), Aliyetungwa kimiujiza kupitia kwa Roho Mtakatifu na Maria (Mathayo 1:18, 20).

Utamaduni wa ki-uhalisi unategemea sana maandishi kadhaa yalimo katika Habari Njema Katika Yohana (Yohana 17:5; 8:58). Haya yanafaa kuonyesha kuwa mwanzo wa Yesu siomimba ya Maria ila Milele. Hivyo basi anahabari kuhusu kuwepo kabla kwa Yesu na baba. Je, aya hizi zinaweza kuyapa uzito Madai haya yanaonekana kumweka Yesu wa Yohana katika kiwango tofauti kutoka kile kya ufupisho? Ama kuna jinsi nyingine ya kusoma yohana itakayoleta ushuhuda wa kusawazisha na injili zingine? Swali hili limenichipuka kwote katika historia ya Ukristo, hasa katika kazi za ya Paulo wa Samosata (c. 200-275), Photimus (c. 300-376), maAnabatisti Adams Pastor (c. 1500-1570), Michael Servetus (1511-1553), WaAnabatisti wa Poland, Mwingereza John Biddle

¹⁷⁴ *Kuzaliwa kwa Masiya*, 140, 141, mkazo unaiongezwa. Cp. Aaron Milavec, “Matthew’s Integration of Sexual and Divine Begetting,” in *Biblical Theology Bulletin* 8 (1978): 108: “Mafundisho ya dini na Ukristo ya kabla-kuwepo ungekuwa tofauti sana na maono ya Mathayo ya historia ya Yesu.”

¹⁷⁵ *Ibid.*, 31, fn. 7.

¹⁷⁶ “L’Annoiation et la Mariologie Biblique,” in *Maria in Sacra Scriptura*, 4:61.

¹⁷⁷ Brown, *The Birth of the Messiah*, 291.

(1615-1662, na wasomi wapinzani wa utatu wa uungu wa Karne ya kumi na tisa walioko Amerika, Uingereza, Ujerumani na hivi karibuni walio Cambridge. Kamili ya Maurice Wiles inaashiria kwa kuisisitiza ile ambayo imekuwa imani mwongoni mwa waumini wachache:

Katika desturi ya Kikristo Agano Jipya kwa muda mrefu limesomwa kupitia kwa imani patanishi za baadaye... kumsema Yesu kuwa mwana wa Mungu kulikuwa na maana tofauti kabisa katika karne ya kwanza kutoka kwa ile iliyokuwa nayo tangu wakati wa baraza la nicea. Kuzungumzia kuwapo kabla kwa Yesu katika maandiko matakatifu kwapaswa, labda katika hali karibu zote/ hali zote, kueleweka katika hali sawa na kuwapo kabla kwa *Torah*, ili kuashiria kusudi la kiungu lisilo na mwisho linalofanikishwa kupitia kwake, badala ya kuwapo kabla kwa aina ya kibinafsi.¹⁷⁸

Tatizo la wanaoamini utatu wa uungu ni kwamba lazima watafute kutegemea injili ya Yohana huku wakiingia hatari ya kukinza Mathayo na Luka.¹⁷⁹ Hata hivyo kuna njia nyingine ya kusoma injili ya Yohana njia inayompatanisha na maandishi wa injili wenzake. Kwamba Mathayo na Yohana wanakubaliana kuhusu kuwa Yesu alikuwa nani inaashiria kwa ukweli mwepesi: Mathayo 16:16,18 inarekodi Yesu akiaminisha kwamba yeye ndiye Masiya, msingi wa imani ya Ukristo. Yohana 20:31 inatangaza sababu ya Yohana katika kuandika injili yake ilikuwa kuonyesha hasa ukweli ule, ule, kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu.

Neno Katika Matangulizi Ya Yohana

Mafafanuzi ya hivi karibuni juu ya Yohana yanakiri kuwa ingawa imani ya muda ya kidehuri imekuwa katika hali ya kukinza, neno 'Neno' katika mafafanuzi maarufu ya Yohana hayapaswi kurejelea mwana wa Mungu kabla ya kuzaliwa kwake. Tafsihi zetu zinadokeza imani katika kanuni za kidini za kidehuri juu ya utwaji wa utu kwa kuendeleza neno 'Neno' kwa kulitanguliza kwa herufi kubwa. Ni nini kilichokuja kuwa nyama katika Yohana 1:14? Ilikuwa nafsi iliyokuwa kabla? Au ulikuwa ni utendaji wa Mungu Baba wa kujieleza kibinafsi, mpango wake usio na mwisho? Kwa mfano, mpango unaweza ukachukua nyama, wakati ambapo mtindo unatwaa umbo kama nyumba katika akili ya (Mwaandishi wa ramani za mijengo) mjenzi. Kilichotangulia matofali yanayoonekana na chano ni nia iliyokuwapo akilini mwa mjenzi. Hivyo ni sawa kusoma Yohana.1:1-3a: "Mwanzoni palikuwa nia bunifu ya Mungu,"¹⁸⁰ ilikuwa na Mungu na ilidhihirisha Mungu kikamilifu [*theos*]"¹⁸¹(vile ambavyo busara ilikuwa na Mungu kabla ya uumbaji Methali 8:30). "Vitu vyote vilikuja kuwa kupitia kwake." Urejeshi huu unafaa matumizi ya 'neno' kwa kuvutia katika Agano la Kale: "Ndivyo neno litokalo kinywani mwangu litakavyokuwa; halitarudi kwangu bure, bila kutimiza upendo wangu na bila kufanikiwa katika jambo ambalo nililituma" (Isayah 55:11).¹⁸² Yesu ndilo neno hilo

¹⁷⁸ *Ujenzi Upya wa Mafundisho ya Ukristo*, 52, 53.

¹⁷⁹ Maoni ya wengi wa MSS, Mathayo anaandika kuwa mwanzo wa Yesu katika Mathayo 1:18. Haikuwa kuzaliwa kwake tu, Mariko na Luka hawajui lolote kuhusu Yesu aliyekuwepo kabla kuzaliwa kwake, Maelezo ya Luka ya kuzaliwa kwake hayajahusisha "Uzao wa milele" wa Mwana, anayekuwa Mwana wa Mungu katika kutungwa kwake. Uwezekano ni kuwa maoni ya Yohana kuhusu Kristo yana uwiano na maandishi wengine wa Habari Njema.

¹⁸⁰ Gabriel Fackré kwa *Hadithi ya Ukristo* (Eerdmans, 1978), 103, inahusika na kibali cha ujumbe wa Theophilus wa Antioch wa "logos" Kama mpango wa Mungu, nia, sababu na tokeo na shauri kama tafsihi ya Yohana 1:1, "Akili ni Mungu na ilikua naye Mungu."

¹⁸¹ The NEB anajaribu kuonyesha maana na "Kile ambacho ni neno, ni Mungu."

¹⁸² Kwa matumizi ya "neno" katika Agano la Kale, angalia Zaburi 33:6-12 na James Dunn, *Christology in the Making*, 217, 218.

lililoelezwa kama binadamu- neno la Mungu la mwisho kwa ulimwengu, mwana ambaye Mungu anazungumza kwake mwishoni mwa nyakati hizi, (Wahebraniya 1:1, 2). Ni muhimu kwamba mwandishi kwa Wahebraniya anamuweka mwana “Katika nyakati hizi za mwisho” kama ajenti wa kiungu anayefuata manabii, hamuweki katika hali ya milele, ila anamfikiria mwana kama Kristo wa kihistoria.

Shaka katika neno la kigiriki (*dia atou*, “kupitia kwako, au “Kupitia kwake”, Yohana 1:3) inalikubali neno lisilokuwa na nafsi kabla ya Yesu kuzaliwa. Fafanuzi la Yohana mwenyewe linapendekeza ukosefu wa nafsi kwa neno Yohana 1:1 katika 1Yohana 1:2. Uzima wa milele usio na nafsi ndio uliokuwa “na baba”(Pros ton theo,) yaani, ahadi ya maisha ya milele itakayotolewa kupitia kwa Yesu. Petro anaelekea kusisitiza wazo lilo hilo hasa anapofasiri Yesu kama mwana kondoo wa Mungu “aliyefahamika kabla kuanzishwa kwa dunia, lakini aliyedhihirishwa katika nyakati hizi za mwisho” (1Petro 1:20). Ni katika mistari michache tu ya awali anamotumia dhana iyo hiyo ya ufahamu wa kabla anapozungumzia mpango wa Mungu wa kuwaalika wakristo uokovuni (1Petro. 1:2). Mungu aliwaashiria wale ambao aliwaita baadaye, lakini hawakuwapo kabla katika uhalisi. Utumizi wa Petro wa shana hii kwa Yesu katika mistari wa 20 unaashiria kuwapo kabla kwa dhahania katika mabaraza ya Mungu yasiyo na mwisho, si kuwapo kwa hakika katika hali nyingine kabla ya kuzaliwa kama binadamu. Usambamba wa kuvutia unatokea katika kitabu cha Ufunuo; ambapo vitu vyote “vilikuwa na vilipata kuumbua”(Ufunuo 4:11). Mounce anafafanua kuwa “Kauli hii isiyo ya kawaida inapendekeza kuwa vitu vyote ambavyo vipo, vilikuwapo kwanza katika mpango wa Mungu bila mwisho na kupitia kwa mpango wake vikaja kuwa halisi kwa wakati mwafaka aliochagua.”¹⁸³

Wafafanuzi waaminio utatu wa uungu wanatambua kuwa hapana sababu iliyo na msukumo kuaminisha kuwa wasomaji watangulizi wa matangulizi ya Yohana wangewazia 'Neno' kama Mwana aliyekuwapo kabla kihalisi kama nafsi: Hadi Yohana 1.14 (“Neno lilikuja kuwa nyama”), ingewezekana kwa msomaji kulichukulia neno kwa maana ya kiumbe fulani chenye enzi cha kidunia au kingine kama hicho.”¹⁸⁴ Ni ukweli unaofahamika kidogo kwamba tafsiri za kiingereza za Yohana 1:2 zilifasiri neno kama 'ki' si 'yeye' kabla ya tafsiri ya “King James.” Jambo hili linaangaziwa na James Dunn. Katika uchunguzi wake mpana wa kanuni za kidini za kdesturi juu ya utaaaji wa utu, anabisha, kuwa nje ya injili ya Yohana, hakuna kanuni ya imani juu ya kuwapo kabla halisi. Hata hivyo, Dunn anatoa taarifa muhimu kuwa kabla ya Yohana 1:14 hakuna haja ya kufikiria 'Neno' kama nafsi binafsi ya pili na Mungu. Kuhusu Yohana 1:1 anasema:

Uamuzi unaoelekea kutokea katika uchambuzi wetu [waYohana 1:1-14] hadi hapo ni kuwa ni mistari wa 14 tu [“Neno lilikuja likawa nyama”] ambapo tunaweza kuanza kuzungumza juu ya neno la kibinafsi (ilikuja nyama), lakini hakuna mkristo ambaye angekosia kutambua hapa kuwa urejeshi huu ulikuwa ni kwa Yesu – neno halikuja kuwa nyama kijumla ila Yesu kristo. Kabla ya mistari wa 14 tu katika kiwango kile kile na kama yalivyo mazungumzo juu ya hekima na neno enzi za kabla Kristo; lugha ile ile na dhana zile zile tunazozipata katika Philo, ambapo kama ambavyo tumeona, tunashugulika na uhuishi zaidi ya nafsi, vitendo vya Mungu vilivyohusishwa kuliko kiumbe cha kiungu cha kibinafsi. Jambo muhimu linafichwa na ule ukweli kwamba tunalazimika kutafsiri neno lenye hali ya kiume logos kama “yeye-hali ya kiume” kwenye shairi zima lakini kama

¹⁸³ R.H. Mounce, *Kitabu Cha Ufunuo* (Marshall, Morgan and Scott, 1977), 140 (kuhusu Ufunuo 4:11).

¹⁸⁴ Leon Morris, *The Gospel According to Yohana*, New International Commentary on the New Testament (Grand Rapids: Eerdmans, 1971), 102.

tungetafsiri neno logos kama “uneni wa Mungu” ingekuwa wazi zaidi kwamba shairi halikunua logos ya mstari 1-13 kufikiriwa kama kiumbe cha kiungu cha kibinafsi. Yaani, umuhimu wa kimageuzi wa mstari 14 waweza kuwa kwamba unaashiria siyo tu mpito katika mawazo ya shairi kutoka kuwapo kabla mpaka utwaji wa utu, bali pia mpito kutoka uhuishi usio wakibinafsi hadi nafsi yenyewe.¹⁸⁵

Lakini kwa nini 'tulazimike kutafsiri' logos ya kiumbe hivyo? Ili tutetee matangulizi ya Yohana yenye maelezo ya kidesturi. Logos likichukuliwa kama “Mpango wa Mungu”, na wala sio kama mwana hai kabla ya kuzaliwa kwake, utetezi mkubwa unaondolewa kutoka kwa jinsi mtazamo wa kidesturi wa kuwapo kabla wa utatu wa uungu katika injili ya Yohana.

UTAZAMAJI ZAIDI WA YOHANA 1:1

Tafsiri iliopo ya Yohana 1:1 ni tafsiri kwa vyovyote vile, ikiwa kwa tafsiri tunamaanisha kupitishwa kwa kilicho asili hadi kisawazishi chake chenye mantiki katika lugha iliyolengwa?? kauli “Neno lilikuwa na Mungu” ina maana yoyote katika kiingereza? Neno lako “lilikuwa nawe” lini mara ya mwisho. Tunashuku kuwa tafsiri zetu za wastani za nyakati hizi ingawa ni sahihi kihalisi, kwa udogo zinamruhusu msomaji kuhisi vizuri juu ya upokeaji wa dini halisi kwa njia ya kikristo kuhusu mwana asiye na mwisho akitwaa ubinadamu. Herufi kubwa katika 'Neno' mara moja linapendekeza nafsi inayoishi tayari. Na wasomaji wengi (Nakala milioni II ulimwenguni kota katika lugha nyingi) wametolewa fafanuzi kama vile *Good News Bible*: “Kabla ya kuwapo kwa kitu chochote kingine, Yesu alikuwapo, na Mungu. Daima amekuwapo hai na mwenyewe ni Mungu. Aliumba vitu vyote viliopo. Hakuna kilichopo ambacho hakukiumba.”¹⁸⁶25 imani halisi ya msomaji inadhibitishwa zaidi. lakini msomi mkatoloki wa kiroma Karl Josef Kuschel latika kulishughulikia swali la asili ya kristo anauliza “Mbona tunasoma bila ushauri:” “Mwanzoni alikuwa mwana na mwana alikuwa Mungu?”¹⁸⁷26

Inatuokania kuwa Bibilia ya Kiibraniya yapaswa kutupa mstari wetu wa kwanza wa uchunguzi, iwapo tutafikia nia ya Yohana katika matangulizi. Alivyoniambia profesa katika chuo, “ukielewa vingine Agano la Kale, utaelewa vingine Agano Jipya” kiajabu kutotokea kwa neno la kiebraniya *davar* (Neno) linaloelekeana na neno la kigiriki la Yohana Logos hakutoi ushahidi wowote kuwa “Neno kutoka mwanzoni” linamaanisha nafsi, mwana wa Mungu, sambamba na Mungu mmoja wa Imani ya Kiisraeli. *Davar* katika agano la kale linamaanisha “neno”, “kitu”, mara nyingi “ahadi” “nia” lakini kamwe si nafsi/mtu. Kuwapo potepote kwa herufi kubwa ‘W’ katika neno ‘Word’ katika tafsiri zetu za kiingereza hakuna sababu. Yohana hakusema kuwa neno lililokuwapo kabla lilikuwa mtu wa pili kabla ya kuja kuchopekwa ndani ya Masiya.

Kwa hivyo kwa nini Yohana asiwe akisema kwamba kitendo cha Mungu cha uumbaji, neno lake au hekima yake, orodha ya mambo katika mawazo yake, yalikuwa “naye”, vile ambavyo hekima ilikuwa “na [*para*] yeye” katika Methali 8:30 (LXX)? Methali 8 ina usambamba na kile ambacho Yohana anasema baadaye kuhusu Yesu. Uhai unapatikana katika maneno ya Yesu (Yohana 6:63), jinsi unavyopatikana katika hekima. Hekima inaita kwa sauti jinsi ambavyo Yesu anafanya (Yohana 12:44), akiwahimiza watu kusikiliza funzo lake. Kinachotabiriwa kuhusu hekima katika Methali kwingineko kinaelekezwa Mungu (Ayubu 12:13-16).

¹⁸⁵ *Christology in the Making*, 243, emphasis added.

¹⁸⁶ Cp. GNB on 1 Yohana 1:1: “Kristo alikuwa hai ulimwengu ulipoanza.”

¹⁸⁷ *Born Before All Time? The Debate About the Origin of Christ* (New York: Crossroads, 1992), 381.

Kimuhimu, mara kwa mara Yohana hutumia kihusishi. *Para* (pamoja na)kuonyesha kukaribiana kwa mtu mmoja kwa mwingine (1:39; 4:40; 8:38, n.k) ilhali katika matangulizi yake anachagua *pros* (pamoja na), pendekezo la kuwa 'neni' halikusudiwi kumaanisha mtu sambamba na Mungu. Mstari wa kwanza wa Yohana pia ni kumbukumbuku la inachosema hekima katika Ecclesiasticus 24:9 "Mungu alinimba tangu mwanzo kabla dunia." Kunao ushahidi mzuri kuwa kihusishi cha Kiebraniya *im au et* chenye maana ya "Pamoja na," chaweza kufafanua uhusiano katika ya *mtu na kilicho moyoni au akilini mwake*. Hapa pana baadhi ya mifano ya kuvutia ya matumizi wa vihushishi vya KiEbrania *im na et* kutoka kwenye Biblia ya KiEbrania:

"*Im* (pamoja na), pekee = katika ufahamu wa nafsini wa mtu, iwe ni ujuzi, ukumbuko au nia."¹⁸⁸27

Num. 14:24: "Alikuwa na roho ingine ndani yake" (ukifanya kazi akilini mwake)

1 Wafalme 11:11: "Hii ni pamoja na wewe [Suleiman]" (Kile ambacho unataka)

1 Tarehe. 28:12: "Mfano wa yale yote yaliyo katika Roho pamoja naye" (kwa akili yake)

Job 10:13: "Najua kwamba hii ilikuwa na wewe" (sambamba na "iliyofichika kwa roho yako"; "katika akili yako," NIV; "Najua kuwa vitu hivi ndizo kusudi," NASV)

Job 15:9: "ambayo sio na sisi" (hatukielewi)

Job 23:10: "anajua njia iliyo na mimi (njia ambayo ninaifahamu)

Job 23:14: "Anatenda yale ambayo yaliagizwa kwangu na mengi aliyo nayo" (anazo kusudi nyingi ya aina hizo); LXX: "Amefanya kwa hiari yake."

Job 27:11: "Kile ambacho kiko na Mwenyezi Mungu sitakisetiri." (Kusudi zake)

Zb.50:11: "Nyumbu wa eneo za nchi wako na mimi" (na kujulikana kwangu, kwa fikira yangu na hadhari)

Zb.73:23: "Ninaendelea kuwa naye" (kwa mafikira yako)

Et: " ndoto au neno la Yahweh inasemekana kuwa na nabii."¹⁸⁹

Mwanzo 40:14: "Iweke kwa akili kikiwa sawa na wewe" (lit."Nikumbuke ndani yako"). (Mungu alikuwa na neno kwa akili yake.)

2 Mfalme 3:12: "Anayo neno la Bwana" (cp.2 Yohana 2: "ukweli uko nasi"; Wagal.2:5: "ukweli unabaki nawe")

Isa.59:12: "Dhambi/uhalifu uko nasi" (kwa hekima yetu, na kwa akili). (Cp.Yohana 17:5, fahari/utukufu ambayo Yesu alikuwa na Mungu - kwa akili ya Mungu na kusudi yake.)

Jer.12:3:"Unaikagua kikao cha roho yangu na wewe." (lit."Umejaribu roho yangu")

Jer. 23:28:"Mtume ambaye naye kuna ndoto" (yule mtume aliye na ndoto)

Jer.27:18:"Kama neno la Mungu liko naye"

Job 14:5:" Siku zake ni dhahiri. Nambari ya miezi yake yanajulikana" (yanajulikana kwako)

Zb.2:1:"Tunu amri zangu kumi za Nabii Musa ndani yako" (= na wewe)

Zb.11:2: "Hekima imo na wale wanyenyekevu."

Kwa maoni ya mahali pa KiEbrania tunapenyeza tafsiri ya Yohana 1:1, 14 ifuatavyo: "Hapo mwanzo Mungu alikuwa na mpango na mpango huo ulikuwa thabiti kama hukumu ya Mungu na mpango ulielezwa kikamilifu kwa akili ya Mungu, na mpango ukawa mfano hasa katika Mtu Masiya Yesu."

Nia ya Yohana

Yohana katika matangulizi yake anatangua/zuia maelekezo ya maarifa kwa wazo la wingi wa Mungu. Mkristo mwenye maarifa aliamini kuwa yule Mungu

¹⁸⁸ Brown, Driver and Briggs, Hebrew and English Lexicon of the Old Testament, 768.

¹⁸⁹ Ibid., 86

mwema/mtukufu asiyeambilika, na ambaye alikuwa mbali na ulimwengu wake, alikusudiwa kwa dunia yake na viumbe vilivyo na utukufu ndogo zaidi - "aions," au kiumbe mmoja wa utukufu ndogo zaidi (aina mbalimbali ya jamii nzima ya maarifa yalitofautiana na neno hilo). Justin Martyr, ambaye hakudai ushirika wowote wa maarifa, hana mashaka ya kuzungumza kuhusu Mwana kabla kuwapo ambaye ni "Mungu wa pili kwa hesabu," na bali haujaumbwa na sio wa milele kama Mwana katika shauri ya Utatu iliyoendelezwa, lakini anayeishi kabla kuwapo kama Mwana na kuja mbele wakati kabla ya utinzi wa Mwanzo. Justin anafuta njia ambayo haijulikani kwa Agano Jipya ambapo anaona Mwana wa Mungu katika wakati wa Agano la Kale kama malaika wa Yesu.

Katikati ya karne ya pili Justin alitunga Udhuru na Mazungumzo na kwa hii shawishi ya falsafa katika Ukristo unaonekana wazi kwa kikamilifu... Alidhihirisha uhusiano kati ya hali falsafa ya watu wasiomwamini Mungu, daraja ambayo yule wa kwanza aliipita katika jimbo yake... [Ukristo] unaopatikana kwa Dini na desturi za kiyahudi za kiyunani za Alexandria, uliosaidia wakati kuhifadhi imani kwa ufunuo wa Ukristo na Ebrania, na ungekubali mafikra za kifalsafa na kushika dhana ya siku.¹⁹⁰

Tertillian, anayejulikana na mwanzilishi wa Ukristo wa Kirumi, kama Justin anajua kuhusu binadamu mtukufu wa pili ambaye anatokezwa katika wakati kwa Baba¹⁹¹. Usomi huu wa Ukristo ambao uko na ukoo wa kuogofya na maarifa ya msingi mbili, haungefanikiwa ila kwamba Yohana alimaanisha kuwa Mwana kama tofauti na neno la Mungu la hekima ilikuwepo hapo mwanzo. Taifa linaendelea kutegemea katika Yohana 1:1 kwa mafundisho ya dini ya Uungu wa usawa ya Kristo. Lakini, Je, kama walisomeshwa kuhusu tafsiri nane ya Kiingereza ambayo ilifuatwa na toleo la King James Version mnamo 1611?¹⁹²

Kuchungua mwingine wa maana ya Yohana ni vitabu vya zaidi vya kibibilia ya dini ya desturi za kiyahudi. Katika "Qumran" Kitabu cha maelezo cha maadili tunajifunza kuwa "Kutikana na maarifa ya Mungu kila kitu huja kupita; na kila kitu ambacho anaanzisha kwa nia yake; na bila yeye [au hiyo?] hakitafanyika." Kwa kweli hii ni sauti yake Yohana "kwa hiyo [neni] vitu vyote vilikuja kuwa na bila hiyo hakungekuwa na chochote" (1:3). Katika I QS iii 15 tunasoma: "Kutoka kwa Mungu wa maarifa kuna yale yote yaliyomo na yale yote ambayo yangekuwa," na katika "Apocrypha", "Mungu aliyetengeneza vitu vyote kwa neno" (Hekima 9:1) na tena "Sirach" 42:15: "Nitakumbuka kazi ya Kristo, na nitatangaza kile ambacho nimeona: katika maneno ya Kristo na kazi yake." Katika "Odes ya Suleiman, tunajifunza kuwa " dunia ilijengwa na maneno ya Mungu," na kwa "wazo la Roho yake" (16:19).

Kwa kweli tuko katika ulimwengu wa Mungu aliyezungumza na alichozungumza kilifanyika katika Mwanzo 1, na katika Yohana 1:1 tunajifunza zaidi kuhusu elezo la

¹⁹⁰ G.T. Purves, "Ushawishi wa Wasiomwamini Yesu kwa Ukristo ya mitume ya baadaye." *Presbyterian Review* 36 (Oct., 1888). Mpambano wa teketezo/msiba wa falsafa wa Alexandria unajulikana na wasomi wa sasa. Katika Maandiko ya maoni ya Bibilia ya Juni 1997, Profesa J. Harold Ellens alitazama kwamba "kutoka Nicea hadi Chalcedon maoni ya kukisia ya Usomi wa Ukristo ya Alexandria uliendelea mbele na ukakuwa imani halisi la fundisho la kanuni la Ukristo katika 451 C.E. "

¹⁹¹ "Kulikuwa na wakati ambapo Mwana hakuwepo; Mungu hakuwa mara kwa mara Baba" (*Against Hermogenes*, ch. 3).

¹⁹² Kwa kinzano hili moja lililjulikana, matafsiri yafuatayo yalifasiri Yohana 1:3, "Kwa hayo yote yalitengenezwa. Bila hayo hakuna kile ambacho kingetengenezwa": Tyndale Bible (1535), Coverdale (1550; tafsiri hii iko na "usawa" afadhali kuliko "hiyo"), Mathayo (1535), Taverner (1539), The Great (Cranmer's) Bible (1539), Whittingham (1557), Geneva (1560), Bishops' Bible (1568).

kibinafsi na tendo la neno ambalo (na sio "nani") likawa Yesu. Yesu hivi basi aligeuka akawa neno. Ninaamini kuwa wasomi wengi wangepikia tafsiri kama huu kama hawangekuwa katika zuio la imani halisi. Ni jambo la kuvutia kwa mfano, kwamba F.F.Bruce, jambo la kushangaza, aliandika kuhusu Yohana 1:1 na tatizo la kabla kuwapo kwa Kristo: "Kwa swala la Yohana 1:1, mmoja anaweza kubali kuwa kabla kuwapo kwa neno la milele au hekima ya Mungu ambayo (ambaye?) ulikuwa wenye asili na umbo la binadamu kwa Yesu. Lakini si wazi kwamba mwaandishi yeyote wa Agano Jipya aliyekuwapo na tofauti na aliyofahamu moyoni kama 'mtu wa pili wa fahari'... Sina hakika kuwa Paulo aliamini hivo."¹⁹³ Je, hii ni tofauti kweli na maelezo yaliyotolewa na "standard lexicon of Arndt na Gingrich? Wanasema kuwa "neno" katika Yohana 1:1: "Vitabu vyetu vinaonyesha dalili ya njia za kufikiria ambazo zilijulikana kote katika "syncretism", kama vile katika vitabu vya hekima vya kiyahudi na "Philo", umbo ya kutokeza ambayo ni wazo la "Logos", 'neno' (ya Mungu) iliyojitegemea na kwa nafsi yake... 'Neno' hili tukufu lilichukua maumbile ya binadamu katika mtu kihistoria."¹⁹⁴ Ni jambo la kutumainisha kuwa na maelezo iliyotolewa kwa amri ya heshima. Unatazama kuwa Arndt na Gingrich hawakusema chochote kuhusu neno kumaanisha Mwana kabla kuzaliwa kwa Yesu. "Neno" katika Yohana 1:1, wanakihisi kuwa ni kufanya kama kwamba ni nafsi ya mtu, na sio mtu.

Si jambo linalowezezekana kuonekana kama mwaminifu wa kweli bila kuamini kuwapo kabla kwa Mwana wa pili. Hii ni kitendawili la kutunduwaza/kushangaza. Kikao/Hali hii ni cha kiwango tofauti ya usomi wa Bibilia.

Ni yapi ya kutatanisha katika neno "neno"? Je, ni mtu anayeishi kabla kuwapo au ni kusudi? Wanaoamini Utatu kwa mara nyingine hubishana kama ifuatavyo: 1) Neno lilikuwa Mungu; 2) Yesu alikuwa Neno; 3) Hivyo basi Yesu ni Mungu. Makao haya lazima yakaguliwe. Neno hilo si la kufananisha na Mungu.¹⁹⁵ Inatofautishwa na Mungu kwa njia ingine kwa kuwa "na yeye." Neno halikuwa Mungu wa pili. Kama kweli Neno si mfano moja na Mungu (inawezaje kuwa kama ni "na Mungu") wala sio Mungu wa kujitegemea, fungu la maneno "Neno lilikuwa na Mungu" Inaweza kumaanisha, kama anavyosema A.E Harvey, " Neno lilikuwa elezo au mawazo ya Mungu (cf. Hekima 7:25-6), kwamba ilikuwa tukufu, yaani tukufu ya Mungu."¹⁹⁶

Kikao cha pili, Yesu alikuwa neno," si lazima imaanishe kwamba neno una usawa na Yesu kutoka kwa milele. Yesu ndiye alikuwa neno. Yeye ni maelezo ya neno kutoka kuzaliwa kwake kama Mwana wa Mungu (Yohana 1:14). Kusema kuwa Yesu ni elezo la tendo la Mungu haitoi ushuhuda kuwa Mwana wa Mungu alikuwa mwanachama wa utatu ambaye hakuumbwa.

Kufikiria kama Wayahudi

Swala lote la kabla kuwepo unageuzwa na jinsi tunavyosoma maneno/masimulizi ya kibibilia. Inamaanisha nini kwa jambo "kuwa" kabla iishi duniani? Je, tunahusika na wakati kabla kasisi kwa kutiwa mkono na askofu au hasa kabla kuwapo? Hakika ni kwamba "wakati myahudi alitamani kuagiza/chagua kama azimu ya hali ya mbele, aliizungumzia kama ilivyoishi tayari mbinguni."¹⁹⁷ Hivi katika Wakolosai 1:5 Paulo anazungumza kuhusu tumaini ya urithi wa wakristo ya Ufalme ujao ukiwa " umetandaziwa humo mbinguni."Urithi ulioaweka miadi kwa maisha yajayo umekuwa

¹⁹³ Kutoka ulinganifu, Juni 13, 1981.

¹⁹⁴ William F. Arndt and F. Wilbur Gingrich, *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature* (Chicago: University of Chicago Press, 1957), 480.

¹⁹⁵ Usawa unaeza elezwa kwa "o theos," not "theos."

¹⁹⁶ Yesu na zuio ya Historia (Philadelphia: Westminster Press, 1982), app. III, 176, 177.

¹⁹⁷ E.G. Selwyn, *First Epistle of St. Peter*, 124, mkazo unaongezwa.

kwa mpango wa Mungu wa milele. Wakati ujao ni nini kwetu mbali na Mungu. Vile vile, fumbo ya ufalme wa wakati ujao umefichiwa Mungu katika kusudi lake la milele (Kirumi. 16:25). Na pia hekiam tunayopewa uliekeleye mkono na askofu mbele ya dunia kwa neema (1Kor.2:7-9). Kulingana na hali hii ya kueleza kusudi ya Mungu iliyoamuriwa mbeleni, Bibilia inaweza kusema kuwa Yesu "alisubuliwa kabla ya msingi ya dunia" (Ufunuo 13:8, KJV, RV). Kile ambacho kinahukumiwa unaeza semekana kufanyika kwa nia ya Mungu, ingawa tendo hilo bado halijatendeka. Kanuni muhimu ya bibilia inaonekana pia kwa mafikira ya Paulo: "Mungu anaita vitu ambavyo viko ni kama viko" (Kiru. 4:17, KJV). Katika matangulizi ya maneno kumbukumbu ni kwa Isaka ambaye alikuwa "wa ukweli kwa fikra na kudusi ya Mungu kabla ya kuzaliwa."¹⁹⁸ "Mwenyezi Mungu anasimulia... kuhusu vitu ambavyo havina uhai... kama vina uhai, kwa sababu vita ishi hivi karibuni kulingana na kusudi lake."¹⁹⁹ Katika waraka uu huu Paulo anaweza sema kuwa Mungu "amewasifu" waaminifu, kumaanisha kuwa sifa yao ya wakati ujao ni wa hakika/umehakikishwa kwa sababu Mungu ameamuru. (Zb.8:30). Maandishi yanatangaza miaka mia saba kabla ya akuzaliwa kwa Yesu kwamba "tumepewa mwana" (Isa 9:6). Maandishi mengine ya kisasa yanatafsiri vitenzi haya yaliyopita kwa wakati ujao - "tutapewa mwana" - kwa sababu hiyo ndiyo wanadokeza.²⁰⁰ Ni sawa kuuliza kama "unabii au nia katika tenzi ya wakati uliopita hakionekani katika Injili ya Yohana.

Hatuna ugumu wowote katika kufahamu kuwa ahadi yake Mungu kumpa Abrahamu shamba/ardhi ikihusika na wakati ujao. Walakini ilielezwa katika wakati uliopita: Kwa mbegu yako nimepeana ardhi/shamba hii" (Gen. 15:18) Tafsiri/Mafafanuzi ya Socino inatazama kuwa:

"Ahadi ya Mungu ina maneno yanayosimiliza kuwa kilishatimizwa."²⁰¹ Wakati uliopita hapa haupaswi kuchukuliwa kama ya kweli kwa sababu shamba hilo bado halikuwa la Abrahamu (na bado si chake²⁰²). Stephen anasema kikavu: "Mungu hakumpa hata futi moja la eneo la shamba hili kukiita chake, bali alimpa miadi ya kumpa" (Matendo 7:5). mabishano/ubishi dhahiri kati ya Mwanzo 15:18 ("Nimepeana") na Matendo 7:5 ("Mungu hakupeana") inatatuliwa virahisi kwa kufahamu "wakati uliopita wa kinabii" ambayo unaeleza kuhusu hakika wa mwisho wa wakati uajo kwa sababu ya amri iliyopita ya kusudi/nia kuu ya Mungu. Sawa na hii, Mungu alipea Abrahamu na Isaka ardhi/shamba hilo (Mwanzo 35:12), ingawa hawakuipata.²⁰³ Tutatoa maoni ya matumizi ya mahsuri haya kwa lugha kabla kuwepo katika Yohana tunapotazama Yohana 17:5 (hapo chini) Lakini kwanza mtazamo wa maneno wa "kuwepo kabla" kwa Yohana.

Je, Yohana anamaanisha nini kwa kuja na kutumwa kwa Yesu?

Tukitegemea wazo kuwa Yesu katika Injili ya Yohana ulitokana na kuwepo kabla wa binadamu wa hapo awali mbinguni, wasomi wa Injili ya nne wanadai kuwa "kuja kwa Yesu kutoka kwa Baba," "kuja mbele kutoka kwa Baba" au "kutumwa kutoka kwa

¹⁹⁸ Harrison, *Romans, Expositor's Bible Commentary* (Zondervan, 1976), 52, mkazo unaongezwa.

¹⁹⁹ Moule, *Romans, Cambridge Bible for Schools and Colleges* (Cambridge UP, 1918), 95.

²⁰⁰ "Unabii wa wakati uliopita" ufuatayo katika nabii ni kawaida ya njia ya kufikiria ya waEbrania: "Watu wangu wameenda katika utumwa/kifungo" (Isa.5:13); "kwetu sisi mwana amepewa" (9:6); Watu waliotembea gizani wameona mwangaza mkuu: (9:2); "Wameteketeka/angamiza Israeli" (9:12); "Amekuja kwa Aiath" (10:28); "Nimewekelea Zion..." (28:16); "Amewaharibu/angamiza kwa ukweli" (34:2).

²⁰¹ Morris Simon, *The Soncino Chumash* (London: Soncino Press, 1947), 34.

²⁰² Ijapokuwa urithi wa hapo awali wa shamba chini Joshua (Josh.21;43-45), wanabii wanatarajia ahadi ya zamani kwa Abrahamu kupokea tekelezo/utekelezaji wa mwisho wa wakati ujao. (Jer. 3:18; 30:3).

²⁰³ Mwaandishi ya kitaabu cha Waebrania ana amini kwamba Abrahamu atapokea ahadi la shamba/ardhi katika inchi ambaye aliishi kama 'mgeni' (Waebrania 11: 9).

Mungu" ni ushahidi wazi wa mafundisho ya dini ya kutwaa utu - kwamba Mwana aliishi kabla kuzaliwa kwake na akawa binadamu. Zaidi ya hayo lugha ii hii inatumika kwa wale ambao hawadaiwi kuishi kabla kuwepo. Yohana Mbatizaji pia "alitungwa kutoka Mungu" (Yohana 1:6). Nicodemus alifikiria kwamba Yesu alikuwa mwalimu "kuja" kutoka kwa Mungu, na si kumaanisha kuwa Yesu alikuwepokabla, lakini/ila aliamuriwa na Mungu (Yohana 3:2). Yesu alitoka " kwa Mungu" (ek theou), lakini wafuasi pia wametoka kwa Mungu (ek theou) (Yohana 8:47). Kwa lugha ya Yohana, manabii wa uwongo wamejitokeza "mbele" (exerchesthai) duniani (1 Yohana 4:1) kwa mfano kuhubiri. Yesu pia alidai kuwa "alikuja mbele" kuhubiri Injili ya Ufalme (Marko 1:38). Marko hana onyesho lolote la kuishi kabla kuwepo popote katika Injili yake, na tafsiri ya Luka ya msembo uo huo ni kwamba Yesu "alitungwa" na Mungu (Luka 4:43). "Kuja" na "kutungwa" ni njia yenye maana mmoja ya kueleza wazo kwamba Yesu aliamriwa na Mungu kama ajenti wake, kwa njia ya akili ya Kiyahudi ya Shaliach, au mjumbe/balozzi aliyepewa hukumu/mamlaka ya ruhusa kutoka kwa "aliyemtuma" na habari.²⁰⁴

Dunn anasisitiza kuwa Musa na manabii na wengine waliotungwa na Mungu: "Ni wazi... kwamba kutungwa mbele [exapostellein] ikitungwa na Mungu hakituambii chochote kuhusu mwanzo wa kuondoka kwa aliyetungwa; unasisitiza mwanzo wa ki mbinguni wa kuamuriwa, lakini si wa aliyeamuriwa."²⁰⁵

Neno hili linaendelezwa na maneno ya Rengstorf. Fasiri yake inaonyesha mwenendo wa mara kwa mara wa mwenye kufasiri kuwinda wazo hilo la kuwepo kabla katika hali "isiokosa hatia" na ya ki Bibilia: "Kwa lugha mbalimbali hakuna tegemezi ya maandiko ya Zn (Zn Gl. 199 ad Wagalatia 4:4, 6, kama vile wafasiri wakale na hata wa sasa) kwamba katika Wagalatia 4:4 herufi ex katika neno exapostellein unaonyesha kuwa kabla kutungwa kwake, aliyetungwa alikuwapo kwa hadhara ya aliyemtuma."²⁰⁶

Onyo ii hii inafaa kutungwa katika matumizi ya kutungwa (exapostellein) katika Yohana. Hii haimaanishi kuwa Mwana alikuwapo pamoja na Baba kabla ya kutungwa.

"Kutungwa kutoka kwa Mungu" unamaanisha kupewa amri ya kutenda kazi ya Mungu isio na kifani; na "kuja mbele duniani" ni kujitokeza mbele ya umati ukiwa na maagizo. Hauna chochote kwa uhusiano na kuwapo kabla ya kuzaliwa. Yohana inasomwa mara kwa mara na neno lisilohakikishwa kwamba Yesu alitungwa kutoka kwa kuwapo kabla kwa dunia katika duara tofauti. Sawa na hayo, "kuja chini kutoka mbinguni" hauna taarifa wa kuwapo mbinguni kwa kikweli. Katika lugha la Agano Jipya "zawadi lolote ile inatoka mbinguni" (James 1:17; cp. 3:15), na sio kuwa kila zawadi kinashuka kutoka angani. Mji mkuu takatifu pia kitashuka kutoka mbinguni (Ufunuo 21:2). Lakini hii haina ushahidi kuwa unaelea chini kutoka anga. Lugha hii ya "kushuka" unaonyesha tabia ya kufikiria ya ki Ebrania kuwa watu wengi au viumbe katika mpango wa Mungu "ulikuwapo" mbinguni kabla yao kuonwa duniani.²⁰⁷

Wakati Yesu alienda sambamba kati ya "kuja chini" kwake kutoka mbinguni (Yohana 6:33, 38, 50, 51, 58) na kushuka kwa mbegu kutoka mbinguni (Mwanzo 16:4, 15; Nambari 11:9, LXX), hakupeana onyesho kuwa alishuka kweli. Mbegu huo pia kwa kweli haukupitia anga kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu kwa msitu. Ilionekana kama jambo la ajabu duniani. "Kuja chini kwa Yesu kutoka mbinguni" unamaanisha kuwa yeye

²⁰⁴ Cp. P. Borgen, "Ajenti wa Mungu katika Injili ya Nne," katika kitabu cha Religions in Antiquity: Essays in Memory of E.R. Goodenough, ed. J. Neusner (Leiden, 1968), 137-148.

²⁰⁵ *Christology in the Making*, 39.

²⁰⁶ Theological Dictionary of the New Testament, ed. Gerhard Kittel, Gerhard Friedrich and Geoffrey W. Bromiley, trans. Geoffrey W. Bromiley, 10 vols. (Grand Rapids: Eerdmans, 1964-1976), 1:406.

²⁰⁷ Cp. Emil Schurer alisema kuwa katika mafikira/hisia ya Kiyahudi, "kila kitu cha thamana ya kweli kilikuwapo kabla katika mbingu" (Historia ya watu wa Kiyahudi kwa wakati wa Yesu Kristo), *The History of the Jewish People in the Age of Jesus Christ*, T&T Clark, 1979, 2:522).

ndiye zawadi wa ajabu kwa binadamu, aliyekuwa katika mpango wake wa maonyo ya milele. Yesu pia "alikuja duniani," lakini katika lugha ya Johannine kila mwanadamu akiwa sawa "anakuja duniani" (Yohana 1:9) na maneno hayo kwa urahisi yanamaanisha kuzaliwa: "Mimi ni mfalme. Kwa mwisho huu nilizaliwa, na kwa sababu hii nilikuja duniani" (Yohana 18:37). Tafsiri ya muhtasari ya maneno hayo yanayo maana sawa, ingawa kwa lugha tofauti: "Lazima nitangaze Habari Nzuri ya Ufalme wa Mungu... Hii ndiyo sababu nilitumwa" (Luka 4:43; cp. Marko 1:38).²⁰⁸

Yesu kabla Yohana

Yohana Mbatizaji anasema kuhusu Yesu kuwa "alikuwa mbele yangu" (Yohana 1:15). Wasomi wengi kwa kawaida wanachukulia maneno haya kama thibitisho la uaminifu wao kwamba Mwana alikuwa hai mbinguni kabla kuzaliwa kwake. Morris anaonyesha kuwa maneno yasiyodhihirika kwa maneno "kabla" unaweza maanisha cheo cha hali ya juu zaidi ya umuhimu katika wakati. Fungu hilo linaweza fasiriwa, "Mwandamizi wangu amenitangulia, kwani yeye (mara kwa mara) alikuwa kabla yangu, mkuu zaidi." Ingawa ufafanuzi huu unasaidia wazo kwamba Yesu alimtangulia Yohana kwa wakati, inadai kuwa "wengine wanachukua neno 'kwanza' kumaanisha si 'kwanza kwa wakati,' 'kabla,' lakini kwanza kwa umuhimu,' ambao utakuwa na maana wa kuonyesha' alikuwa mkubwa wangu"²⁰⁹ Hivi ndivyo Murray na Abbot wanaielewa fungu hili.²¹⁰ Yohana 1:15, 30 haiwezi kudaiwa kama ushahidi kwamba Yesu alikuwapo kabla kuzaliwa.

Yohana 3:13 na 6:62

Kumekuwa na majadiliano mengi kuhusu matamshi ya wakati wa baadaye kwamba "hakuna aliyepanda mbinguni ila aliyeshuka kutoka mbinguni, Mwana wa Binadamu." Kama maneno haya yangechukuliwa kama maneno ya Yesu mwenyewe, badala ya maoni ya baadaye ya Yohana, Yesu anaonekana kusema kuwa yeye pekee ndiye aliyepanda mbinguni.

Wachambuzi wanashangazwa na matumizi mema zaidi wa maneno. "Maneno haya mema 'imepanda' hayajarajiwi."²¹¹ "Matumizi ya maneno haya mema ni ngumu, kwa sababu inaashiria kwamba Mwana wa Binadamu ashopanda mbinguni."²¹² "Ugumu wa fungu hilo unatokana na neno 'amepanda.' Unaashiria kwamba Mwana wa Binadamu alikuwa ashopanda mbinguni kwa wakati huo walipokuwa wakizungumza."²¹³

Ni kwa maana gani Yesu alidai kuwa ashopanda mbinguni? Taarifa hii imechukuliwa na wengine kama kumaanisha kuwa kwa wakati mwingine katika historia ya kuhubiri Yesu alikuwa amesafirishwa mbele ya Baba yake. Lakini Injili haionyeshi popote tukio kama hilo. Wengine wamebisha katika wakati uliopita, mfano, kwamba Mwana wa Binadamu aliamuriwa kupanda, unabii wa kupanda kwake baada ya kufufuka. Kuna maelezo rahisi ya kueleza jinsi Yesu alipaa mbinguni kwa msingi wa Biblia hapo awali na njia za kuzungumza za Kiyahudi. "Hakuna aliyepaa mbinguni ila yule ambaye aliyeshuka kutoka mbinguni, Mwana wa Binadamu, ambaye yuko mbinguni" ni maelezo

²⁰⁸ Cp. John A.T. Robinson, *The Human Face of God* (London: SCM Press, 1973), 172-179, kwa uchunguzi wa matumizi ya lugha ya Yohana iliyo sawa kwa Yesu na waaminifu.

²⁰⁹ Leon Morris, *The Gospel According to John*, 108, 109.

²¹⁰ J.O.F. Murray, *Jesus According to St. John* (London: Longmans, Green, 1936); E.A. Abbot, *Johannine Grammar* (London: A. and C. Black, 1906) cited by Leon Morris in *The Gospel According to John*, 109.

²¹¹ "Vitu vy mbingu" katika kitabu cha Waebrania vinamaanisha vitu ambavyo vitakuwepo wakati wa kurudi kwake Yesu (Waebrania 11:16, 20; cp. 13:14).

²¹² Morris, *The Gospel According to John*, 223.

²¹³ Raymond Brown, *The Gospel According to John*, 1:132.

ya mifano ya mafikira ya kipekee ya Yesu ya mpango wa Yesu wa wokovu. Yesu ana kuelewa wa kipekee wa siri za dunia ambazo anawaonyesha wote ambao watamsikiliza. Maneno "yule aliye mbinguni," ambayo inaonekana katika maandiko/miswada ya Giriki na kama vile Latina na Syria, inaonyesha kuwa Yesu, wakati alipoishi duniani, alikuwa pia kwa wakati uo huo "mbinguni", katika ushirika wa mara kwa mara na Baba yake ambaye alimtegemea kwa kila kitu. Kama daraja kati ya mbingu na anga, alidai kuwa na ruhusa ya kipekee ya habari takatifu. Maneno sawa na haya unatumika kwa waaminifu wote ambao wanaelezwa na Paulo kama "walioketi katika mahala takatifu mbinguni" (Waefeso 2:6).

Kupaa kwa Yesu mbinguni wakati wa mahubiri yake unaonyesha uhusiano wake wa karibu na Baba yake. Kama Mwana, anakaa "karibu na Baba" (Yohana 1:18). Mazingira ya Yohana 3:13 kwa maandishi yake, yanaonyesha Yesu katika mazungumzo na Nicodomeo kuhusu siri za kutokufa. Yesu "anazungumza kuhusu kile ambacho tunakifahamu" (Yohana 3:11). Kinyume na kutoelewa kwa Nicodomeo kuhusu njia ya kuingia katika ufalme/utawala na umuhimu wa kupata wokovu, Yesu anasema, "kwa kweli ninakuambia, tunatoa ushuhuda kwa kile ambacho tumekiona, lakini nyinyi watu hamkubali ushuhuda wetu" (Yohana 3:11) Yesu anashuku uwezo wa Nicodomeo kupata "vitu vya mbinguni." NI siri hizi za mbinguni ambazo Yesu anaweza kuonyesha kwa sababu "amepaa mbinguni" na "yuko mbinguni." Katika Methali 30:3, 4 maneno ya Agur una maana sawa na kupaa mbinguni. Kiumbe/kifaa kama hiki cha "kupaa" ni kupata welevu na ufunuo takatifu. "Kweli mimi ni mjinga kuliko binadamu yeyote. Sina welevu wa mwanadamu. Wala sijajifunza hekima. Wala akili ya Yule Mtakatifu. Nani amepanda mbinguni na akashuka?" Sawa na hayo Baruch 3:29 inauliza: "Nani ameenda juu mbinguni na akaupata [hekima] na kuuleta chini kutoka wingu?" (cp. Kumb. 30:12).²¹⁴ Katika hali ya Yesu, anayedhihirisha mkuu na wa mwisho, wa nia ya Mungu, ambapo daraja ya kutoka mbinguni kwenda duniani umejengwa. Mwana "alimweleza" Baba. (Yohana 1:18) Hakuna yeyote ila Mwana wa Binadamu aliyepata kipimo/kiwango kama hicho cha hekima takatifu. Kwa wakati huo Mwana wa Binadamu - Yule Mwanadamu - ameshuka kutoka mbinguni, ambayo ni maan aya kiyahudi ya kujieleza na sio kwamba yeye ni zawadi ya Mungu kwa dunia. (cp. James 1:17; 3:15)

Adam Clarke alifasiri fungu letu hivi: Hii inaonekana kuwa maelezo ya mfano "hakuna aliyefahamu siri/fumbo za ufalme," kama katika Kumbukumbu 30:12 na Warumi 10:6; na maelezo haya yanapatikana katika fumbo la kawaida kwamba, ili mtu aweze kujitambulisha na shughuli ya mahali, ni muhimu kwake kuwa hapo.²¹⁵

Mfasiri Mjerumani, Christian Schoettgen, katika Horae Hebraicae yake alitazama Yohana 3:13 hivi "Ilikuwa elezo iliyo kawaida kati ya Wayahudi ambao wanasema kuhusu Musa kuwa alipanda mbinguni na hapo akapata ufunuo wa desturi ya kuabudu kwa utakatifu." Anadondoa maneno ya walimu/mapadre wa Kiyahudi kwa kusema, "Si mbinguni ambapo unafaa kusema, 'Ah kwamba tulikuwa na mmoja kama Musa yule nabii wa Mungu kupanda/kupaa mbinguni na kuileta (sheria) kwetu hapa chini'" (Jerusalem Targum katika Kumb.30:12). Katika Yohana 6:62 Yesu alitoa maneno ya kubisha/kukaidi kuhusu anavyokusudiwa kama Mwana wa binadamu alivyotabiriwa. Baada ya kuonyesha "maneno yake mwenyewe magumu" kuhusu kuwa "mkate ulioshuka chini kutoka mbinguni" Yohana 6:58-60), Yesu aliuliza kama fundisho hili linaweza kufanya wanaohudhuria kukosa: "Je, kama ungemwona Mwana wa Binadamu akipaa pahali ambapo alikuwa hapo awali?" Yesu alijizungumzia katika fungu hili kama Mwana wa Binadamu. Kama Inavyojulikana, jina hilo la heshima linatoka katika kitabu cha Danieli

²¹⁴ C.K. Barrett, *The Gospel According to St. John* (London: SPCK, 1972), 177.

²¹⁵ J.H. Bernard, *St. John, International Critical Commentary* (Edinburgh: T&T Clark, 1948), 1:cxix, cxxxi.

7:13 ambapo, miaka 550 kabla ya Yesu kuzaliwa, Danieli aliona tokeo la Mwana na Binadamu mbinguni akipokea ruhusa ya kuongoza pamoja na walii/watawa katika ufalme wa Masiya wa wakati ujao:

Yesu alitumia [jina la heshima la Mwana wa Mungu] kwake pamoja na kidokezo kuwa kwake yeye kulikuwa na utekelezaji /utumilizo wa tokeo la Danieli....Ni jina la heshima ambalo amezoea kutumia wakati alipokuwa akiwatabiria wafuasi wake kuhusu maumivu makali ya Yesu msalabani aliposubuliwa kama wazo isiyoepekika na iliyoamuriwa hali ya baadaye ya mahubiri yake kwa umati.⁵⁵

Maneno yafuatayo kutoka kwa Injili ya Muhtasari yanaonyesha jumlisha. Kwa kila hali Yesu anajizungumzia kama Mwana wa Binadamu - jina hili la heshima linalomaanisha "mwanachama wa ujamaa wa binadamu" - ambaye amekusudiwa kuteseka, kufa na kufufuka: "Mwana wa Binadamu anafaa kuenda kama ilivyoandikwa kumhusu " (Mathayo 26:24). Marko anazungumza kuhusu uvumilivu wa Yesu aliposubuliwa kwake Mwana wa Binadamu kama jambo la unabii/ubashiri wa Agano la Kale: "Je, imeandikwa vipi kuhusu Mwana wa Binadamu kwamba anapaswa kuteseka kwa vitu vingi na kudharauliwa?" (Marko 9:12).

Katika Injili ya Yohana pia, jina la heshima "Mwana wa Binadamu" unahusiana na ubashiri/uaguzi na kile ambacho kimekusudiwa kumfanyikia Yesu katika timizo la ubashiri wa Agano la Kale: "Na kama Musa alivyoinua nyoka...ndivyo Mwana wa Binadamu anafaa muinuliwa juu (Yohana 3:14).

Jambo la maneno ya fumbo katika Yohana 6:62 ni Mwana wa Binadamu, jina la heshima ambalo linamchagua Yesu kama Mwanadamu. Tukiuliza alipokuwa Mwana wa Binadamu hapo awali, jibu la kiBibilia linapatikana katika Danieli 7:13. Masiya Binadamu alionekana mbinguni katika tokeo la wakati ujao ambao ulikuja ukawa wa sasa/ukweli wakati wa kupaa (Matendo 2:33), ambapo Yesu alisifiwa katika mkono wa kulia wa Mungu. Daudi hakuwa amepaa mbinguni (Matendo 2:34). Tofauti na mapokeo ya kisasa, wazee wakuu/askofu "hawajaenda mbinguni." Wanalala kwa makaburi yao walingoja kufufuka kwa wale wote waaminifu (Dan.12:2; Yohana 5:28, 29) Ni Masiya pekee aliyekusudiwa kwa cheo/daraja. Katika Yohana 6:62 anatarajia kupaa kwa wakati ujao ili kutimiza kile ambacho aliazimiwa mbeleni kulingana na mpango takatifu ulioonyeshwa katika tokeo la Danieli.

Fungu hizi hazina ruzuku kwa mafundisho ya dini kwamba mwanachama wa pili wa Uungu, "yule Mwana wa Mungu wa milele," alikuwa mbinguni kabla ya kuzaliwa. Ni "Mwana wa Binadamu," mwanadamu anayeishi kabla mbinguni. Hakuna "Mwana wa Milele" mbinguni kabla kuzaliwa kwa Yesu. Mwana wa Binadamu haonyeshi mwanadamu mtakatifu wa pili ambaye hajaumbwa, kama ilivyotakikana kwa Uteolojia wa Waunitaria. Maneno hayo yanalingana na/yana uhusiano na matendo ya Mwana wa Binadamu. Wanaoamini Utatu hawadai kuwa Mwana wa Binadamu aliishi kabla kuzaliwa kwake. Mwanzo wa ugumu wa Yohana 6:62 ni wazo rahisi kweli kweli, ambayo wasomi wa Yohana lazima wajitambulishe nayo. Yesu alijiona akitimiza "orodha" iliyoamuriwa mbele na iliwekwa mbele mwanzoni katika maandiko. Kile ambacho aliahidiwa kinaweza kusemekana kama kile kilichotendeka kwa ukweli katika tokeo au ubashiri mwingine kabla kifanyika kwa ukweli. Mwana wa Binadamu alikuwa mbinguni, na kuonekana katika "maonyesho ya mbele ya mbinguni" kabla yake kufika huko (Yohana 6:62) Jmabo sawa na hilo lilisimuliwa na muhtasari ambayo ni onyesho la tokeo la Elija na Musa (Mathayo 17:1-9) Katika Yohana 3:13 Mwana wa Binadamu alikuwa ashapokea ruhusa ya kukaribiwa hekima ya kiMbinguni. Lakini baadaye katika Yohana 20:17 Yesu anasema kuwa "bado hajapaa kwa Baba." Maneno ya kwanza (Yohana 3:13) ni ya kuchukuliwa kama mafumbo, wakati uliofuata unarejelea kuondoka kwa Yesu kwenda kwa Baba.

Tunafaa tifikiri kwa makini katika Injili ya Yohana , tukikumbika kuwa Yohana alikuwa mtu wa fikira/akili nyingi na mteolojia ambaye alifurahia kutoa habari ya Uyahudi wa Yesu na saa zingine hali yake ya kuzungumza kwa mafumbo na kubadilishana na watu waliopo. Hii inafaa kutuonya/kutushauri kwa kusoma Yohana kwa njia ambayo ukristo wake unaenda kinyume na Mathayo, Marko, Luka na pia kitabu cha Matendo. Ni muhimu kwa Ukristo wa mapokeo ambao unaegemeza kanuni za Imani za wanaoamini Utatu, unaotoka kwa Yohana bila shughuli yoyote y a mchoro wa muhtasari wa Yesu, wala ile ya Petero katika mahubiri yake kwa kitabu cha Matendo na mabarua yake. Ni kwa maungamo ya Petero kwa Yesu kama Masiya kwamba kanisa inafaa ianzoshwe (Mathayo 16:16, 18) Petero hatupatii sababu yoyote ya kuamini kwamba alifikiri kuwa Yesu alikuwapo kabla kuzaliwa kwake. Na Yohana aliandika "Yesu ndiye kristo, Mwana wa Mungu," na sio Mungu mwenyewe (Yohana 20:31)

Utukufu Kabla Dunia Ulikuwa

Mtu akiangalia maneno kwa uaminifu mkuu kwamba Yesu alikuwapo kabla kuzaliwa kwake, bila shaka Yohana 17:5 unaunga mkono thibitisho hilo la kosa. "Na sasa, Baba, nitukuze mimi wewe mwenyewe ukiwa na utukufu niliyo nayo mimi pamoja na wewe kabla dunia ulikuwa. Kwa mawazo ya Yohana, ni swali kuu kama kwamba fungu hili linaweza tajwa kama ushahidi/ushuhuda kwamba Yesu alikuwa hai kutoka milele uliopita. Kwa njia za ki Bibilia za kuzungumza na kufikiria, mmoja anaweza "kuwa" na kitu ambacho kiliahidiwa katika mpango wa Mungu hata kabla kuwa nayo. Abrahamu alipewa ardhi kama maagano (maafikiano) hata Ingawa haikuwa yake bado. Ahadi inasoma hivi: "Kwa mbegu yako nimepeana ardhi hii" (Mwanzo 15:18). Kwa wakati huo mbegu hiyo haikuwapo. Lakini walipewa ardhi. Ahadi ya Mungu ina maneno kama ingawa Ilikuwa ushatimizwa.

Kwa hivyo katika Yohana 17:5 utukufu aliyokuwa nayo Yesu pamoja na Baba ulikuwa utukufu uliotayarishwa kwake katika nia/kusudi ya Mungu kwa Mwana wake. Onyesho la kutisha wa matumizi ya wakati uliopita unapatikana katika fungu la 22. Hapa, utukufu uo huo ulioahidiwa kwa Mwana ulipewa kwa wafuasi ambao hawakuwa wameanza kuishi. Walikuwa wafuasi ambao wangebadihishwa baadaye (fungu la 20) Tukiwazungumzia, Yesu alisema, "Utukufu ambao ulinipa, nimewapa wao." Maana yake ni kuwa Yesu aliahidi kuwa atawapa. Walikuwa wameimiliki lakini si kwa kweli. Kama Mungu, Yesu alizungumza kuhusu "vitu ambavyo havijaumbwa lakini vinaonekana kama vilikuwapo" (Kirumi 4:17). Alipoomba ili apate utukufu kama aliyojua aliahidiwa na Mungu, anazungumzia utukufu huo kama ambayo "alikuwa" nayo pamoja na Baba, kumaanisha kuwa alikuwa nayo ilivyowekwa na Baba," kama akiba/amana yake katika mpango wa Mungu. Kwingine aliwahimiza wafuasi wa ahadi kwamba "zawadi yao ni kuu mbinguni" (Mathayo 5:12) Zawadi hiyo ilikuwa tayari kupewa kwa wakati ujao kwa kurejea kwa Kristo (Math.16:27). Kwa hivyo pia utukufu utakaopewa Yesu ulikuwa umeamuriwa kama miliki kutoka mwanzo. Sasa aliomba kuupata.

Fasiri ya matumizi ya lugha, na H. H. Wendt, profesa wa somo la Teolojia katika Heidelberg aliandika:

Ni kituo cha kufahamu vema kwa njia ya maneno na wazo ya \agano Jipya, tukifahamu kuwa ilani/habari ya Yesu [katika Yohana 17:5] kuwa alikuwa na utukufu pamoja na Baba kabla dunia ilijengwa, ni sawa kwa maana na wazo kuwa yeye mwenyewe alikuwapo kabla...kulingana na hali ya maneno na wazo la kuenea katika Agano Jipya, uzuri wa ki Mbinguni, na pia utukufu wa ki Mbinguniunaweza fahamika na kuzungumziwa kama inayoishi pamoja na Mungu

na mali ya mtu, na sio kwa sababu mtu huyu anaishi na kuzingiwa na utukufu, lakini kwa sababu utukufu wa Mungu kwa njia moja kiliwekwa na kuhifadhiwa kwa mtu huyu mbinguni. Tunakumbuka kuwa, kulingana na habari ya Mathayo, Yesu pia anazungumzia mali/tunu (Math.6:20 au zawadi (Math. 5:12,46; 6:1) ambayo wafuasi wake wanayo mbinguni pamoja na Mungu...;na zaidi, vile katika habari ya hukumu ya mwisho ya dunia ufalme ambao wale waliobarikiwa kwa Baba wataridhi, inaelezwa kama aliyetayarishwa kwao kutoka kujengwa/kuumbwa kwa dunia (Mathayo 25:34); na pia vile katika (Wakolosai 1:5 na Petro 1:4) tumaini ya wokovu ya wakristo unabainisha kama Baraka/radhi iliyotayarishwa kwao mbinguni.... Yesu hajiulizii kitu kigeugeu, lakini kile ambacho alifaa kupewa kulingana na amri/agizo ya Mungu na kile ambacho ni chake...; jambo ambalo lisilothibitika kwa taarifa/ilani hii, ingawa ni fikira hii ambayo inapata maneno iliyokubaliwa kwa timizo ya maombi katika fungu 24, kwamba Yesu mwenyewe, kama Masiya, hakuwapo kutoka mwanzo pamoja na Mungu, lakini alikuwa chombo cha pendo la Mungu, wa mafikira yake ya mapendo, mipango na kusudi.²¹⁶

Ni jambo la kuonya kutafuta maana za kiBibilia kwa maneno ya kiBibilia. Tukisoma Yohana kwa njia ya kumwamini Mungu mmoja ambayo anathibitisha (Yohana 17:3; 5:44), tunafaa kuwa waangalifu kuhusu kudani au kuona kuwapo kwa Masiya kabla kuzaliwa kama mwanachama wa pili ambaye hajaumbwa kwa Uungu. Shida ya ghafla ya mapatano ya kiBibilia ya uaminifu wa Mungu mmoja unaweza epukika tukinena kwa uthabiti, pamoja na Yohana na Yesu, kwamba Baba "pekee yake ni Mungu," (Yohana 5:44) na kwamba yeye ndiye Mungu wa pekee wa ukweli (Yohana 17:3). Hatufai kuelewa/kusoma maneno kwa wazo la wakati wa baadaye ya Bibilia uliopatikana kutoka Imani, wakati suluhisho sawa kuliko hiyo kwa fumba ya Ukristo wa Yohana ulio katika eneo lake mwenyewe la uaminifu wa Mungu mmoja wa Mkristo wa Kiyahudi.

Wazo hili ambalo tunashindania ulionekana katika vitabu vingi vilivyoandikwa kwa geuzi la karne na Profesa wa maandiko wa lugha ya Agano Jipya katika chuo/madarasa ya ki Teolojia ya 'Chicago, G.H Gilbert. Anaandika kuwa:

haifuatii kutoka [kukubali kwa Yesu 'kuabudu'] kwamba mtu kipofu alimtazama Yesu kama kuwa katika asili moja na Mungu. Neno ambalo linalotafsiriwa kama abudu linatumika kama hehsima kuu ambayo inamhitaji mwenye enzi kulipa na inaonyesha bila kutaja kuwa yule ambaye aliipokea ana heshima kuu kuliko yule ambaye aliyetoa. (cp. Ufunuo 22:8)

Kwa masimulizi ya Tomaso kwa Yesu kama "Mungu," anasema, "Yesu alikubali heshima kuu ya Tomaso kama heshima kuu aliyopea Umasiya.... Hakuna maoni kuwa aliona heshima hii kama inadokeza kuwa alikuwa wa kadiri moja na Baba."²¹⁷

Jambo hili la muhimu linashindana nna wazo kuwa, kwa sababu Yesu aliabudiwa basi lazima awe ni Mungu. "Abudu," walakini, unaweza kutolewa kwa wafalme kama namna ya Mungu na pia watawa wasifiwe (1 Korintho 29:20; Ufunuo 3:9) Ni

²¹⁶ Mafundisho ya Yesu (*The Teaching of Jesus*) (Edinburgh: T & T Clark, 1892), 2:169-172, mkazo unaongezwa.

²¹⁷ Ufunuo wa Yesu, Somo la Asili ya Msingi ya Ukristo (*The Revelation of Jesus, A Study of the Primary Sources of Christianity* (New York: Macmillan Co., 1899), 225, 226. Gilbert alikuwa pia mwaandishi wa "The Student's Life of Jesus" na "The Student's Life of Paul."

udanganyifu kwa hii, kubusha kuwa kwa sababu Yesu "anaabudiwa," lazima awe ni Mungu. Yesu anaweza "abudiwa" kama Masiya. Ni Baba pekee anayeabudiwa kama Mungu. Kiarifa cha Giriki sawa na hiyo una maana sawa kwa asili zote za "kuabudu."

Gilbert alitatu swala la kuwapa kabla, katika Yohana, akitazama kuwa Injili za Muhtasari hazionyeshi wazo hili. Tukizungumza kuhusu utukufu Yesu aliomba katika Yohana 17:5, Gilbert anaiona kama zawadi kwa kazi ambayo Yesu alikuwa amekamilisha:

Yesu alimiliki utukufu huu kabla msingi wa dunia kwa maan asawa kuwa ilikusudiwa kwake kitakatifu. Alijua kuwa kazi yake ya kiMasiya ilipangwa na mungu tangu milele, na kwamba matokeo ya utukufu uliwekwa akiba kwake... Tunamaliza/Tunakomesha kwamba mafungu haya matatu katika Yohana [6:62 ; 8:58 ; 17:5], ambapo Yesu anataja juujuu kuwa kuwapa kwake kabla, hauhusiki na dai kuwa kuwapa kabla huu ulikuwa wa binafsi na ukweli. Zinawekwa katika kiwango moja na wazo/ njia ya kufikiria wa kiMasiya kwa Yesu, usiokuwa na uhusiano na Muhtasari au katika Injili ya nne wala ushirikiano wa Baba.²¹⁸

Je, ufasiri wa sura hii kinathibitisha kuwa hii ni njia sawa ya kuelewa lugha yake Yohana ya kuwapa kabla? Matumizi ya wakati uliopita katika Yohana 17 unahitaji kutazamwa kwa makini. Kuna maonyesho wazi katika sura hii kwamba wakati uliopita unaweza kueleza /onyesha si kile ambacho hakijafanyika bali kilichokusudiwa kufanyika, kwa sababu Mungu alikuwa tayari ameamuru. Tunafaa kutazama kwanza onyo la Brown: "Katika onyesho za 'Johannine' kwa Yesu, kuna kutojali kwa maandamano ya wakati ambayo lazima itegemewe."²¹⁹ Bernard anatazama kuwa "mwisho wa hali ya baadaye unaonekana kutoka mwanzo."²²⁰ Katika mchanganuo wake Yohana 17, Morris anatazama kuwa "ya kawaida kwa sheemu hizi zote [ya Yohana 17] ni taraji kwamba kusudi la Baba litawekwa mbele."²²¹ Katika Yohana 17:2 "Tuna wazo takatifu ya hali ya baadaye."²²² Brown anatazama kuwa "nguvu ya kuruzuku maisha haungekuwa kamilifu bila / adhama/utukufu ya Yesu," ingawa Yesu anasema kuwa nguvu hii "ilitolewa."²²³ Tunaweza kulinganisha Yohana 5:27 : "Mungu alimpa ruhusa ya kutekeleza hukumu." Alikuwa amepewa ruhusa lakini, kuanzishwa kwake ungenjoja kufufuka kama ilivyoandikwa katika fungu inayofuata. Katika Yohana 17:4 Yesu alizungumza ni kama kitendo hicho kilikuwa kimekamilishwa."²²⁴ Katika Yohana 13:35 pia Baba amempa Yesu vitu vyote na kuviweka mkononi mwake. Ebrania 2:8 inakubali kuwa: "umeweka vitu vyote chini ya miguu yake... Kando na hayo, hatuoni vitu vyote ni kama viko chini yake" (Ebr. 2:8). Mipango takatifu ya matokeo ya baadaye yanaelezwa kwa wakati uliopita.

Jambo la kawaida katika maneno ya Yesu ulikuwa kwamba Mungu ameamuru kumpa nguvu na ruhusa, mengi ambayo hayajanzishwa. Mwendo huu wakati uliopita pamoja na maana ya baadaye unaendelea: Ya Yohana 17:4, Meyer alishikilia kuwa Yesu "ashakichukua katika wazo hili...hakika ya kifo kama ilivyotimizwa tayari,"²²⁵ lakini Yesu bado amekufa. Alford anatazama kuwa "Bwana wetu anasimama kwa matarajio

²¹⁸ Ibid., 221, 222

²¹⁹ Injili kulingana na Yohana, 1:132.

²²⁰ "St. John, International Critical Commentary," 1:76.

²²¹ Injili kulingana na Yohana, 716.

²²² Ibid., 719.

²²³ Injili kulingana na Yohana, 2:740.

²²⁴ Ibid., 2:741.

²²⁵ Ufafanuzi wa Agano Jipya: Injili ya Yohana (New York: Funk and Wagnalls, 1884), 46

kwa mwisho wa alichotimiza na inaonekana nyuma kwake kama ya kitambo."²²⁶ Hata katika Yohana 17:9, tangu "wafuasi wa kihistoria ni kama mfano kwa Wakristo wote..., Wakristo wa wakati wa baadaye wanavyofikiriwa."²²⁷ Lakini Yesu alizungumza ni kama kitendo chake kwa niaba ya Kanisa ilikuwa imekamilishwa. Yesu akisema "Nimetukuzwa ndani yao," hali nzuri ni inayotarajiwa [ikitarajia wakati wa baadaye], ikizungumzia mbele kwa utukufu ambao bado haujakuja, lakini ni wa hakika."²²⁸ "Kile ambacho kimeshaanza na kwa hakika kitatimizwa kwa wakati wa baadaye unaokaribia, anavyoona Yesu akizungumza halisi kwa matarajio ya kinabii, kama Iliyokamilishwa na ulivyoishi ukweli" (fungu 10).²²⁹ 69

Maombi ya Yesu yanaendelea: "Siko tena duniani" (Yohana 17:11). Anazungumza ni kama alikuwa ashaenda. "Kwenda kwake umekaribia sana hadi anaweza kutumia wakati wa sasa kuieleza."²³⁰ 70 Hata katika fungu ka 12, kuongea kwa ukali, Judas hakuwa bado amefariki. Hata sasa imedokezwa kuwa amefariki, katika kutimiza maandishi kama "maisha/hali takatifu."²³¹ 71

Wakati uliopita wa baadaye kwa maana unaendelea: "nimewatuma...." (Yohana 17:18), Morris anatazama kuwa "tukija kwa mitume tunafaaa kutarajia wakati wa sasa au baadaye katika pahali pa 'Nimetuma.... Ni labda jambo linalowezezekana kuwa limetumika kama linalotarajiwa. Inaongeza wazo la hakika kwa wafuasi wanaotumwa nje."²³² Meyer pia anakubaliana: "Maagizo haikuwa ya kweli (Yohana 20:21; Math. 28:19), lakini tayari katika wazo la kuteuliwa na mafundisho ya ofisi ya mitume."²³³

Mwisho, Yesu anawaomba wafuasi ambao hawajabadilishwa lakini watakuwa Wakristo kutokana na mahubiri ya kitume. Yesu anasema kuwa utukufu ambayo Mungu "alimpa" yeye "amewapa" wafuasi wa wakati wote (Yohana 17:22). Utukufu kama swali: Baba amempa ingawa hajamiliki, lakini kama miliki salama ya wakati wa baadaye unaokaribia; ameipokea kutoka kwa Mungu, iliyodhaniwa kama mali, na miliki wa kweli kwa umekaribia. Kwa njia ii hii amewapa utukufu huu... kwa waaminifu ambao wataingia kwa miliki wa kweli katika kuja kwa Yesu kwa mara ya pili, ambapo watatuluzwa pamoja (Kirumi 8:17) baada yao kuokolewa kwa tumaini (Kir.8:24) Wao tayari ni warithi walioshikana na roho ambayo wanafaa kupata/kupokea, utakuwa malipo wa kwanza (Waefeso 1:14; 2 Kor. 1:22; 5:5) ; lakini mlango wa ukweli unaoelekea kwa uroithi unatimizwa katika kuja kwa Yesu kwa mara ya pili.²³⁴

Hapa pia wakati uliopita unaonyesha vitu vya hakika ambavyo viko katika mpango wa Mungu kwa wakati ujao.

Yesu anazungumza tena kuhusu utukufu ambao "umenipa" (Yohana 17:24). Morris anahisi kuwa "Yesu anaweza kuwa anazungumzia adhama na fahari itakaykuwa

²²⁶ Agano Jipya ya Giriki, 823.

²²⁷ Brown, *Injili kulingana na Yohana*, 758.

²²⁸ Morris, *Injili kulingana na Yohana*, 726, mkazo unaongezwa.

²²⁹ Meyer, *Ufafanuzi wa Agano Jipya: Injili ya Yohana*, 465.

²³⁰ Morris, *Injili kulingana na Yohana*, 726.

²³¹ Meyer, *Ufafanuzi wa Agano Jipya: Injili ya Yohana*, 466.

²³² Morris, *Injili kulingana na Yohana*, 731.

²³³ Meyer, *Ufafanuzi wa Agano Jipya: Injili ya Yohana*, 468.

²³⁴ Meyer, *Ufafanuzi wa Agano Jipya: Injili ya Yohana*, 470.

maishani mwake baadaye." ²³⁵ Utukufu huu ulikuwa "ushawekewa [wafuasi], lakini kabla kama miliki ya tumaini." ²³⁶

Kote katika Yohana 17 Yesu mara kwa mara anazungumza kuhusu vitu vinavyongoja utimilizo baadaye, na vilivyofanyika tayari. Anatumia wakati uliopita wa tokeo ambayo inajulikana katika maandiko. Katika Yohana 17:5 anaomba utukufu ambayo amekuwa nayo pamoja na [Baba] kabla msingi wa dunia." Katika maono ya matamshi katika fungu hili; ni wazi kuwa utukufu "aliokuwa nayo ni utukufu aliyotayarishiwa katika mpango wa Mungu. Ni utukufu uo huo ambao wafuasi "walikuwa" nayo (kwa mfano, "ilikuwa imepeanwa," Yohana 17:22) ingawa hawakuwa nayo bado. Ni utukufu uliokusudiwa Yesu katika kusudi la Mungu lililotambuliwa awali. Ilikuwa tayari inamsubiri kutoka milele, kama vile Wakristo wakati huu wanayo urithi wa baadaye wa ufalme wa Mungu. Itatimizwa duniani kwa Kuja wa Pili (1 Pet. 1:4, 5). Yesu katika Yohana 17 aliomba apokee kile ambacho Mungu alimuagiza. Yohana 17:5, ikisomwa katika njia ya maana, hauonyeshi uhusiano wowote wa kuishi kabla kwa Yesu. ²³⁷ Ikitoka kwa maana hiyo na kwa maoni ya mafundisho ya wakati baada ya Biblia kuhusu Utatu, itaonekana kutegemeza wazo kuwa Mwana alikuwapo kwa kweli bali si kwa fikira, kutoka milele.

Yohana 17:5 iliekeweka kwa njia tunayoshauri na Polish Anabaptist wa karne ya kumi na saba aliyeandika katika *Racovian Catechism*:

Kwamba mtu anaweza kuwa alisikia kitu, na kwa sababu hiyo akawa na utukufu, pamoja na Baba kabla ya kuwapo kwa dunia, bila kukomesha kwamba alikuwapo kwa kweli ni dhahiri kutoka Timotheo 1:9, ambapo Mitume anasema kuhusu wanaoamini kwamba walipokea neema kabla kuwapo kwa dunia. Hata hivyo iko hapa [katika Yohana 17] iliandikwa kuwa Kristo aliomba utukufu. Kristo anamsihi Mungu kumpa, kwa miliki wa ukweli, pamoja na ye, utukufu aliyokuwa nayo, kwa kusudi na hukumu/amri, kabla kuwapo kwa dunia. Walakini inasemwa kuwa mtu ana kitu na mt u yeyote, ikiwa ni ahadi au ilikusudiwa kwake. Kwa hii, wanaamini mara kwa mara wanasemwa na mweneza Injili kuishi milele. Hivi basi inaendelea kuwa Kristo hasemi kwa hakika kwamba alikuwa na utukufu huo, lakini alikuwa nayo na Baba; ni kama alikuwa amesema kuwa sasa anaomba kufanya shauri pamoja naye kwamba utukufu ambao ulitayarishwa kwake pamoja na Baba wa kitambo na kabla kuumbwa kwa dunia. ²³⁸

Yesu kabla ya Abrahamu

Katika Yohana 8:58 Yesu alidai kuwa mkuu kumliko Abrahamu. Ukuu wake, ingawa, unategemea Baba anayemtukuza Mwana wake (Yohana 8:54). Alisema kuwa Abrahamu alifurahi "kuona siku yangu" (Yohana 8:56) - yaani, Abrahamu kwa imani

²³⁵ Morris, *Injili kulingana na Yohana*, 736.

²³⁶ Meyer, *Ufafanuzi wa Agano Jipya: Injili ya Yohana*, 471, 472.

²³⁷ Brown, *Injili kulingana na Yohana*, inaonyesha maneno ya kiini sawa kwa Yohana 17:5: "Kati ya Mababa wa kilatina na wengine wa Ethiopia MSS, kuna himili kwa masomo, 'kuwa utukufu uliokuwa naye,' ikisomwa *een* = 'ulikuwa,' badala ya 'nilikuwa nayo'" (743).

²³⁸ Mafundisho ya Teolojia ya 'Italy' (*The Racovian Catechism*) (London: Longman, Hurst, Rees, Orme and Brown, walifasiri kutoka Latina T. Rees, 1818), 144, 145. Mwaandishi wa maneno ya mwanzo (1609), B. Wissowatius, anatazama katika onyesho: "kwamba hii ni ukweli wa fungu hili unaonyeshwa na Augustine and Beda...Inafaa kutazamwa hapa, kuwa ni maoni ya wengi ya Wayahudi hadi wakati huu, kuwa Masiya hakuwapo kabla kuumbwa wa dunia, ila kwa amri takatifu." Nakala zote za mwongozo wa maelekezo ya dini ya Ukristo katika 'England' iliamuriwa na Bunge kuchomwa mnamo Aprili, 1652.

aliona kuja kwa Masiya hapo awali kabla yake kuwadia. Siku ya Masiya "ilikuwapo," kwa akili/fikira ya Abrahamu.²³⁹ Wayahudi hawakuelewa kile ambacho Yesu alisema, wakiamini kuwa alidai kuwa alikuwa wa rika lile lile la Abrahamu (Yohana 8:57). Yesu alithibitisha tena manufaa ya hakika katika mpango wa Mungu pamoja na dai lake, "Kabla kuwapo la Abrahamu, nilikuwapo [mimi]" (Yohana 8:58).

Kushikilia maana ya neno hili "mimi ni", ni muhimu kuilinganisha na matumizi ya kila mara ya Yohana ya neno lilo hilo, ambapo mahali pengi inahusiana na Umasiya wa Yesu:

Yohana 18:5: "Yesu aliwaambia, 'Mimi ni [yeye]'" (akijijulisha kama ule ambaye walikuwa wakimtafuta).

Yohana 6:20: "Yesu [akitembea kwa maji] aliwaambia: 'Ni mimi'" (hakika, "Mimi ni").

Yohana 9:9: "[Mtu aliye kipofu aliponywa] alisema mara kwa mara, 'Mimi ni [yeye]'" (kwa mfano, "Mimi ndiye.")

Yohana 4:26: "Yesu alimwambia [mwanamke aliyekuwa katika kisima], 'Mimi ninayezungumza nawe ni [yeye]' " (yaani, *yule Masiya*, fungu 25).

Yohana 8:24: "Isipokuwa unaamini kuwa mimi ndiye [yeye], utakufa kwa dhambi zako."

Yohana 8:28: "Ukimuinua Mwana wa Binadamu, basi utajua kuwa mimi ndiye [yeye]."

Yohana 13:19: "Ninawaambia kabla ipite na wakati itafanyika labdamutaamini mimi ndiye [yeye]"

Yohana 9:35-37: "Je, munamwamini Mwana wa Binadamu?...Anayezungumza nanyi ndiye [yeye]."

Cp. Yohana 10:24, 25: " 'Kama wewe ni Kristo, tuambie wazi.' Yesu aliwajibu, 'Niliwaambia na hamuamini.' "

Yohana 8:58: "Kabla kuwapo kwa Abrahamu, nilikuwapo [yeye]."

Kwa wakati huu Yohana alieleza kusudi lake la kuandika Injili lazima ikumbukwe. Nia yake ilikuwa kuwa "tunafaa kuamini kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu" (Yohana 20:31). Hakika kuwa katika Agano la Kale Mungu anajizungumzia kama "Mimi ndiye [yeye]" haituelekezi kama inavyofikiriwa, kwa mwisho kuwa kwa mdomo yake Yesu "Mimi ndiye [yeye]" inamaanisha "Mimi ni Mungu" kwa asili ya wanaoamini Utatu. Dai la Yesu kuwa "Mimi ndiye" kaitika Yohana inaweza elezwa kama dai la *kuwa Masiya*. Yesu anajitokeza kama ajenti wa Mungu mmoja na aliyepata amri kutenda kwa niaba yake.

Hata tukilinganisha maneno ya Yesu *ego eimi* ("Mimi ndiye") na yale ya Mungu katika Agano la Kale, bado hakutakuwa na sababu au njia ya uhusiano kati ya Yesu na Mungu kwa asili ya wanaoamini Utatu. Yesu, kama Masiya, anaweza kuwa na jina la heshima bila kuwa Mungu. Wakati wazo la "ajenti" linatiwa maanani, itaeleweka kuwa Yesu ni wakili wa Baba. Kama ajenti anatenda kwa niaba ya na kuzungumzia mkuu wake, ili matendo ya Mungu yanajitokeza kwa Yesu. Hakuna yoyote kwa hii inayomfanya Yesu kuwa Mungu. Anabaki kama Masiya binadamu aliyeahidiwa na maandishi. Teolojia ya wanaoamini Utatu inaonyesha upendeleo wa ukatili wa Umasiya na inaweka juu ushuhuda wa Yohana, na kukosa kuwaza na maneno yake ya kuamini

²³⁹ Mila ya walimu wa kiyahudi inasema kuwa Abrahamu aliona tokeo la historia yote ya wazao wake (*Midrash Rabbah*, XLIV, katika Mwanzo 15:18). IV Ezra 3:14 anasema kuwa Mungu alimpa Abrahamu tokeo la siku za mwisho za wakati.

Mungu mmoja yanayoeleza Baba kama "Mungu wa kipekee," tofauti na Mwana wake (Yohana 17:3; 5:44). Maendeleo/mwenendo huu unamtenga Yohana na Mathayo, Marko na Luka/Matendo. Unaziba pia Agano Jipya kukubali nafsi ya Yesu kama Masiya.

Ushuhuda mbele yetu (ulioonyeshwa hapa juu) unaonyesha kuwa neno linalotumika mara kwa mara *ego eimi* unamaanisha "Mimi ndiye niliyeahidiwa," "yule anayeuliziwa." Mtu kipofu anajitambulisha kwa kusema "Mimi ndiye mtu unayemtafuta"; "Mimi ndiye yeye." Kwa maneno ambapo Mwana wa Binadamu au Kristo wanazungumziwa, Yesu anadai kuwa "yule," yaani, Mwana wa Bindamu, Kristo. Kwa njia zote ni sawa (kama wafasiri wanavyojua) kuongeza neno "yeye" kwa "Mimi ndiye." Kuna kila sababu kuendeleza na kutumia "yeye" katika Yohana 8:58 pia. Hivi basi katika Yohana 4:26, "Mimi ndiye" = "Mimi ndiye [yule, Masiya]." Katika Yohana 8:58 Yesu pia anadai: "Kabla Abrahamu kuzaliwa, Mimi ndiye [yeye, Masiya aliyeamuriwa]."

Ni muhimu kutazama kuwa Yesu hakutumia neno lilatambua jinalake Mungu kwa Musa. Katika msitu uliokuwa ukichomeka, Mungu mmoja alijitambulisha kama "Mimi ndiye mimi" au "Mimi ndiye yule mmoja anayeishi pekee (Msafara 3:14). Neno hilo katika tafsiri ya kigiriki ya Agano la Kale inasoma *ego eimi ho hown*, ambalo ni tofauti na "Mimi ni yeye" ilivyotumika na Yesu. Kama Yesu kwa kweli alidai kuwa Mungu, si jambo la kawaida kushirikiana na Wayahudi wa kushindana anadai kuwa yeye si Mungu, lakini ajenti wa Mungu ambaye ana jina la heshima "Mwana wa Mungu" (Yohana 10:34-36).

Ni haki kuuliza kama mtu anaweza "kuwapo" kabla yake kuwapo kwa kweli. Je, hii ni njia ya mila ya mafundisho ya kutwaa utu ya mtu wa pili mtakatifu, ya pekee ya kutatua kuwapo kabla ya maneno ya 'Johannine'? Mfano wa lugha iliyoamuriwa mbele na inayopatikana katika Injili ya Yohana haihitaji kuwapo kabla kwa Mwana. Abrahamu alijawa na furaha alipotarajia kuja kwa Masiya. Siku ya Masiya ilikuwa ya kweli kwa macho ya Abrahamu kwa imani. Kwa hivyo pia Masiya "alikuwapo" kama mkuu wa asili ya mpango wa Mungu kitambo kabla kuzaliwa kwa Abrahamu. "Kabla kuwapo wa Abrahamu, Nilikuwapo [wa kipekee]" ni neno kubwa kuhusu mpango wa Mungu wa dunia Yesu akiwa katikati, ambaye Yohana anaweza mweleza kama "aliyesubuliwa kabla mwanzo wa dunia" (Ufun.13:8). Hatuna ugumu wowote kuelewa jinsi: Yesu ndiye aliyeamuriwa – na akaamuriwa kufa – kitambo kabla Abrahamu kama ajenti mkuu wa mpango wa Mungu. Kama Yesu "alisubuliwa kabla Abrahamu," yeye mwenyewe amesemekana "kuwapo" katika mashauri ya Mungu ya milele. Kwa maana hii, aliamuriwa kama mwokozi wa dunia kabla kuzaliwa kwa Abrahamu.

Katika kuunga mkono tafsiri hii tunataja tena elezo/fafanuzi ya Gilbert. Ya Yohana 8:58 anasema:

Yesu amekuwa akisisitiza dai lake la Umasiya. Hasemi kwamba kabla Abrahamu azaliwe 'logos' ilikuwapo; anasema "mimi ndiye." Ni Yesu Masiya, Yesu binadamu amabaye Baba alifanya wakfu kwa kazi ya Umasiya anayozungumzia. Kabla ya hii, alizungumzia "siku yake," ambayo Abrahamu aliona (Yohana 8:56), ambayo lazima tuelewe kuonekana kihistoria kwa Yesu kama Masiya. Abrahamu alikuwa ashakiona kwa kweli ingawa haionekani kuwa katika ahadi ya Mungu ya mbegu (Mwanzo 12:3; 15:4, 5) na kuamkua kwa mbali (Ebr.11:13) Na sasa ni yeye anayegundua toleo la mbali la Abrahamu anayesema, "Kabla Abrahamu azaliwe, nilikuwapo." Yesu hivi basi anashikilia kuwa utu wa Umasiya wa kihistoria ulikuwapo kabla Abrahamu azaliwe. Kama hivi

ndvyo ilikuwa, basi kuwapo kabla Abrahamu lazima ifikiriwe kama muhimu.²⁴⁰

Mafumbo ya Yohana 8:58

Wafasiri wa kitabu cha Yohana mara kwa mara wanatazama mafumbo katika misemo ya Yesu, hasa katika uhusiano wa ukosefu wa Wayahudi wa uhasama kuelewa Yesu alichosema. Imani halisi mara kwa mara iko makini kuunga mkono maoni ya Wayahudi juu ya Yesu. Inabishwa kuwa Wayahudi walifikiri kuwa Yesu alidai kuwa Mungu. Hivi basi ndiye. Lakini umati wa kupinzana wa Yesu si mwongozo mwema kwa nia za Kristo. Tushatazama kuwa ilimbidi Yesu kurekebisha fikira za Kiyahudi kwamba alidai kuwa Mungu. Dai lake lilikuwa kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, ambayo ni daraja/cheo ya binadamu, si Mungu. Katika Yohana 8:58 Kuna mafumbo ya kitenzi ambayo yanawezesha tafsiri tofauti. Ufasiri wa kawaida: “Kabla kuwapo wa Abrahamu, Nilikuwapo mimi” sio njia ya pekee ya kufasiri Giriki.

Ni mwanzo hakika ya lugha kwamba ni namnaya kiarifa ya Giriki ikichukua maana yake kutoka maneno ya awali. Inaweza kueleza matokeo yaliyopita au ya kitambo. Basi Mathayo anaandika, “Kabla jogoo awike” (Math.26:34; prin, “kabla,” + ya namna ya kiarifa). Lakini hapo awali katika Injili ii hii tuna “kabla waje pamoja” (Math.1:18 prin + ya namna ya kiarifa) Katika Injili ya Yohana tunatazama “Mkubwa, njoo chini kabla mwanangu afariki” (Yohana 4:49; prin + namna ya kiarifa); “Nimewaambia kabla ije kupita” (Yohana 14:29; prin + namna ya kiarifa). Swali linaloulizwa, Ni njia ipi nzuri ya kufasiri Yohana 8:58? Je, Yesu alisema: “Kabla kuwapowa Abrahamu [mfano, afufuke kutoka kusulubiwa], Mimi ndiye,” au “kabla kuwapo wa Abrahamu [kuzaliwa] Mimi ndiye [yeye]”?

Inaweza kuwa: kwamba Imani halisi imesomwa vibaya katika fungu hili kama ushahidi wa kuwapo kabla wa Kristo. Katika fungu za awali, Yesu alizungumzia kufufuka kama kupasisha maisha ya milele kwa wale wanaomfuata (Yohana 8:51). Wayahudi walitokubali kwamba hii ilimfanya Yesu mkuu kuliko Abrahamu, ambaye wakati huo alikuwa amekufa. Yesu anathibitisha dai lake kwa kuonyesha kuwa Abrahamu alikuwa ametazama mbele kwa siku ya Masiya. Wayahudi hawakumwelewa Yesu kumaanisha kuwa yeye na Abrahamu walikuwa wa rika lile lile (“Je, umemwona Abrahamu?” Yohana 8:53, 56, 57). Ni wezekano kuwa Yesu anaenda kinyume na dai kubwa mno kwamba atamtangulia Abrahamu katika ufufuo. Kabla Abrahamu apokee maisha ya milele katika ufufuo, Yesu atakuwa tayari hai na ataishi milele. Hii itathibitisha dai kuwa kuu kuliko ya Abrahamu. “Kuja kuwa” (namna ya kiarifa ya ginomai) inatumika kwa hakika kazi 14:14: “Nitangoja haadi nirudi tena.”

Kama maneno yanayosomwa kama fasiri ya kawaida, Yesu atadai kuwa Masiya aliyeamuriwa kutoka milele. Au anaweza kutaja ukuu wake kwa Abrahamu kwa njia tofauti. Abrahamu alitarajia shangwe la Masiya. Yesu kwa hakika atafurahia maisha ya milele kama mwokozi aliyefufuka kabla Abrahamu aonekane katika ufufuo wa baadaye.

Kuwapo kabla halisi

Kuwapo kabla katika shauri la Mungu, zaidi kuliko kuwapo kabla wa ukweli, unatoshea kwa mazingira ya Kiyahudi ambapo Injili ziliandikwa. Katika maandishi ya

²⁴⁰ Ufunuo wa Yesu, somo la asili za msingi za Ukristo, 214, 215. Wazo kuwa maneno *ego eimi* ya Yesu vinahusika na Umasiya umefanywa na Edwin Freed katika “Ego Eimi katika Yohana 8:24 kwa mwangaza wa maana na uaminifu wa Umasiya wa Kiyahudi,” Kitabu cha masomo ya kiteolojia (1982);163-167. Cp pia Barrett, Mashairi ya Yohana (London: SPCK, 1982), 71: “ego eimi ya Yesu si dai la utakatifu; Yohana ana njia zingine, zote dhahiri zaidi nay a hadhari, ya kudai hivo.”

Kiyahudi, yanaandaa mazingira mema ya kuelewa Agano Jipya: “Kuwapo kabla inadhaniwa kwa Masiya, lakini kwa ile inayojulikana na vitu vingine na watu pia, kama vile hema ya ibada, sharia, mji mkubwa wa Jerusalem, mwana sharia Musa mwenyewe, watu wa Israeli.”²⁴¹

Picha iliyochorwa na Wayahudi ya Masiya kutoka kwa Agano la Kale haukuwa na wazo kuwa Masiya alikuwapo kabla yake kuzaliwa:

Picha cha ufunuo [ya Masiya] ni ya mfalme, yenye enzi kujaliwa kwa dhamana – ambaye mjio wake utanzisha wakati wa baadaye tukufu kwa Israeli. Masiya atakuwa chombo cha hukumu kwa binadamu wadhalimu, mlipizaji mshindi wa uadilifu. [kama Yesu atakavyokuwa kwa kuja kwake kwa mara ya pili]. Yeye ni binadamu, kama Mwana wa Binadamu, ingawa anayemiliki zawadi bora sana ya hekima na nguvu. Kulingana na maoni, ataonekana kwa siku za taabu/huzuni za wale waadilifu uliofika juu zaidi, na utawala/mamlaka yake itaanza na buharibifu mkuu wa maadui wake, ambapo baadaye ataongoza/amuru kwa utulivu na amani, ardhi takatifu kikiwa kiti chake cha utawala/amri... Kutajwa juujuu wa kuonyesha ukuu kuliko kuishi kabla katika kusudi takatifu na kujua mbele.²⁴²

Msomi mwingine vile vile anapata katika mazingira ya kuishi kabla kwa Agano Jipya wa Masiya pekee yake katika mpango wa Mungu: “Dalman, kuliko ambaye ninafikiria ana mamlaka kuu kwa wazo la kiyahudi, [anasema]: ‘Dini ya desturi ya Kiyahudi haijui chochote kuhusu kuishi kabla ya Masiya, ya kutangulia kuzaliwa kwake kama binadamu.’”²⁴³

²⁴¹ C. Ottley, *Mafundisho ya kutwaa utu* (Methuen and Co., 1896), 59, mkazo unaongezwa.

²⁴² *Ibid.*, 59, 60.

²⁴³ Charles Gore, *Uaminifu katika Kristo*, 31.

IX. ROHO MTAKATIFU: MTU WA TATU AU MUNGU KATIKA HATUA

“Mkataba wa kuzaliwa kwa roho mtakatifu ukiwa mtu tofauti na Mungu ni ukuaji. Haikuaminiwa kwa ukristo wa mwanzoni.” — Basil Wilberforce, D.D.

Kulingana na uhalisi wa utatu, roho mtakatifu ni mwanachama wa uungu wa milele unaosawazishwa na usawa wa milele wa Baba na Mwana. Huyu “mtu” au “tofauti” wa uungu hauna jina binafsi. Swali linaloulizwa na wasioamini utatu ni; Je, Bibilia kweli unahamasisha uaminifu wa mtu wa tatu “wadogo wadogo” (kwa kutumia lugha ya wanaoamini utatu), amabaye ni tofauti na Baba kama Mwana kwa hakika alivyo? Ni ngumu kwetu kuamini kuwa neon likisomwa bila faida la kanuni la imani ya kitambo, linaonyesha wazi kwamba roho mtakatifu ni “mtu” (chochote kinachomaanisha – wanaoamini utatu wanaonekana hawawezi kulifafanua neon la Mungu kwa pasipo imani yoyote), tofauti na Baba na Mwana. Matumizi ya neno hilo kwa kimila na kiholela “yeye” kwa ajili ya roho umetusababisha kufikiria mtu wa tatu. Taswira tofauti sana inajitokeza tunapomfikiri roho kama “ni.”²⁴⁴

Ugumu wetu wa kuukataa roho kama mtu wa tatu wa utatu mtakatifu unanonekana kama uingilizi wa kiongozi halisi maarufu wa kigiriki, Gregory wa Nazianzen ambaye mnamo 381 AD alisema: “Kati yetu wenye hekima, wengine wetu wanashikilia roho mtakatifu kikiwa na nguvu [*energeia*], wengine kama kiumbe cha uhai, wengine kama Mungu na wengine wasio na nia ya kuamua kwa kukosa heshima. (kama wanavyosema) kwa maandishi, yasiyozungumza wazi kuhusu jambo hilo.”²⁴⁵

Utatu basi ulikua wapi kwa miaka mia tatu itenganisha mapokeo ya kigiriki kwa kifo cha watume? Msomi wetu alichukua mud asana kujua kile ambacho kimekua kitume halisi. Je, kusoma Bibilia kutoka mwanzo hadi mwishi kinaendeleza mavuno ya wanaoamini utatu katika roho? Katika kuchambua matokeo ya Bibilia, ni wazi kwamba asilimia tisini na nane ya maandishi ya bibilia yanaridhisha yakitambua Roho kama Mungu kwa hali ya kufanya, Mungu kwa kuwasiliana, nguvu na utu wake katika ushawishi wa viumbe kwa njia tofauti tofauti/nyingi. Ushahidi unaobaki kutolewa unaweza kuweka kando hadi wakati wa utatu ujao, lakini hii ni haki kweli? Roho ni kitu kweli bali nguvu aliyonayo Mungu, ya kuwahimiza binadamu kutenda vitendo vya ajabu vya vita, akiwapa vipawa vya muujiza, na hasa kuwasiliana kwa kikweli? Ijapokuwa jambo jipya kilichotendeka tangu sikukuu ya kristo – hakuna nia ya kubadilisha maana ya “roho” iliyotolewa hapo awali, ikiwa na umuhimu kwa Mungu, ikihamasisha nguvu na akili yake takatifu, inayoonyeshwa wazi na zinaa kwa sababu ya roho, kwa wale wanaomtafuta na kumuamini.

Neno “Roho” katika Bibilia kina maana nyingi tofauti, zote zinazohusiana, walakini, kwa msingi la wazo la nguvu na akili lililotokomea. Katika agano zote mbili “roho mtakatifu” unaelezea nguvu ya mungu ikiwa imeelekezwa katika viumbe na maongozi. Ni Mungu kwa kitendo na maendelezi ya utu wake. Pahali popote ambapo roho unafanya kazi, tunafahamu kuwepo kwa Mungu ukifanya kazi: “Ufanye upya roho ulio ndani yangu. Usishushe moyo wangu kutokana na kuwepo kwako na usikichukue

²⁴⁴ Kwa mfano katika kitabu cha “KJV” kitabu cha warumi 8:16 *Roho mtakatifu* unatoa ushahidi kwamba katika roho mtakatifu sisi ni watoto/wana wa mungu” Lakini “KJV” mahali pengine unazungumzia roho mtakatifu kama “mtu”.

²⁴⁵ Maandiko ya kushuhudia kwa “Macedonius,” *The New Schaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge* (Grand Rapids: Baker Book House, 1963), 7:112.

Roho mtakatifu kutoka kwangu” (Zaburi 51:10, 11). Katika mstari za awali Daudi anatamani kuwa na “ukweli kwa (yake) kwa utu wake wa ndani” na uwezo wa kupata hekima (Zab 51:6).²⁴⁶ Kazi ya Roho wa Mungu kwa Daudi ungeleta matokeo yanayotakikana. Katika kifungu kingine “Roho” na kuwepo kwa Mungu unasawazishwa: “Niende wapi kutoka kwa roho yako? Au ni kimbie wapi kutoka kwa kuwepo kwako?” (Zab.139:7) Kuna uhusiano wa karibu kati ya Zaburi 33:6 kati ya Roho wa Mungu na kitendo chake cha kuumba: “Kwa jina la Mungu mbingu zilitengenezwa, na viumbe wote kupumua kutokana na[Ebrania.*ruach*; LXX *pneuma*] mdomo wake.” Hakuna shaka kuwa “roho” na “pumzi” ni tafsiri ya ile ile maneno ya kiyahudi na kigiriki, ambayo ni kiini cha mizizi ya maana ya roho kama kipawa cha Mungu cha uvumbuzi, nguvu iliyoweza usemi wake. Huu unaweza kataliwa na binadamu wanaotenda dhambi. Hivi basi uhalifu wa Waisraeli ulihuzunisha roho wa Mungu (Isa.63:10) Kwa maneno yanayodhihirisha maana sawa tunajifunza kuwa “malaika wa eneo lake” walihusika kwa uokovu wa wafuasi wa Mungu (Isa.63:9) Kuna ushahidi hapa kuwa malaika walihusika na mawazoya vitendo vyenye asili ya roho ya Mungu katika mienendo za binadamu. Luka alichungua kuwa “malaika alizungumza na Filipo” (Matendo 8:26) Mistari mitatu baada ya hii anasema kuwa “Roho ulimzungumzia Filipo” (mstari 29). “Malaika wa Roho” inapatikana katika vitabu vya Kiyahudi, upande wa nje wa Bibilia na unaeza elezea sababu Luka anatumia kumbukumbu usiyo dhahiri kwa mtumwa mtukufu anayepatanisha roho ya Mungu.²⁴⁷

Huu unaenda kupita ushuhudi wa maandishi kusawazisha Roho ya Mungu na mtu tofauti na Mungu mmoja, *kwa maana sawa Mwana ni tofauti na Baba*. Kuna tofauti dhahiri kati ya neno la Bibilia linalosema kuhusu Bwana na Mwana, na kinachosema kuhusu roho. Mungu na Yesu Kristo ni mojawapo tofauti na lililotengwa kustahili kupokea ibada, yule Bwana kwa uwezo wake wa kuweka vitu kama muumbaji, Bwana Yesu kama chombo na mtendaji kwa wokovu wa binadamu. Hata sasa Roho Mtakatifu hauna jina yenyewe. Ni kwa nini hakuna onyesho lolote katika maneno ya maandiko mtakatifu ambapo Roho Mtakatifu unaabudiwa au kuombwa? Hakuna hata siku moja Roho Mtakatifu umetuma salamu kwa makanisa. Wakati watume wanapoandikia makanisa, salamu lazima itumwe na watu wawili, Baba na Mwana. Ni jambo la ajabu kwamba Paulo mara kwa mara angekosa kutaja mtu wa tatu wa utatu, kama aliamini uzima wake. Akimuamuru Timothy aweke imani yake, alizungumza kwa eneo la “Mungu lisiloonekana na la Yesu Kristo na malaika wake waliochaguliwa” (1 Tim.5:21).

Mchunguzi mkuu wa kibibilia wa karne hii, na mwanachama maarufu wa kanisa la Uingereza, anaonekana kukataa kwamba Bibilia unabainisha roho kama mtu wa tatu:

Kuuliza kama kwa Agano Jipya roho ni mtu kwa busara ya kisasa kwa neno, ni kama kuuliza kama roho ya Elijah ni mtu. Roho ya Mungu ni yake mwenyewe; ni nguvu ya Mungu (*dunamis*) [nguvu] kwa kitendo. Lakini Roho Mtakatifu si mtu anayeishi kwa utegemezi wa Mungu; hii ni njia ya kuzungumzia kuhusu kile ambacho Mungu alitenda kwa historia, au ya Kristo mwenyewe akitenda kwa maisha na ushahidi wa kanisa. Agano Jipya (na kweli wazee na walimu wa kale wa kikristo walifikiria

²⁴⁶ Cp. “Roho kwa undani wa mtu” (Eph.3:16), ukionyesha uhusiano baina ya ukweli na roho, kama kwa kitabu cha Yohana 6:63

²⁴⁷ Mpao wa Isaya 4:21;723:9:36, 39; 10:4; 11:35 “ Malaika pengine anatambulika na Gabriel (Mpandao 3:16;11:4) cp Uhusiano wa Gabriel na juhudi ya roho katika Luka 1:26, 35

mara nyingi) hauelezi popote kuhusu Roho au hekima ya Mungu kikiwa na utu wa kujitegemea.²⁴⁸

Uangalifu wa Luka kwa maneno yake kwa fungu tatu ya maneno yanaonyesha jinsi Roho na nguvu ni matamshi yanayoweza kubadilikana: Yohana mbatizaji atakua kama mtangulizi kabla ya Masiya “kwa roho na nguvu ya Elijah” (Luka 1:17). Katika mtungo wa mamba ya mwana wa Mungu, Maria anaambiwa kuwa “Roho Mtakatifu [hakuna nakala kwa Giriki] utakuja juu yako na nguvu yake iliyopita wote utakutia kivuli (Luka 1:35). Wakati Mungu alitangaza kukuja kwa Roho Mtakatifu kwa siku kuu ya Kristo, alieleza nia yake ku.. “Tuma tena ahadi ya Baba yangu juu yako; lakini mkae humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu” (Luka 24:49). Neno “Roho ya Mungu” katika kifungu kimoja hubadilishwa na “Kidole cha Mungu” katika maandiko sambamba (Mathayo 12:28; Luka 11:20). “Kidole cha Mungu” hakielezi kuhusu mtu.

Roho iliyiofanya kazi kwa kanisa ya hapo awali imejulikana kama “Roho ya Yesu,” nafsi yake iliyowawezesha kuwapa waumini tumaini. Luka anaandika: “Na wakapita katika nchi ya Frigia na Galatia, wakikatazwa na Roho Mtakatifu, wasihubiri neno katika Asia; na walikuja Misia, walijaribu kuenda Bithinia, na Roho wa Yesu haikuwaruhusu” (Matendo 16:6,7). Inaonekana ya kuwa hakuna tofauti kati ya Roho wa Mungu na roho wa Yesu: “Hauishi kutokana na mwili bali kwa Roho kama kweli Roho wa Mungu unaishi ndani yako. Lakini kama kunaye ambaye hana Roho wa Kristo ndani yake, yeye si wake” (Warumi 8:9). Katika kifungu hicho Paulo anaongea juu ya Roho ikiombea watakatifu. Kwa sababu hakuna mahali pengine anafahamu Roho kama mtu wa tatu, ni sawa kufikiria kuwa haoni tofauti kati ya maombezi ya Roho na maombezi ya Kristo ilivyotajwa kwa mstari huo. (Warumi 8:27, 34). Wakati Kristo mwenyewe yu pamoja na Baba, Roho yake yenye kutenda iko katika mioyo ya waumini.

Wengine wamepingana kuwa lazima kuwe na mtu wa tatu anayehusiana na Mungu na Kristo kwa sababu welekevu na uzuri unahesabia kwa Roho Mtakatifu. Kwa mfano, Nehemia anaandika kuhusu Mungu akiwapa “Roho uliokuwa na wema ili uwaelimishe.” (Neh. 9:20). Ni jambo la hakika kuwa Roho wa Mungu una cheo bora kwa Mungu. Lakini haina haja kufikiria Roho kama mtu mwenye hekima. Maelezo rahisi yanapewa na Paulo wakati analinganisha roho wa Mungu na roho wa binadamu. Anaanza kwa kuzungumza kuhusu Roho wa Mungu: “Roho unatafuta vitu vyote, hata undani wa Mungu.” Baada ya hii analinganisha kitendo cha “Roho” na utu na undani wa binadamu. “Nani mwingine anajua fikira za binadamu isipokuwa Roho wa mtu ambao uko ndani wake? Hata hivyo fikira ya Mungu hakuna anayejua isipokua Roho wa Mungu” (1 Wakorintho 2:10, 11). Roho ya mtu ni kwa fikira zake mwenyewe kama vile Roho ya Mungu kwa fikira zake. Roho Mtakatifu kwa hivyo ni “welekevu takatifu,” ufunuo wa akili ya Mungu. Roho na moyo wakati wengi unauhusiano unaokaribiana, hata na kubadilishana, katika Bibilia ya Hebrania. Nini kingine kitakua cha hakika kuliko Mungu kufungua mipango na utumizi wake wa ndani kabisa kwetu, akiongea roho kwa roho na binadamu, kiumbe chake, na kuhimiza ujumbe kwa utu wake na Roho.

Waandishi maarufu wanaoamini utatu wanaonekana kuwa wamekwenda mbali na mashahidi ya maandiko wanapodai kuwa, mtu wa tatu wa Utatu alishiriki katika mazungumzo Mungu aliposema, “na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu” (Mwanzo 1:26). Torrey aliandika:

²⁴⁸ Alan Richardson, Tangazo ya elimu ya tabia na sifa za Mungu na dini ya Agano Jipya. (London: SCM Press, 1958), 120.

Wengi wanasema kuwa mafundisho ya dini ya utatu hayapatikani katika Agano la Kale, kwamba bali iko katika Agano Jipya haiku katika Agano la Kale. Lakini mafundisho ya dini ilioko kwenye Agano la Kale katika sura ya kwanza ya Bibilia. Katika Mwanzo 1:26 tunasoma, “Na Mungu alisema, ‘Hebu tufanye mtu kwa mfano wetu *kwa sura yetu*.”²⁴⁹

Inaonekana ubunifu tukisema kwamba Mungu alizungumza na Roho Mtakatifu. Mungu hawezi zungumza na roho wake mwenyewe. Atakua anajizungumzia akinfanya hivi (isipokuwa kama “roho” inamaanisha malaika-mtume wa Mungu). Je, kuna mahali popote katika Bibilia ambapo Mungu anasema na Roho wake mtakatifu? Wazo hilo ni kama cha kigeni kwa Bibilia kama dhana ya kwamba Roho Mtakatifu anafaa kuabudiwa ama kutolewa asanti kama Torrey anavyopendekeza.²⁵⁰ Wimbo inayotuhimiza, “tumsifu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu” ilitoka katika wazo lililopoteza mafundisho ya kibibilia ya Roho. Torrey hata anatueleza ya kwamba *Shema* ya Israeli (Kum. 6:4) ni imani ya Utatu.²⁵¹ Wengi wa Elohim ndiyo msingi wa hoja yake, ambayo imekataliwa na umati na wasomi wa Utatu. Ni kwa nini maandiko maarufu hufanya rufaa na uchunguzi vya uhakika zaidi mamlaka ya kutambuliwa katika lugha ya Kiyahudi bila kutambuliwa?

Katika mazungumzo ya Yesu ya mwisho kwa wanafunzi wake anasema ya kuwa, “Mfariji” ambaye atakuja kuhamasisha waamini baada ya Yesu kuchukuliwa kwa Baba. Kwa vile ‘Mfariji’ (*parakletos*) ni neno la kiume kwa Kigiriki, Watafsiri wanaoamini katika “nafsi ya tatu ya Utatu” wakatamia kiwakilishi ‘yeye’. Huyu “mfariji” pia ni “roho wa ukweli”. Hiyo jina haipendekezi mtu. Kama hatumchukui Roho mtakatifu kuwa mtu tofauti na Baba na Mwana, maandiko yatakuwa kama ifuatavyo:

Mkinipenda mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa mfariji mwingine ili akae nanyi hata milele, na ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea kwa kuwa haumuoni wala haumtambui; bali nyinyi mtamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha muwe yatima, naja kwenu...lakini huyo mfariji, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamleta kwa jina langu ni [*Ekeinos*, ume katika Kigiriki kwa kubaliana na *parakletos*, lakini kinatafsiriwa kama ‘yeye’ tu kama kimedhaniwa] kumaanisha mtu atawafundisha kila kitu na kuwakumbusha yote niliyowaambia (Yohana 14: 15-18, 26).

Maoni ya Mtatu, James Denny ni ya kufundisha:

Kinachoonekana hapa ni jina jipya ambalo Roho anapewa, ‘mfariji mwingine’. Ni kweli ni jina pekee ambayo ni mpya. Wazo hilo ni la karibu na majibu ya ahadi ya Roho inayopatikana katika muhtasari wa Injili. Usemi wa “mfariji mwingine” ina maana kwamba wanafunzi tayari walikuwa na uzoefu wa mmoja, yaani, Yesu mwenyewe. Kwa muda ambayo Yesu alikuwa pamoja nao, nguvu yao ilitoka kwake, na wakati atakapoenda, mahali pake patachukuliwa na Roho. Kuna nguvu nyingine nao sasa inayofanya Yesu alichokuwa akifanya awali. Hata hivyo, kweli ni mwingine? Katika 1 Yohana 2:1 ni Yesu ambaye ni Roho Mtakatifu [mfariji], hata baada ya Siku kuu ya Kristo, na hata hapa (Yohana 14:18),

²⁴⁹ R.A. Torrey, *The Holy Spirit* (Fleming Revell Co., 1977), 20.

²⁵⁰ *Ibid.*, 13, 19.

²⁵¹ *Ibid.*, 21, 22

Anasema, “Nakuja kwako.” *Kuwepo kwa Roho ni Yesu mwenyewe katika Roho.*²⁵²

Kusawazisha kwa Roho wa Mungu au Yesu na nguvu ya utu ni dhahiri zaidi katika maeneo mengine ya Maandiko. Yesu anawaambia wanafunzi wake, “Na watakapowachukua na kuwakabidhi, msitafakari kwanza mtakayoyasema, lakini lolote mtakalopewa saa ile, lisemeni; kwa maana si nyinyi msemao, bali ni Roho Mtakatifu”. (Marko 13:11). Masimulizi ya Luka yanadhihirisha kuwa Roho inayozungumza ndani ya wanafunzi wake ni Kristo mwenyewe: “Basi kusudieni moyoni mwenu, kutofikiri-fikiri kwanza mtakavyojibu; kwa sababu nitawapa kinywa na hekima ambayo watesi wenyu wote hawataweza kushindana nayo wala kulipinga”. (Luka 21: 14,15). Ahadi hii ilitiimizika wakati maadui wa Stephen walishindwa “kuukataa hekima na roho ambayo alitumia kuzungumza” (Matendo 6:10). Inatia nuru tukipata kuwa “Roho Mtakatifu” ya Marko 13:11 kwa urahisi, iko katika fungu zilizoambuana kwa Mathayo 10:20, Roho wa Baba wako”. Vifungu vyote viwili vinaelezwa zaidi na Luka mabaya anaona Roho wa Mungu kama Mungu kwa kitendo cha kuwasilisha maneno na maarifa kwa wanafunzi waliozingia (Luka 21:15). Mtazamo huu wa Roho unalingana sana na Bibilia wa Kihebrania. Lakini haliwezekani kutia maana ya Roho kama mtu tofauti na Baba na Mwana vifungu hivi.

Je, ushahidi wazi wa karibu kila sehemu ya Bibilia unafaa kuharibiwa na vifungu vichache katika injili ya Yohana? Alan Richardson anakomesha kwa kusema kwamba, kwa Yohana, “Kristo mwenyewe anakuja katika Roho...Roho ambaye anatafsiri maandiko si mwingine ila Bwana mwenyewe.”²⁵³ Yohana anamwita Kristo mfasiri katika barua yake ya kwanza (1 Yohana 2:1). Hili ni tokeo lingine la *parakletos*. Maoni ya Paulo ni sawa na hayo. Anasema, “Bwana ni Roho na pale alipo Roho wa Bwana, kuna uhuru” (2 Wakorinto 3:17).

Mwanachuoni Mtatu wa Injili ya Yohana alijumlisha matokeo yake: “Hatufai kutakabari ya kwamba Yohana aliangalia Roho kama mtu katika mafundisho ya dini ya Kanisa ya baadaye. Mazungumzo ya Yohana inaeleza sana juu ya uhusiano wa Baba na Mwana bila mawazo ya mtu wa tatu kulingana sawa nao katika Uungu mmoja.”²⁵⁴

Mwanachuoni mwingine wa kibibilia wa karne iliyopita anafafanua mfaraji: “Nguvu ya Mungu, iliyofanywa kama kwamba ni mtu inalinganishwa hapa kama katika Yohana 15:26 na, balozi mkuu wa mtawala anayeongea tu kwa mujibu wa dhamana iliyokabidhiwa kwake na aliyemtuma, kukubaliana na mapenzi yake na furaha.”²⁵⁵

Kuna upungufu wa ushahidi kuonyesha kwamba Paulo aliamini kuwepo kwa, “nafsi ya tatu ya Mungu mmoja.” Tumeona kwamba Paulo anaelewa Roho kama kujitambua na akili ya Mungu. Anapoongea juu ya Roho kama nguvu ya mbinguni iliyotofauti na Baba na kusaidia Wakristo kwa maombi, anataja kifungu hicho inayosema Kristo mwenyewe “anatuomba” (Warumi 8:26,34). Roho ni Kristo mwenyewe akinyosha ushawishi wake kwa Waumini.

Kwa mukhtasari, tunaweza kusema kwamba Roho Mtakatifu wa Bibilia ya Kiyahudi (Agano la Kale) hakuwa mtu tofauti na Baba. Taarifa zifuatazo zilifanywa na Profesa maarufu wa lugha ya Kibibilia:

²⁵² “Roho Mtakatifu,” *Kamusi ya Kristo na Injili* (Edinburgh: T & T Clark, 1917), 742.

²⁵³ Tangazo la elimu ya sifa katika Agano Jipya, 121.

²⁵⁴ E.F. Scott, *The Fourth Gospel* (T & T Clark, 1926), 342, mkazo unaongezwa.

²⁵⁵ C.T. Kuinoel, cited by Wilson, *Concessions*, 372, mkazo unaongezwa.

Hakuna ushahidi katika vifungu vyote vya Agano la Kale ambapo Roho Mtakatifu ametajwa kuwa mtu katika Uungu mmoja, na sasa [c.1775] karibu ulimwengu wote umepokea maoni ya wachambuzi, kwamba, katika lugha ya Kiyahudi, “Roho Mtakatifu” haimanishi chochote zaidi ya moyo takatifu bila kuhusisha mtu.²⁵⁶

Je, na Agano Jipya? Katika wakati wetu wenyewe Karl Rahner anasema wazi wazi: “*Ho theos* [Mungu] haitumiki katika Agano Jipya kuongea kuhusu *pneuma hagion* [Roho Mtakatifu].”²⁵⁷ Matendo 5:3,4 si ubaguzi. Baadhi ya wanaoamini utatu hutoa mistari hii kama ushahidi wa mtu wa tatu katika Utatu - Mungu, Roho Mtakatifu. Maandiko haya yanasawazisha kumdanganya Roho Mtakatifu kuwa sawa kumdanganya Mungu. Roho Mtakatifu hapa inamaanisha uwezo na mamlaka ambayo Mungu alimpa Petro. Wale wanaosema uongo kwa jina la Mungu na ya Roho wake wanasemekana kudanganya Roho na Mungu. Hili linadhibitishwa na maoni kutoka kwa Paulo: “Basi yule ambaye anatudharau, hadharau mwanadamu bali Mungu ambaye ametupatia Roho wake”. (1 Wathesalonika 4:8). Kuna kifungo sambamba katika Agano Kale wakati Waisraeli waliasi dhidi ya Musa na Haruni. Musa akawaambia ya kwamba maasi yao hayakuwa “dhidi yao bali dhidi ya Mungu ambaye sisi ni wajumbe”. “Mlinganyo” wa Musa na Haruni na Mungu, bila shaka, haifanyi sehemu ya Uungu ya zamani (Kutoka 16:2,8). Roho wa Mungu aliishi hata hivyo, katika Musa na inawezekana kuwa, kuasi kwa Waisraeli katika Zaburi ilikuwa dhidi ya “roho ya Musa” (Zab. 106:33, AV, RV, RSV,) au huenda, dhidi ya uwepo wa malaika wa Mungu aliyekuwa na mamlaka na nguvu ya Bwana (Isaya 63:9-11).²⁵⁸

Hisia zetu ni kwamba wakati mwingine wanaoamini utatu wamefungwa kwa imani rasmi ijapokuwa usetiri wao wenyewe kwa njia iliyoelezwa. Luther hakupenda jina Utatu: “Neno Utatu halipatikani katika maandishi takatifu, bali ni uzushi wa kibinadamu, na kwa hiyo, inaskika bila huruma.”²⁵⁹ Calvin alihisi kuwa sala ya Utatu si maandiko matakatifu: “Sipendi sala hii ya kishenzi, ‘Utatu Mtakatifu, Mungu Mmoja! Utuhurumie!’ iliyokabisa ya ukafiri. Tunajitenga na maneno kama hayo yakiwa mazito na ya ukafiri.”²⁶⁰

Lakini kwa nini tupinge kama kwamba kweli Mungu ni utatu? Ni nani kwa hakika amekosea kwa maneno “mama ya Mungu” (ambayo Maria ni mama yake?) kama kweli Yesu ni Mungu na Maria ni mamake? Na kama roho mtakatifu kweli una utu tofauti, yeye ndiye baba wa Yesu, wa afadhali kuliko Mungu, aliye baba? Ni roho uliosababisha mimba ya Mary (Luka 1:35).

Wakati Yohana ambaye ni mtume alikomaa, aliandika waraka wake wa kwanza na kuweka mipaka katika matumizi wake wa “roho” kwa kitendo cha Mungu na matoleo yaliyopewa wakristo: “Kwa hivyo tunajua kuwa tutangojana kwa sababu ametupa [sehemu] ya roho yake [*ek tou pneumatou autou*]” (1 Yohana 4:13). Mungu hapeani sehemu ya mtu, bali kipimo cha akili na nguvu yake. Yohana anafikiria kuhusu kitu kinachoweza kukaguliwa, kama anavyofanya Peter akidondoa maneno yanayohusika na kumwagika “Kutoka kwa roho yangu” (Matendo 2:17). Watu kwa kweli hawawezi miminika. Lakini Mungu anaweza ridhia madaraka ya nguvu yake iliyo pita kiasi. Lugha

²⁵⁶ J.D. Michaelis, *Remarks on John 16:13-15*, cited by Wilson, *Unitarian Principles Confirmed by Trinitarian Testimonies*, 477.

²⁵⁷ *Theological Investigations* (Baltimore: Helicon Press, 1963), 1:143.

²⁵⁸ Cp. Mwanzo. 23:21 ambapo malaika wana jina la Mungu.

²⁵⁹ *Makubaliano* [*Concessions*], 331.

²⁶⁰ *Makubaliano*, 40

inayotumika si muafaka kwa roho kama mtu wa tatu. Kwa kifungu kingine cha maneno Yohana anazungumza kuhusu roho kama “ile ambayo ina ushahidi” kwa sababu ni hiyo ambayo iliyo ya kweli kwa akili yetu (1Yohana 5:6). Kama ilivyojulikana mstari maarufu wa uwongo unafuata neno hiyo. Inazungumza kuhusu washahidi watatu “Mbinguni, Baba, neno na roho mtakatifu; na hizi tatu ni kitu kimoja.” Maneno haya hayana haki ya kua katika Agano Jipya.”²⁶¹ Zimeondolewa kutoka kwa tafsiri ya kisasa ya Biblia. Onyesho lao la kwanza katika Giriki ni 1215 na kama tafsiri ya Kirumi peke yake [*Acts of the Lateran Council*]. Ni hadi mnamo karne ya kumi na sita ndio tunayapata maneno haya kwa muswada wa kigiriki, na ni wakati huo ndipo tafsiri ya habari ya Kirumi ya Biblia.²⁶²

Yesu aliamuru ubatizo “kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu” (Mathayo 28:19) hauna uzani kwa kushuhudia kwamba Mungu aliamini utatu wa watu watatu waliotoshelezwa, kwani alimfahamu Baba kama “Mungu wa kipekee wa kikweli” (Yohana 17:3) na kutoa idhini kwa shahada ya Israeli ya wasioamini utatu. (Mark 12:29). Kama mwaminifu wa utatu, malaika mkuu Mikael, alisema: Haiwezekani kuelewa kutoka kwa fungu ya maneno hii, kama kwamba Roho Mtakatifu ni mtu. Maana ya Mungu unaweza kuwa unamaanisha hivi: wale ambao walibatizwa, walipobatizwa, waliungama kuwa waliamini Baba na Mwana, na mafundisho yote ya dini yaliyosisitizwa na Roho Mtakatifu.”²⁶³

Baraka ya Paul iliyozungumza kuhusu”neema ya yesu kristo mkombozi, upendo wa mungu na ushirika wa roho mtakatifu” (2 Kor.13:14) pia si kanuni ya mwaminifu wa utatu, lakini itaonekana kama uaminifu wa utatu ikikaribia maneno kabla wazoya Paulo aliyeamini kuwepo kwa watu watatu wanaoishi milele. Paulo pahali pengine alizungumza kuhusu “ushirika wa roho” na “fariji kwa kristo”(Filipino 2:1) Mafungu haya ya shawishi ya Mungu kutoka roho yake inayofanya kazi kwa uaminifu. Haina haja kuitwalia kuwepo kwa mwanachama wa tatu wa utatu. Matumizi yasio ya kawaida ya Roho Mtakatifu (*pneuma hagion*) inatumiwa na Luka ambaye ni mwandamizi wa Paulo, akitoa shauri ya kwamba kwake roho kila mara ni shawishi tukufu, na sio mtu wa tatu. Anazungumzia “Roho Mtakatifu wa mdomo wa Yakobo”(Bk of Jubilees 25:14) Lugha hii yote haitoshi katika wazo la mtu mwingine. Ugumu huu huu unaupata utatu wakati roho unapopimwa , kama vile Malachi anapozungumza na Mungu akiwa “na mabaki ya Roho” (Mal.2:15) Yohana pia anaifikiri Roho ikiwa pia na vipimo tofauti tofauti. Yesu aliipata kwa “kipimo” kizima (Yohana 3:34). Paulo pia anazungumza kwa “kadiri ya kupata roho ya Yesu Kristo” (Fil.1:19) Lugha hii inadhihirisha hifadhi ya nguvu bali siyo mtu. Ni jambo la maana kwamba Paulo anategemea maombi ya kanisa kwa uendelezi wa usaidizi wa Roho Mtakatifu.

Ugumu mkuu wa uaminifu wa utatu ni hakika kwamba hakuna kitu kinachosemwa kwa wakati unaopita wa bibilia hapo awali, ya Roho kama mtu wa tatu kwa kichwa cha Mungu. Hakuna desturi ya mwaminifu wa utatu inayo elezo ya Roho mtakatifu ikionekana tangu “381AD” kwenye baraza la “constantinople.” Ni wakati huo pekee ilitangazwa kuwa kuna watu watatu kwa Mungu mmoja.” Kupita miaka mia tatu baada ya ukasisi wa Mungu, viongozi wa kanisa hawakuwa na hakika kuhusu maumbile ya Roho Mtakatifu. Hata wakati huo wengi wao hawakufikiri Roho Mtakatifu kama

²⁶¹ B.M Metzger, *Maneno mafafanuzi ya Agano Jipya ya Kigiriki* (United Bible Society,1971), 715

²⁶² Ibid.,

²⁶³ *Maziko na kufufuka kwa Yesu Kristo*, 325 – 327, ilitajwa kwa “Concessions” au Makubaliano, 281

mtu.²⁶⁴ Kwa hivyo hakuna mafundisho yaliyotokea zamani ya mwaminifu wa utatu ilivunjwa na ni kiungo chetu na maandishi ya mitume.

Mambo ya hakika ya kibibilia yameelezwa ya kutosha kwa kuifikiria roho kama akili, roho na utu wa Mungu na Kristo akinyoshwa kwa ulimwengu. Roho una utu kwa sababu ni mfano kwa watu wa Baba na Mwana kwa kitendo, kufundisha, kueleza na maongozi ya kanisa. Hatuoni haja ya kutangaza kuwepo wa mtu wa tatu, tofauti na Mungu na mwana wake. Kuna hakika ya kuwa tegemeo ya Bibilia ya “Roho” ya Baba, Mwana na waaminifu wanaounganishwa na dhamana ya Roho Mtakatifu. Hivi Yohana anamuandika Yesu akiomba “Ndio waeza kitu kimoja, kama wewe, Baba ndani yangu nami ndani yako, na wao wawe moja kwetu sisi... mimi kwao, wao kwangu, na wawe kamili kwa umoja.” (Yohana 17:21,23). Roho Mtakatifu, roho ya ukweli, ni akili ya muumbaji ikiwa tayari kwa mateso ya binadamu. Ruhusa ya kukaribia roho mtakatifu unapatikana kwa maneno ya Yesu, ambayo ni “roho na ni maisha” (Yohana 6:63) Wakristo wanamiliki wakfu kwa kupaka mafuta ambayo inawafunza madhehebu ya ukweli, inawalinda kutoka uongo na uharibifu w shetani, na unawaezesha kukaa kwa umoja wa Kristo (1 Yohana 2:27) Tunafikiria kuwa matumizi ya roho mtakatifu unafanywa siri wakati utumishi unaelekezwa kwa swali kuhusu roho kama mwanachama wa tatu wa kichwa cha Mungu. Maana kubwa mno wa roho ni kwamba unalinganishwa na Mungu mwenyewe kwa uvumbuzi wake na kazi ya ushirikiano, akifungua roho yake kwa viumbe vyake. “Roho inazungumza” si tofauti na “Mungu anazungumza.” Neno, hekima na roho zina uhusiano wa karibu. Hizi ni toleo za fahari za Mungu mmoja, si watu tofauti kutoka kwake kueleza roho kama mtu wa tatu si muhimu. Inaleta shida ya hatari (ikiwa na matokeo ya machafuko). Shida ilitokea wakati sifa takatifu (ambayo saa zingine kutoka Bibilia inafanywa kama kwamba ni mtu) ilibadilishwa kuwa mtu.

Hakuna sababu ya muhimu ya kujitenga na ulinganifu wa tabia kati ya maneno “roho ya Eliya” (Luka 1:7) na “roho ya Mungu.” Roho ya Eliya, si mtu tofauti na Eliya, wala Roho ya Mungu si tofauti na Mungu. Roho wa Mungu hutupa ufahamu katika kuona undani wa kiungu. Tunakutana na Mungu anapojinyosha mwenyewe kupitia kwa Roho yake, kwa nguvu katika maandiko ambayo ‘ni ya kiroho’ (2 Tim 3:16). Tunaposoma ya kuwa “Bwana akaghairi ya kuwa amemfanya mwanadamu duniani akahuzunika moyo” (Mwanzo 6:6), ilikuwa ni Roho ya Mungu iliyokuwa imeghairi (Linganisha Waefeso 4:30). Macho na Roho ya Mungu ilipokuwa katika hekalu (1 Wafalme 9:3), kwa usawa mtu anaweza kusema kuwa Roho yake, ilikuwepo hapo. Uhusiano wa karibu wa Roho, akili, moyo na maneno unaonekana katika maneno dhahiri ya Methali 1:23 : “Geukeni kwa ajili ya maonyo yangu, tazama, ‘nitawamwagia’ Roho yangu, na kuwajulisheni maneno yangu”. Moffat anaonyesha upande mwingine wa “ nitafanya akili yangu ijulikane kwenu.” Revised Standard Version, inaonyesha kiakili hali ya Roho: “nitawamwagia mawazo yangu juu yenu”, na Jerusalem Bible inatuwezesha kuona tena maana nyingine: “nitawafungulia moyo wangu kwenu.”

Roho wa Mungu ni akili yake takatifu, sifa njema na tabia, elezo ya mipango na maksudi ya moyo wake. Kupitia kwa Roho tunaalikwa kushiriki katika matendo ya Kiungu kuwa “mtakatifu kama vile Mungu ni mtakatifu” na kushiriki katika mashauri ya kisiri ambayo anatamani kushirikiana na sisi: “Siri ya Bwana iko kwao wamchao, naye atawajulisha agano lake” (Zaburi 25:14).

Bila kujua mafundisho ya baadaye, Paulo bila kuzuiwa hubadilisha “Roho” na “Akili”, hivyo kutupatia maelezo ya Kiutume juu ya Roho Mtakatifu. “Ni nani aliyejua

²⁶⁴ Philip Schaff, *Historia ya Kanisa ya Wakristo*, 3:664.

nia (nous) ya Bwana, au ni nani aliyekuwa mshauri wake?” (Warumi 11:34). Kifungu katika Waebrania ambacho Paulo anatumia inasema “ Ni nani aliyemwongoza roho ya Bwana?” (Isaya 40:13). Kwa kupokea Roho, ambayo ni sawa na “ kupokea ujuzi wa kweli” (Waebrania 10:26), tunapata njia ya kufikia Uungu tulionyoshewa kwetu katika roho.

X. VITA JUU YA UTATU KATIKA HISTORIA YA KANISA NA MJADALA WA SASA

“Katika karne ya tano Ukristo ulishinda upagani na upangani ulikuwa unaadhini virusi Ukristo” - Macaulay

Matarajio ya Historia ya Mjadiliano wa Kisasa kuhusu Kuwepo

Shida ya kuwepo (kwa hivyo ya Utatu), na matokeo yake ya kawaida kwa Mwokozi, amekua na historia ndefu kwa Kanisa. Kwa miaka yaliyopita imekua zoezi kwa akili za wasomi kadhaa wa Bibilia ambao wameshangaa kama kweli urithi wa Baba wa Kanisa hufanya kidogo kuliko haki kwa kitu kimoja kumwamini Mungu mmoja kama ilivyoandikwa na mitume.²⁶⁵ Swali ambalo limedumu linauliza kuaminiwa kwa Yesu kanuni za imani kama binadamu wa ukweli.²⁶⁶ Mchoro wa kihistoria utasaidia kuweka mfano wa mandhari wa mjadala wa miaka ile ile.

Tunafahamu kwanza kuwa Justin Martyr (c. 114 – 165) alikuwa mmoja wa waandishi wa kwanza wa Bibilia walioendeleza mafundisho ya dini ya kuwepo kwa Kristo, ingawa alikiri ya kwamba si waumini wenzake wote walikubaliana na mtazamo huu. Alikiri wazi kwa Myahudi, Trypho, kwamba:

Yesu anaweza bado kuwa kristo wa Mungu, ingawa siwezi thibitisha kuwepo kwake kama Mwana Wa Mungu aliyewezesha kila kitu...Ingawa siwezi thibitisha kwamba yeye alikuwako mbele, itakuwa haki kusema kwamba katika heshima nimedanganya na sitasema kwamba yeye si Kristo...., ijapo inaonekana alizaliwa mwanamume wanaume ... na kuna wengine...wa taifa/kabila letu ambao hakubali kwamba yeye ni Kristo, wakati kumfanya yeye kuwa mtu wa watu; na ambaye mimi si kubaliani naye.²⁶⁷

Trypho, matarajio ya Wayahudi juu ya Masihi, anaongeza sauti yake kwa wale ambao hufikiri kwamba Yesu alikuwa ni mtu, na kuwa mteule wa Mungu, naona maoni haya zaidi ya maoni ya Justin ijapokuwa Trypho hapa anaonekana akimaanisha Kristologia “adoptionist” (yaani, Yesu alikua Mwana wa Mungu wakati wa ubatizo wake), kama tofauti na Kristologia ya Luka (Yesu ni Mwana wa Mungu kwa mujibu ya kutungwa kwake kimuujiza, Luka 1: 35), inaonekana wazi kutoka wa mjadala wa Justin kwamba imani katika kutoka mbele ulimwenguni umepitia madhehebu iliyofanya halisi. Pia ni ajabu kwamba “hakuna popote ambapo Justin anadai kwamba Baba, Mwana na Roho ni Mungu mmoja, kama ilivyotakikana kuwa desturi enzi ya baadaye. Kuongea kwa ukali, alikuwa mwaminifu wa Mungu mmoja (waunitara), kama vile Baba wenye amani wa wakati huo: kwamba waliamini Mwana kuwa tofauti na Baba na wa chini kumliko yeye.”²⁶⁸

²⁶⁵ Marko 12:29-34; Yohana 5:44; 17:3; 1 Kor. 8:4-6; Eph. 4:6; 1 Tim. 2:5, etc.

²⁶⁶ Cp. Thomas Hart, *To Know and Follow Jesus and the well-known God Was in Christ* by Donald Baillie (London: Faber, 1961).

²⁶⁷ *Dialogue with Trypho*, chs. 48, 49.

²⁶⁸ Alvan Lamson, D. D., *The Church of the First Three Centuries* (Boston: Houghton, Osgood & Co., 1880), 80. Justin, ingawa, aliweka mwelekeo wa baadaye wa ujenzi wa Utatu kwa kuisisitiza kuwepo-kabla kwa Yesu. Utatu ulikua hauaminiki kwa wakati kabla ya urumi kwa miaka 80, kama ilivyoonyeshwa kwa *The New Schaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge* wakati wa 100-180 “hakuna kitu cha kuonyesha kuwa wakati huo Kristo alitambuliwa kama Uungu wa kweli” (Harnack, “Monarchianism,”

Ishara zaidi ya mzozo juu ya injili ya Yohana na kabla kuwepo inapatikana katika maandiko ya Epiphanius, Baba wa kanisa ya kigiriki (c.310 – 403), ambaye alikuwa na nia ya kutambua “uzushi”. Analihusisha na kundi la waumini wa wayahudi, kwa Alogi c.180), ambaye alishtakiwa kwa kuukataa Injili ya Yohana.

Joseph Priestley alikuwa na maoni kwamba Alogi alikosa Epiphanius kwa sababu “walielezea ‘logos’ katika uanzilishi wa Injili ya Yohana kwa namna tofauti na yake.”²⁶⁹ Jambo muhimu ya maana ya logo” katika matangulizi ya Yohana ilikuwa tayari sababu ya kutokuwa na uhakika. Azimio la swali juu ya asili ya kabla kuwepo katika Yohana ilikuwa neema ya imani katika kabla kuwepo kwa Mwana na adhari ya kudumu na halisi ya Christologia ya imani. Mafundisho ya dini ya Utatu hauwezi kuwa na uendelevu isipokuwa inaweza kuonyesha kwamba Yesu alikuwepo kama Mwana wa Mungu anayeishi milele kabla ya kuzaliwa kwake. Maandamano dhidi ya maandiko maalum ya Yohana, yaliyoanzisha mvutano kati yake na muhtasari wa Kristo iliibuka tena.

Nguvu ya Kumaliki

Kabla ya muda mrefu ya matokeo yalitokea dhidi ya tishio dhahiri ya uaminifu wa Mungu mmoja iliotokana na uanzilishi wa “Mungu wa Pili” katika kuwepo-kabla kwa Kristo. Justin na waandishi wengine wa hapo awali walifunzwa sana kuhusu busara kabla ya kuja kwa Wakristo. Ilikuwa rahisi sana kwao kutimiza uwezo wao na kusoma utanguliza wa Yohana kama ilivyokubaliwa kwa maoni ya Kigiriki ya ulimwengu:

Yule “Mrumi” wa karne ya pili walifahamu uzoefu na upendo wa elimu wa ulimwengu mzima na matengenezo na taratibu zake kuliko yale ya Bibilia, na kuongeza mafundisho ya Kikristo kutosha iliyo tulivu. Walifahamu Mungu kuliko kiini chote, kisichoelezeka kuwa tukufu, kisichotoleka wazi, kisiopitika, kinachoabudiwa kuliko biashara yoyote ya kadiri, wakati au nafasi. Mungu aliye na Upendo huu wa akili aliiweka mbele neno....kwa kitendo cha hiari chake kiwe kiamuzi chake cha viumbe, ufunuo na ukombozi. *Mafundisho ya dini yanaeleza Mwana kama kuwepo-kabla.*²⁷⁰

Urejeo ulitokea wakati kundi la waumini halikukubaliana kuwa utatu kwa kweli kilikuwa kimoja – cha “ufalme.” Theodotus, mtengenezaji wa ngozi, alikuza kisa hiki cha walimwengu wa Yesu katika “Rome” wakati wa 190 – 200. Inatazamisha masimulizi ya Paulo kwa 1 Tim 2:5, alithibitisha kwamba Yesu hastahili kuitwa Mungu. Mrithi wake, Theodotus mwingine, aliendelea kushindania maono ya Yesu kama binadamu aliyezaliwa kimwujiza. Miaka thelathini baadaye, Artemas, ambaye alishikilia kuelewa “ufalme” ule ule wa kichwa cha Mungu, alishindana kwa maneno dhidi ya askofu wa kirumi kwamba Ukristo wa kale ambao ulitetewa na ufalme na ulipotoshwa na wakubwa rasmi wa Kanisa.

Paulo wa Samosata

Swala la asili ya kabla kuwepo, kinajitokeza kwa teolojia ya Paulo wa Samosata,

7:453).

²⁶⁹ *Historia ya Ufisadi wa Ukristo* (J. & J.W. Prentiss, 1838), 21.

²⁷⁰ William Childs Robinson, “Jesus Christ Is Jehovah” (Part 2), *Evangelical Quarterly* 5:3 (1933): 275, emphasis added. Kwa ujenzi upya wa utatu kabla ya Bibilia kuandikwa, angalia M. M. Mattison, *The Making of a Tradition* (Ministry School Publications, 1991).

askofu wa Antiokia, ijayo kati kati ya karne ya tatu. Ingawa Paulo alitiwa hatia kirasmi kwa uzushi wa 268 AD, waandishi wa kisasa wamefahamu nguvu ya maandamano wake dhidi ya “imani halisi”. “Teolojia letu limetiwa kwa harakati za shule,” alivyoandika askofu mkuu Temple. “Sisi tuna haja na tunaendelea kulazimishwa katika teolojia kwa msingi wa elimu ya mambo ya roho. Ugeuzi huu, unaogopesha, hautakosa uchungu mwingi; lakini hakuna kizuizi.” Templa aliendelea kusema kwamba “hatufai kusahau kwamba kulikuwa na wakati hapo awali ambapo awali wa Samosata alitoa jaribio. Aliona ugumu kwa utunzi wa uaminifu wa kanisa kuhusu Kristo kwa sababu kimeelezwa dhidi ya uthabiti, na kujaribu kukieleza dhidi ya hiari.”²⁷¹

Mshiriki mwingine wa mazungumzo huu, Profesa Bethune-Baker, alieleza kusadiki kwake kwamba “Paulo wa Samosata alikua na historia zuri ya mapokeo ya zamani, ambayo, mafundisho, lazima tuyarudishe.”²⁷² Loofs, mhistoria wa Ukristo alikua na hitimisho kwamba Paulo wa Samosata “ni mmoja wapo wa mteolojia wa kuvutia wa kabla wakati wa Nicene, kwa sababu anasimama kwa mstari wa mapokeo ambayo ilikuwa na mizizi ya wakati kabla gharika ya Hellenism ilifagilia Kanisa.”²⁷³

Kuelewa kwa Paulo wa Samosata kuhusu “logos” ilikuwa kwamba hakikuwa na kuwepo unaojitegemea ila kutoka Mungu; kwa maneno mengine kwamba hakuna Mwana mpaka *mimba* ya Yesu. Ujuzi mkuu wa mapokeo yayo hayo yanasisitizwa na maono ya Origen kwa ufafanuzi wa Yohana. Alisema kuwa kulikuwa na “Wakristo wengi ambao walikichukua jina la ‘logos’ kwa kuwepo-kabla Kristo (bila matamshi ya falsafa na kwa hisia ya *kutamka* kwa Yesu) ambayo ilijieleza kwa Mwana wakati Yesu alitungwa katika mimba” (cp. Kir.1:1, 2). Hawakukipa “logos” fumbo tofauti la imani au ubinafsi.²⁷⁴ Ni jambo la kuvutia kwamba Tertullian (c.155 – 230) anatafsiri “logos” kwa *sermo*, “hotuba” kama “kile ambacho unakielewa.” Akimaanisha wakati kabla ya viumbe, anaendelea kusema kuwa “ingawa Mungu hakuwa ametuma neno lake, alikua nayo na kwa sababu ndani yake mwenyewe.”²⁷⁵ Ni wazi kwamba “neni” halikueleweka kama Mwana kabla-kuwepo milele, kama uhalisi.

Green anasema kwamba mafundisho ya Paulo wa Samosata kuhusu Utatu (sio Utatu kama ilivyotungwa baadaye) ilikuwa “kama maandishi yale ya origin, dhidi ya sauti na mapokeo yaliyo katika Kanisa.”²⁷⁶ Anaendelea kusema kwamba:

Haiwezi kusisitizwa zaidi kuwa mapokeo ya Antiochene hakujuua chochote kwa tamko Mwana kama ilivyo katika kuwepo-kabla ya Logos, kwa maelezo yoyote yaliyotumiwa. Neno “Mwana” walimaanisha Kristo wa Kihistoria...Loofs ana maono kuwa ubadilishaji wa mimba ya Mwana kwa kuwepo-kabla Logos na teolojia ya “Alexandrian” ambabyo ilikuwa ya muhimu sana kwa uanzilishi wa wingi wa tabia ya mafundisho ya Ukristo.²⁷⁷

Kuongea kuhusu Yesu kama Mwana kabla-kuwepo kilikuwa janga la kuhamisha ambacho kilitoa Mwokozi kutoka kwa jamii ya binadamu na ilizindua mfululizo wa

²⁷¹ *Foundations* (London: Macmillan & Co., 1913), 226.

²⁷² Iliyoandikwa na F.W. Green, “Maendeleo ya baadaye ya Mafundisho ya Dini ya Utatu,” kwa *Essays on the Trinity and the Incarnation* (Longmans, Green & Co., 1928), 259.

²⁷³ 9 Ibid. Cp. Maoni ya Canon Goudge kwamba “wakati akili ya wagiriki na warumi badala ya akili ya waebrania zilikuja kutawala Kanisa, kulitokea maafaka katika mafundisho ya dini na mazoezi ambapo hakuna kilichookolewa” (“Wito wa Waebrania,” kwa maandishi yaliyokusanywa kwa *Judaism na Christianity*).

²⁷⁴ F.W. Green, *Essays on the Trinity and the Incarnation*, 262.

²⁷⁵ Tertullian, *Ad Praxeus*, 5.

²⁷⁶ F.W. Green, *Essays on the Trinity and the Incarnation*, 64.

²⁷⁷ Ibid.

migogoro ya kutisha kuhusu Kristo. Wakati wa mwanzo wa Yesu uliacha kuwa katika utunzi wa mimba, uvumi ulizusha, na umoja wa Uungu ulitishiwa na Yesu alikuwa si tena “binadamu masiya” ilivyotabiriwa na Bibilia ya Waebrania. Ujenzi upya ambao unafunga neno “mwana” kwa Yesu kama binadamu angeonekana kuwa msingi imara katika Kanisa ya hapo awali kwa historia, kama vile katika Bibilia yenyewe. Ni jambo linalotia moyo kupata William Temple akikubaliana na uelezi halisi wa asili ya kabla-kuwepo kwa Yohana: “Kitambulisho cha Johannine ya Kristo pamoja na ‘logos’ awali kilimaanisha, kwa maandishi ya mhubiri, ‘Unaamini kanuni la neon moja lakini huijui tabia yake; tunajua;ilitengenezwa kuwa mwili kwa mtu wa Yesu kutoka Nazareth.’”²⁷⁸

Msomi halisi aliyefariki F.F. Bruce, anashikilia maono ya kabla-kuwepo ambayo inaiacha wazi swali kamakweli katika Yohana 1:1 *mwana* akiishi kabla-kuwepo. Anasema: “kuhusu swala la kabla-kuwepo, mmoja anaweza angalau kubali kabla-kuwepo kwa neno linaloishi milele au hekima ya Mungu ambayo (nani?) kilifanyika mwili kwa yesu. Lakini kama mwandishi wowote wa Angano Jipya aliamini kwa kuwepo kwa fahamu tofauti kama ‘mtu wa pili mtakatifu’ kabla yake kufanyika mwili si wazi.”²⁷⁹

Swali lake Bruce lililowazi kabisa lilikuwa na ushahidi mwingi. Kama kweli hakuna mwandishi wa Agano Jipya aliyeamini kwamba mwana wa Mungu alikuwa mtu wa pili mtakatifu kabla-kuwepo, inafaa ifuate kuwa hamna mwandishi wa Agano Jipya aliyeamini utatu.

Photinus na Photinians

Vikwazo kwa kabla-kuwepo kwa Yesu unajitokeza tena katika karne ya nne askofu Photinus wa Sirmium. Kuelewa kwake wa Yesu ulikuwa pengine unafanana na ule wa Paulo wa Samosata. Photinus aliimarisha kuwa Uana wa Yesu ulianza wakati usio wa kawaida wa mimba huo. Baraza kadha zilimshtaki kwa kusema kuwa Mwana aliishi kabla Maria kwa ujuzi na utumishi wa Mungu. Mwana historia wa kanisa, Sozomen, anamueleza Photinus kama anavyotambua kuwa “kuna Mungu mmoja mkuu, ambaye kwa maneno yake vitu vyote viliumbwa.” Lakini Photinus hangekubali kwamba “kizazi na kuwepo kwa mwana ulikuwa kabla miaka za awali; kinyume ni kwamba alidai kuwa Kristo alitoa kuwepo/kuishi kwake kutoka kwa Maria.” Mapokeo yaliyokataa kabla-kuwepo kwa Mwana ulinusurika katika Uhispania na kusini Gaul hadi karne ya saba. Photinians, pamoja na wafuasi wengine wa Askofu Bonosus ambaye aliukana kabla-kuwepo wa Kristo, walilaaniwa kama wazushi na yule *Synod* wa Toledo mnamo wa 675.²⁸⁰

Michael Servetus na Adam Pastor

Mhispania Michael Servetus (1511 – 1551) alikuwa mmoja wa watambulishi dhahiri wa kupinga Usomi wa ukristo ya Nicene. Msingi wa insha yake ni kwamba kuanguka wa kanisa kutoka kuingilia kwa Constantine katika mambo ya Mafundisho ya

²⁷⁸ *Foundations*, 227.

²⁷⁹ From correspondence, June 13th, 1981

²⁸⁰ Angalia M. M. Mattison, “Utatu wa Kibibilia kutoka Kanisa ya hapo awali kutoka enzi za katikati,” *A Journal from the Radical Reformation: A Testimony to Biblical Unitarianism* 1 (winter 1992): 4-13. Mali ya habari kuhusu vipengele vyote vya utata wa Utatu ambao unapatikana katika kitabu hiki, kilichochapishwa kutoka 1991-2000. Shida za nyuma zinaweza patikana kutoka 800-347-4261. Rasilimali zaidi inaweza patikana kwa www.restorationfellowship.org.

dini ya Kikristo Nicea. Alipinga kuwa kukubali kwa Yesu Kristo kama Mwana kimasihhi wa Mungu lazima iwe msingi wa kujenga tena usomi wa Ukristo. Mwana, alidai, alipata uhai katika mimba yake Maria. Kisha akaondosha falsafa ya Kigiriki uvumi wote wa kidunia kuhusu “kizazi cha milele” cha Mwana. Akaona Roho Mtakatifu kama nguvu na utu wa Mungu ukiendelezwa kwa viumbe, na sio mtu tofauti katika Uungu. Servetus anasisitiza kwamba Mwana anaenza fikiriwa kama kuishi milele kwa heshima ya nia ya Mungu kumzalisha kwa wakati mwingine wa baadaye kwa historia.²⁸¹ Kama ilivyojulikana, Servetus alilipa kwa “uzushi” wake wa Ukristo na maisha yake. Alichomwa kwa hisa katika Geneva, kwa uchochezi wa Kanisa ya katoliki ya Kirumi na mgeuzi mpotestanti, John Calvin, mnamo Oktoba 27, 1553. Mpango huu wa kutisha ni kumbusho la vurugu la kutisha na bidii potofu uliotiwa alama baadhiya wali wanaokiri Ukristo.²⁸²

Swala la kabla-kuwepo ulikuwa jambo la muhimu kati ya Anabaptist wa Kiholanzi wa karne ya kumi na sita katika mgogoro kati ya Menno Simons na mwenzake Anabaptist, Adam Pastor (c. 1500 – 1570). Mtawa wa zamani aliyejulikana kama Rodolf Martens, Pastor alikuwa “mtu wa kipaji cha juu na msomi katika jamii kuu la Anabaptist wa Kiholanzi wa wakati wake.”²⁸³ Ukristo wa Pastor unatarajia maswali ya kisasa ya aili ya kabla-kuwepo, na ukristo ulio sawa ulijitokeza katika kazi ya karne ya ishirini wa wa teolojia wa Kihispania Hendrikus Berkhof na Ellen Flesseman.²⁸⁴ Pastor alikana uhalisi wa Utatu mnamo 1547 katika Emden na akakatazwa mawasiliano na Simons na Obbe Philips. Kama tunavyoona kutoka kwa maandishi ya Pastor katika *Difference Between True Doctrine and False Doctrine*,²⁸⁵ aliukana kabla-kuwepo wa Kristo. Haukuwa mshangao, Snadius na maandishi wengine wanaokana utatu wanamtaja Pastor kama “mwanadamu katika mababu yetu ambao walikua wa kwanza na walieza kuandika kwa mwelekeo huo,” kwa mfano, mtazamo kwamba “neon” la Yohana 1:1 haukuwa mtu, bali neon la Mungu ubunifu au utu wa mapanzi wa Mungu.²⁸⁶ H.E. Dosker anasema kuwa “Tunaposoma kuhusu Adam Pastor lazoma tufute macho yetu tuone kama tunaota ama ilhali tuko macho. Kile ambacho anataka kusema ni cha kisasa na kinatisha wasomaji. Na tunaamka kuona kuwa si yote ni ya usasa... ni ya kisasa.”²⁸⁷

Pastor ni wa muhimu kwa mafundisho ya Menno na Melchior Hoffman kwamba neon ilipitishwa kwa Maria bila hata kushika mwili wake. Hii ingemfanya Maria awe mama kinaibu ambaye hakutunga mimba ya Yesu kama inavyoonyeshwa kwa neon. Ukristo kama huu haungekosa shtaka la docetism na Gnosticism. Pastor anasisitiza kuwa Kristo ni mwanadamu kikweli na wa ukoo ya Daudi, aliyetungwa kwa njia isiyo ya kawaida. Maono yake unasanjari vyema na ule wa Raymond Brown anaeleza kama ile ya Luka na Mathayo. Ni hakika kuwa Anabaptist wa “Poland” karne moja iliyopita alisema kuwa Pastor kama mtu wa kwanza ambaye alitoa maoni yao kuhusu kabla-kuwepo. Bila shaka, Adam Pastor anatarajia mazungumzo ya kisasa kuhusu uanadamu wa Yesu wakati anaitambua “logos” sio kama Mtu kabla-kuwepo, lakini kama kitendo inayojieleza

²⁸¹ G.H. Williams, *The Radical Reformation* (Philadelphia: Westminster Press, 1962), 271, 322, 333.

²⁸² For details of Calvin’s treatment of Servetus, see R.H. Bainton, *Hunted Heretic: The Life and Death of Michael Servetus* (Beacon Press, 1953), and Stefan Zweig, *The Right to Heresy* (Beacon Press, 1951).

²⁸³ H.E. Dosker, *The Dutch Anabaptists* (Judson Press, 1921), 58.

²⁸⁴ See Hendrikus Berkhof, *Christian Faith* (Grand Rapids: Eerdmans, 1979), and Ellen Flesseman, *A Faith for Today*, trans. J.E. Steely, (Association of Baptist Professors of Religion, Box A, Mercer University, 1980).

²⁸⁵ *Underscheit tusschen rechte und falsche leer* (Bibliotheca Reformatoria Nederlandica), 5:315-581.

²⁸⁶ Dosker, *The Dutch Anabaptists*, 163.

²⁸⁷ *Ibid.*, 93.

kipekee ya Mungu ikiweka mbele nguvu yake katika viumbe, ikionyesha ukweli na katika kumzalisha Masiya.²⁸⁸

John Biddle, Baba wa Waiingereza Wanaopinga Utatu

John Biddle (1615-1662), msomi wa Falsafa katika chuo cha Oxford, alirejelea kutafuta maandiko²⁸⁸ baada yake kuwa na swali kuhusu mafundisho ya Kanisa. Kutoka 1641 hadi 1645 Biddle alikuwa mwalimu mkuu wa Shule ya Crypt, Gloucester. Ilikuwa kwa wakati huu ambapo usomi huu wa Agano Jipya ulimsababisha kutokabiliana na mafundisho ya Utatu. Jambo hili lilikuwa la asili muhimu sana hadi mawakili wakatoa amri akamatwe na kutiwa korokoroni. Kufuatia mjadala wa Askofu mkuu Ussher (wa sifa za wakati), Biddle akakusanya matokeo yake ya utafiti wa Ukristo wa hapo awali. “Baba wa karne hizo mbili za kwanza, au wakati huo, wakati ambapo hukumu ya Wakristo ulikuwa uwachiliwe huru, na si mtumwa wa mabaraza, wakidai kuwa Baba ndiye pekee Mungu mmoja.”

Biddle alilalamika kwamba lugya ya wagiriki ya kifalsafa ya fumbo la imani “ilizaliwa kwanza na udanganyifu wa shetani katika wakuu wa Plato na kubatilisha ibada ya Mungu wa kweli” Bunge hawakupoteza muda wa kuagiza kwamba kazi ya Biddle ichomwe. Katika mwaka 1648 serikali ya Uingereza ilipitisha kinachoitwa “Sheria ya Uteshi” kwa ajili ya adhabu ya kifo kwa “Kashfa na uzushi,” kwa lengo la udai wa Biddle ya kwamba mafundisho ya Utatu ulileta, “Miungu mitatu, na kwa hivyo inagawa Umoja wa Mungu, kama inavyofundishwa mara nyingi katika Maandiko.” Imani ya Kiathanasia halina jibu kwa tatizo hilo: “Kwani nani yupo (kama angalau angedhubutu kutumia sababu ya dini yake) asiyeona kwamba hii ni kama ujinga kama lazima aseme, “Petro ni Mtume, James ni Mtume, Yohana ni Mtume; lakini hakuna Mitume watatu bali ni Mtume mmoja?”

Katika mwaka wa 1655, Biddle alifungwa katika gereza la Newgate, kwa “kukana hadharani kwamba Yesu Kristo alikuwa ni Mungu Mkuu.”

Wafuasi wa Biddle walisema kwa haraka kuwa, Wakristo wote lazima wachukuliwe hatua ya kifo na Bunge kwa kujaribu kuzuia wasio amini katika Utatu Mtakatifu kwani, “Asemaye kwamba Kristo alikufa, asema kwamba Kristo hakuwa Mungu, maana Mungu asingeweza kufa. Lakini kila Mkristo asema kwamba Kristo alikufa, hivyo, kila Mkristo asema kwamba Kristo hakuwa Mungu.”

Ombi kwa ajili ya kuachiliwa Biddle yanamweleza kama, “mtu, aliyetofauti na wengi wetu katika mambo mengi ya imani, lakini kwa sababu ya masomo yake ya bidii ya Kitabu Kitakatifu, na mazungumzo ya busara na amani, ambayo baadhi yetu tuna fahamu ya elimu bora, si lazima tuhukumu kwa kila njia uwezo wa uhuru kama ilivoahadiwa na Serikali.”

Ingawa tu miaka arubaini na saba, Biddle alitimia karibu miaka kumi ya maisha yake gerezani kwa kushiritisha kwamba Mungu alikuwa Mtu mmoja. Alikufa gerezani mwaka wa 1662, “mwathirika wa *‘odium theologicum’* na hali chafu ya mahali ambapo aliishi.” Mwandishi aliyekuwa na huruma aliandika kuhusu bidii ya Biddle “kwa ajili ya kukuza utakatifu wa maisha na tabia; kwa maana, hii ilikuwa nia yake katika mafundisho

²⁸⁸ For a fuller account of Adam Pastor, see A.H. Newman, “Adam Pastor, Anti-trinitarian, Anti-paedobaptist” in *Papers of the American Society of Church History* (G. Putnam’s Sons, 1917), 2nd series, 5:98. See also Anthony Buzzard, “Adam Pastor: Anti-Trinitarian Anabaptist,” *A Journal from the Radical Reformation* 3:3 (Spring 1994): 23-30.

yake. Hakuthamini mafundisho yake ya uvumi bali ili itendwe.”²⁸⁹

John Milton, Sir Isaac Newton, John Locke

Mshahiri wa Uingereza aliyesherehekewa, John Milton (1608 -1674), hajulikani vile kwa *Treatise on Christian Doctrine*, ambayo yalipotezwa kwa umati kwa miaka 150 baada ya kifo yake. Iilitambuliwa tena katika mwaka 1823, makala yalionyesha kuwa mabishano ya kibibilia ya Milton dhidi ya mafundisho ya Utatu. Milton alitamani:

kuwasilisha matokeo ya maswali zangu kwa dunia yote kwa jumla; kama, Mungu ni shahidi wangu, iwe ni wa urafiki na hisia ya upole unaoelekea watu, ambayo niko tayari kuipa kama mzunguko kama iwezekananyo kwa ile ambayo ninaiheshimu na ni mali yangu ya thamana ya juu, natarajia kukutana naye kwa mapokezi ya uadilifu kutoka kila mtu..., ingawa vitu vingi vinafaa kudhihirishwa ambayo yanaonekana kuwa tofauti na maoni yaliyopokewa.

Anaendelea na ombi kwa “wapenzi wote wa kweli” kwamba “kuadhibisha mambo yote” katika mwanga wa maandiko. Kile anachotamani tu ni kuilinda Bibilia kutoka kwa mapokeo:

Kwa upande wangu, ninafuata maandiko matakatifu pekee – Sifupati uzushi au kundi kingine. Sikuwa nimesoma kazi ya uzushi, unavyoitwa, wakati makosa ya wale wanaofikiriwa kuwa halisi, na utunzi wao wa tahadhari ya Maandishi, mara ya kwanza ilinifundisha kuelewana na wapinzani wao wakati wowote wapinzani hao walikubaliana na Maandishi.²⁹⁰

Milton anajenga kesi yake ya kutoamini Utatu kwa kupanga taarifa ya Waunitaria ya Agano Jipya. Ubishi wake unalinganishwa kwa tabia ya mantiki, na maarifa ya undani ya lugha za kibibilia na matatizo ya majaribio ya mapokeo kuepuka taarifa Waunitaria ya Paulo kwamba “hakuna Mungu bali Baba”: “Ni ajabu kwamba kile wapotovu wapole, watu binafsi wameamua kuutoroka maana ya vifungu hivi.”²⁹¹

Milton anayafahamu na mabishano mbalimbali ya Utatu na jibu lake linaleta mchango usio na dhamana kwa majadiliano ya kisasa.

Sir Isaac Newton (1642 – 1727) na John Locke (1632 – 1704) wanadhaniwa kuwa kati ya wale ambao wana akili ya ustadi zaidi wa karne ya kumi na saba. Pamoja na Milton walipinga viumbe vya kilinge ambayo hayapatikani katika Bibilia. Mabishano yao ni “hatimaye mantiki nay a akili ya kawaida.”²⁹² Wote wanahifadhi kuwa kiini ya ukristo inafaa kukubali Yesu kama Masiya, na si Mungu.²⁹³

Majadiliano ya Kisasa kuhusu Kabla-Kuwepo

Swala la kabla kuwepo ulikua lengo la insha ya John Knox inayodhihirisha kwa *Humanity and Divinity of Christ*. Uhakika wake ukubwa ni kwamba “madai ya kabla-

²⁸⁹ Habari hii wa kipande hii ni imetolewa kutoka H.J. McLachlan’s *Socinianism in Seventeenth-Century England* (Oxford University Press, 1951), 163-217.

²⁹⁰ John Milton, *Treatise on Christian Doctrine* (London: British and Foreign Unitarian Association, 1908), x, xi.

²⁹¹ *Ibid.*, 20

²⁹² Christopher Hill, *Milton and the English Revolution* (New York: Viking Press, 1977), 286, 296.

²⁹³ See Locke’s *The Reasonableness of Christianity as Delivered in the Scriptures* (1695).

kuwepo kwa Kristo, yaliweka mvutano juu ya ubinadamu wa Yesu ambayo haikuweza kushikilia.”²⁹⁴ Anaendelea kushikilia kwamba katika Injili ya Yohana ubinadamu wa Kristo ni “kwa hisia rasmi, kinashikiliwa kwa nguvu na bila mafumbo, lakini ukweli halisi, umebadilishwa sana na Uungu wa pande zote, kama ilivyo, na si tena chemchemi kwa njia yoyote kawaida.” Na maneno haya huonyesha vikwazo vyake kwa fikira yake Yohana kwake Yesu. Lakini Yohana kweli anaenda kinyume mwenyewe? Ni sisi peke yetu tunawasilisha wakati tafsiri unafanywa na wana imani wa kitambo. Knox anaweka masharti kwa mjadala ambao umeendelea na maslahi maalum katika Ukristo wa Yohana na asili ya kabla-kuwepo. Kama kweli Yohana alimfikiri Yesu akiishi kabla-kuwepo kama *Mwana*, jambo hili moja kwa moja linaenda kinyume sana na ubinadamu wa kikweli? Knox anaamini kuwa: “Tunaeza kuwa na uanadamu bila kabla-kuwepo na kabla-kuwepo bila uanadamu. Hakuna njia yoyote tunaeza kuwa na zote mbili.”²⁹⁵ Knox anaamini kuwa “Ni jambo la ajabu kwamba mtu mtukufu angekuwa binadamu wa kawaida – kama angeendelea kutambulika, mtu sawa.”²⁹⁶

Picha jadi ya Yesu kama alivyogeuka kuwa mwili wa Mwana kabla-kuwepo ni shida papo hapo kwa Knox. Anaona uhalisi wa Ukristo kama “habari nusu na fundisho kuu nusu, kiwanja cha uhadithi na falsafa, wa shairi na mantiki, ngumu kueleza kama vile kutetea... Hii ni kweli kwa Ukristo wa parokia kwa ujumla (na basi wa Ukristo rasmi ambayo tumerithi).”²⁹⁷

Wasiwasi huu hivi karibuni umekubaliwa na wateolojia kadhaa tofauti, ikionyesha kuwa shida ya kale ya asili ya utukufu na binadamu katika Yesu ni hai kama milele.

Knox anaifikiria maendeleo ya Kristo kabla-kuwepo kuwa na vurugu, inayohusu, tupende au tusipende, kukana kwa ukweli kamili wa ubinadamu wa Yesu. Anasema kuwa Waprotestanti wa Kanisa ya Mababa kwamba Mungu wao alikuwa binadamu kamili kwa sababu “Kuna njia, ukizingatia maneno bila vitu vingine ambapo kuna njia za kuchukua tena kwa mkono mmoja kile mtu alitoa kwa mwingine. Mtu anaweza kuthibitisha ubinadamu kama kweli rasmi na kisha kuendelea kwa kudhihirisha au kuonyesha kuwa ni kukataa ukweli wake kwa njia yoyote ya kawaida inayokubaliwa.”²⁹⁸

Anaungwa mkono katika maoni haya na Norman Pittenger, ambaye anafanya hukumu muhimu ifuatayo kuhusu Ukristo wa Uparokia, iliyopata uongozi wake kutokana na kusoma kwa Yohana:

Katika hukumu langu, tatizo la msingi katika Ukristo ya uparokia ni kuwa neno lilidai ubinadamu wa Yesu Krsito, lakini ukweli ni kwamba haikuchukua ubinadamu huo kwa uzito wa kutosha...[Inafurahisha, kuwa anatenga Paulo wa Samosata kutoka kwa upinzani huu]. Tabia ya kufikiri kwa Ukristo katika mkondo wa kile kilichoaminika kuwa “halisi” ilikuwa imejilaza upande wa Uungu kuliko ubinadamu katika Yesu.²⁹⁹ Uhalisi ya Ukristo, hata wakati wa mazidio ya mafundisho ya Alexandrine ilizuiwa Chalcedon katika AD 451 inaelekea kwa utu usio na nafsi ambayo ni, ninavyoamini, si ubinadamu halisi.³⁰⁰

²⁹⁴ John Knox, *The Humanity and Divinity of Christ* (Cambridge University Press, 1987), 53.

²⁹⁵ *Ibid.*, 98.

²⁹⁶ *Ibid.*, 106.

²⁹⁷ *Ibid.*, 98, 99.

²⁹⁸ *Ibid.*, 62.

²⁹⁹ Cp. Thomas Hart, *To Know and Follow Jesus*, especially 44-48.

³⁰⁰ *The Word Incarnate* (Nisbet, 1959), 89.

Hii inaonekana kuwa tatizo. Lakini Knox amekosa kwa kumlaumu Yohana kwa kusema alianzisha uharibifu huu. Yohana hakuwa na hatia kwa kutoanisha chochote kile juu ya ubinadamu wa Yesu. Badala yake, tatizo linatokana na kutoelewa kwa viongozi wa kanisa ya Nicene, na baadhi ya watangulizi wao, wa “logos” ya Yohana na kwa hiyo, maana ya kabla-kuwepo. Utaratibu rasmi wa baadaye ni kwamba Yesu alikuwa “mtu” lakini si “mtu” (ambayo bado iko kwenye vitabu vya wanaoamini Uutatu hadi leo) haionyeshi nia ya Yohana kabisa, kwa kuwa hakuna njia yoyote ya kuwa “mtu” ila kwa kuwa “mtu.”³⁰¹

Katika mwanga wa mazingatio haya, si vigumu kuona kuwa dhamana ya ukali imefanywa sawa katika ufafanuzi halisi wa Kristo. Kama kuwa binadamu ni kuwa mtu, na uhalisi una aibu wa kusema kwamba Yesu alikuwa “mtu”, labda upinzani huu unafaa kukubaliwa. Lakini, Yohana anatulazimisha tuamini, “Mungu, Mwana kutoka mbele?” Wengi walidhani hivyo, na wameshikilia imani halisi katika kabla-kuwepo, pamoja na hatari yoyote ya ukaribifu na “Upollo” (Yaani, ni uzushi ambao unakanusha ubinadamu wa Kristo) unaoweza kuhusika. Kazi ya hivi karibuni ya wasomi watatu wa kiwango ya juu inaonyesha uzito wa shida hii na inadokeza njia kwa suluhisho - ambayo si mpya ingawa haupewi heshima na waandishi wa sasa kwa wale wa Kanisa la awali la historia ambao walikuwa wameelekeza katika mwelekeo sahihi. Suluhisho inafuata maelezo ya Yohana ambayo tulipendeleza mapema.

James Dunn na James Mackey

James Dunn, katika utafiti wa kina, uchunguza swali ya kutwaa kugeuka kuwa mwili (na kwa hivyo Utatu) katika Agano Jipya.³⁰² Yeye huokoa mtazamo jadi iliyo katika Injili ya Yohana tu, akisema kwamba Paulo na waandishi wengine wa Agano Jipya. Yeye huokoa mtazamo jadi iliyo katika Injili ya Yohana tu, akisema kwamba Paulo na waandishi wengine wa Agano Jipya hufikiri tu juu ya ubora wa kabla-kuwepo wa Kristo na kwa hiyo si wa Mwana kabla-kuwepo. Mchango muhimu katika mjadala huo, ulifanywa na James Mackey mwaka wa 1983.³⁰³ Katika sura iliyo na jina, “Tatizo la kabla-kuwepo wa Mwana,” anaanza kwa kushangaa jinsi kitu kinaweza kuishi kabla-kuwepo yenyewe, “nini hasa, kulingana na hili neno [kabla-kuwepo] kile kingine kipo na kwa njia gani ipo”. Anasema kuwa ni maswali haya yanayosababisha matatizo ya kushiriki katika jadi ya kutwaa utu na teolojia ya Utatu. Anaona kwamba waelezi ni “mara nyingi wanaoathiri bila fahamu katika shughuli ya kazi yao ya kitaalamu ya

³⁰¹ Cp.Linganisha butwaa la A.T. Hanson alipowaza katika seminari kuhusu tafsiri halisi ya Yesu: “Katika malezi yangu ya kiteolojia nilielimishwa vizuri katika jadi ya kugeuka mwili kwa Mungu katika Yesu Kristo. Ninakumbuka kuambiwa kwamba Neno la Mungu alipodhani asili ya binadamu, alidhani ubinadamu bila nafsi; kwamba Yesu Kristo hakuwa na utu wa binadamu, kwamba Mungu akawa mtu katika Kristo Yesu, lakini ya kwamba hakuwa mtu... Fikira mbili zimenishawishi kuwa jadi hii ya Ukristo ni ya ajabu” (*Grace and Truth: A Study in the Doctrine of the Incarnation*, London: SPCK,1975,1).

Tatizo hilo linadhihirishwa na Oliver Quick, *Doctrines of the Creed* (Nisbet,1938): “Tukithibitisha ya kwamba Yesu alikuwa binadamu, tunasukumwa aidha ndani ya uanzilishi wa miujiza wa utu mara mbili katika kugeuka kuwa mwili wa Mwana wa Mungu, au ndani ya Ukristo wa Uprotestanti ambayo tumegundua kuwa duni.Tukikana kuwa Yesu alikuwa binadamu, tunakana kidokezo cha ukamilifu wa uanadamu wake na kusimamia na hatia Uapollo(*Apollinarianism*). Daktari Raven anayenywa (Tazama kitabu chake, *Apollinarianism*) kwamba wengi wa wale ambao jana ya Katoliki imewaheshimu kama madaktari wa uhalisi walikuwa kwa kweli Waapollo, ingawa walihukumu Uapollo” (178). Cp.Linganisha uchunguzi wa Norman Pittenger ya kwamba “Chalcedon alishindwa kuzuia Uapollo iliyogeuzwa kuwa ya uhalisi wa “miaka ya kati” (*The Word Incarnate*,102).

³⁰² *Christology in the Making*.

³⁰³ *The Christian Experience of God as Trinity* (London: SCM Press, 1983).

mawazo ya sharti kabisa (bila kupima).”³⁰⁴

Jaribio la Mackey kutafuta asili halisi ya neon “kabla-kuwepo” katika uhusiano na Kristo, na kubainisha kuwa wasomi mara kwa mara huisoma kwa vifungu ambayo kwa jadi unafaa kuwa nayo. Katika vitabu vya Injili, anabisha kuwa, neon Mwana wa Mungu kwa hakika hakitakuwa na maana “Mwana kabla-kuwepo,” lakini unafaa sana uteule wa Agano la Kale wa Mfalme wa Israeli kama Mwana wa Mungu. “Njia mantiki inayofaa ya kabla-kuwepo,” anasisitiza, “ni wa mateso mengi.”³⁰⁵ Kwanza, vyanzo vya kiyahudi vilivyoishi vinaelekeza kwa “aina ya wazo la kabla-kuwepo kwa Masiya hadi mpaka wa jina lake. Kwa mfano, kiini na asili, kabla utunzi wa mwanga siku ya kwanza ya uumbaji....Kwa fikira ya Kiyahudi kabla-kuwepo mbinguni kwa Masiya hauathiri ubinadamu wake.”³⁰⁶

Zaidi ya hayo, aina hii ya kabla-kuwepo ni:

sehemu ya mfano wa ufunuo katika mawazo ya binadamu ambayo Mungu, ambaye hajafungwa na wakati wetu, aliyekuwa nayo katika akili yake milele na kabla kitu chochote kiumbwe, yule ambaye anaumuhimu kwa kuwepo kwa vitu vyote, ambaye ataleta ukamilifu, na kutoka kwake (kwake yeye, kutoka kwake) vitu vyote basi vingesemekana kuumbwa.³⁰⁷

Mackey anaendelea kuisitiza hatua yake Yohana anavyomweleza Yesu kama *monogenes* (wa kipekee) hauna ashiria wa *unigenitus* (pekee) wa Vulgate, kama kwamba Yesu alikuwa Mwana wa kipekee. Ina maana kuwa yeye alikuwa wa kipekee kati ya wengine. Anatumia maneno ya Schillebeeckx, ambayae anasema kuwa kivumishi cha Yohana hakitupi “msingi wowote katika teolojia ya Johannine kwa usomi wa baadaye wa teolojia wa maandamano ya Mwana kutoka Baba ndani ya Utatu, *per modum generationis* (kwa kuzaliwa).”³⁰⁸ Kwa ushahidi huu, uthibitisho unalindwa kwa utafiti kwamba Yohana haendi nje ya wazo wa “Ukristo” wa Luka, tangu Uana kwa Yohana hautajwi popote, licha ya maoni ya waandhishi wa hapo awali, Uana wa milele.

Zaidi ya hayo, Mackey anasema kuwa hakuna haja ya kusoma “Neno” la Yohana mbali na wanavyoona “hekima” ya Wayahudi kama ilivyofikiriwa, kama mpango wa Mungu kabla-kuwepo. “Neno hili, kama hekima [methali 8:30] alikuwa na Mungu mwanzoni na kutoka huo [si yeye] vitu vyote vilijengwa.”³⁰⁹ Mara ingine tena Schillebeeckx anamuunga mkono. “Injili ya Yohana inazungumza kuhusu Yesu wa Nazareth alipoonekana duniani.”³¹⁰ Mackey anaongeza kuwa “kushuka” (Yesu “alikuja chini kutoka mbinguni”) lugha katika Yohana hauna uhusiano na uaminifu wa kabla-kuwepo. Bali, Yohana inaamana kuwa Yesu kwa maelezo wa ufunuo ya asili ya Mungu. Hata madai ya Yesu kwamba “kabla Abrahamu hajazaliwa, nilikuwepo” hailekei kufahamisha maisha kabla kuishi, lakini kwa umuhimu wake kamili kwa mpango tukufu, hasa ofisini mwake Masiya anavyoona Abrahamu. Mackey anamaliza kwa msembo:

Kama tunaheshima hata kidogo iliyobaki kwa ile ambayo tunayoitaja kama nia ya maandishi, hatuwezi kujifanya kuwa maandishi hayatapatii habari kuhusu “mtu” wa pili mtukufu au

³⁰⁴ Ibid., 51.

³⁰⁵ Ibid., 56

³⁰⁶ Ibid., 56, 57.

³⁰⁷ Ibid., 57.

³⁰⁸ Ibid., 59.

³⁰⁹ Ibid.

³¹⁰ Ibid.

wazo tofauti dhidi ya Mungu pamoja na Baba na Yesu wa kihistoria kabla kuzaliwa kwa Yesu, au “kabla ujenzi wa dunia.”³¹¹

Onyo kali ni kwamba mafundisho ya jadi ya Utatu haupatikani katika Bibilia.

John A.T. Robinson

Swala hili la zamani kuhusu kabla-kuwepo, na kwa ubinafsi, swali kwamba Yohana anatarajia kuelewa kwamba Yesu alikuwa mbinafsi mtukufu kabla-kuwepo, alijadiliwa vikali kwa gazeti ya *Teolojia*.³¹² Mazungumzo haya yalianza na kubadilishana mabarua kati ya James Dunn na Maurice Wiles. Umuhimu wa swala hili linatokana na mazungumzo yaliyotamkwa na Robinson.³¹³

Robinson anaanza kwa mtazamo kwamba Wiles na Dunn wanakubali kuwa katika Agano Jipya, ni Yohana peke yake anamweleza Yesu kama aliyeishi kabla-kuwepo kwa binadamu. Wiles anafikiria jambo hili kuwa utunzi wa Ukristo wa maafa, ukidunisha ubinadamu wa Yesu, na hivyo basi kusisitiza madai ya “docetism.” Robinson, ingawa, anasema kuwa nyaraka yake Yohana anatoa maoni kwamba Yesu ni zaidi ya binadamu – “kujakwa mwili.” Hii inamfanya Robinson kutoelewana na Wiles pamoja na Dunn kwamba kwa Injili ya Yohana anatumaanisha tuelewe kwamba Yesu alikuwa mtukufu kabla-kuwepo. Mazungumzo haya yanarejelea shida iliyotambuliwa na Paulo wa Samosata na baadaye na Anabaptist wengine haswa wanaotoka Poland.

Robinson anauliza swali kama kwamba tunasoma Yohana kama ilivyokuwa nia yake. Je, kweli pengine tunamwangalia Yohana kwa miwani na utenzi wa waandishi wa hapo awali katika Ukristo? Matumizi ya onyo la Dunn linamfanya Robinson kuelewa maneno ya Yohana kama vile wasomi wa kwanza wangeelewa. Robinson anamkumbusha Dunn kwamba aliitikia kwamba kwake Paulo, Yesu alikuwa maelezo wa hekima ya Mungu, “mtu aligeuka kuwa hekima.”³¹⁴ Dunn alikubali kwamba hata Yohana 1:14 hauna ngao ya jadi ya mafundisho ya kugeuka mwili. Kwa hakika, inaonyesha “mabadiliko kutoka ukosefu wa ubinafsi wa utu kwa mtu.”³¹⁵ Kwa hiyo Robinson anakubaliana nayo. Dunn na Robinson wanakubaliana kuwa “neon” la Yohana ni matamshi ya Mungu kwa nafsi, si mtu mtakatifu, tofauti kutoka kwa Mungu. Ni wakati wa mimba ya Yesu pekee ambapo “neon” linakuwa la kibinafsi kama tofauti na kufanywa kuwa mtu.

Robinson alishindwa kukubaliana na Dunn, ingawa, kwamba “kabla-kuwepo neon kama mtu na Mungu unasisitizwa kote [kwa Injili].”³¹⁶ Robinson anatusihi tushikilie kuelewa kwetu kwa neon kabla-kuwepo, hata katika Yohana, kwa “matamshi ya Mungu,” “nguvu na kusudi lake.” Swala hili kwa urahisi ni: Tunafaa kuona mabadiliko kutoka kuelewa kwa “neon” la Yohana kama maelezo ya Mungu kwa wazo kwamba inamaanisha mtu mtakatifu kabla-kuwepo, *nje ya Agano Jipya mbalimbali*. Yohana hafai kuwajibika kwa mabadiliko. Mabadiliko ulimtendelea Yohana wakati alipodhihinishwa na tabia ya Gnostic wa hapo awali, ambayo iliacha alama kwa waandishi wa awali wa teolojia. Hii haifanyiki kwa Yohana. Robinson anaamini kwamba “neon,” ambayo

³¹¹ Ibid., 64.

³¹² 85 (Mar. and Sep. 1982). Kwa matumizi mazuri wa muhtasari wa mjadiliano wa kisasa, ona Klaas Runia, *The Present-Day Christological Debate*.

³¹³ “Dunn on John,” *Theology* 85 (Sept 1982): 332-338.

³¹⁴ *Christology in the Making*, 212.

³¹⁵ Ibid., 243.

³¹⁶ Ibid., 250

ilikuwa *theos* (“Mungu,” Yohana 1:1), alikuwa mwelezi wa mpango wa Mungu, kusudi lake na tabia. Kwamba “neni” ilikuwa kamilifu kwa binadamu ilipokuwa mwili (Yohana 1:14). Yesu basi ni kile ambacho neon *kilikuwa*. Hawezi tambuliwa moja kwa moja na neon kabla-kuwepo, kama yeye mwenyewe aliishi kabla-kuwepo. Tofauti ni ndogo lakini unaleta madhara kwa maendeleo wa Ukristo. Hivyo basi haikuwa neon ni mtu, fumbo la imani, ambaye alidhani asili ya binadamu kama vile yake, lakini neon lilikuwa “lilikuwa bila fumbo la imani,” bila ubinafsi, ingawa ulieleza Mungu kikamilifu, hadi ukawa mtu binafsi kihistoria katika Yesu. Yesu, hivyo basi, ni binadamu mkamilifu “exegeting” Mungu mmoja wa uanadamu (Yohana 1:18).

Kifungu hiki cha Yohana kina faida kubwa ya kuepuka madhara ya kuweka mbele picha ya Kristo, pamoja na ubaguzi kati ya Yohana na vitabu vingine vya Injili, ambavyo havijui chochote kuhusu Kristo kabla-kuwepo. Inaendelea kuruhusu “neon” kubeba Agano la Kale, kwa maana ya Kiyahudi ya, “lengo” au “mpango,” au pia “ahadi.” Basi Yesu anaeza kuonekana kutimiza ahadi la kale kwake Abrahamu ambayo ni ya muhimu kwake Mathayo na Luka. Yesu ni ubunifu wa Mungu, mpango wa wokovu unaoelezwa katika binadamu. “Uungu” wa Yesu haupungui tangu “mtu ambaye amemwona amemwona Baba” (Yohana 14:9). Lakini hii ni “uungu” kwa hisia ya maana nyingine zaidi ya kama inavyoelezwa katika utatu halisi. Kwa uungu ni vitendo vya Mungu vikifanya kazi katika na kupitia binadamu aliyejitolea kikamilifu. Yesu, katika kifungu hiki, si Mungu kwa hisia ya Utatu, bali kwa binadamu anayeeleza Mungu kikamilifu, Kikali wake wa kupatanisha dunia. Jambo la kupendeza ambalo Mungu ametenda linaonekana kama utukuzi wa binadamu mtiifu ambaye alijaribiwa kama sisi. Picha hii inaainisha maoni ya kiinjili ya Yesu. Zaidi ya yote, inaepuka kuonyesha Yesu kama binadamu asiyekamilifu ambaye tangu milele alikuwa Mungu mwenyewe. Ukweli unabuka kwamba yesu alikuwa “katika namna ya Mungu” (Wafilipo 2:6), si kwamba *alikuwa* Mungu. “Mungu alikuwa *ndani* ya Kristo” (2 Wakorintho 5:19), lakini Kristo hakuwa Mungu.

Pamoja na uchunguzi wake mkubwa wa Maandiko Robinson anaelekeza njia kwa picha ya kibibilia ya Yesu kama mfano kamili wa Baba yake, kristo ambaye kutii na kujitolea kwake kikamilifu kinamfanya kuwa kweli, “Mwana wa Mungu.” Inasikitisha kwamba Robinson hakuthibitisha imani katika kuzaliwa kwa miujiza wa Yesu ambayo Vitabu vya Mathayo na Luka wanaeleza kuwa Mungu mmoja alileta kwa uhai Mkuu wa uumbaji mpya, Masiya bila dhambi, Mwana wa Mungu.

Frances Young

Ni rahisi kuwahurumia wasomi wa kibibilia waliokubaliana na *Myth of God Incarnate*.³¹⁷ Ilionekana kana kwamba nguzo za Ukristo zilikuwa zikitikisika. Baadhi ya wale walio na mtazamo mpya wa Yesu hawakuamini mengi kuhusu Bibilia. John Stott, anayewakilisha imani ya Injili, anarudia sababu halisi za kuamini Uungu kamili wa Yesu. Anasisitiza kwamba Yesu alikuwa mtu halisi, lakini hatuambii ni kwa jinsi gani, hasa katika mtazamo wa Leo Tome (uliodhinishwa na Kifungu cha Anglican cha pili, 1563) kwamba Mwana wa milele “alichukua hali ya utu”. Wengi walihisi kuwa kiumbe ambaye ni “binadamu” bila ya kuwa “binadamu” ana utu ya kadiri ya chini kuliko “mtu Masiya Yesu” wa imani ya Paulo (1 Tim 2:5). Stott anaruzuku kwamba Yesu hakutangazatangaza bila fumbo kwamba alikuwa Mungu. Hata hivyo, “uhamisho wa vyeo vya Mungu na

³¹⁷ Ed. John Hick (London: SCM Press, 1977)

maandiko ya Mungu kutoka kwa Bwana hadi Yesu inadokeza kisichoweza kuepuka. Ni kubainisha Yesu kama Mungu.”³¹⁸ Zaidi ya hayo, Yesu anaabudiwa, nah ii ni thibitisho kuwa yeye ni Mungu.

Frances Young alikuwa miongoni mwa wachangiaji wa *Myth of God Incarnate*. Ni muafaka kuongeza katika sura hii muhtasari wa insha yake ya ajabu, “Wingu la Mashahidi,” kwa sababu inawakilisha hisia za wengi ambao walimtetea Yesu wa Bibilia bila kutia mkono kwa Ukristo halisi. Profesa Young anaanika udhaifu wa maoni ya jadi kuhusu Yesu. Yeye analalamika kwamba utajiri wa ufahamu wa Ukristo wa Agano Jipya imekuwa dhahiri na kumkiri Yesu kama Mwana wa Mungu. Kuna njia mpya ya kusoma ushahidi wa Agano Jipya kwa Kristo: “Tukiepuka kusoma kwa Agano Jipya kwa kutumia miwani iliyo na rangi ya mafundisho ya baadaye, tunapata picha ya Ukristo inayojitokeza - au tuseme picha - tofauti kabisa na uhalisi.”³¹⁹ “[Yesu] alikuwa ahadi halisi ya Mungu iliyoletwa kwa matumizi. Ukristo huo, ningependa kutoa ushauri, uwakilishe Ukristo wa Agano Jipya ulio bora kuliko wazo la kubadilika kuwa mwili, na ilikuwa kwa kweli mbegu ya mawazo mengi ya Ukristo kama vile Agano la Kale linaonekana kamili katika Kristo.”³²⁰

Frances young anatengeneza picha ya kibibilia ya Yesu kufanya kazi ya Mungu bila ya kuwa Mungu: “Paulo hamwiti [Yesu] Mungu, wala hamhusishi mahali popote na Mungu. Ni kweli anafanya kazi ya Mungu, kwa uhakika yeye ni wakala wa Mungu, ambaye anatenda kwa sababu ya mpango wa Mungu.”³²¹

Mtazamo wazi wa mwandishi kuhusu tofauti kwenye Bibilia kati ya Mungu na Yesu inamwezesha kuona makosa ya akina baba. Hajashawishiwa kuwa katika maendeleo ya Ukristo “maswali yaliulizwa kwa njia sawa, au ufumbuzi kupatikana.”³²² Uhalisi ambao uliojitokeza hatimaye uliungwa mkono na hoja isiyotosha ya uharibifu wa (exegesis).³²³ Kuelewa Yesu kama Mungu aliyefanyika mwili ilionyeshwa na mazingira ya falsafa iliyopo. Hakika kuna mengi yanayofanana kati ya “*neo-Platonism’s triadic cosmology*” na Utatu.

Upinzani wa Frances unamanufaa zaidi ya wazo kwamba ni Mungu mwenyewe tu anayeweza kutupatia wokovu na kwa hivyo, Yesu ni Mungu. Tatizo na maoni halisi ni kwamba Mungu hawezi kupitia mateso, majaribu, au kifo. Shughuli ya Athanasius ya majaribu ya yesu, inaanguka katika ukali na husababisha hitimisho yake isiyoeleweka kwamba Yesu “aliteswa bila kuteseka:” “maoni ya kuwa wakati ‘mwili’ au ‘mtu Yesu’ aliteswa msalabani, aliteseka kwa huruma kwa sababu ilikuwa ‘mwili wake’ au ‘mtu wake,’ hata kama kwa asili yake yeye hakuwa na uwezekano wa kuteseka.”³²⁴

Insha hii inatoa kwa lazima maoni ya starehe kwamba mababa walipeleka picha ya Kristo ya Agano Jipya kwa uaminifu. Badala yake uthabiti wao ulisababisha “vichochoro vipofu vya kutoelewa na vya ukali.”³²⁵

³¹⁸ *The Authentic Jesus* (Marshall, Morgan and Scott, 1985), 33.

³¹⁹ *The Myth of God Incarnate*, 14.

³²⁰ *Ibid.*, 19.

³²¹ *Ibid.*, 21.

³²² *Ibid.*, 23.

³²³ *Ibid.*

³²⁴ *Ibid.*, 27.

³²⁵ *Ibid.*, 29.

George Carey

George Carey, ambaye hatimaye alikuwa Askofu Mkuu wa Canterbury, aliinuka kutetea mafundisho ya asili ya maandishi jadi ya kufanyika mwili katika *God Incarnate: Meeting the Contemporary Challenges to a Classic Christian Doctrine*. Nguvu yake ya insha ipo katika maandamano yake yanayoeleweka dhidi ya tabia ya maandishi wa *Myth of God Incarnate* kumtafsiri Yesu upya kwa maslahi ya kumfanya azidi kukubaliwa na wanasayansi wa kisasa. Carey anasumbuka na kukataa kwa kuzaliwa kwa Kristo kutoka kwa bikira, kutokuwa na dhambi kwake, kufufuka kwake kama lengo wa ukweli wa historia. Wachangiaji wa *hadithi* walidhoofisha nguvu ya vikwazo vyao vya Kibibilia kwa kufanyika kuwa mwili halisi. Maoni yao ya kusikitisha juu ya miujiza, hasa ufufuo, bila kuepushwa kutoka kwa wapinzani wao wa Utatu Mtakatifu. “Walio na huru” mara nyingi huinua bendera nyekundu kwa wale wanaohifadhi desturi ya kale. Aliye ‘huria’ anaweza kuchunguza Bibilia bila upendeleo wowote, kwani hana nia ya kutetea mfumo wa jadi kama mhafidhina.

Inawezekana kuamini Carey anavyoita “Dhamana mahsusi ya kipekee na Mungu,”³²⁶ bila kukubali imani ya kwamba alikuwa Mungu. Hata Carey anasitasita kumuita Mungu wazi wazi. Anapendelea maelezo ya kumuita “aina ya Mungu.”³²⁷ Njia hiyo inafungua ufahamu wa Yesu kati ya shupavu ya baadhi ya wafuasi wa *Myth* na Utatu Mtakatifu. Kama Ukristo wa sasa ungethibitisha miujiza wa picha ya Kibibilia ya Yesu, na kama Carey angeliangalia upya, udhaifu wa lugha ya “kutumwa” kama ushahidi wa kabla-kuwepo, Ukristo wa Maandiko zaidi unaweza kujitokeza. Yesu bila shaka, lazima atangazwe kufuatia mitume waliotangulia, kama njia ya pekee ya wokovu. Lakini uwezekano wa Wakristo “kujazwa na utimilifu wote wa Mungu” (Waefeso 3:19) lazima usawazishe mkazo wa uhalisi juu ya “utimilifu wa Uungu” (Wakolosai 1:19, 2:9) katika Yesu kama ushahidi kwamba alikuwa Mungu. Udhuru wa Carey mara nyingi si dhabiti. Wapi msaada wa madai ya imani ya kwamba alikuwa “amezaliwa kabla ya wote,” ambayo Carey anaonekana kuthibitisha bila msaada wa ushahidi wa Agano Jipya? Na kwa nini ni wazi kuwa Mungu “alimtuma Mwana wake” inamaanisha ya kwamba Mwana alikuwa hai kabla ya kutungwa kwa mimba yake? Petro hana mawazo ya kabla-kuwepo akilini anaposema kwamba Mungu “aliyemlea Yesu, alimtuma” kuhubiria Israeli (Matendo 3:26). Yesu aliagizwa kuhubiri, hakutumwa kutoka kwa maisha ya awali. Inaonekana ya kwamba mamlaka wa kiwango cha ubuni walitambua udhaifu wa hoja wa neno “kutuma,” wakati wa shindikizo la kudumisha hali hiyohiyo katika Ukristo unaweza sababisha waelezaji kuyasahau hayo.

Karl-Josef Kuschel

Katika mwaka wa 1990 huko Ujerumani, kutoka kambi ya elimu ya Wanakatoliki Warumi, utafiti wa swala la kabla-kuwepo kwa awali na Utatu Mtakatifu: *Born Before All Time? (Kuzaliwa Jadi/ Kabla ya Wakati?) The Dispute over Christ's Origin (Mzozo Kuhusu Mwanzo wa Yesu)*. Karl-Josef Kuschel alichunguza mashindano ya Christologia ya Harnack, Barth na Bultmann na kisha kujiingiza katika uchambuzi wake mwenyewe wa takwimu za Agano Jipya. Yeye anauliza maswali yanayofaa: “Je, Yesu wa historia anaangaliwa kwa uzito?” na “Je, si maana thabiti ya ‘mwili’ ilikuwa usahaulifu tu katika

³²⁶ *God Incarnate: Meeting the Contemporary Challenges to a Classic Christian Doctrine* (InterVarsity Press, 1977), 7.

³²⁷ *Ibid.*, 18

Barth na Bultmann?”³²⁸ Anashangaa kama hawa wasomi wa dini, ambao ushawishi wao umekuwa kubwa, “kama walielewa Agano Jipya sawa”³²⁹ katika njia walizotumia kumtambua Yesu Kristo. Inashtua kuwa, msomi Mjerumani mwingine, Wolfgang Pannenberg, alisema, “Barth haendelezi msingi wake wa mafundisho ya Utatu Mtakatifu juu ya msingi wa ushahidi unaoonekana,” akirudia maneno ya Ernst Fuchs ya kwamba “kama hakungekuwa na maandiko ya Kibibilia, dokezo ya Barth itakuwa inafaa zaidi.”³³⁰

Profesa Kuschel anaendelea kwa kuangalia jukumu la hekima katika Bibilia ya Kiyahudi, akipata kuwa inafanana na neno la Mungu lililo na ubunifu na kwa Torati kama mwongozo uliomwongoza Mungu wakati wa uumbaji. Anasema kuwa Yesu mtu ni mfano hasa wa hii hekima iliopo na si Mwana wa milele aliyekuwapo kabla ya kuzaliwa kwake Bethlehemu. Kuschel anasisitiza kuwa katika Wafilipi 2 hakuna taarifa kuhusu Kristo kuwa sawa na Mungu. Bali Kristo ni “tofauti kubwa kwa kumlinganisha na Adamu.”³³¹ Kuschel anakubaliana na James Dunn kwamba hakuna Mwana aliwepo katika Paulo. Katika Injili ya Yohana, “Mungu si mwingine kamwe isipokuwa Baba wa Yesu Kristo.”³³² Yeye anauliza kwa nini katika utangulizi wa kitabu cha Yohana hauanzi (kama vile wengi bila ufahamu husoma), “Hapo mwanzo kulikuwa Mwana na Mwana alikuwa na Mungu na Mwana alikuwa Mungu.”³³³

Ukosoaji huu mkuu wa wanaoamini katika Utatu Mtakatifu halisi unaunga mkono kusadiki kwetu ya kuwa “historia ya Christologia ya Ukristo wa Kiyahudi...inahitaji uchunguzi wa upesi...sio tu kwa sababu ya haki ya kihistoria lakini pia kwa sababu ya kuelewa kwa Wakristo wote ulimwenguni.”³³⁴ Masomo ya dini yanayotawala Baraza la Kalkedoni “haigusii sana kuhusu maisha ya dunia na historia ya Yesu akiwa duniani.”³³⁵ 71 Hakika uhusiano kati ya Baba na Mwana ilivyopendekezwa na Baraza “haungeeleweka na Wakristo wa Kiyahudi kama Paulo na Yohana.”³³⁶ Utafiti bora wa Profesa Kuschel, wenye kibali cha Hans Kung aliyehandika utangulizi, anatuonya tuwe macho juu ya tisho ya elimu ya Utatu Mtakatifu kwa imani ya Mungu mmoja na pia nguvu zake zisilete vikwazo visivyo muhimu dhidi ya mazungumzo na Wayahudi na Waisilamu. *Born Before All Time? (Kuzaliwa Jadi/ Kabla ya Wakati?)* inaskika katika wakati wetu, inaonyesha upinzani dhidi ya maoni ‘halisi’ ya Yesu yanayoonekana kuzuia ubinadamu wake na, kwa hiyo, kuficha umasiya wake.

Karl-Heinz Ohlig

Katika mwaka wa 1999, historia nzuri juu ya shida ya imani katika Utatu Mtakatifu ilitolewa, katika nchi ya Ujerumani. Kitabu cha Karl-Heinz Ohlig *Ein Gott in drei Personen? Vom Vater Jesu zum Vater Jesu “Mysterium” der Trinitat (Mungu Mmoja katika utatu? Kutoka kwa Babake Yesu kwa “siri” ya Utatu)* inaonyesha wazi, uhusiano wa karibu sana wa Bibilia na elimu ya Utatu. Mwandishi anasema kuwa fundisho hili la kanuni kwa muda mrefu, limezuia Wayahudi na Waisilamu kukaribia Ukristo. Ohlig anaachana na mwiko wa muda mrefu. Yeye hatumii majadiliano

³²⁸ *Born Before All Time? The Dispute over Christ’s Origin*, 174.

³²⁹ Ibid.

³³⁰ Ibid., 179.

³³¹ Ibid., 251.

³³² Ibid., 276.

³³³ Ibid., 381.

³³⁴ Ibid., 394, 395

³³⁵ Ibid., 425.

³³⁶ Ibid., 409.

yasiyoeleweka ya “siri” kama maelezo kwa Utatu. Yeye anatupa maelezo ya ajabu yaliyojaa utakatifu. Yeye anaona ya kuwa maendeleo haya yaliletwa na mshurutisho wa kitamaduni wa kanisa, mwanzo mwa karne ya pili. Analaumu kupoteza kwa imani katika Mungu mmoja iliyo asili ya Kiyahudi na huonyesha hoja ya kuwa, kama Yesu hakuamini katika Utatu Mtakatifu, kwa nini wafuasi waamini? Tena hali ya imani ya Utatu haikukamilika mpaka karne ya tano, na kwa hakika haikuwepo katika karne ya pili kama imani juu ya watu watatu wa milele, ni katika wakati gani katika mageuzi yake lazima Wakristo wana wajibu kuzingatia? Ohlig anasisitiza kuwa ni haramu kihistoria na kiteolojia kufanya mafundisho ya Utatu Mtakatifu kuwa kawaida kwa Waumini:

Ikifikiriwa kulingana na masomo ya dini, Utatu ulikua kutoka kwa uungano wa Uyahudi na Ukristo, na Wayahudi wa Kiyunani, na kutoka kwa mchanganyiko wa imani ya Mungu mmoja pamoja na imani ya Wayahudi wa Kiyunani [kuamini katika Mungu mmoja]...Msomi wa dini anagundua mambo yanayoleta swali kuhusu uhalali na tafsiri. Inavyokuwa wazi kuwa Yesu mwenyewe alijua tu Mungu wa Israeli, aliyemwita Baba, na hakujua chochote kumhusu yeye mwenyewe baadaye “kufanywa kuwa Mungu,” tuna haki gani kuita mafundisho ya Utatu Mtakatifu kuwa kawaida na ya Wakristo?...Kwa vyovyote tunavyofafanua hatua mbalimbali za maendeleo ya Utatu Mtakatifu, ni wazi kwamba mafundisho haya, ambayo yakawa “imani” katika Mashariki na Magharibi, hayana msingi wa Kibibilia na hayawezi kuonekana katika Agano Jipya...Kidogo kidogo, masomo ya kidini lazima yakubali ukweli.³³⁷

Uchunguzi wa Ohlig wa kuthibitisha matokeo yaliyotokea mapema ya profesa mmoja mkuu wa historia ya mafundisho, ambaye aliandika:

Apollogists waliweka msingi kwa ajili ya upotoshaji/ufisadi wa Ukristo katika mafundisho yaliyodhihirishwa. Hasa, elimu yao ya Ukristo, iliathiri maendeleo ya baadaye. Kwa kudharau uhamisho wa dhana ya Mwana wa Mungu kwenye Kristo aliyekuwepo walisababisha tatizo la elimu ya Ukristo katika karne ya nne. Wao walisababisha mabadiliko katika hatua ya fikira juu ya elimu ya Ukristo-mbali na Kristo wa kihistoria na kuingia kwenye swala la kuwepo tangu jadi. Kwa hiyo, walitoa mtazamo wa watu kutoka kwa maisha ya kihistoria ya Yesu, na kuyaweka pasipo pa muhimu na kukuza badala yake Yesu alivyofanyika mtu. Wao walifunganisha elimu ya Ukristo kwa elimu ya ulimwengu mzima na kufunganisha na matengenezo na taratibu zake. Mafundisho ya Logos si “elimu juu ya Ukristo zaidi ya ile ya kimila. Inabaki nyuma sana ya shukrani ya kweli ya Kristo. Kulingana na mafundisho yao si Mungu tena anayejifunua katika Kristo, lakina Logos, Mungu duni, Mungu ambaye kama Mungu yu chini Mungu aliye juu (hafifu au wa chini).

Zaidi ya hayo, kuzuia mawazo ya kiuchumi - utatu na dhana ya mawazo mengi ya Uungu katika Utatu Mtakatifu (*Trias*) kunaweza kupatikana kwa Wanaojitetea [Apologists].³³⁸

³³⁷ *Ein Gott in drei Personen?* Mainz: Matthias Grünewald-Verlag, 1999, 123-125, kwa tafsiri yetu.

³³⁸ Friedrich Loofs, *Leitfaden zum Studium der Dogmengeschichte (Manual for the Study of the History of Dogma*, 1890), Halle-Saale: Max Niemeyer Verlag, 1951, part 1, sec. 18: “Christianity as a Revealed Philosophy. The Greek Apologists,” 97, translation ours.

XI. CHANGAMOTO INAYOKABILI IMANI KATIKA UTATU MTAKATIFU

“Wazo lilokua linalohusu washirika waliosawa katika Uungu ambalo hupatikana katika maelezo ya kanuni ya baadaye haliwezi kupatikana kwa wazi katika kanuni ya kanisa.”

- *Oxford Bible Companion*

Elimu ya Utatu Mtakatifu wa kisasa inakabiliwa na mabishano makali ambayo yamedhoofisha baadhi ya “ushahidi” wa kibibilia uliohifadhiwa. Wengi wanaoenda kanisani hawajui maandiko mengi kinyume cha elimu ya Utatu (kwa hakika, kama si kwa jina) kuliko vitabu ambavyo kwa njia mbalimbali vimeacha baadhi ya nguzo kuu za elimu ya Utatu wanaeleza mistari muhimu ya Utatu katika njia ya wasioamini Utatu. Mukhtasari wa ajabu wa makubaliano ya wanaoamini Utatu ulitolewa na John Wilson katika mwaka wa 1845.³³⁹ Kazi yake ina umuhimu kwa mjadala unaoendelea wa Utatu. Uchunguzi wa kiasi kikubwa sana cha maandishi ya wataalamu, unaonyesha wasioamini maelezo ya elimu ya utatu na wanaoamini elimu ya Utatu juu ya mistari inayodhaniwa na wengi kuwa inashikilia Utatu. Maandiko ya masomo ya dini ya kisasa pamoja na ya karne ya kumi na tisa hutoa ushahidi wa makubaliano sawa. Sura hii inachunguza baadhi ya alama ya hoja iliyotolewa kama “ushahidi” wa Utatu Mtakatiifu katika maandiko maaarufu kwenye Bibilia. Inaonekana kwamba idadi kubwa ya wanaoamini katika Utatu Mtakatifu haitegemei tena hoja hizi kama msaada na mtazamo halisi wa Uungu.

Hali ya wingi wa Elohim

Shirika la Wayahudi kwa Ajili ya Yesu na Makundi mengine ya wenye imani ya Injili wanaendelea kupata Utatu wa Mungu katika maandiko ya Kihebrania. Hali ya wingi wa Mungu katika neno la Kiyunani, Elohim, hata hivyo, haitoi dalili ya kuonyesha Utatu. Ni kama kupotosha kwa majadiliano ya Elohim kama neno “lililokatika hali ya wingi, ilhali liko katika hali ya umoja” kama kusema kwamba Echad, “Moja,” inadokeza Uungu kwa wingi. Mtu hawezi kutoa hoja ya kuthibitisha Utatu Mtakatifu kutokana na kweli kwamba Echad inaweza kugeuza kidogo jina kama “kishada” au “kundi” na kwa hiyo inaweza kutufanya tufikirie ya kwamba Mungu ni mwenye sehemu zaidi ya moja. Echad ni “mmoja” katika Kihebrania. “Yahweh ni Bwana mmoja,” hivyo ndivyo imani ya Israeli inaonekana (Kumbukumbu 6;4). Echad inaonekana kama chombo cha ugeuzi kwa Ibrahimu (Ezekieli 33:24, Isa 51:2), na inawezekana wakati mwingine kuwa cha “kipekee” (Ezekieli 7;5). Maana yake ya kawaida ni “moja na sio mbili” (Mhubiri 4:8). Hakuna kitu chochote katika neno “Yahweh” ambacho kinapendekeza wingi, hasa kwa vile neno hutokea kwa umoja katika hali ya utendaji na hali ya jina katika yote maelfu zake mbalimbali (kufikia 5500) ya matukio. Kama viwakilishi pekee, kila wakati vya kutoa maana fulani ya Mungu mmoja haviwezi kuwafanya watu waamini kuwa Mungu ni mmoja, basi hakuna jinsi lugha itawafanya waamini hivi. Kitu kisicho kawaida mara kwa mara ni kuwa bwana wa Yusufu anatajwa kwa kutumia jina la wingi mara kadhaa (Mwanzo 39:2, 3, 7, 8, 19, 20). Je, mtu yeyote atakuwa na ubishi kwamba “bwana wa Yusufu [wingi katika Kihebrania] alimchukua [umoja katika kitendo] yeye” imetafsiriwa vilivyo? Abrahamu ndiye “mabwana” (wingi katika Kihebrania) wa mtumishi wake (Mwanzo 24:9, 10). Je, kuna wingi katika Abrahamu? Hakuna mmoja angeweza kubadilisha tafsiri ya kifungu kingine katika Mwanzo: “Mtu Yule aliye Bwana wa nchi alisema nasi kwa maneno makali”. Lakini ingawa kitenzi kiko katika hali ya umoja, hali

³³⁹ Boston: Munroe & Co.

ya jina iko kwa hali ya wingi, “mabwana wa nchi” (Mwanzo 42:30).³⁴⁰ Katika mifano hii tuko na wingi katika Abrahamu, Potifa na Yusufu kama inavyodhaniwa kupatikana katika *Elohim* wakati inahusu Mungu Mkuu. Mambo haya yanasababisha uchunguzi wa mwandishi katika Encyclopedia ya Dini na Maadili: “Maelezo kinaganaga ya fitina ya namna ya kidini yanayoeleza mafunzo ya Utatu Mtakatifu katika wingi “*Elohim*.”³⁴¹ Maandishi kumhusu Mungu kwa kazi hiyo yanamalizia kwa kusema ifuatavyo: “Katika Agano la Kale hakuna ishara yoyote ya kuonyesha nafsi tofauti katika Uungu; ni makosa kupata aidha mafundisho ya kudumu maisha au ya Utatu Mtakatifu katika kurasa zake.”³⁴² Ufafanuzi wa *elohim* (“Mungu”) utokao katika kamusi dhahiri ya Biblia yanaeda kinyume na wazo kwamba Mungu ni “watu watatu”: “Ingawa katika hali ya wingi, *elohim* inaweza kutumiwa pia katika hali ya umoja, hali inayoleta maana ya Mungu mmoja Mtukufu Mwenyezi... Kuna Mungu mmoja tu mkuu na Yeye ni mtu.”³⁴³

Mungu Ni Mmoja

Kuzingatia matumizi ya “moja” ya tarakimu katika uhusiano na Mungu unatupa mwangaza. Hakuna mtu yeyote aonaye ugumu kuelewa kauli zifuatazo. Kulingana na Ezekieli, “Abrahamu alikuwa mmoja [Kihebrania - *echad*, Kigiriki - *heis*]” (Eze 33:24). NIV inatafsiri ukweli huu kwa Kiingereza wazi: “Abrahamu alikuwa mtu mmoja tu.” Yesu alitumia neoni “moja” kwa njia sawa na ile ya kumaanisha binafsi: “Usiitwe Mwalimu, maana [*heis*] mwalimu wenu ni mmoja, na nyinyi nyote ni ndugu. Na wala kumuita mtu yeyote juu ya nchi baba yako, kwa sababu [*heis*] Baba yenu ni mmoja, ambaye yuko mbinguni. Na wala kuitwa viongozi, kwa maana [*heis*] Kiongozi wenu ni mmoja, Kristo” (Mathayo 23:8-10). Katika kila kesi “mmoja” ina maana ya mtu mmoja. Kwa Paulo, Kristo ni “mtu mmoja” (*heis*): “[Mungu] hakusema, 'na wazawa wake, 'yaani wengi, lakini badala ya mmoja, na uzao wako, 'kwamba ni Kristo” (Wagalatia 3:16). Mistari michache baadaye lugha sawia inatumika kwa Mungu. Paulo anasema: “Basi aliye mjumbe si kwa ajili ya chama kimoja tu [hasa 'si ya mtu mmoja,' *heis*]. Lakini Mungu ni mmoja [*heis*]” (Wagalatia 3:20). Maana yake ni kwamba Mungu ni “nafsi moja” au “mtu mmoja.” Yote hii ni thabiti na ushahidi wa kufanana katika Maandiko Mungu Mmoja ni Baba wa kuteua umoja wa pamoja: “nyinyi ni kitu kimoja katika Kristo” (Wagalatia 3:28). Maana hii ni muafaka kabisa katika kesi ya Mungu ambaye daima anaelezwa kwa kutumia viwakilishi katika hali ya umoja na sawa pamoja na Baba, ambaye ni wazi kuwa ni mtu mmoja.

Ukweli huu unazua tatizo kwa waumini wa Utatu Mtakatifu. Baadhi yao wamekuwa wanaendeshwa kwa maoni yaliokithiri na kudumisha kwamba neno “Baba” katika Agano Jipya halitumiki kuleta maana ya mtu mmoja wa Utatu pekee, bali nafsi zote tatu, “Baba, Mwana na Roho Mtakatifu”:

Wakati mwingine “Baba” limetumika si kwa umoja ambao ni tofauti kutoka kwa Mwana na Roho Mtakatifu - ni Mtu tofauti katika Uungu - lakini Mungu mwenyewe. Hebu tutoe baadhi ya mifano ya hili ... [Paulo anasema kwamba] yupo Mungu mmoja tu ambaye kuwepo halisi, naye ndiye ambaye Wakristo humuabudu. Hivyo yeye anaandika, “Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, Baba” (1 Wakorintho 8:06). Hapa neno “Baba” ni sawa na maneno “Mungu mmoja.” Paulo anasema kwamba kuna

³⁴⁰ Tazama pia Mwanzo 42:33: “Mtu aliye “mabwana” wa nchi.”

³⁴¹ W. Fulton, “Utatu,” katika kamusi ya Dini na Maadili, 12:458.

³⁴² W. T. Davison, “Mungu (Bibilia na Ukristo),” katika kamusi ya Dini na Maadili, 6:252-269.

³⁴³ (InterVarsity Press, 1980), 571, kutilia mkazo.

Mungu mmoja tu, na hafikirii mawazo ya Watu walio katika Uungu. Ni kwa maana hii ndivyo anatumia neno "Baba," kama alivyolitumia katika Waefeso 4:06, ambapo anaandika "Mungu mmoja na Baba wa wote."³⁴⁴

Mwandishi anapambana na ufafanuzi wa Paulo waziwazi wa Mungu kama "Mungu mmoja, Baba." Nguvu za kauli ya Olyott mwenye imani kwamba Mungu yupo katika Utatu Mtakatifu unamlazimisha kufikiria kwamba "Baba" hasa maana yake ni watu watatu. Wazo hili ni la dhana tu. Mwandishi hawezi kujiruhusu mwenyewe kufikiri kuwa Paulo hakuamini katika Utatu Mtakatifu.

Je, Yesu ni "Mwendawazimu, Mbaya au Mungu?"

Kwa usawa, Yesu anasema, “Nilikuja kutoka kwa Baba” (Yohana 16:28). Brown anatuonya kwamba “kutoka' [ek] haiwezi kutafsiriwa kiteolojia kwa marejeo ya uhusiano wa ndani wa uaminifu wa Utatu wa Baba na Mwana ('kutoka kwa Baba).” Tamko hili halimaanishi kile “ambacho kingeitwa kwa teolojia wa baadaye mafuatano ya Mwana.”⁴¹⁴ Zaidi ya hayo, Brown anonyesha kuwa katika Yohana 8:47 tamko “kutoka Mungu” (*ek tou theou*) inatumika “ kueleza mwaminifu wa kawaida: 'mtu wa Mungu.”⁴¹⁵ Lugha inayotumika kwa Yesu unatumika kwa Wakristo. Kwa hivyo pia katika Yohana 17:8, “Nilikuja kutoka kwako” “inaonyesha ujumbe wa Mwana bali sio mafuatano wa uaminifu wa Utatu wa kindani.”⁴¹⁶ Tunaweza kuongeza tamshi “kutumwa” ambayo wakati mwingine unatumika kusaidia kabla-kuwepo milele wa Mwana ambao hautasikia uzani/uzito unaowekelewa juu yake. Maneno haya pia yanatumika na waaminifu, ambao pia “wametumwa,” “kama vile” Yesu alivyotumwa (Yohana 17:18; 20:21).

Ijapokuwa ushahidi huu wazi, mafafanuzi yameendelea kukisoma vibaya nia ya Yohana dhidi ya kuiendeleza teolojia ya Nicea. Plummer anasema kwa sharti, lakini bila elezo kutoka kwa maandishi, “Nilitoka kutoka' ni pamoja na wakati wa milele wa Mwana.”⁴¹⁷ Hii inaonekana kuwa mfano wa kusoma Yohana kutokana na jukwaa la baada ya Bibilia, badala ya kukubali kuwa Yohana hakuwa na “mguu mmoja katika nchi ya falsafa ya kigiriki na teolojia ya Nicene, kama anavyoonyeshwa mara nyingi.”⁴¹⁸

Wanaojiita Mababa wa Kanisa wa Karne za pili na tatu walibadilisha lugha ya Bibilia kwa kusoma maana ya kifalsafa katika maneno ya kibibilia badala ya kuruhusu

⁴¹² Edward Schillebeeckx, *Christ* (London: SCM Press, 1980), 875, fn. 57.

⁴¹³ *The Gospel of John, Anchor Bible* (New York: Doubleday & Co., Inc., 1966), 357.

⁴¹⁴ *Ibid.*, 274.

⁴¹⁵ *Ibid.*, 725.

⁴¹⁶ *Ibid.*, 744.

⁴¹⁷ *Gospel of John, Cambridge Bible for Schools and Colleges* (Cambridge University Press, 1882), 296.

⁴¹⁸ J. A. T. Robinson, *Twelve More New Testament Studies*, 178.

maandishi matakatifu kuwaongelesha ndani ya asili ya Ebrania kimasiya. Matokeo ulikuwa ujenzi upya wa mtu wa Yesu ambayo iligeuza kuwa katika hali ya usahaulifu, kinyume na matamshi ya Luka kuwa Yesu ni kiumbe kipya kutokana na utunzi wa mimba ya Maria: “Roho mtakatifu [*pneuma hagion*] atakuja kwako wewe [Maria] na nguvu ya aliye juu kabisa itakupa ngao, na kwa sababu hii kile ambacho ni takatifu kitaitwa Mwana wa Mungu” (Luka 1:35). Huu ni Uwana uliotengenezwa kwa historia, na sio milele. Iitimiza kamili ngao kuu ya maandishi katika 2 Samueli 7:14, ile ahadi kwake Daudi kwamba Mungu, kwa siku zijazo, alikuwa Baba wa mzao wake. Uwana wa Masiya umeshikiliwa kwa nguvu katika mienendo ya kihistoria wakati wa 3 BC. Uzazi wake ulitokea wakati Mungu alileta Mwana wake katika uhai (Matendo 13:33, akiigiza Zab. 2:7).⁴¹⁹

Matokeo ya kutosoma vyema kwa lugha ya Bibilia kwa Baba ulikuwa uumbaji wa Yesu anayeamini Utatu na ni sawa na “mwili” na yule Mungu mmoja. Ijapokuwa ni wazi katika Injili ya Yohana kuwa :

Yesu anakataa dai la kua Mungu (Yohana 10:33) au kwa njia lolote kunyang'anya kikao cha Baba.... Yesu ako tayari kutupilia mbali mashtaka kwamba kwa kumuita Mungu baba yake anadai kuwa yeye ni sawa na Mungu (Yohana 5:18) na kukubali yale ya kuwa yeye ni Mwana wa Mungu (10:36), huku akikana vikali ukufuru wa kuwa Mungu au naibu wake.⁴²⁰

Jacob Jervell anakubali: “Yesu si Mungu bali mjumbe wake na, hivi basi, kwa njia yote anatenda kwa niaba ya Mungu kwamba anasimama kwa mahali pa Mungu mbele ya dunia. Injili inasema wazi kuwa Mungu na Yesu hawafai kueleweka kama watu sawa/wanaofana, kama vila katika 14:28, 'Baba ni mkubwa kuniliko mimi.’”⁴²¹

Kwa kitendawili, teolojia ya kimapokeo imehesabia Yesu kudai kuwa Mungu, ukufuru amabao umesababishwa na kushikilia dai lake kuwa Mwana wa Mungu. Mwana wa Mungu ni jina halali la heshima kwa mjumbe mkuu wa Mungu, kwani wakili wenyewe walitambuliwa kama miungu (Yohana 10:34; Zab. 82:6), ambayo kwa Yesu ni sawa na Mwana wa Mungu (Yohana 10:36). Kuwa Mwana wa Mungu ulimaanisha kuonyesha kamili utiifu kwa Baba, asili sawa ya Israeli ambao raia wake wanatarajia kuwa “Wana wa Mungu anayeishi” (Hos.1:10). “Mwana wa Mungu” pia anajulikana kwa jina ka heshima ya Masiya, Kiongozi aliyechaguliwa na Mungu.⁴²² 15 Na ilikuwa iwe dhibitisho la Umasiya wa Yesu kwamba Yohana aliutia tundu Injili wake wote (Yohana 20:31). Kila mahali katika Agano Jipya Yesu anaamuliwa kuwa “Yesu Masiya” au “Yesu Kristo Masiya.”⁴²³ 16 Tamko “Maulana” himaanishi kama inavyofikiwa kwamba Yesu ni Mungu Maulana (hivi basi kuleta “shida” ya uaminifu wa Utatu. Yesu ni “Masiya Maulana,” kulingana na Zaburi 110:1 amabapo ya pili “Maulana” ni Masiya wa ahadi. Petero alijua kuwa Zaburi ilieleza kuhusu kuandikwa kwa Kristo kama “Maulana (Matendo 2:34-36). Umuhimu mkuu wa Zaburi 110:1 kaitika Ukristo wa Agano Jipya umekataliwa vikubwa na wanaoamini Utatu. Hakika ya kuwa fungu hili limeandikwa katika Agano Jipya mara nyingi kuliko fungu lingine kutoka maandiko ya Kiebrania yangetuonyesha na tungepaswa kufahamu umuhimu wake. Matumizi ya *adoni*, na sio

⁴¹⁹ Matendo 13:34 inaendelea kuzungumza kuhusu *Ufufuo* wa Yesu.

⁴²⁰ Ibid., 175, 176.

⁴²¹ *Jesus in the Gospel of John* (Minneapolis: Augsburg, 1984), 21.

⁴²² Ps. 2:6, 7; 89:26, 27, 35, 36; Matt. 16:16; 2 Sam. 7:14.

⁴²³ See Luke 2:11 for the Messianic title *christos kurios* — Lord Messiah.

adonai, kumchagua Masiya katika mwaenzi mtakatifu ungewafanya wanafunzi wa Biblia washindwe kufikiria kwamba Yesu angefaa kuwa Mungu.

Yesu, kwa hakika, alidai kutenda kwa niaba ya Mungu kama ajenti wake. Maneno yake ni maneno ya Mungu. Matendo yake ni matenso ya Mungu; na Baba ametoa amri ya kusamehe dhambi, kutoa hukumu la dunia na pia kuwaamsha waliokufa. Hivi basi ni kwamba mafungu yaliyo katika Agano la Kale amabayo ziko na Yaweh kama mtu inaeza ikatumika katika Agano Jipya kwa tendo la Mwana ambaye anatenda kwa niaba ya Yahweh. Wanaoamini Utatu wanashindwa kuelewa jambo la asili la Kiebrania ya wakili wanapojaribu kuonyesha kutoka fungu hizi kuwa Yesu ni Yahweh. Yeye si Yahweh lakini amepewa cheo ya mjumbe mkuu. Usawa wa Yesu na matumizi wake ukilinganishwa na Baba yake haimaanishi kuwa Yesu ni Mungu. Wazo kama hili ni jambo lisilowezekana katika Injili ya Yohana ambayo inashikilia kuwa Baba ni “Mungu wa kweli wa kipekee” (17:3) na “yeye pekee ndiye Mungu” (5:44). “Inafaa kujulikana,” Robinson anasema, “kwamba Yohana ni shahidi asiyeweza kupotoka/enda upande kama ilivyo katika Agano Jipya kwa msingi wa madhehebu/mafundisho ya dini ya desturi za kiyahudi, ya uaminifu wa Mungu mmoja. Kuna Mungu mmoja wa kweli na wa kipekee (yohana 5:44; 17:3): kila kingine ni miungu (1 Yohana 5:21).”⁴²⁴

Maneno matakatifu yanafaa kusomwa katika lugha yake na jukwaa la ustaarabu. Zaidi ya hayo msingi wake wa chini kabisa katika shema ya Israeli lazima itambuliwe. Kwa sasa wasomaji Biblia na watafsiri “wanasikiza” kwa makini Yohana kwa njia ya Imani waliofunzwa, na kukisoma kwa kutumia miwani yaliyozibwa na falsafa ya Kigiriki.

Kamusi ya Biblia na Mwana wa Mungu

Ni jambo muhimu kutazama ugumu uliotokana na teolojia “yenye imani halisi” inapojaribu kuthibitisha kuwa ya ukweli maana mpya isiyo ya kibibilia iliyoagizwa kwa neno “Mwana wa Mungu” na linauliza swali kama kwamba fungu hilo kama lilivotumiwa kwa Agano Jipya kama kinaonyesha pahali popote kuwepo-kabla. Je, “Mwana wa Mungu” katika bibilia elekeza kwa Yesu baada ya kuzaliwa kwake, au inaeza maanisha kuwa alikuwepo kama Mwana kabla kuzaliwa kwake? Swali hilo ni la muhimu sana kwa shida yote ya wanaoamini utatu. Bila Mwana anayeishi milele hakuna Utatu. Ni nini basi, ni ya hakika kwenye Biblia kuhusu Mwana wa Mungu?

Je, kinaonyesha au hakionyeshi kabla-kuwepo? Ni mwisho upi wa maneno unaoweza kuondolewa kutoka Injili hizi? Kwa habari iya haya hakuna wasiwasi kuwa kwa hali mengi makuu maneno yangeridhishwa na onyesho la Kristo kugeuka utu. Mifano mengi katika Mathayo, Alama na Luka ungekuwa kwa upande huo. [Je, Yohana humzungumzia Yesu kama Mwana kabla-kuwepo?] *Hiyo inaweza kujadiliwa. Lazima tuangalie maelezo yaliyo wazi. Labda hakuna yoyote.*⁴²⁵

Lililokubaliwa kwamba kuna hakika kuwa hakuna maonyesho katika Yohana kwa Yesu kama Mwana kabla-kuwepo anayefahamisha kuondoka kwa uhalisi kutoka kwa ushahidi wake wa maneno matakatifu na elezo ya Yesu. Fundisho la kanuni la baadaye kuhusu kuamini katika “Mwana wa milele,” cheo ambacho maandishi matakatifu hayakubaliani,⁴²⁶ kama inavyotakikana kwa wokovu, ulipatikana tulivyoona

⁴²⁴ *Twelve More New Testament Studies*, 175.

⁴²⁵ W. Sanday, “Son of God” in *Hastings Dictionary of the Bible*, 4:576, mkazo unaongezwa

⁴²⁶ Cp. Matazamo ya Buswell kwamba “tunaweza sema kwa ujasiri kuwa Biblia hauna la kusema kuhusu ‘kuzaliwa’ kama uhusiano wa milele kati ya Baba na Mwana” (*A Systematic Theology of the Christian Religion*, Zondervan, 1962, p. 111). Lakini bila mafundisho ya Uwana wa milele, mafundisho ya Utatu yanaanguka.

yalivyosomwa vibaya katika maneno ya Yohana na kubadilishwa kwa maana mapya kwa matamshi ya “Johannine” yanayoeleza Yesu. Maendeleo ya ukristo unaweza kuwa tofauti kama waelezi wa maandiko matakatifu yangukuwa na maana ya Mwana wa Mungu “kama usomi wa hali ya juu uliochaguliwa, katika asili ya Myahudi-kimasiya.”⁴²⁷

Hekima ya James Denny

James Denny (1856-1917) alikuwa mteolojia mashuhuri wa kanisa la “Scottish” ambao walitambua kuwa kuna jambo lisilo la kibibilia kuhusu taarifa kuwa “Yesu ni Mungu,” ingawa alikubali kuwa yeye ni mwaminifu wa Utatu kwa mabarua yaliyoandikiwa W.Robertson Nicoll, alisema:

“Yesu ni Mungu” inaonekana kuwa njia ya kukasirisha [ya keuleza uaminifu katika Uungu wa Kristo] Ikona usawa na kumuita Maria mama ya Mungu...Katika Giriki, na karne ya kwanza, unaeza kusema “Yesu ni Mungu.” Lakini kwa kiingereza neno sawa na hilo sio “Yesu ni Mungu” (kwa herufi kubwa M), lakini, ninasema ni mwaminifu katika Uungu wake wa ukweli, “Yesu ni mungu” (kwa herufi ndogo m – na sio miungu, lakini ambaye ana asili ya Mungu mmoja)...Aina ya madhumuni ambayo katika ufasaha wetu wa maneno unatoa maoni kuhusu ilinganifu wa Yesu na Mungu ambao unakosea ukweli.⁴²⁸

Uteto wa Denny unahitaji uangalifu wa makini kutoka kwa wale ambao wanasisitiza kwamba Yesu ni Mungu. Binadamu ambaye Uungu unaeleza sana aliyestahili kuwa Mwokozi. Huyu ndiye mwokozi aliyepewa na Mungu.

Maelekeo katika Mafundisho ya Mapokeo ya Utatu

Hakika ya historia ya kanisa unaeleza kuwa wazushi walitumia vibaya Injili ya Yohana: “Yohana alichaguliwa kama Injili “yao” na mkazo wa waraka wa “Johannine” kwa Yesu ilivyokuja kwa mwili [kwa mfano, kama binadamu wa ukweli] (1 Yohana 4:2; 2 Yohana 7) lazima ionekane kama matokeo ya hisia ambayo mafundisho yake ulifutuka.”⁴²⁹ Yesu-binadamu asiye mkamilifu alijengwa kwa msingi wa kutoelewana wa Yohana na wale “Gnostics”. Mmenyuko wa Yohana wa kutosoma vyema Injili yake ilikuwa ibandikwe maafikano kama “ya uwongo” (1 Yohana 4:3; 2 Yohana 7). “Ilikuwa ni matafsiri mabaya ya nia yake.”⁴³⁰

Lakini je, “imani halisi” imeepukana na mtego huo sawa na wakati ulibadilisha lugha ya Yohana katika suala la falsafa ya kigiriki? Wengi wamezusha kuwa maelezo ya imani ya Yesu kama “Mungu mkamilifu na binadamu makamilifu” zimewakilisha vibaya kile ambachi kiliandikwa na Yohana na unatupilia mbali maelezo mkavu wa Yesu-binadamu uliopewa na Mathayo, Alama na Luka. Lazima iwe ya muhimu kwamba mafunzo kuhusu “Mwana wa milele” unategemea katika Injili ya Yohana, ingawa kamusi ya Bibilia inakubali kuwa labda, hata katika Yohana, hakuna nakala Fulani ya kuegemeza Uungu wa kabla kuwa binadamu kwa Yesu.

⁴²⁷ Matthew Black, *Romans, New Century Bible* (Marshall, Morgan and Scott, 1973), 35.

⁴²⁸ *Letters of Principal James Denny to W. Robertson Nicoll*, 124, 125.

⁴²⁹ J.A.T. Robinson, *Twelve More New Testament Studies*, 142.

⁴³⁰ *Ibid.*

Muhtasari na Hitimisho

Ubinadamu wa Yesu ni chini ya yale ya ukweli wakati ulipendekezwa kuwa hakukuja katika kuwepo katika tumbo la Maria. Ukosefu wa ushahidi wowote wa Biblia kwa Yesu kuwa *Mwana wa Mungu kabla kuzaliwa* kwake unapendekeza kuwa imani hiyo iliyoshikoliwa na wengi katika kuwepo-kabla kwa binadamu hauna msingi katika maandiko matakatifu. Tunaeleza kuwa ukona msingi wa kutosoma vyema Injili ya Yohana, katika kutupilia mbali dhana ya Kiyahudi isiyo ya kawaida ya daraja ya mbele iliyopatikana hapa. Hakika kuwa hakuna kitu kinachosemwa kuhusu kuwepo-kabla Mathayo, Mariko, Luka na Matendo (na waraka ya Petro) inatupasa tuulize swali kama kwamba Yohana kweli ni ametupatia sura ya Yesu iliyotofauti kwa kukipa sifa ya maisha ya fahamu kabla kuzaliwa. Je, Yohana kweli aliweka katika kikao “shida la wanaoamini Utatu” ambao ulisababisha shida katika karne za awali?

Nakala ya Yohana ambayo imedaiwa kama ushahidi wa kuwepo-kabla wa Yesu ambao watu hawakuelewa, kwa sababu tahadhari kidogo sana imewekwa kwa aina ya Kiyahudi ya fikira za Yohana na za yesu. Uzushi kwamba wakati uliopita huwa mara kwa mara haumaanishi kerejea kwa matukio yaliyopita, umepuuzwa. Katika Yohana 3:13 Yesu hakusema kwamba alikuwa “amepaa mbinguni,” wala Mwana wa Mungu kuwa mbinguni milele. Alikusudiwa kwenda kwa Baba, akitimiza maono ya Danieli ya Mwana wa Mungu (Yohana 6:62). Yohana 13:3, 16:28 na 20:17 vimetafsiriwa vibaya katika kitabu cha NIV kupeana hisia kwamba Yesu alikuwa anarudi kwa Babake (ona KJV, RSV). Utukufu wake ulikuwa umetayarishwa kwake kabla kuwepo kwa dunia (Yohana 17:5; cp. Matt 6:1: tuzo za baadaye ni salama tayari), na alichaguliwa kama mwakilishi binadamu mkufuzu wa Mungu, Masiya, mbali kabla ya Abrahamu (Yohana 8:58). Ilikuwa kama *mwana binadamu wa mtu* ambaye “alikuwepo-kabla” katika hukumu mtakatifu. Yesu anasadikishwa kuwa lazima afanye mpango wa Mungu kabla ya kuamua: “Ilikuwa ni lazima Kristo ateseke?...Vitu vyote ambavyo vimeandikwa katika sheria ya Musa, manabii na Zaburi *lazima yatimizwe*” (Luka 24:26, 44).

Wazo halisi la kuwepo kabla ya mimba ulisababisha hatimaye kwa utata unaogofya na migogoro kuhusu asili ya Yesu ambayo haijawahi tatuliwa. Hoja zilikimya kwa kuwekewa fundisho kuu la Ukristo (katika Nicea na Chalcedon), ambao ulilazimisha suluhisho rasmi kwa shida hilo. Suluhisho, hsts hivyo, unajaribu kutatua suala kwa msingi mkubwa wa teolojia ya kiyahudi wa Yohana ambayo haukeleweka kwa urahisi na kusikitisha na waGiriki. Waliojeruhiwa katika mgogoro huu kuhusu asili ya Mungu na Yesu ulikuwa ukweli wa Biblia wa maana kuhusu ubinafsi wa Mungu na ubinadamu wa ukweli wa Yesu.⁴³¹ Tangu jinsi maisha ya milele inianza na shukrani sahihi ya Baba kama Mungu wa kweli wa kipekee, na Yesu kama Masiya (Yohana 17:3), wasomi wa Biblia lazima waambiwe kuhusu uharibifu mbaya unaowezezana kufanyika kwa imani wakati wagiriki wanaohisi kifalsafa walisoma Injili ya Yohana bila msingi wa sauti katika Agano la Kale, na heshima kidogo kuhusu Ukristo wa Mathayo, Alama, Luka na Matendo, ambao umefukuza kwa haraka kama “mali.” Kwa uhusiano huu maneno ya Karl Rahner ni faraja ya kurejea kwa tabaka ya ukristo. Anakiri kwamba:

Mara kwa mara tunapata ukristo wa mapokeo ukiwa ngumu kuelewa...na hivi basi tuna maswali ya kuweka kwa chanzo chake, Maandiko. Kwa mfano, tuchukue madai ya kati ya Maandiko kama taarifa kuwa Yesuni Masiya na kama vile amekua Bwana katika mwendo wa maisha yake, kifo na ufufuo. Imekubaliwa kuwa madai yake yamefanywa ya kikale na mafundisho ya asili na mwanzo wa uhai wa Uwana, kama tunavyoijua na kuieleza katika taarifa ya Chalcedonian, na kuwa kwa faida ya ukweli

⁴³¹ John 17:3; 5:44; Deut. 6:4; Mark 12:29ff. 1 Cor. 8:4-6; Eph. 4:6; 1 Tim. 2:5; Jude 25.

kwetu sisi kwa historia...? Je, Ukristo wa matendo ta mitume, ambayo inaanza kutoka chini, na uzoefu wa binadamu wa Yesu, ya kale? Au kina kitu maalum cha kusema ambacho Ukristo hauseremi na uwazi sawa?⁴³²

Uchambuzi wa Karl Rahner wa matumizi ya Agano Jipya ya neno “Mungu” huzaa marudio: “Hakuna popote kwa maandishi ya Agano Jipya ambapo *theos* [Mungu] inayotumika katika hali kama kutambua Yesu naye ambapo mahali pengine katika Agano Jipya mfano kama *ho theos*, ambayo ni Mungu Mkuu.”⁴³³ “Hakuna popote katika Agano Jipya ambapo kunapatikana nakala na *ho theos* [Mungu] ambayo inajulikana kwa Mungu kama anayeishi kikamilifu kwa nafsi ya tatu.”⁴³⁴

Tunatoa maoni kuwa uongo tofauti umechorwa kati ya Ukristo wa hali ya “juu” ya Yohana Ukristo wa hali ya “chini” ya muhtasari. Wote Yohana na ya muhtasari wanaonyesha Yesu anayekuja si pekee “kutoka juu” (Mathayo na Luka kwa kueleza mwanzo wa utakatifu wa Yesu katika tumbo ya Maria), lakini pia “kutoka nyuma,” ambapo Yesu ndiye kilele cha ahadi la Agano la Kale kuwa Mwana wa Daudi mkuu zaidi ataonekana. Kwa hakika, usomi wa Ukristo wote wa Agano Jipya ni wa kiMasiya. Kila mwandishi anachangia, kwa masisitizo tofauti, kwa mchoro mmoja wa Yesu kama Mwana wa Mungu, *katika asili ya kimasiya*. Ni mabadiliko kutoka “Mwana wa Mungu” katika hisia ya kibibilia, kwa “Mungu Mwana” ambayo yameonekana makubwa katika kuweka mbele kitume cha Yesu. Lampe anatoa maoni kwa lazima kuwa utangulizi wa dhana ya kuwepo kabla inaleta shaka kwa ubinadamu wa Yesu:

Dhana ya Ukristo ya kabla-kuwepo kwa Mwana mtakatifu unarudisha chini utu wa kijamii na kiutamaduni wa Yesu kwa usahaulifu wa asili wa mwanzo wa uhai “asili ay binadamu...” Asili ya binadamu, kulingana na mapokeo ya Alexandrine ulikuwa na fumbo la Imani katika mtu mtakatifu wa Mwana; ikawa asili ya binadamu ya kiumbe hicho kitakatifu...Kulingana na Ukristo huu, Mwana wa milele angepata asili ya binadamu, au kutengeneza yake mwenyewe; ni asili ya binadamu ambayo hakidaiwi chochote cha muhimu kwa mazingira ya kijiografia; hakiendi sambamba na chochote katika dunia halisi; *Yesu, baada ya yote, ukweli “hajakuja katika mwili.”*⁴³⁵

Onyo sawa na hilo kuhusu hatari ya kumbadilisha Yesu awe kiumbe cha uhai ambaye alikuwepo milele kabla kuzaliwa kutoke kwa Paulo Van Buren:

hakuna dalili kamili kuwa ukuu [wa Yesu] ulitarajiwa katika hisia ya maisha. Tunaweza hitimisha kuwa kwa kanisa ya hapo awali, Yesu alipewa ukuu wa hali ya kweli kwamba Walimu wa kiyahudi walichaguliwa kwa Torah. Kama mmoja angedai ukuu katika asili ya maisha, angekuwa akidai kuwa Yesu wa Nazareti, aliyezaliwa na Maria, alikuwepo na Mungu kabla kuumbwa/kujengwa kwa dunia. Dai hilo linaweza kuwa mbaya kuliko ya akili; inaweza kuharibu mshikamano wote katika madai muhimu ya wakristo kuwa Yesu kweli ni binadamu, kwamba

⁴³² *Theological Investigations*, 1:155ff.

⁴³³ *Ibid.*

⁴³⁴ *Ibid.*, 1:143.

⁴³⁵ *God as Spirit*, 144, msisitizo unaongezwa.

neni lilikuwa *mwili*... Yesu wa Nazreti alianza maisha yake, alianza kuishi, kwa wakati hakika katika historia: Neno kikawa *mwili*⁴³⁶

Sehemu ya sasa uliongozwa na hamu ya kuepuka fumbo lolote la Yesu na kuwaomba rejeo la Yesu wa kihistoria, Masiya wa Israeli aliyeahidiwa. Masomo ya Yohana ambayo tunadokeza kiruhusu Yohana wa Mungu, kuwa bunadamu kama ya muhtasari.

Kupata Mwana kabla-kuwepo katika Yohana utaeleza njia ya matusi ambayo wachambuzi “halisi” mara kwa mara wanafukuza usomi wa ukristo wa Luka kama “unaojulikana.” Hakika inaweza kuwa kwamba Luka ni mwakilishi wa usomi wa Ukristo wa kimasiya wa Agano Jipya ambayo haiambatani na kile ambacho kilikuwa “halisi” katika wakati wa baada ya Bibilia. Kutazama katika Luka 1:35, “kile kitu takatifu ambacho kinazalishwa...,” Strachan anasema, “Hii ni ya mazingira ambapo wazo la kiteolojia ya kuwepo-kabla ya Yesu imepatiana njia ya mimba maarufu ya kuzaliwa kwake kimwili.”⁴³⁷ 30 Lakini hii ni hoja ya mzunguko. Luka kweli aliacha wazo la Yesu kuwepo-kabla kwa mweleo unaoeleweka? Badala, inaonekana kuwa ya kitume ya baadaye “kihalisi” aliendeleza maoni ambayo yalibadilisha ya Luka na Yohana pia. Mabadiliko hayo yalitimizwa kwa urahisi kwa kufanya kazi kutoka Ukristo wa Yohana wa lugha ya Kiyahudi, na Yohana wakati huo alifikiriwa kusimulia Yesu vitofauti na ile ya picha ya muhtasari. Matengenezo mapya ya usomi wa kimasiya ma umoja kati ya waandishi wote wanne wa Injili na kile ambacho wangepanya kuwaleta pamoja tena waaminifu katika thibitisho la Agano Jipya kuwa Kristo, Mwana wa Mungu, mjumbe wa kuja kwa ufalme wa Mungu. Hii, ndiyo Yohana aliunga mkono, akidai kuwa maisha inapatikana kwa Yesu ambaye ni Mwana wa Mungu na Masiya (Yohana 20:31; cp. Mathayo. 16:16). Alikuwa kutii na kuamini kuwa Yesu anabaki kama wa sasa na wa muhimu kama kitambo. Rejeo kwa Yesu, Masiya, utahitaji kujua upya Injili ya Muhtasari na Injili kuhusu ufalme wa Mungu, ya taarifa ya kuokoa iliyotupiliwa mbali kwa Yesu kihistoria na mitume. Mahabiri mengi ya kisasa unaendelea ni kama yale ya muhimu ni sehemu zilizochaguliwa au fungu la waraka la Paulo na msalaba wa Yesu.

Migogoro mengine yaliyoendelea kwa dhana ya mafundisho ya Utatu ni yakukosesha. Kaitika Bibilia, inasemwa, kuna mmoja anayeitwa Baba ambaye ni Mungu, mmoja anayeitwa Mwana ambaye ni Mungu na mmoja anayeitwa Roho Mtakatifu ambaye ni Mungu. Lakini tunajua kuwa kuna Mungu mmoja pekee. Kwa hii, lazima kuwe na watu watatu ambao wanaunga Mungu mmoja. Hii ni njia isoyoyote ya kawaida ya kupeana ushahidi. Kwa hakika kuna kimoja katika Agano Jipya anayeitwa Baba ambaye alisemekana kuwa Mungu mmoja (*ho theos*) kwa mara 1300. Alichaguliwa pia kama “Mungu wa kipekee” (Warumi 16:27; Jude 25), “yeye pekee ambaye ni Mungu” (Yohana 5:44) na “Mungu wa kipekee” (Yohana 17:3). Kuna mmoja anayeitwa Mwana, Yesu Kristo, ambaye anaipatia jina la heshima la Mungu (*theos*) mara mbili kwa hakika (Yohana 20:28; Ebr. 1:8), lakini hajawahi itwa *ho theos* (unaotumika mara kwa mara), “Mungu wa kipekee,” “yule ambaye ni Mungu pekee,” au “Mungu wa ukweli wa pekee.” Mambo ya hakika yanaonyesha kuwa kuna wawili ambao unahesabiwa kama sawa na Mungu, wote wakiwa Mungu mmoja. Kuongeza kwa hii hakika kuwa Mungu katika Agano la Kale inasemekana kuwa mbinafsi mara maelfu, na inafaa iwe wazi kuwa uaminifu wa Utatu hauna haki katika mambo ya hakika ya Bibilia. Zaidi ya hayo, majina ya heshima “Mungu wa kipekee,” “yule ambaye pekee ni Mungu” “na wa ukweli,” kutumiwa pekee kwa Baba, unaelekeza katika uainishaji kwake kama tofauti na Mwana. Umami wa maandiko ya Agano Jipya inaonyesha Yesu kama mjakazi wa Baba, hakika

⁴³⁶ A *Theology of Jewish-Christian Reality* (Harper & Row, 1983), 82.

⁴³⁷ R. H. Strachan, “Holiness” in *Dictionary of the Apostolic Church*, 1:568.

ambayo si rahisi kurudiana na wazo kuwa Mwana akiwa wa uwiano sawa na Baba.⁴³⁸ Paulo aliamini kuwa Mwana kwa mara yote atakubaliwa kwa Baba, baada ya kurudisha nyuma (baadaye) ufalme wa Mungu (1 Wakorintho 15:28).

Kama Utatu ungefundishwa katika Agano Jipya, mmoja angetarajia angalau fungu moja mahali inayosema kuwa Mungu mmoja ni “Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.” Taarifa hii haipatikani katika murasa za maandiko. Wakati Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanawekwa pamoja katika kifungu kimoja cha Bibilia, huwa hazisemekika kama “Mungu mmoja” (Math.28:19; 2Wakorintho 13:14). Ni ajabu kuwa salamu ilioko katika mwanzo wa waraka wa Paulo haujatumiwa kutoka Roho Mtakatifu. Wala Roho Mtakatifu kuwahi jishughulisha wala kumuomba.

Wakati Paulo, hata hivyo, anaeleza kuhusu uaminifu wa Mungu mmoja kama tofauti na wa miungu wengi, anasema kuwa kuna Mungu mmoja, *Baba*, na kuwa hakuna Mungu mwingine ila huyo Mungu mmoja, Baba (1Wakorintho 8:4, 6).⁴³⁹ Hayo kwa uzuri wa urahisi ni Imani ya Bibilia. Inafaa imalize migogoro/mabishanno yote. Uungu haujaongezwa. Mungu bado ni Baba pekee kama ilivyo katika Bibilia ya Ebrania. Yeye ndiye Mungu Bwana wa Imani ya Yesu. Wa mwisho anajitambua kama “Bwana” ambaye si Bwana peke yake wa *Shema* (Alama 12:35-37). Yesu ndiye Bwana Masiya na hivyo basi aliyechaguliwa daima “Bwana Yesu Kristo [Masiya].”⁴⁴⁰ Jina lake la heshima la Masiya “Bwana” unatolewa kutoka Zaburi 110:1. Kuchanganyikiwa mara yote kwa wanaoamini Utatu kwa jina la kimasiya “Bwana” na “Bwana” kumaanisha “Bwana Yesu” ndiyo sababu ya ugumu wote. Hakuna sababu nzuri wa kuziba tofauti ulio wazi kati ya Bwana Masiya (*adoni*) na Bwana Mungu (*Yahweh* na *adonai*) (Zb.110:1, 5).⁴⁴¹ Tunaeza kukiri leo kuwa Yesu anafanya kazi kwa niaba ya Mungu. Jambo muhimu lilisemwa na Caird wakati alielezea zoezi la Wayahudi ya kuwasiliana na ajenti kama yeye ndiye mkuu:

[katika 2 Ezra 5:43-56)...msemaji wa Mungu, malaika Urieli, anaulizwa maswali na Ezra kama alikuwa muumbaji na hakimu. Ezra anatumia njia sawa ya uwasilishi kwake Urieli (Bwana wangu, hababi wangu”) kama anavyotumia katika ombi moja kwa moja kwa Mungu. Zoezi hili la kumtendea ajenti ni kama ndiye mkuu ni ya muhimu sana kwa usomi wa Ukristo wa Agano Jipya.⁴⁴²

Wengi wanaoamini Utatu wametoshika kwa kushikilia mapendekezo mawili ya utata kwa wakati mmoja bila kujaribu kuyaeka kwa umoja: Mungu ni mmoja na bali watatu. Hii ndio kanuni za Imani rasmi inaonekana kuwauliza. Lakini Bibilia haihitaji tendo hili kubwa la akili. Wengine wanaoamini Utatu wanajaribu kutoroka shtaka kuwa imani katika watu watatu, kila ambaye ni Mungu, lazima ihusishe imani katika Mungu kwa nafsi tatu. Wanajibu kuwa Mungu na Yesu si watu kwa njia ambayo tunatumia kila

⁴³⁸ Ni faraja kwa maandiko yetu kuwa maelezo mashuhuri I. Howard Marshall anaweza kuandika, “Usomi wote wa Ukristo wa Agano Jipya ni wa chini” (book review of Jervell, *The Theology of the Acts of the Apostles*, in *Evangelical Quarterly* 70:1, Jan. 1998, 76).”

⁴³⁹ Ya onyo ya chafuko juu ya Uungu ni hakika kuwa wasomi kwa mara ingine kwa kutajwa vibaya katika Imani ya Paulo. Hivi, Klaas Runia anasema: “Paulo anaandika kwa Wakorintho: ‘Kuwa kuna Mungu ambaye kwake kila kitu na vyote vinaishi’”(An Introduction to the Christian Faith, Lynx Communications, 1992, 114). Lakini Paulo aliandika: “Kwetu sisi kuna Mungu mmoja, *Baba*...” Runia anaongeza kuwa James na mitume wengine “wanasema, kwa masisitizo ya usawa, kuwa *Yesu Kristo pia ni Mungu*”(Ibid., emphasis his). Lakini ni wapi James au Petero alisema kuwa Yesu ni Mungu?

⁴⁴⁰ Luke 2:11; Rom. 16:18; Col. 3:24. Cp. Luke 1:43 na ya sheria zaidi ya kitabu cha Zaburi wa Suleiman 17:32; 18:7.

⁴⁴¹ Katika Giriki ya LXX maneno yote tatu yanaonekana kama *kurios*.

⁴⁴² G.B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible* (Philadelphia: Westminster Press, 1980), 181.

mara maandiko kumuita. Jambo la hakika ni kuwa kila mwandishi katika Agano Jipya anaeleza Yesu kama kujitegemea kwa uangalifu tofauti na Babake. Hakuna kilinge kuhusu kumuita Mwana na bila neno kuhusu “kizazi milele.”Mapendekezo utata ilivyo katika Utatu si wa muhimu, kama vile si wa kibibilia. Huelekea kikadhoofisha yote mafundisho/madhehebu ya maana ya kiBibilia kuwa Mungu ni mmoja na msingi wa ukweli wote kuwa Yesu ni Masiya, Mwana wa Mungu na Mwana wa Daudi (Math. 16:16; 2 Sam. 7:14; Ebr. 1:5).

Wakristo wana haki ya kujua mawazo yaliyotengeneza mfumo wa Imani ambayo imependekezwa kwao kama imani. Wengi hawajui kuhusu sehemu ya ujuzi wa siri ambayo imepewa kwetu sisi katika usomi wa Ukristo wa Utatu. Katika kazi yake ya kasisi Paulo alijishughulisha na kupigana na kuondoa hatari ya ujuzi [gnosis] ya uongo unavyoitwa” (1Tim.6:20). katika kanisa ya baada ya mitume hatari ya falsafa ya ujuzi ilishambulia imani haukugeuzwa. Ingawa kanisa ilidai kukana aina ya ujuzi huo, ilikosa kuzuia shawishi lililo la ustadi mwingi wa ujuzi kwa kuharibu mafundisho ya hapo mwanzoni kuhusu Mungu na Kristo. Jaribio la kutangaza Uungu wa Yesu ulisababisha mashaka ambayo hayakutambuliwa kwa “asili zake mbili” na kuchukua wazo lisilomuamini Yesu na halina mahali popote katika Maandiko. Maelezo ya mhalisi huyu kuhusu Ujuzi wa hapo awali unastahili kusikizwa:

Mababa wakristo wa hapo awali, wa kwanza Irenaeus na Tertullian, walifanya bidii kutafuta aina kadha ya hekima bila asili ya ujuzi, aina moja ya Yesu Kristo mmoja. Kwa ukweli hakufaulu. Tayari Harnack alilazimishwa kusema: “Nani anaweza kushikilia kuwa kanisa ilishinda mafundisho ya dini ya ujuzi ya asili hizo mbili?” Hata mabaraza ya baadaye ambayo yalijadiliana kuhusu mashida ya usomi wa Ukristo ni ya kutatanisha, na siku hizi si yenye akili, maana pia haikufaulu kufanya hivi; *umoja wa kanisa ulitungwa kwa hii...Imesahaulika mara kwa mara kuwa wateolojia wa ujuzi waliona Kristo kama “wa kutoshelezana” na Baba, kabla teolojia ya kihubiri ulitunga kama kanuni, ili kuhifadhi utakatifu wake wote.*⁴⁴³

Kama ingekubaliwa kuwa Wakristo wana nia ya kumjua na kumtumikia Kristo wa maandiko ya Mungu, Baba, lazima ifuate kuwa watataka kuelewa nani ni Kristo. Kuelewa huu utashikilia maelezo/picha ya Yesu kama yalivyo katika maandishi ya Kristo. Tunaweza kuuliza kama kwamba maelezo ya mapokeo halisi ya Yesu inaipatia nafasi Bibilia ya maana. Matangulizi ya Yohana yamekuwa ya tumaini muhimu kwa maelezo ya Yesu kuwa ushahidi wowote mwingine unaipatia nafasi ule ambao umeonekana kama ukweli wa fungu hilo. Nakala ya Ukristo ya Paulo iliyojulikana katika Wafilipi 2 imechukuliwa kama ya kawaida nay a maonyesho yote ya Yesu, kuwa Paulo anasema mtu kabla-kuwepo. Bali anawasihi waaminifu kuiga mwenendo wa maisha ya Yesu Masiya ambaye kwa hayo yote ni hoja ya taarifa ya Paulo (Wafilipi 2:5).⁴⁴⁴

⁴⁴³ Kurt Rudolph, *Gnosis: The Nature and History of Gnosticism* (Harper & Row, 1983), 372, masisitizo yanaongezwa.

⁴⁴⁴ Cp. Mtazamo wa A.H. McNeile kuwa “Wengi wameshuku kama Paulo angevutia maandiko kwa ajabu iliyo bora sana.” Katika Wafil.2 Paulo anawasihi Wafilipino waache kutopatana na kutenda kwa unyenyekevu kwao wenyewe. Katika 2 Kor.8:9 anawashauri wasomaji kuwa na ukarimu kwa kupeana sadaka. Inaulizwa kama kwamba ni jambo la kawaida kwake kufanya imara mafunzo haya mawili ya maonyesho ya nasibu (onyesho lake la pekee) kwa shida kubwa ya desturi ya kutwaa utu. Na inafikiriwa na wengi kuwa msaada wake ungekuwa na matokeo mengi zaidi kama angezungumzia mfano unaohimiza wa ukarimu wa Kristo na kuwa kipaji katika maisha yake kama binadamu katika 2 Kor.10:1: ‘Ninakutia moyo

Kama uzito wote ungepewa ushahidi wa Muhtasari pamoja na Matendo na waraka usio wa Pauline, inakuwa wazi kuwa ushuhuda wao ulioshikanishwa ni kwa Yesu kama Masiya, na sio Mungu katika shauri ya Chalcedonian. Sawa na hayo yanaweza kubishwa kwa Yohana. Taarifa ya muhtasari ya Yohana kuhusu nia ya Injili kuwa Yesu aliaminiwa kama Masiya (Yohana 20:31), unaongoza katika kuwa ako kiwango moja na washahidi wenzake kwa imani. Hata Ebrania 1:10, ambapo fungu zote zinazoonekana kuandikia uumbaji wa chimbuko wa Yesu, na kwa hakika haufanyi hivyo.⁴⁴⁵ 38 Mwandishi anaeleza kuwa “wenyeji wa dunia ya baadaye” (Ebr.2:5), kuwa amekuwa akizungumza; na ni Mungu alipumzika wakati wa kuumba (Ebr.4:4), kama vile, kulingana na Yesu, ilikuwa ni Mungu “aliyetengeneza mwanamume na mwanamke” (Alama 10:6; cp. 13:19). Kama katika NASV tunasoma “wakati analeta tena motto wa kwanza kuzaliwa katika dunia” (Ebr.1:6), ni wazi kuwa mwandishi anatarajia tuelewe onyesho kwa matumizi ya Yesu kama mwanzilishi wa dunia unaokuja wa ufalme (cp. Isa. 51:16, NASV). Tukio ya “mafungu magumu” hayafai kutangua ushahidi ulioonekana kote kwa maandishi.

kwa uvumilivu na ustahimilivu wa Kristo” (*mafunzo ya Agano Jipya kwa mwanga wa st. Paulo*, Cambridge University Press, 1923, 65). Kwa hali ya Wafil.2:5ff. ikiwa maelezo ya binadamu-Yesu unaweza kukaguliwa katika nakala ya C.H. Talbert, “Shida ya kuwepo-kabla katika Wafilipino 2:6-11,” *Journal of Biblical Literature* 86 (1967): 141-153; J. Murphy O’Connor, “Christological Anthropology in Phil. 2:6-11,” *Revue Biblique* (1976): 26-50; G. Howard, “Philippians 2:6-11 and the Human Christ,” *Catholic Biblical Quarterly* 40 (1978): 368-387.

⁴⁴⁵ Kwa ukaguzi zaidi ya Ebr. 1:10, masisitizo ya F.F. Bruce katika *New International Commentary on Hebrews* (Eerdmans, 1964) ni muhimu. Mwandishi wa Ebrania anaonyesha haya LXX taarifa uliotofauti na taarifa ya Ebrania “Masoretic”

XIV. MUHTASARI: KUAMINI MANENO YA YESU

“*Bwana Mungu wetu ni mmoja.*” — *Yesu Kristo*

Ni jambo la muhimu sana, hupuuzwa mara nyingi, kuwa Yesu anasawazisha/linganisha ukweli halisi na imani katika *misemo na maneno yake*. “Yule ambaye anasikiza ujumbe wake na kuamini aliyenituma ako na uhai katika wakati ujao” (Yohana 5:24). Msisitizo wa ujumbe na mafundisho ya Yesu umetiliwa mkazo na muhtasari pia, na inatuonya tusimuache Yesu kutoka kwa maneno yake na hivyo basi tujijengee sura ya Yesu mwingine. Yohana anatoa habari ya Yesu akisema, “Yule ambaye ananikana na mafundisho yangu... atahumkumiwa na mafundisho yayo hayo” (Yohana 12:48). “Kumuamini Musa” ni sawa na “kuamini maandishi yake” (Yohana 5:46, 47), na kwa maelezo sawa “kumuamini Yesu” ni sawa na kuamini *maneno yake* (Yohana 5:47). Hii inamaliza maswali yoyote kuhusu umuhimu wa “mafundisho ya dini” ukilinganishwa na “zoezi,” “kwa yule ambaye... hatabaki katika mafundisho ya Yesu hana Mungu ndani yake” (2 Yohana 9).⁴⁴⁶ Imani ya Yesu ni roho ya kila ambacho alisema na kufanya. Lakini mapokeo yetu yanasingizia kweli imani ya “Myahudi”? Kulingana na Mwokozi si jambo linalowezekana kumuamini kama hatuko tayari kumuamini Musa (Yohana 5:46,47). Kukosa kushikilia imani ya Israeli na kile ambacho Musa alisema kuhusu kuja kwa Masiya – inavyoonekana katika Kumbukumbu ya Torati 18:15-18 — utaleta matokeo mabaya ikija katika kuamini Kristo.

Wakristo wanatakiwa kuamini kila kitu Yesu anachosema, kama ni maonyo ya Wakristo wanavyojiweka au mafundisho yenye habari kwa mtu mwenyewe. Hayo mawili hayatengeki katika Bibilia, hata “mafundisho ya dini” hayawezi kuwa tayari kwa jambo la mwenedno/maisha. Uhusiano na Yesu unaweza kujengwa kwa neno lake peke yake. Neno la Kristo ni chombo cha kujishirikisha mwenyewe. Kwa hayo “hewa” na akili ya roho inageuziwa mwaminifu. Inaweza kuwa Wakristo wanapumua hewa chafu ya falsafa ya Giriki na watatoa ushahidi wa matengenezo ya kushangaza katika afya yenye asili ya roho kama wangejaribu kupumua hewa ya dunia ya Ebrania kibibilia.

Ukristo wa kustawi unategemea maagizo ya mwokozi kuwa “utanifuata mimi na maneno yangu yatakufuata wewe” (Yohana 15:7; cp. 2 Yohana 9). Imani yote ya uwongo ni ya hatari, kwa sababu imejengwa kwa kile ambacho Yesu alikataa. Hakuna haja ya kutoa pole, kwa hii, ya kujaribu kile ambacho kwa hakika, kulingana na Yohana na Injili zingine, Yesu alivyosema kumhusu yeye na uhusiano wake na Mungu. Katika Injili zote imani katika Yesu kinahusika na imani katika kile ambacho Yesu alisema kama vile alichofanya na anachofanya – na kwa hakika atafanya kwa kurejea kwake katika nguvu na utukufu ya kuthibitisha ufalme wake hapa duniani. Ni la muhimu kile ambacho Mkristo anaamini na kuelewa. Maoni ya sasa mara kwa mara inatuambia kuwa “mafundisho ya dini” unatenganisha na unafaa kuepukwa. Kinyume pia ni ukweli: mafundisho ya dini wa msingi wa ushahidi wa maneno ya yesu kwa tumaini ya umoja katika mgawo uliochafuka wa makanisa. Kanisa inaoonekana kutupilia mbali kiini cha mafundisho ya Yesu: kuwa kutubu na kusameheana unategemea kupokea kwa utambuzi wa mgeuzi wa Injili ya Masiya kuhusu ufalme wa Mungu (Alama 4:11, 12; Luka 8:12).

⁴⁴⁶ Tunakanganywa kuwa Dr. James Kennedy anaonekana kutoona sisitizo kubwa linalowekwa katika mafundisho ya Yesu. Anaandika, “Watu wengi leo wanafikiri kuwa umuhimu wa Ukristo ni mafundisho ya Yesu, lakini sivyo... Ukristo hauweki katikati mafundisho ya Yesu, bali katika utu wa Yesu kama Mungu kutwaa utu ambaye alikuja duniani kuchukua mwenyewe uovu wetu na kukufa kwa niaba yetu” (“How I know Jesus is God,” *Truths that Transform*, 11th Nov., 1989).

Marko 12:28ff. unaonyesha Yesu akithibitisha imani yake mwenyewe katika uaminifu wa Mungu mmoja wa Wayahudi. Ni kwa fungu hilo la maandishi ambapo mazungumzo yote ya Uungu unfaa uangaliwe. Uaminifu wa Mungu mmoja wa “Kiyahudi” wa Yohana hauna tashwishi/shaka. Baba bado ni “Mungu wa kipekee wa ukweli” (Yohana 17:3), “yule ambaye ni Mungu pekee” (Yohana 5:44), na kwa sababu Yesu ni mtu tofauti na Baba, Yesu si Mungu. Yeye ni ajenti aliyechaguliwa kikamilifu na Mungu, mfalme kamili wa Israeli ambaye Agano la Kale ilitamani sana. Yesu anaeleza tabia ya Babake na anatoa ujumbe ya Ufalme (Luka 4:43). Hivi basi inaeza semwa kuwa “ukamilifu wa Uungu unashinda katika Yesu” (Wakolosai 2:9).⁴⁴⁷ Lakini hii haimaanishi kuwa yeye ni Mungu mwenyewe.

Binadamu mkamilifu wa Yesu wa Yohana si Yesu pekee anavyopendekezwa na kanuni ya maandishi, lakini pia kielezo cha kupendeza zaidi ya kuiga kuliko tafsiri ya mapokeo mengine ya Yesu. Yule ambaye ni Mungu wa ukweli (ya hila?) angeonekana kuinuliwa juu yetu kuwa hatungekuwa na fursa ya kuishi kama alivyoishi yeye. Lakini Yesu wa Yohana, ingawa yeye hana kifani kwa nguvu ya roho aliyopewa “bila kipimo” (Yohana 3:34), hajatengi kutoka kwa wafuasi, na ka ma wanaeza kufanya kile ambacho alifanya yeye. Anazidi kuwaahidi kuwa “kama” alivyotumwa duniani, “watatumwa pia wao duniani” kutenda kazi kuu au kuu kuliko yake (Yohana 17:18; 14:12). Na “kama alivyo” moja na Baba, pia wafuasi wanapaswa kuwa (Yohana 17:11, 21). Kama alivyotumwa kutangaza Ufalme wa Mungu (Luka 4:43), ndivyo walivyo.

Toridhia ya kitabu hiki, kwa hivi, umekuwa njia za kuamini zaidi kile amabcho Yesu aliamini kuhusu Mungu na mwenyewe na basi kuleta mafundisho ya dini yetu sisi wenyewe kwa laini moja na yake. “Yule ambaye atafuata mafundisho [ya Kristo] ako na wote Baba na Mwana” (2 Yohana 9). Neno lolote linalotamkwa na Masiya ni ya thamani, kwa kua maneno anayetamka yanabeba “roho na maishi” (Yohana 6:63). Hayo ni maneno ya pekee, kwa hakika ambayo yanaweza kutuopngoza katika “maisha ya wakati ujao,” maisha ya ufalme wa Mungu. Yohana hatofautishi kuelewa kwake kutoka muhtasari kwa kuondoa matumizi ya kila mara ya neno “Ufalme wa Mungu.” Yesu wa Yohana anazungumza kuhusu Ufalme kama “maisha ya milele,” unaonyeshwa vizuri kulingana na maana ya Kiebrania, “maisha kwa wakati ujao.” Matamshi ya Yohana, katika taarifa zote za hali moja ya Yesu na ujumbe wake, lazima itafsiriwe katika “KiEbrania” iliyo lugha yake ya mwanzo ndiyo picha ya Yesu ambayo haijapotea na inaweza patikana kutoka chini ya tabaka yaliyopotovu ya mapokeo ambayo ya tamgeuza. Ni kwa haya yote akilini kuwa tunaomba kufikiria upya kuhusu njia za baada Bibilia ya kuelewa Yohana amabyo yanatatanisha/zuia usomi wa juu wa Bibilia na kueguza imani katika Yesu kama Masiya na usisikivu kwa yale ambayo alifunzwa na aliamini.

Kupata tena kwa imani katika Yesu kama Masiya utaondoa kuchanganyikiwa ambao umefunika Injili kama ilivyosemwa na Yesu. Kwa sasa usomi wa imani ya Injili unaendelea ni kama hakukuwa na mahubiri ya Injili mpaka kifo ya Yesu. Tazamo katika kuhtasari unaonyesha kuwa hii si ya ukweli. Yesu alitangaza Injili *kuhusu ufalme* kabla onyesho lolote la kifo chake na ufufuo.⁴⁴⁸ Ni jambo la kukosesha kujenga matengeneo ta teolojia kwa taarifa fulani katika waraka ya Paulo bila kushikilia Bibilia ya Ebrania na muhtasari wa Injili kama ilivyotoka kwa mdomo ya Yesu.

Upotevu wa mwelewano kamili kuhusu nani nin Yesu umehusiwa na mapokeo ya teolojia kuwa Yesu hakuipenda jina la heshima la “Masiya” na kwamba Agano Jipya unajishughulisha kugeuza Umasiya na sehemu ya kupatana na wageuzi Myahudi. Mafundisho ya dini ya Utatu ni mageuzi ya shari ambayo unabadilisha maoni ya Bibilia

⁴⁴⁷ Lugha ilio sawa kuhusu ukamilifu wa Mungu anayeishi katika Wakristo unaopatikana katika Eph. 3:19.

⁴⁴⁸ Ona kwa mfano Marko 1:14, 15; Luka 4:43; Luka 18:31-34.

katika Masiya na Ufalme wake unaokuja pamoja na maswali ya elimu ya kuchunguza asili na mwanzo wa uhai na “uhusiano” katika Uungu. Wakristo wameangalia kwa muda mrefu upande mbaya: nyuma kuelekea ukoo kutoka mbinguni inavyoitwa “Mwana wa milele” badala ya mbele kwa kuwadia kwa Masiya kwa utukufu ya Ufalme.

Si muhimu tena kudai kusawazisha “Yesu na Mungu” kama mawazo thabiti ya Agano Jipya. Yesu haitwi popote *ho theos*.⁴⁴⁹ Inaonekana yenye kushangaza kwetu sisi kuwa hakuna hali moja katika Maandishi ya neno “Mungu,” kwa rejeo ya Muunbaji mkuu, ambayo inaweza kumaanisha “Mungu kwa nafsi tatu.” Kama hakuna popote ambapo “Mungu” anabeba maana ya “Mungu kwa nafsi tatu,” hali ya Utatu unaanguka. Ushahidi unaonyesha kuwa Mungu wa nafsi tatu ni geni kwa ufunuo wa kiBibilia. Usomi wa Bibilia lazima utafute Ukristo upya ambao unaruhusu kuweka chini kwa Yesu kuwa Mungu mmoja. Aina ya Masiya, ajenti mkuu mtakatifu wa Mungu, atakuwa wa muhimu kwa kilakitu kinachosemwa katika Agano Jipya kumhusu yesu. Huduma za dini ilivyoelezwa kwa kiGiriki kwa neno *latreuo* unaelekezwa kwa onyesho 21 kwa Mungu Baba, huku heshima unalipwa kwa Masiya kama ajenti wa Mungu mmoja.

Profesa wa teolojia alisema katika mfululizo wa usomi wa Ukristo kuwa “mapokeo yetu inafurahia sana kwa wito wa *deceitism*.”⁴⁵⁰ Katika riba ya kuupata upya ubinadamu kamili wa Yesu, utukufu wa uMasiya na enzi ya Mungu mmoja, Baba yake, tunapendekeza kuwa inafaa ifurahie tena kwa Bibilia ya Ebrania. Labda hakuna anayeimba wimbo huo kuliko na Yohana.

⁴⁴⁹ Yohana 20:28 na Waebr. 1:8 yasipokuwa dhahiri peke yake. Nakala maalum inatumika katika fungu hizo na maana ya kumtaja mtu. Hakuna kokote katika fungu ambapo Yesu anaitwa Mungu kwa maana kabisa. Cp. C.F.D. Moule, *An Idiom Book of New Testament Greek*, 116, 117.

⁴⁵⁰ D.M. Scholer, Northern Baptist Seminary, winter quarter, 1986.